**24 JUNI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Hamsini na Mbili – Tarehe 24 Juni, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Anton Mwantona.

Na. 663

### Serikali Kuziwezesha Halmashauri Nchini

**MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha wastani wa uwezo wa halmashauri zetu kujitegemea unaongezeka na kuweza kukopa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuweka mikakati ya kuziwezesha halmashauri kuongeza mapato yake ya ndani kwa kuanzisha vyanzo vipya vya mapato na kuweka kwenye miradi ya kimkakati. Miongoni mwa miradi ya kimkakati iliyoanzishwa katika halmashauri ni pamoja na ujenzi wa stendi na masoko. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019 mpaka 2023/2024 Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 300.37 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni uwekezaji kwenye miradi ya kimkakati. Aidha, uwezo wa halmashauri kujitegemea umekuwa ukiongezeka kutoka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri zina wajibu wa kuhakikisha zinakusanya mapato kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura 290. Ukusanyaji wa mapato utaziwezesha halmashauri kutoa huduma stahiki kwa wananchi pamoja na kumudu gharama za kujiendesha

Mheshimiwa Naibu Spika, huhusu mikopo ya halmashauri kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura 290, halmashauri kwa idhini ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha zinaweza kukopa kutoka kwenye taasisi za fedha ikiwemo benki ili kuwekeza kwenye miradi ya kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantona.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe shukurani za pekee sana kwa Serikali, nimepatiwa shilingi bilioni 5.3 kwa ajili ya kujenga soko kubwa na la kisasa la kimataifa la ndizi pale kwetu Rungwe, hizi ni shukurani za pekee sana. Najua hili soko litaongeza uwezo wa halmashauri yetu kujitegemea lakini kurahisisha pia soko kwa wananchi wetu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa swali.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Serikali ina mikakati gani kulegeza masharti ya ukopaji

katika benki na taasisi zingine za fedha ili kuongeza uwezo wake wa kujitegemea kwa sababu halmashauri nyingi zinashindwa kukopa kwa sababu masharti ni magumu sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali ina mikakati gani kuweka angalau hata mradi mmoja kwenye kila halmashauri kuhakikisha kwamba hiyo miradi inasaidia kuongeza mapato ya halmashauri zetu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa maswali yake yenye tija sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza kuhusu masharti ya ukopaji, Ofisi ya Rais, TAMISEMI yenyewe kwanza ina mfuko maalumu ambao tuseme ni Bodi ya Mkopo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambayo ipo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ambayo na yenyewe inatoa mikopo nafuu kwa halmashauri kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati. Kwa hiyo hilo ni eneo moja ambalo Serikali imetengeneza kwa ajili ya kutoa mikopo nafuu kwa halmashauri kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata kwenye majibu ya msingi nimejibu nimesema kwamba kwa idhini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI lakini kwa kushirikiana pia na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, inaweza halmashauri ikaenda kwenye benki kwa ajili ya kutafuta mikopo. Kwa hiyo sasa katika ngazi hiyo ni makubaliano ya kimkataba ya kuhusiana na riba na kwamba fedha zitakopwa kwa utaratibu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lako la pili sasa Mheshimiwa Mbunge, umeuliza Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba kila halmashauri inaendelea kupata miradi hii ya kimkakati. Naomba nikuhakikishie kwamba Serikali tayari imekuwa ikihamasisha halmashauri kuanzisha miradi ya kimkakati na kipindi cha mwaka 2018/2019 mpaka 2023/2024 Mei, miradi ya

kimkakati iliyoidhinishwa ni 42 na yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 357.72 lakini miradi ambayo tayari imekamilika mpaka muda huu ipo kadhaa nitataja michache kama mfano, kuna Stendi ya Mabasi ya NaneNane iliyopo Dodoma, kuna Stendi ya Mabasi ya Magufuli Dar es Salaam...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nichukue fursa hii kuendelea kuzihamasisha halmashauri zote kuweza kuanza kubuni miradi ya kimkakati ilete na ifuate taratibu ili sasa halmashauri ziweze kuwa na miradi itakayowezesha kuanzisha au kuwa na mapato zaidi ili Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweze kujitegemea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bilakwate.

Na. 664

**Hitaji la Zahanati Kata ya Songambele - Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Songambele – Kyerwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022 Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Rutunguru ambacho kimekamilika na kilianza kutoa huduma Disemba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Songambele ina jumla ya wananchi 24,481 na ipo umbali wa kilometa 12 kutoka kwenye kituo cha karibu na hivyo inakidhi vigezo vya kujengewa kituo cha

afya. Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa katika mwaka 2025/2026 itatenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuanza ujenzi na Serikali Kuu itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa kituo hicho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na halmashauri kutenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuanza ujenzi na Kata ya Nkwenda imezidiwa ambayo ipo karibu na Kata ya Songambele, je, hamwoni kuna haja ya Serikali kuu kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi haraka ili kuondoa adha wanayoipata wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Zahanati ya Omukitembe Kata ya Kikukuru wananchi wamejenga, wameshaezeka ni zaidi ya miaka 10. Hamwoni kuna haja ya Serikali kutoa fedha ili kukamilisha zahanati hii ili wananchi waweze kupata huduma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu amekuwa akifuatilia masuala ya ujenzi wa miundombinu ya afya msingi kwenye jimbo lake mara kwa mara. Kuhusiana na swali lake lwa kwanza kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi kwamba japokuwa kuna fedha ambayo itatengwa kutoka kwenye mapato ya ndani ya halmashauri, yaani jumla ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya hichi cha Songambele lakini pia Serikali Kuu itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya kuendeleza kituo hicho. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge, toa hofu Serikali Kuu itaendelea kuunga mkono jitihada hizi za ujenzi wa kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, nichukue nafasi hii kwanza kuwapongeza wananchi kwa jitihada zao za kuhakikisha kwamba wameunga mkono jitihada za kimaendeleo kwa kuanza kujenga boma hili la zahanati katika Kata ya Kikukuru. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali itaendelea kutafuta fedha kuhakikisha kwamba inakuja kukamilisha zahanati hii ili iweze kutoa huduma ya afya msingi kwa wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Baada ya Serikali ya Awamu ya Sita kujenga Kituo cha Afya Bomela, Mtana na Kwihancha. Sasa wananchi wanapenda kujua ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba ili wapate huduma ya afya iliyokusudiwa katika maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali tayari imeshafanya jitihada kubwa ya kukamilisha vituo vya afya ulivyovitaja. Katika mwaka wa bajeti unaokuja mwaka wa bajeti 2024/2025 Serikali imejielekeza na imeweka kipaumbele katika kununua vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya kwenda kwenye vituo vyetu vya kutolea afya msingi kama hivi vya kituo cha afya kwenye jimbo lako. Kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali imetenga fedha na katika mwaka wa bajeti ujao Serikali itahakikisha inanunua vifaa tiba kuleta katika vituo vyako vya afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kata ya Kihanga ipo pembezoni sana, je, ni lini sasa Serikali itatupelekea kituo cha afya sawasawa na tulivyoomba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alishaleta taarifa waheshimiwa wabunge mtoe vipaumbele vyenu vya ujenzi wa kituo cha afya katika majimbo yenu. Mheshimiwa Mbunge, bila shaka kituo chako hiki ulikiorodhesha, naomba nikuhakikishie kwamba Serikali inahakikisha inatafuta hizi fedha kwa ajili ya kuja kujenga vituo vya afya hivi vya kimkakati mlivyoviahinisha waheshimiwa wabunge, ikiwemo kituo hichi cha afya kilichopo katika Kata ya Kihanga. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka.

Na. 665

**Upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi Vijijini**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la upungufu wa walimu wa shule za msingi katika maeneo ya vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuajiri walimu wa shule za msingi ambapo katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023, walimu 16,598 wa shule za msingi waliajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 wa shule za msingi na sekondari ambao watapangiwa vituo vya kazi katika maeneo yenye upungufu hususani maeneo ya vijijini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tabora Mjini lenye kata 29 na vijiji zaidi ya 43 lina upungufu mkubwa sana wa walimu na hasa vijijini katika Kata za Tumbi lakini katika Kata za Itonjanda, Kabila na kata zingine. Kwa mfano Kata ya Tumbi shule ya Itema ina wanafunzi 328 lakini ni walimu watatu tu waliyopo pale, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha katika hizo ajira 12,000 kuipa upendeleo Jimbo la Tabora Mjini ili kupata walimu wa kutosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa walimu wengi hawapendi kwenda vijijini na wamejaa shule za mjini, je, Serikali ina mpango gani wa kuweka vivutio ambavyo vitawafanya walimu wengi wapende kukaa vijijini kama ambavyo wamejaa katika shule za mjini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza Mheshimiwa Mbunge, Manispaa ya Tabora ina uhitaji wa walimu 778 na walimu waliopo ni 702 kwa hiyo kuna upungufu wa walimu 85 lakini katika shule za msingi mahitaji ya walimu ni 1,214, walimu waliyopo ni 901, kwa hiyo kuna upungufu wa walimu 313. Mheshimiwa Mbunge kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu ya msingi ni kwamba katika mwaka wa fedha unaokuja na katika awamu inayokuja Serikali inampango wa kuajiri walimu 12,000. Kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba na wewe utapata mgao wa walimu katika walimu hawa watakao ajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mgao huo utazingatia uwiano wa kila mkoa, utazingatia uwiano katika halmashauri, mahitaji katika

shule na maeneo tofauti tofauti ili maeneo yote ya Tanzania yaweze kupata mgao huo wa walimu. Nikuhakikishie na wewe (Mheshimiwa Mbunge) katika jimbo lako utapata mgao huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, tunatoa maelekezo na tumekuwa tukisisitiza halmashauri ziweze kufanya msawazo wa walimu. Yaani walimu wale ambao wapo kwenye maeneo ya mjini halafu kuna uhitaji mkubwa wa walimu kwenye maeneo ya vijijini basi halmashauri zinaweza kufanya msawazo kwa kupunguza walimu kuwapeleka vijijini ili kupunguza ukali wa upungufu huko kwenye maeneo ya vijijini. Kwa hiyo Serikali pia inaendelea kuhakikisha inaboresha mazingira ya kufundishia na yakujifunzia kwenye maeneo ya vijijini. Ndiyo maana kwenye mradi wa *SEQUIP* lakini kwenye mradi wa *GPETSP* Serikali imekuwa ikiwekeza zaidi katika kujenga nyumba za walimu lakini kuimarisha na kuiboresha miundombinu ya shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali kwa kutumia mbinu hizo inajitahidi sana kuhakikisha kwamba inatengeneza mazingira mazuri ambayo yatawavutia walimu kuweza kufanya kazi pia vijijini ili kupunguza ule upungufu wa walimu katika maeneo ya vijijini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna walimu wanajitolea kwa miaka mingi sana kwenye shule zetu, zinapokuja ajira hawafikiriwi, mnafikiria watu wapya kabisa, ambao ndiyo mnawaajiri. Hii siyo sawa na tulishawahi kushauri, wekeni *data* ya walimu wote wanaojitolea, nafasi zinapokuja wapewe wao kipaumbele sababu tayari wameshaonesha uwezo, uzalendo na utiifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kumsisitiza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa walimu wanaojitolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Rungwe kuna walimu walijitolea zaidi ya miaka mitatu, ajira mpya zitakapokuja mnaonaje mkalitazama jimbo hilo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mwongozo wako na ushauri wako kwetu na nikiwa namjibu Mheshimiwa Mbunge pia tumepokea hayo mawazo na maoni mazuri sana yakuweza kuwatazama wale walimu wanaojitolea ili na wenyewe waweze kupata nafasi ya kuajiriwa katika ajira mpya. Sisi kama Serikali tumepokea na tutashirikiana na wenzetu wa utumishi kulichakata na kuona namna nzuri ya utekelezaji wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Taska Mbogo. Kwa niaba Mheshimiwa Neema.

Na. 666

**Ongezeko la Vifo vya Mama na Mtoto Mkoani Katavi**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA K.n.y. MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza vifo vya mama na mtoto katika Mkoa wa Katavi ambapo kuna ongezeko kubwa kwa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitaifa vifo vimepungua kutoka vifo 556 mwaka 2016 hadi vifo 104 mwaka 2023, ambapo kwa mujibu wa *WHO* ilitegemewa vifo vipungue kufikia 225 ifikapo mwaka 2025. Hivyo Serikali imefanikiwa kupunguza kabla ya muda uliotegemewa na kuvunja rekodi ya kufikia 104 badala ya 225 iliyotegemewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za Mfumo wa Utoaji Taarifa za Afya (MTUHA) vifo vitokanavyo na uzazi unaonesha kwamba, tangu mwaka 2020 hadi 2024 mtiririko wa

vifo vya akina mama Mkoa wa katavi ni kama ifuatavyo: Mwaka 2020 vifo 56; mwaka 2021 vifo 41; mwaka 2022 vifo 36; mwaka 2023 vifo 33; na mwaka 2024 kuanzia Januari hadi Mei kuna vifo 15. Hivyo kwa mujibu wa takwimu hizi kuna kupungua kwa vifo vitokanavyo na sababu za uzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimba kama ifuatavyo: -

(i) Kutoa mafunzo kwa jamii na kwa watoa huduma za Afya ndani ya Mkoa wa Katavi;

(ii) Ujenzi wa vituo vya Afya vinavyotoa huduma za upasuaji ambapo kwa mwaka 2021 hadi 2024 vituo vya Afya nane vimejengwa;

(iii) Kuimarisha mfumo wa rufaa kutoka ngazi ya Jamii, vituo vya Afya hadi Hospitali ya Mkoa;

(iv) Kuongeza idadi ya watumishi ambapo kwa mwaka 2021 hadi 2024 Mkoa umeajiri jumla ya watumishi 468 kwa kada mbalimbali za afya; na

(v) Kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa ajili ya huduma za mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, japo kuwa vifo vinaendelea kushuka bado vifo vipo. Nikitolea mathalani kwenye Wilaya ya Muleba tangu Januari mpaka sasa wameshafariki wanawake sita wajawazito na mwingine amefariki tarehe 21, mwezi huu Juni. Vivyo hivyo, kwa Bukoba Mjini kati ya Januari mpaka Aprili wameshafariki wanawake nane. Moja ya

changamoto kubwa ni idadi ya wakunga, nikichukulia Bukoba Mjini tuna jumla ya wakunga 72, wakati tunahitaji wakunga 195. Kwa hiyo, kuna upungufu wa wakunga 61. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na idadi ya wakunga wa kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali ina jitihada gani ya kuhakikisha kwamba katika kila kituo cha afya kuna kuwa na wataalamu wa kutoa elimu ya lishe, kwa sababu moja ya visababishi ya vifo vya kimama na watoto ni suala zima la lishe? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze Mbunge kwa sababu kwa kweli maswali yake yote mawili hasa hili la pili ni maswali kwa kweli yanayohitaji tafakari kina na amefikiria vizuri ndiyo eneo lenyewe ambalo sasa hivi Serikali inahangaika nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge moja umeona kwamba Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliposimama hapa Bungeni eneo ambalo alilolisimamia na kulizungumzia kwa kusisitiza tukiwa wote hapa Bungeni alipofika eneo la vifo vya wakina mama na watoto alirudia mara mbili mbili. Wakati huo anasimama vifo vilikuwa ni 556 na umeona hapa wakati anasimama hapa kwanza ilitegemewa mwakani tuwe tumeshusha 225 lakini mwaka jana vimeshashuka vimefika 104. Tunasema bado vifo vipo, bado 104 ni vifo lakini Serikali imevunja *record* ukilinganishwa na kilichotegemewa na na *WHO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunachoweza kukuambia moja kwenye eneo la watumishi umeona kuna madaktari wamekuja hapa wanaitwa Madaktari wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambao wanazunguka nchi nzima kwenda kuwajengea uwezo kule chini wa mambo mbalimbali hasa huduma za mama kwa watendaji wetu. Kwa hiyo, wakati tunaendelea kuajiri kama kawaida ambapo mwezi wa Julai mwaka huu ajira nyingine zinatoka, lakini kuna hao madaktari

wanaozunguka wanawajengea uwezo kule chini kwa watumishi wengine kuhakikisha kuziba lile *gap*. Hilo ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu na lishe, tushirikane kwa pamoja kwenye eneo la lishe, moja, wote tuendelee kuhamasishana lakini *capacity* inayojengwa kule chini na kila mama anayekuja kliniki mmeona kwamba *enrollment* ya wakina mama kuja kliniki imeongezeka imefika 92% tunataka ifike 100% ili tuweze kushughulikia hilo unalolisema.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anaifahamu Halmashauri ya Mbogwe nilishaenda naye na akaona Kituo changu cha Masumbwe. Mpaka leo vifaa tiba havijakamilika changamoto hii ya vifo kwa mama na mtoto bado inaendelea na mtu akipewa rufaa kwenye Kahama au Bukombe ni safari ndefu mpaka kufika wanakuwa wameshaumia. Sasa ni lini Serikali itatoa vifaa kwenye Kituo cha Masumbwe ili kusudi wananchi waweze kupata huduma? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mimi na Mheshimiwa Mbunge, tulienda kwenye kituo hicho. Mheshimiwa Mbunge nikuombe tukimaliza hapa, nikitoka nikienda kukaa pale njoo tukae hapo tupige simu kwa *DMO* wako alete idadi ya vifaa anavyovihitaji kwa ajili ya kupeleka pale na tupige simu *MSD* vifaa vipelekwe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika jitihada za kupunguza vifo vya mama na mtoto Serikali ilikuwa inawatumia hawa wakunga wa jadi. Je, Serikali bado ina mpango wa kuwatumia hawa wakunga ambao walikuwa wanasaidia wanawake walioko vijijini ambako hakuna huduma ya afya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu hata mimi niliyesimama hapa ni mkunga wa jadi ndiye aliyesaidia nikazaliwa lakini kwa sasa ninachoweza kusema ni kwamba tunashirikiana nao kwa karibu, lakini kwa kuwaelimisha zaidi kwamba wao wawe sehemu nzuri kwenye lishe kama anavyosema dada yangu pale Mheshimiwa Neema. Pia wawe ni wazuri wa kuwashauri wakina mama kuhudhuria kliniki na kwenda haraka hospitalini kwenye vituo vyetu vya afya panapooneka dalili za huyo mama kujifungua.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

Na. 667

**Ujenzi wa Barabara ya Tengeru kwenda Mererani kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya Tengeru kwenda Mererani utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Tengeru – Mererani yenye urefu wa kilometa 28 ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mwezi Julai, 2024. Baada ya kukamilika kwa usanifu na gharama za ujenzi kujulikana Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini ikikumbukwe kwamba barabara hii ni muhimu sana inaunganisha Mikoa miwili ya Manyara na Arusha. Pia ni kiunganishi cha Soko la *Tanzanite* inayochimbwa pale Mererani. Je, Waziri yupo tayari kuambatana nami twende tukazungumze na wananchi ili wajue kwamba hili analolisema ni la kweli? Maana tulikuwa tunaizungumzia muda mrefu lakini kila siku halifanyiki**.** *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, upo tayari kuambatana na Mheshimiwa Dkt. Pallangyo?

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tunazo ahadi za Mheshimiwa Rais nyingi sana kule Arumeru Mashariki kilometa tano za lami pale Mji wa *Usa River;* kilometa 33 za barabara ya King'ori kuanzia Malula - Kibaoni kwenye mpaka Ngarenanyuki – Oldonyosambu. Je, hizi ahadi zitatekelezwa lini maana ni za muda mrefu sana? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, si mtazungumza huko mkikutana *site*? Si umemwomba Waziri mtakutana huko *site*?

Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nipo tayari kwenda kwenye Jimbo la Arumeru la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo na kuwaeleza wananchi mipango Serikali ya kuhusu miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi za viongozi nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tutazitekeleza na

tunategemea kukamilisha sasa usanifu wa barabara hiyo ya *Usa River* - Ngarenanyuki hadi Oldonyosambu ikiwa ni maandilizi pia ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea. Kwa niaba Mheshimiwa Shangazi.

Na. 668

**_TANROADS_ Kuweka Taa za Barabarani Korogwe**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza:-

Je, lini *TANROADS* watamalizia zoezi la kuweka taa za barabara ya Dar es Salaam – Arusha katika Mji wa Korogwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya taa 67 zimewekwa katika Mji wa Korogwe kwenye eneo la urefu wa kilometa mbili. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia *TANROADS* imepanga kukamilisha uwekaji wa taa za barabarani katika Mji wa Korogwe ambapo taa 22 zitawekwa katika eneo lenye urefu wa meta 700 na katika Mji wa Kabuku taa 22 zitawekwa katika eneo lenye urefu wa meta 700, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika. katika Mji wa Mlalo ambapo kuna ujenzi wa barabara kiwango cha lami kwa eneo la kilometa tatu mradi huu ni pamoja na uwekaji ama ufungaji wa taa za

barabarani. Je, mradi huu wa ufungaji wa taa za barabarani utaanza lini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, katika Mji wa Mlalo ni kweli tunajenga hizo kilometa tatu kwenye mji na tunategemea kwamba mara tutakapokamilisha mwaka wa 2024/2025 kwa maana ya bajeti tunayokwenda kuiendea tuweze kukalisha hiyo ahadi ya kuweka taa katika Mji wa Mlalo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kutupatia taa katika Jimbo la Ngara lakini hizo taa hazitoshi. Ningeomba Serikali watuongezee taa ili kutoa fursa kwa wananchi waweze kufanya biashara nyakati za usiku. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nichukue nafasi hii kumwelekeza *Manager* wa Mkoa wa Kagera aende Mji wa Ngara na afanye tathmini aone ni kiasi gani cha taa ambazo zitahitajika ili tuweze kuongeza idadi ya taa katika Mji wa Ngara. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

Na. 669

**Kufunguliwa Akaunti ya Pamoja ya Fedha ya Zanzibar na Tanzania Bara**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza:-

Je, lini Akaunti ya Pamoja ya Fedha ya Zanzibar na Tanzania Bara itafunguliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, utaratibu wa kuchangia fedha zitakazowekwa kwenye Akaunti ya Fedha ya Pamoja na matumizi ya fedha hizo, umependekezwa na Tume ya Pamoja ya Fedha na kuwasilishwa katika Serikali mbili kupitia Ripoti ya Mapendekezo ya Vigezo vya Kugawana Mapato na Kuchangia Matumizi ya Uendeshaji wa Shughuli za Muungano. Hadi sasa, Serikali mbili zimeendelea na mashauriano na majadiliano kuhusu kufikia uamuzi wa pamoja kuhusu utaratibu wa kudumu wa kuchangia matumizi na kugawana mapato ya Muungano. Maamuzi ya pamoja yatakapofikiwa na pande zote mbili za Muungano, ndiyo yatakayowezesha kufunguliwa kwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Ibara ya 133 na 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelekeza kufunguliwa kwa akaunti hiyo. Je, ni nini kilichokwamisha mpaka leo haijafunguliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Serikali ya Muungano wa Tanzania ina kofia mbili Serikali ya Muungano na Serikali ya Tanzania bara. Je, ikitokea sasa mapato haya upande mmoja umelalamikia mgawanyo hatuoni kwamba tutakuwa tumeutia doa Muungano wetu huu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Issa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimtoe wasiwasi na nimtoe shaka kwamba Serikali haijakwama ndiyo maana tukasema utaratibu unaendelea na mapendekezo yakikamilika basi Akaunti ya Pamoja itafunguliwa. Kwa hiyo, nikutoe shaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hatuwezi kusema kwamba upande mmoja unaweza kulalamika. Tunasema tunashauriana, mashauriano hayakatazwi katika kujenga nchi ya pamoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani. Kwa niaba Mheshimiwa Asia.

Na. 670

**Mkakati wa Kupambana na Uraibu wa Mchezo wa Kamari**

**MHE. ASIA A. HALAMGA K.n.y. MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na uraibu wa mchezo wa kamari unaoongezeka kwa kasi kwa vijana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na faida za kiuchumi zinazotokana na michezo ya kubahatisha, Serikali inatambua athari hasi katika jamii endapo haitaendeshwa kwa uweledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(2)(i) cha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura 41, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ina jukumu la kuhakikisha kuwa jamii inalindwa ipasavyo dhidi ya athari hasi za michezo ya kubahatisha. Katika kutekeleza jukumu hilo, Bodi imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuzuia na kudhibiti athari hasi zitokanazo na michezo ya kubahatisha. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha udhibiti na uratibu wa sekta kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa waendeshaji;

(ii) Kuendelea kutoa elimu kwa jamii na wadau kuhusu athari hasi za michezo ya kubahatisha;

(iii) Kutoa maelekezo na kusimamia utekelezaji wake kwa waendeshaji wa michezo ya kubahatisha kuhusu kuchukua hatua mbalimbali za kulinda jamii ikiwemo kuwazuia wachezaji wanaobainika kuelekea katika uraibu;

(iv) Kuzuia na kudhibiti michezo ya kubahatisha isiyo na usajili ambayo ni chanzo kikubwa cha athari mbaya kwa jamii; na

(v) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Watoa Habari yenye lengo la kuishirikisha jamii kutoa taarifa kuhusiana na michezo ya kubahatisha ikiwemo waendeshaji haramu, ushiriki wa watoto chini ya umri wa miaka 18 na ushiriki uliopitiliza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwanza, napongeza kwa majibu mazuri ya Serikali lakini bado tumekuwa tukishuhudia kuna changamoto kubwa ya uchezeshaji wa michezo ya kamari haswa kwenye makazi ya watu na imekuwa ikiathiri sana vijana. Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuleta sheria kali zaidi ili kuweza kuwabana waendeshaji na kuweza kutatua athari ambayo wanapata vijana pamoja na wananchi hasa kwenye makazi na kulijenga Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu namba mbili, changamoto ya uraibu imekuwa ingeendana sambamba na ugonjwa wa afya ya akili. Je, ni kiasi gani cha mapato

yanayotokana na fedha kamari yanayosaidia huduma ya afya ya akili kwa Watanzania?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia, michezo hii ipo mitaani kwetu tunazo Kamati za Ulinzi na Usalama mitaani kwetu, wapo Madiwani, wapo Wabunge na vipo vyombo vya dola. Tuisaidie Serikali kupambana na haya mambo.

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza, nikushukuru kwa kuweka ufafanuzi lakini kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba Serikali inapitia Sheria yake Na. 41 mara kwa mara ili kuona kwamba kuna mapungufu ambayo yametokea na kuweka vifungu ambavyo baadaye vitaleta maamuzi ya Sheria ambayo ni hatua kali sana. Nikuhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba hili linafanyiwa kazi siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba baadhi ya vijana wanaweza kuingia kwenye uraibu na kupata tatizo la afya ya akili lakini Serikali imelisimamia hilo na imeweka mafungu maalumu ya kutoa elimu kwa jamii lakini pia hata kuongezea kipato katika sekta ya afya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Margaret Sitta.

Na. 671

**Kukabiliana na Ongezeko la Bei za Pembejeo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isiruhusu mbolea kuwekwa kwenye vifungashio kuanzia kilo moja na zaidi ili kukidhi mahitaji ya wakulima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba nijibu swali la Mheshimiwa Margaret Sitta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 32 (4) cha Kanuni za Mbolea za Mwaka 2011 kimeainisha kuwa mbolea yabisi *(Solid Fertilizers)* zitafungashwa kwenye uzito wa kilo tano, kilo 10, kilo 25 na kilo 50. Kifungu cha 32 (5) cha Kanuni hizo kimeainisha kuwa visaidizi vya mbolea *(Fertilizer supplements)* vitafungwa katika ujazo wa lita tano, lita 10, lita 20, lita 50 na lita 100. Aidha, Kifungu cha 33 (1) kimeainisha kuwa mbolea za kimiminika *(Liquid fertilizers)* zitafungwa katika ujazo wa nusu lita, lita moja, lita tano na lita 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwepo kwa fursa hiyo ya kisheria, wazalishaji/waingizaji wa mbolea wanaotaka kufungasha mbolea katika ujazo wa kilo moja wanaruhusiwa kuomba kibali maalumu kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania *(TFRA)*. Aidha, Serikali kupitia *TFRA* inaendelea kudhibiti wafanyabiashara wadogo kupima mbolea katika mizani kama bidhaa za kawaida kwa kuwa kufanya hivyo kunapoteza ubora wa mbolea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba sasa ajibu maswali yangu mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, je, Serikali inatuhakikishiaje kwamba, mbolea ya tumbaku itafika kabla ya Mwezi wa Julai ili wakulima wawaanze kutengeneza ma-*bed* yao kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Serikali safari hii ipo tayari kupeleka mbolea yenye ruzuku karibu na wakulima ili wasifuate kwa muda mrefu kwenda kuchukua mbolea hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, kwanza tunashukuru kwamba mmeshaipitisha bajeti ya Wizara ya Kilimo tunaenda kwenye utekelezaji baada ya kupitishwa kwa Bajeti Kuu. Kuhusu mbolea ya ruzuku nimtoe wasiwasi mbolea zitafika kwa wakati kwenye maeneo husika kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kuanza matayarisho ya awali. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itahamasisha kilimo kinachotumia mbolea katika Wilaya Kilwa ili kukabiliana na changamoto ya kilimo cha kuhamahama kinachosababisha uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kilimo cha mbolea ni kampeni iyokwenda nchi nzima. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge mnajua watu wengine wanalima kwa imani kwamba akitumia mbolea labda anapoteza uhai wa ile ardhi ya asili. Kwa hiyo, niwaombe tuungane wote kuwapa hamasa wakulima ili waweze kutambua umuhimu wa mbolea na ndyio maana Serikali imekuwa ikiingiza mbolea kila wakati kwa matumizi ya Watanzania hawa, ahsante

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi niulize Serikali kwanza nimefurahi jinsi alivyoainisha kwenye Kanuni ufungashaji wa kilo moja kilo tano na kuendelea ya mbolea lakini kwa sababu mbolea hizo hazipatikani madukani. Je, sasa ni lini Serikali itaviamrisha viwanda na wafungashaji wote hizi mbolea zipatikane madukani ili wakulima waweze kununua mbolea hizo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa viwanda vyote hapa nchini kuhakikisha vinazingatia utaratibu ambao umewekwa kisheria wafungashe mbolea hii kwa ujazo ambao tumeutaja kisheria ili kuwasaidia watu kufikiwa na viwango wanavyovihitaji kwa wakati, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tunaendelea, Wizara ya Utamaduni na Michezo Mheshimiwa Kanyasu.

Na. 672

**Kuhamasisha Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kutengeneza vipaji vya wachezaji wa mpira wa miguu nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza mpira wa miguu nchini Wizara kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka nchini *(TFF)* na wadau inaratibu na kusimamia programu mbalimbali za kutengeneza vipaji vya wachezaji wa mpira wa miguu ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa vituo vya kulea vipaji (Akademia) vya michezo, kuratibu ligi na mashindano ya Kimataifa ya vijana ya miaka 20 na miaka 17; kuratibu na kushiriki mashindano ya Kimataifa ya Shule *(CAF African School Football Championship)*; na kupeleka vijana wenye vipaji kwenye vituo vya kulea vipaji vya michezo nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetenga shule 56 za sekondari katika mikoa yote kwa ajili ya kukuza na kulea vipaji vya michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu pamoja na kuendelea kuratibu mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA ambapo wachezaji watakaofanya vizuri watapelekwa kwenye timu za Taifa za chini ya miaka 20 na chini ya miaka 17 kwa ajili ya kuendeleza vipaji vyao kila baada ya mashindano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mikakati hii, tunaamini kwamba tutafanikiwa kuibua, kukuza, na kuendeleza vipaji vya michezo na wachezaji wa mpira wa miguu nchini na hatimaye kuwa na Timu ya Taifa yenye uwezo wa kushindana kimataifa na kuleta heshima kwa nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa michezo hii ya UMITASHUMTA, UMISSETA imekuwa ikifanyika kila mwaka na kila mwaka kuna wachezaji bora ambao wamekuwa wakipatikana kwenye michezo hii. Serikali inazo kumbukumbu za wachezaji hawa za kila mwaka na ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba wachezaji hawa wanalelewa na wanakua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa wachezaji wengi wa sasa wanapatikana kwenye *academy* binafsi na *academy* hizi zinatumia gharama kubwa na gharama zake zenyewe, kuna utaratibu wowote Serikali inafanya ili baada ya mchezaji huyu kuanza kutumika kwenye vilabu vikubwa *academy* zake ziweze kufaidika na ziweze kujiendesha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nimpongeze

Mheshimiwa Kanyasu kwa jiihada kubwa anazofanya kufuatilia maendeleo ya michezo nchini, ni mwanamichezo mzuri japokuwa matokeo hayakuwa upande wake siku ya jumamosi kwenye bonanza lakini naamini haitamkatisha tamaa. Naomba kujibu maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunayo kanzidata ambayo imekuwa ikihifadhi majina ya wachezaji wanaofanya vizuri kwenye michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA na kwa kipindi kirefu sasa wamekuwa wakiendelezwa vipaji vyao kwa kupitia kituo cha *TFF* kule Tanga lakini pia vituo vya *Fountain Gate* na *Alliance* kilichoko Mwanza lakini hali kadhalika Jeshi la Kujenga Taifa mwaka huu linaanzisha kituo chake ambapo tutakuwa tukiwapeleka wachezaji hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika Serikali kuanzia mwaka huu nayo inaanza kutengeneza timu za chini ya miaka 17 na chini ya miaka 20 ambazo tutakuwa tukizihifadhi katika shule moja na kuzipitisha katika programu maalumu kwa ajili ya kulinda na kuendeleza vipaji vyao. Kwa hiyo hili nimtoe wasiwasi linaendelea kufanyika na tutaendelea kufanya kwa kadiri hali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili, kwa kutumia kanuni namba 101 ya *FIFA* inaeleza na inabainisha wazi kabisa kwamba kati ya asilimia tano na asilimia kumi ya ada ya mauzo ya kila mchezaji yanatakiwa kwenda kwa akademia iliyomlea mchezaji huyu na tunapata wakati mgumu kidogo kwa sababu siyo wachezaji wetu wote hapa nchini wanapita katika utaratibu rasmi wa akademia lakini wote waliopita kwenye akademia utaratibu huu unatumika na zimekuwa zikipata malipo kutokana na kazi nzuri ya kulea wachezaji husika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa *Nyerere Stadium* kule Mbulu Mjini ni uwanja muhimu sana na uliwahi kuchezesha michezo ya mashindano ya kanda, je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuendeleza Uwanja wa *Nyerere Stadium* kule Wilayani Mbulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kimsingi Serikali inayo mipango ya kuendeleza miundombinu mingi ya michezo nchini na kwa kuanzia tunaanza viwanja vitano na kama ambavyo nilijibu wiki mbili zilizopita bado tunajadiliana na wamiliki wake ili kutengeneza utaratibu wa kuvikarabati na kuvitumia pamoja na matunzo ya viwanja hivi. Kwa hiyo suala la kutengeneza viwanja na miundombinu mingine ya michezo linakwenda kwa awamu na nina imani Mheshimiwa Mbunge kule Mbulu tutakufikia na tutafanyia ukarabati uwanja wako na kuhakikisha unakuwa katika hali nzuri ya kuchezea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona uibuaji wa vipaji vya mpira wa miguu ume-*base* sana kwa vijana wa kiume na timu za wanaume. Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha vijana wa kike nao wanapata fursa ya kuibuliwa vipaji vya mpira wa miguu na hasa kuleta hamasa kwa timu za wanawake za mpira wa miguu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Sylvia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilieleza kuhusiana na uibuaji na uendelezaji wa vipaji wa vijana wa kiume utaratibu huu haubaki tu kwa vijana wa kiume, ukiangalia hivi vituo ambavyo nimevitaja kwa mfano *Fountain Gate,* kile cha *TFF* kule Tanga na hata *Alliance* vyote vina timu za watoto wa kike na vijana wa kike ambao wanafanya vizuri kwenye mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA wamekuwa wakichukuliwa na wakilelewa kwenye vituo hivyo. Kwa hiyo mkakati tunao mzuri tu

wa kuendeleza mpira wa miguu kwa vijana wa kike na nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge, miongoni mwa michezo ambayo tunafanya vizuri ni mpira wa miguu kwa vijana wa kike na hatuwezi kulifumbia macho jambo hili katika kuendeleza vipaji vya watoto hawa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina, jiandae Mheshimiwa Sanga, jiandae Mheshimiwa Mafuwe. Mheshimiwa Regina au Mheshimiwa Dkt. Mabula? Mheshimiwa Dkt. Mabula, umehama kiti chako naona?

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri, *Tanzania Football House* iliyopo Bwiru Mwanza imekuwa ikijitahidi sana katika kuwatafutia vijana maeneo ya kuweza kuonesha vipaji vyao na mpaka sasa vijana zaidi ya kumi wapo nje ya nchi akiwemo Kelvin John, Adrew Michael, Joseph Seba, Augustin Chalamba...

**NAIBU SPIKA:** Swali Mheshimiwa.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni namna gani Serikali inafuatilia mustakabali wa stahiki zao huko wanakokwenda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo inafahamika masuala ya akademia kuuza ama kupeleka vijana nje ya nchi ni masuala ya kimikataba na yanalindwa na kanuni ambazo zimepangwa chini ya *FIFA*. Kwa hivyo kama kutatokea matatizo, kama kutatokea kutokuelewana kati ya akademia hizi zilizopeleka wachezaji nje ya nchi na kule walikopelekwa Serikali ipo tayari kuingilia kati lakini kwa sasa nafikiri kila kitu kipo sawa na hatujapata malalamiko yoyote kuhusiana na masuala haya.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Sanga, jiandae Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, katika *development model* kuna hatua tatu za wachezaji kukuwa na Zanzibar inatajwa kama ndiyo sehemu ambapo kuna *development model* nzuri ya wachezaji ambapo Ghana imeiga, Nigeria imeiga; wachezaji wanafuata *step* tatu, *grassroot*, *juvenile* na *junior* ili waweze kucheza kwenye *premier league*. Ipi kauli ya Serikali kufuata utaratibu wa Zanzibar mchezaji asicheze ligi kuu kama hajapita kwenye *academy?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, anachouliza Mheshimiwa Sanga ni kuhusiana na kurasimisha kwamba utaratibu wa akademia ufikiwe kwanza kabla ya wachezaji kwenda kwenye ligi kuu. Nafikiri ni wazo zuri isipokuwa kwa sababu hatukuwa na akademia nyingi ambazo zinapitisha wachezaji kwa sasa, pengine lingekuwa gumu kulifanya lakini ni wazo zuri na naomba kulichukua kuona namna ambavyo tunaweza tukali-*implement*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, wakati wa uzinduzi wa *Saashisha Cup* Serikali ilituahidi wale vijana waliofanya vizuri wataingizwa kwenye kanzidata lakini watatafutiwa timu kama sehemu ya kuwa-*motivate* waweze kuendeleza vipaji vyao. Je, ni lini Serikali itafanya na kutekeleza ahadi hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hebu rudia tena swali lako.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uzinduzi wa Ligi ya *Saashisha Cup* ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ndio alikuwa mgeni rasmi, Serikali iliahidi kwamba vijana wale waliofanya vizuri watachukuliwa na kutafutiwa timu za kucheza kama sehemu ya kuwa-*motivate,* je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, utekelezaji wa ahadi ile upo pale pale, haujavunjika. Nimwombe Mheshimiwa Saashisha tuwasiliane na anipe vijana ambao yeye anawaamini na mimi nitawapeleka kwenye hizi akademia zilizopo sehemu mbalimbali nchini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** *Club* ya Simba ilikuwa ya kwanza kuanzisha *under 20* na *under 17,* vilabu vingine viige mfano huo. Mheshimiwa Waziri ahsante. *(Makofi)*

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Saputu. *(Makofi)*

Na. 673

**Eneo la Nengungu**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawakabidhi Wananchi wa Kijiji cha Nengungu eneo lao linalong'ang'aniwa na Chuo cha Jeshi Monduli?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 01 Oktoba, 2014 Bwana Lembusel Mbasha na wenzake watatu walifungua Shauri la Ardhi Na. 73/2015, dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Chuo cha Jeshi Monduli katika Mahakama Kuu – Divisheni ya Ardhi Arusha. Tarehe 05 Disemba, 2016 Mahakama ilisikiliza shauri hilo na kufanya uamuzi kuwa, Bonde la Ole Musa ndiyo mpaka wa ardhi kati ya eneo linalomilikiwa na Chuo cha Jeshi Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uamuzi huo, Mahakama iliamua kwamba Chuo cha Jeshi Monduli kiwalipe Bwana Lembusel Mbasha na wenzake fidia ya kuharibu mazao yao ambayo walidai yameharibiwa na Askari wa Chuo cha Jeshi Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa haikuridhishwa na uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Ardhi Arusha. Hivyo, kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliamua kukata rufaa katika Mahakama ya Rufaa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa shauri hilo liko katika Mahakama ya Rufaa Tanzania likisubiri kupangiwa tarehe ya kusikiliza, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa vile suala hili lipo Mahakamani tunalivuka mpaka Mahakama itakapoamua.

Tunakwenda sasa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Kaboyoka.

Na. 674

**Serikali Kusimamia Utunzaji wa Mandhari za Makazi**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kutenganisha upimaji wa viwanja kila mwananchi aweze kujenga uzio wa kujitegemea ili kuwe na *"no man's land"?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, upangaji na upimaji wa ardhi hufanywa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mipangomiji, Sura 355 na Sheria ya Upimaji Ardhi, Sura 324. Sheria hizi zinaelekeza upangaji na upimaji ardhi kuzingatia utengaji wa ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile makazi, makazi na biashara, biashara, viwanda, kilimo, huduma za kijamii na miundombimu ya msingi ikiwemo barabara, nishati, huduma za maji safi na maji taka na mawasiliano. Aidha, uendelezaji wa ardhi iliyopangwa na kupimwa huongozwa na Sheria ya

Mipangomiji, Sura 355 pamoja na Kanuni zake ambapo pamoja na mambo mengine, mmiliki wa kiwanja anatakiwa kuzingatia mipaka ya kiwanja chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli kwamba ardhi ni rasilimali adimu ambayo inatakiwa kutumika kwa ufanisi na tija, masharti ya uendelezaji yameelekeza uwepo wa mpaka wa pamoja baina ya viwanja vinavyopakana. Utaratibu huu unawezesha kutokuwepo kwa ardhi huru baina ya viwanja na hivyo kuepusha uvamizi, uhalifu, utupaji holela wa taka, kupunguza gharama za ujenzi na kuwa na matumizi endelevu ya ardhi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uvamizi wa uchochoro maana *no mass lands it means* ni uchochoro siyo rahisi sana na kwa kuwa utupaji wa taka kiholela sasa hivi taka zinatupwa kwenye mitaro na kwa kuwa unasema itapunguza gharama za ujenzi, je, kweli mnapotoa ardhi mnaweka wapangaji wawili kwamba nyie mnaopewa ardhi hii mtajenga ukuta huu kwa pamoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kiusalama huoni kwamba nyumba zikishikana wakati wa moto ni rahisi sana nyumba nyingi kuungua kwa wakati mmoja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ni kwamba ardhi yenyewe kwa kweli mkianza kuiacha vipande vipande maana yake hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni kwamba je, baada ya kupima kiwanja kimoja tuache uchochoro halafu tukapime kiwanja cha pili kwa maelezo aliyoyatoa hapo lakini nipende tu kukupa *comfort* kwamba ninaamini hakuna

ambaye anagombana na jirani yake kwa sababu tu ya kutumia jiwe moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana hata sheria imetafsiri vizuri kwamba watashirikiana katika kujenga ukuta ule kwa namna yoyote ile watakayokuwa wamekubaliana kama sehemu ya ujirani wao. Vinginevyo ushauri umepokelewa na sisi tunaenda kuuchakata tuone kama je, una tija yoyote ambayo inaweza kuwaletea maslahi makubwa wananchi wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kuwa Serikali iliruhusu maeneo ya *squater* kupatiwa leseni za makazi na kuruhusu leseni za makazi kwenda kukopea benki, ni kwa nini sasa wametoa kila baada ya miaka miwili kulipia, kwa nini isiongeze muda kwa sababu wanakopea benki lakini wanatakiwa ku-*renew* baada ya miaka miwili tu, Serikali inasemaje kuhusiana na hilo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Mheshimiwa Dkt. Kabati tumeupokea wacha tukauchakate ili tuone namna ya kuongeza muda wa zile leseni za makazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Tarimo.

Na. 675

**Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)***

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa ambao unakwenda taratibu sana lakini ni muhimu sana kwa Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya upatikanaji Vitambulisho vya Taifa imeongezeka katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 ambapo hadi kufikia Mei, 2024 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* imezalisha jumla ya vitambulisho 21,322,098 sawa na 86% ya wananchi 24,818,138 waliosajiliwa na uzalishaji wa vitambulisho unaendelea. Aidha, jumla ya vitambulisho 20,340,713 vimekwishasambazwa kwenye Ofisi za Usajili za Wilaya, Serikali za Mitaa, Vijiji na Shehia kote nchini. Kati ya hivyo, vitambulisho 19,139,601 sawa na 94% vimeshachukuliwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai kwa wananchi wote ambao bado hawajachukua Vitambulisho vyao vya Taifa kufika katika Ofisi za Serikali za Mitaa na vijiji walipojiandikishia kwa ajili ya kuchukua vitambulisho vyao, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali lakini ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na takwimu alizotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwa nini bado kuna urasimu katika kupata vitambulisho hivi jambo linalopelekea mpaka baadhi ya maeneo watu kutoa rushwa mpaka 20,000 ndio wapewe vitambulisho vyao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa limeshakuwa ni hitaji kwa vijana wanaomaliza shule na wanaotimiza umri wa miaka 18 popote wanapotaka kwenda kuomba aidha kazi au kuendelea na shule wanahitaji kuwa na vitambulisho hivi. Kuna mpango gani wa Serikali wa kuhakikisha vijana wanavyofikisha miaka 18 tu vitambulisho vyao vinakuwa tayari kwa sababu sasa vitambulisho vya kuzaliwa vinatolewa *immediately* pale anapozaliwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tarimo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe maelekezo kwa Wafanyakazi wa *NIDA* ambao wanafanya urasimu na hata kudai rushwa kwanza, waache mara moja na watoe vitambulisho hivyo bila kuwa na urasimu na wale watakaobainika kuomba rushwa sheria itachukuwa mkondo wake pamoja na kuwapeleka Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili naomba Mheshimiwa Mbunge arejee kwenye jibu la msingi kwamba katika mwaka wa fedha huu 2023/2024 upatikanaji wa vitambulisho sasa umekuwa wa uhakika na pia katika mwaka wa fedha unaokuja 2024/2025 tayari tuna mkakati wa kusajili na kutambua wananchi milioni mbili ambapo vijana ndio wengi na hata kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi kwa mwaka 2022 vijana ndio wengi. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge vijana watapata Vitambulisho vyao vya Taifa kwa ajili ya matumizi mbalimbali, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na utaratibu mzuri wa Mamlaka ya Vitambulisho vya *NIDA* pamoja na Uhamiaji kuzunguka vijijini kwenda kuandikisha wananchi ili waweze kupata Vitambulisho vya Taifa, hata hivyo utaratibu huo umekuwa ukisuasua hivi karibuni. Ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inawawezesha taasisi zote hizi ili ziende vijijini zikaandikishe wananchi waweze kupata Vitambulisho vya Taifa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Ndaisaba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwenye wilaya za mpakani kumekuwa na ushirikiano mkubwa kati ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA),* Uhamiaji, pamoja na Idara ya Wakimbizi kuhakikisha kwamba wananchi wenye sifa wanapata vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, hata kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha 2024/2025 tumetenga fedha ili kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo hayo wanapata Vitambulisho vya Taifa kwa wakati, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, swali la msingi linaelezea upatikanaji wa utaratibu kwa Vitambulisho vya Taifa; nilipenda kujua je, ni kwa nini kwa upande wa Zanzibar kwa kuwa kuna Vitambulisho vya Mzanzibari kwa upande ule kama vinachelewa kwa nini visitumike kama Vitambulisho vya *NIDA*? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa utaratibu ulipo sasa Zanzibar vinatumika Vitambulisho vya Mkaazi lakini pia kwa upande huu tunatumia Vitambulisho vya Taifa. Kwa hiyo, kwa sasa utaratibu huo unaendelea lakini tutafanya tathmini kuona kama mbele ya safari basi tutabadilisha sheria ili zitumike kwa pande zote za muungano. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Hasunga.

Na. 676

**Ujenzi wa Chuo Kikuu Sasanda – Songwe**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo Kikuu katika Eneo la Sasanda Mkoani Songwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa Chuo Kikuu ni mchakato unaohusisha pamoja na upatikanaji wa rasilimali fedha. Kwa sasa hakuna bajeti iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu Sasanda - Songwe. Hata hivyo, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa katika Mkoa wa Songwe kuna Kampasi ya Taasisi ya Elimu ya juu ambayo ni Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam *(DIT)* iliyopo Kata ya Myunga, Wilaya ya Momba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, katika Mkoa wa Songwe, kuna Tawi la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania lililopo Vwawa. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge awahamasishe Wananchi wa Mkoa wa Songwe na maeneo ya jirani kuitumia Kampasi ya *DIT* Myunga na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kilichopo Vwawa – Songwe pamoja na Vyuo Vikuu vingine vilivyopo katika Mikoa ya Jirani na nchi nzima ili kupata elimu na mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa *DIT* bado hawajaanza kutoa *program* za elimu ya juu, wanatoa

kwenye ngazi ya cheti; je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba wanaanza kutoa *program* za elimu ya juu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, mahitaji ya chuo kikuu ni muhimu sana katika Mkoa wa Songwe na hasa kwa kuzingatia kwamba ni Mkoa wa kimkakati. Je, upi mkakati ya Serikali wa kuhamasisha wadau mbalimbali ili waweze kujenga tawi la chuo kikuu kwa sababu hili la *DIT* liko zaidi ya kilometa 100? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwisha kueleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba uanzishwaji wa vyuo vikuu ni mchakato ambao sisi (Serikali) huwa tunashirikiana na sekta binafsi kama wadau wetu muhimu. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuhamasisha uanzishwaji wa vyuo hivi kufuatana na mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo lakini vilevile tukiwahamasisha na wenzetu wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, Wananchi wa Mkoa wa Songwe pamoja na Wananchi wa Jimbo la Vwawa katika mwaka wa fedha 2024/2025 tayari tumeshatenga fedha zaidi ya shilingi bilioni tatu na hizi fedha zitakwenda kutumika katika ile *campus* yetu ya *DIT* pale Vwawa na tutajenga jengo lenye ghorofa tano litakalokuwa na uwezo wa kubeba wanafunzi 400 kwa wakati mmoja na baada ya ujenzi huu sasa tutapanua wigo wa zile *course* ili kuweza kufikia na zile *course* za shahada na zile shahada ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa vyuo vyetu vikuu ni vyuo vya kitaifa na kimataifa, kwa hiyo havilengi sana kwenye ujenzi katika kanda au majimbo sana sana vinakuwa ni vyuo vya

kimataifa, kwa hiyo mahali popote vyuo vinapojengwa wananchi wanayo nafasi ya kupata fursa ya elimu katika maeneo hayo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa mabweni katika Chuo Kishiriki cha Mkwawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Jesca, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, labda Mheshimiwa Mbunge hajafika pale Mkwawa, ujenzi wa *hostel* unaendelea katika Chuo chetu cha Mkwawa na ninaomba nimhakikishie katika mwaka ujao wa fedha 2024/2025, tumetenga tena fedha katika mradi wetu ule wa *Higher Education for Economic Transformation*; tunakwenda kujenga majengo mengine ikiwemo na haya ya *hostel*. Kwa sasa kazi hiyo iko katika hatua ya manunuzi bila shaka itakapofika Mwezi Julai shughuli hiyo itaanza. Kwa hiyo, nikuondoe wasiwasi, ujenzi unaendelea katika Chuo chetu kile cha Mkwawa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wageni...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Wageni 42 wa Mheshimiwa Naibu Spika; Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli: Makatibu wa Siasa na

wenezi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Ilala na Majimbo ya Ilala, Segerea na Ukonga wakiongozwa na Ndugu Alhaji Said Sultan Sidde, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ilala. Karibuni na hongereni kwa kufanya mafunzo jana kwenye Ukumbi wa *NEC* Dodoma, hongereni sana. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Wabunge wote wa Mkoa wa Njombe; Viongozi wa Serikali na Chama Cha Mapinduzi. Ndugu Antony Mtaka - Mkuu wa Mkoa Njombe; Ndugu Judica Omary - *RAS* Mkoa wa Njombe; Ndugu Daniel Okoka - *MNEC* Mkoa wa Njombe; Ndugu Kissa Gwakisa - *DC* Njombe; Mheshimiwa Cluadia Kitta - *DC* Wanging'ombe; Mheshimiwa Victoria Mwanziva - DC Ludewa; Mheshimiwa Juma Sweda - *DC* Makete; Ndugu Julius Peter - Katibu wa CCM Mkoa wa Njombe; na Ndugu Josaya Luoga - Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; Wageni 176 wa Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu; Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi ngazi ya Matawi kutoka Chamwino Mkoa wa Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo; Familia yake wakiongozwa na Mke wake Ndugu Helga Raymond, pia wamo Viongozi wa Kampuni ya *SkyMax* (Wasambazaji wa *Business card* za kidigiti) kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine sita wa Mheshimiwa Mwinjuma, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo; Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Wanyanyua Vitu Vizito kwa watu wenye Ulemavu, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Wadogo zake kutoka Segerea Mkoani Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Masache Kasaka, Walimu kutoka Chunya Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Ndugu zake kutoka Mkoa wa Shinyanga. Karibuni. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mjasiriamali kutoka Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Tunae Mgeni wa Mheshimiwa Maryam Omar Said, Mpiga Kura wake kutoka Pandani Mkoa wa Pemba Kaskazini. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, Waandaaji wa *Miss Grand Tanzania 2024* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni 80 wa Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro kutoka Ngara Mkoa wa Kagera, familia yake kutoka Ngara, wasaidizi wa Ofisi ya Mbunge, Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi, Wenyeviti 22 wa CCM Kata za Ngara, Makatibu 22 wa CCM Kata za Ngara na Makatibu 22 wa Itikadi na Uenezi wa CCM Kata za Ngara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Abubakari Asenga, Meneja wa *TBA* Mkoa wa Morogoro na Familia yake. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, marafiki zake wa Dodoma kutoka Arumeru Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Ngw'asi Damas Kamani, mmiliki na wafanyakazi wa *Akyoo Motors* kutoka Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Wapo wageni nane wa Mheshimiwa Venant Daud Protas, watoto wake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: Ndugu Consolatha Assey na familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo viongozi wanne kutoka Azania *Foundation* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watano kutoka Chama cha Muziki wa Rhumba Tanzania (CHAMURUTA). *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 30 wa *Yali Alumni Chapter* ambayo ni Programu inayofadhiliwa na Ubalozi wa Marekani kutoka sehemu mbalimbali Nchini Tanzania. *(Makofi)*

Wageni 11 ambao ni Klabu ya Mpira wa Miguu kwa watu wenye Ulemavu kutoka Toroli Chang'ombe Temeke Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, namtangaza tena Mke wa Mwana FA. Najua hakusikia, ahsanteni. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Enhe, Mwongozo wa Spika.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuomba mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 76.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuomba mwongozo wangu kwa kutumia lugha ya Dar es Salaam, wanasema kazini kwako kuna kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kipeperushi kinatembea mitandaoni kuanzia Ijumaa na Jumamosi kuhusiana na wafanyabiashara wa Kariakoo na sehemu zingine kufunga maduka Jumatatu ambayo ni leo na tunavyozungumza sasa hivi Kariakoo imefungwa, hakufanyiki biashara. Pia sisi Waheshimiwa Wabunge kuna mambo tuliya-*raise* kwenye michango yetu, natambuka pia kwamba Kamati ya wafanyabiashara wako hapa kwa ajili ya kuzungumza na Serikali kutatuliwa matatizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba Kauli ya Serikali kulingana na ile hali iliyopo Kariakoo kwa sababu watu

wetu wa vijijini wameenda Dar es Salaam kufuata mahitaji, wamekuta Kariakoo imefungwa na wengine hawana nauli wanaanza tena kuomba kwetu Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mwongozo wako, ni nini Kauli ya Serikali kuhusiana na wafanyabiashara waliofunga maduka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, juzi kwenye mchango wako ulizungumzia habari hii na toka jana na leo Serikali na viongozi wa wafanyabiashara wanakutana na taarifa rasmi tutaipata baada ya kikao hicho kumalizika. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. YONA KURUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**na**

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Ndaisaba, jiandae Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Mheshimiwa Lucy Mayenga, mjiandae.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza siku ya leo. Kabla sijaendelea na mchango wangu, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama kipenzi cha Watanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama anayewajali Watanzania na wananchi wake. Mama huyu anaiweka Tanzania katika ramani nzuri ya kimataifa.

Sasa Taifa letu linatambulika ndani na nje ya nchi na kwenye mabara yote hapa duniani. Hakika Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Rais wa ukweli na mpenda Watanzania na mpenda maendeleo na sisi Wananchi wa Jimbo la Ngara tuko na mama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo hilo ninamshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuma taa za barabarani kwenye Jimbo la Ngara. Hivi ninavyozungumza mkandarasi yupo kazini kwa ajili ya kufunga taa za barabarani Ngara Mjini, Kanazi pamoja na kule Kabanga. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwajali Wananchi wa Jimbo la Ngara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielekeze mchango wangu kwanza kwenye eneo la sukari. Sukari ni chakula; Watanzania wa hali ya chini wanategemea sukari ili waweze kunywa chai. Suala la sukari ni suala la usalama wa nchi kwa sababu chakula ni suala la kiusalama ndani ya Taifa. Hatutakiwi kufanya mchezo na suala ambalo linagusa usalama wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sukari kwa muda mrefu tulikuwa tumeliacha kwenye mikono ya wafanyabiashara watano mpaka saba. Walikuwa wanakwenda kununua sukari kwenye soko la dunia huko, wanachukua sukari kwa bei ndogo wanaileta nchini wanaificha. Mtanzania wa kawaida (maskini) analima mahindi anavuna na kuyauza baada ya miezi mitatu, anauza kilo moja ya mahindi shilingi 300 lakini mfanyabiashara aliye-*monopolize* soko la sukari analeta sukari ndani ya siku 28 anauza kilo moja shilingi 10,000; hatuwezi kukubali kuona wananchi wetu wanateseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo amethibitisha uzalendo wake kwa kuwapigania Watanzania. Mheshimiwa Mama Samia naye hawezi kukubali kuona Mtanzania anauziwa sukari shilingi 10,000 (mwananchi wa kijijini), haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Waheshimiwa Wabunge tuliotumwa na wananchi maskini kuja hapa Bungeni kuwatetea

wananchi maskini, hatuwezi kukubali kuona mwananchi wa chini anauziwa kilo moja ya sukari shilingi 10,000. Ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania wote wenye mapenzi makubwa na mazuri na nchi yao kuunga mkono muswada ulioletwa hapa Bungeni na Mheshimiwa Hussein Bashe wa kuhakikisha tunakwenda kuiwezesha *NFRA* kuingiza sukari kwa sababu ya mambo mawili ya muhimu ninayotaka kuwaambia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, *motive* ya *NFRA* ni kwa ajili ya kupeleka huduma kwa wananchi. *Motive* ya *NFRA* ni *motive* ya Serikali lakini *motive* ya wafanyabiashara ni kupiga faida. Ndiyo maana wakati sisi Wabunge tunapambana kuona wananchi wetu wanapata huduma kwa bei nafuu, wafanyabiashara wenyewe wanapambana kuingiza sukari na kuificha ili kuwapiga wananchi wetu hela nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtanzania anayeuza kilo moja ya maharage shilingi 600, anayeuza kilo moja ya mahindi shilingi 300, hatuwezi kwenda kumuuzia sukari kwa shilingi 10,000. Jambo hilo haliwezekani kamwe asilani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, nitapitisha mwenyewe hapa; nitapiga kura ya kupitisha hiyo sheria. Tuipitishe sheria twenda tuiwezeshe *NFRA* iingize sukari kwa niaba ya Serikali na Mtanzania wa chini kijijini aende kupata sukari kwa bei nafuu. Ninasema tuko na mama, tunaunga mkono Serikali, tutahakikisha jambo hili linapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hoja hiyo ya sukari nataka nizungumze watu wa *TEMESA*. *TEMESA* wananikwaza sana. Hawa *TEMESA* wako chini ya Mheshimiwa Bashungwa kule Ujenzi. *TEMESA* nafikiri ni taasisi ambayo inatakiwa ifumuliwe yote. *TEMESA* tumewapa kazi ya kujenga Kivuko cha Kanyinya na Mayenzi mwaka 2021. Hivi tunavyozungumza *TEMESA* kila mwaka wanatupiga danadana, wakandarasi wamefikisha kila kitu pale lakini hawataki kukamilisha mchakato wa kushusha kivuko ili wananchi wa maeneo yale waanze kupata huduma. *TEMESA* wanatukwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuombe ikiwezekana hawa *TEMESA* wafanyiwe *auditing* tuangalie utendaji kazi wao; *efficiency* na *effectiveness* ya namna wanavyofanya kazi. Haiwezekani kivuko chenye thamani ya shilingi milioni 100 unakijenga kwa miaka minne mpaka mitano. *TEMESA* wameshindwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna Kivuko cha kwenda Rusumo, kile kivuko kimeharibika hii ni wiki ya tatu sasa wananchi hawapati huduma, *TEMESA* wame-*mute* hawafanyi chochote. Nakuomba hawa *TEMESA* wafuatiliwe ili wafanye kazi zao vizuri, Watanzania waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na eneo la barabara Wananchi wa Jimbo la Ngara tuna barabara tuliyoahidiwa muda mrefu sana kwa zaidi ya kipindi cha miaka 15 iliyopita na Serikali haijaanza ujenzi na hii ni barabara ya kutoka Murugarama kwenda Rulenge kwenda *Tembo Nickel*, kwenda Kumubuga mpaka Nyakahura. Barabara hii Serikali imeahidi kuitengeneza kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wameshafanyiwa tathmini lakini fidia haijatoka. Naomba nisimame hapa wananchi wamesubiri sana, kwa unyenyekevu mkubwa naiomba Serikali ihakikishe inakwenda kulipa fidia kwa sababu wananchi wamesubiri na wamechoka. Vilevile, mkandarasi ambaye ameshapatikana sasa awezeshwe apewe fedha aende aanze kujenga ile barabara kwa kiwango cha lami. Wananchi wangu wamesubiri sana na kuna Mheshimiwa Mbunge alisema mpaka apigane ngumi humu Bungeni ndipo mjue kwamba barabara inatakiwa kujengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mheshimiwa Mbunge alisema mpaka aje abebe Siwa hapo aondoke nao yeye nje ndipo mjue barabara inatakiwa kujengwa. Mimi nasema mpaka nipige sarakasi hapa mezani ndipo mjue wananchi wangu wanataka barabara au nilale hapa mezani ndipo mjue kwamba wananchi wangu wanataka barabara. Hizi barabara ambazo zilishahaidiwa na zikawekwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa muda mrefu zipewe kipaumbele na barabara ile

inakwenda kwenye eneo ambalo tunachimba madini ya *nickel*, kama barabara hii haitajengwa *nickel* inachelewa kuchimbwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kwa taarifa yenu ni kwamba wale waliyokuwa wanasubiria madini ya *nickel* wamegundua sasa hivi kuna kemikali wanazitoa kwenye chumvi huenda tukiendelea kuchelewa chelewa *nickel* yetu wakaiacha kwa sababu walichokuwa wanakitafuta kwenye *nickel* sasa hivi wameanza kukipata kwenye chumvi. Hivi tunavyozungumza Wachina waliyokuwa wanachimba madini ya *lithium* hapa Dodoma wametelekeza makarasha, watetelekeza magari wamekimbilia kununua chumvi na kwenda kufanya *extraction* ya kemikali walizokuwa wakizihitaji kwenye madini ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inafika mahali kama Taifa tunachelewa kufanya maamuzi tuwekeze kwenye ile barabara *nickel* ianze kuchimbwa, tuuze *nickel* fedha iende ikajenge barabara na mahali kwingine ambapo hakuna barabara za lami, kupanga ni kuchagua. Namwomba kaka yangu Mheshimiwa Bashugwa anisaidie hii barabara ianze kujengwa hakuna namna vinginevyo tunapoendelea kuchelewa kufanya maamuzi ndivyo hivyo ambavyo tutapitwa na fursa zitatupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ninaunga mkono hoja, ahsante sana Mungu akubariki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wageni waliokuwepo Bungeni wanafunzi 49 na walimu sita wa Shule ya Msingi ya Kilimani kutoka Arusha, karibuni sana.

Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Dkt. Kigwangwalla hayupo, badala yake atachangia Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru lakini nimshukuru sana Mwenyezi Mungu na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu

Lameck Nchemba na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Waheshimiwa Manaibu Mawaziri niwapongeze sana. Hongera sana kaka yangu Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo nina imani kazi hii itafanyika vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu leo utajikita kwenye sekta ya elimu na kwa kuwa natambua nchi nyingi zilizoendelea na zinazoendelea zimeweka kipaumbele suala la elimu na ndiyo maana leo zinafanya vizuri. Kupitia baadhi ya maeneo nimeona Nchi kama *Seychelles* ambao sisi tuliwasaidia kupata uhuru wao leo wamefikia *GDP* ya dola 21,000 takribani na 800 na sisi bado tupo kwenye 1,254 lakini waliwekeza sana kwenye elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametaja elimu kama mara 52 na imeonesha dhahiri kwamba msingi pekee ambao Serikali inautegemea sasa hivi ni kuwekeza kwenye elimu. Tumeona wanajenga *VETA* 54, tumeona watajenga shule za sekondari za ufundi 100 lakini amesema watajenga shule za amali 96, hili ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye maeneo mawili la kwanza ni mikopo ya elimu ya juu lakini la pili ni elimu ya ufundi na ufundi stadi. Bajeti ya Wizara ya Elimu ni takribani shilingi trilioni moja, ndani ya hiyo shilingi trilioni moja, shilingi bilioni 787.4 zimetengwa kwa ajili ya bodi ya elimu ya juu ya mikopo na hela inayobaki kama 39% ndiyo uendeshaji wa Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja hapa nataka tulitazame vizuri kama Serikali kama tunaweza kutenga leo shilingi bilioni 187 na kazi inafanyika vizuri kwa wenzetu wa Bodi ya Mikopo lakini tufanye *projection* ya miaka miwili ijayo, katika miaka miwili ijayo maoteo inawezekana kwenye Bodi tu peke yake ya Mikopo ya elimu ya juu tukawa tunawekeza zaidi ya trilioni moja. Serikali itakuwa inabeba mzigo mkubwa ambao tungeweza kutumia njia nyingine ili kuhakikisha kwamba mzigo huu usiwe wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini nataka kusema? Tunapaswa kuifanya Bodi ya Mikopo kuwa taasisi ambayo inajitegemea

*(operational independence)* ukiifanya kuwa *operational independence* maana yake kazi ya Serikali ni kuweka mtaji kwenye Bodi ya Mikopo ili iweze kujiendesha na unaiwekea tu *KPI* inatengeneza mpango wake ambao utapitiwa na *TR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu sasa unaendelea kusimamia eneo hili la Bodi ya Mikopo na kukopesha wanafunzi wetu itasaidia ku- *accommodate enrolment* ya wanafunzi ambao Serikali imewekeza kwa muda mrefu. Hivi tunavyozungumza bila kufanya hivyo mtoto leo anasoma bure kuanzia darasa la kwanza mpaka *form six,* kwa hiyo maana yake *enrolment* ya wanafunzi kwenda chuo kikuu itazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka na kwa fedha tunayoitenga Serikali inaweza ikashindwa ku-*accommodate* eneo hilo. Nataka kuishauri Serikali wakati ni sasa kuifanya Bodi ya Mikopo kuanza kuwa *operational independence*, hilo jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Serikali imefanya jambo jema sana, mwaka jana tumetenga hapa shilingi bilioni 48 kwa ajili ya vyuo vya elimu ya kati. Fedha hizi zilitengwa kwa makusudi kabisa kusaidia vijana wengi wanaosoma *diploma* kwenye eneo hili ili tuweze kupata vijana wenye ujuzi na vijana mahiri waweze kujiajiri na waweze kuajiriwa. Tulitenga shilingi bilioni 48 tukiwa tume-*target* kuwa *accommodate* wanafunzi 8,000 mpaka tunazungumza tumeweza kupata wanafunzi 2,500 tu ambao wanagharimu shilingi bilioni sita peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unajiuiza swali tatizo ni nini? Sisi tunataka kutoka huko kusema tumesikilizwa kwamba sasa wanafunzi wote wa elimu ya juu na wa elimu ya kati wameweza kupata mikopo. Mambo mawili makuu ambayo nimejaribu kuyatazama, moja inawezekana kabisa tumechelewa kutoa fedha hizi kwenye dirisha la udahili ambalo linaisha Septemba, sisi tunatoa fedha hizi baada ya Septemba maana yake wanafunzi wachache ndiyo wanaweza kujua kwamba sasa kuna mikopo ya elimu ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Serikali imeweka vipaumbele vyake kwamba tunahitaji walimu ambao watakwenda kufundisha kwenye shule zetu hizi za amali na shule

zetu hizi za ufundi kwa hiyo imeweka vipaumbele vyake. Kama umeweka vipaumbele vyako masomo ambayo unamtaka mtoto huyu asome kwa vipaumbele vya Serikali maana yake tunaacha na maeneo mengine vipaumbele vya kijamii, jamii inataka nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuishauri Serikali, kwanza iwahi kutoa fedha za mikopo na jamii, wanafunzi na wazazi waweze kujua mapema ili waweze kuomba fedha hizo. Pili, utakapokuwa umeshapata wanafunzi unaowataka kama Serikali kwenye vipaumbele vya masomo yako ruhusu na masomo mengine ili iweze kusaidia jamii uweke *option B*. Mfano tunahitaji kuwa na vijana wahandisi wa umeme, wahandisi wa *computer*, *civil engineering* na maeneo mengine ambayo hayapo kwenye vipaumbele vya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji *clinical medicine*, tunahitaji wafamasia, tunahitaji wauguzi na wakunga. Hawa wote tunaowazungumza hawapo kwenye vipaumbele vya Serikali. Serikali itoe *option b* ili kuwasaidia na wengine ambao wanahitaji kwenda huku na kuisaidia jamii eneo hili tunaweza ku-*accommodate* wanafunzi. Leo kwenye bajeti tunahitaji ku-*accommodate* wanafunzi 100,000 tunawapataje kwa sababu mazingira tuliyoyatengeneza tumetengeneza mazingira kwenye maeneo yetu sisi Serikali tunayoyataka *well and good* unaweza kuyapata lakini huwezi kupata 100,000. Sasa wanaobaki badala ya kubaki na hela toa *room* ya wengine kwenye masomo mfano niliyoyatoa ili waweze kuomba. Huo ulikuwa ni ushauri kwenye eneo hilo la bodi ya mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye eneo lingine la Wizara ya Elimu imebaki 39% ya uendeshaji wa Wizara ya Elimu katika 39% mimi nataka kuzungumzia kwenye eneo la elimu ya ufundi na ufundi stadi ambao Serikali imetenga asilimia mbili tu kama unatenga asilimia mbili kwenye *technical and vocational training* maana yake usitarajie ku-*achieve* hayo maendeleo tunayoyataka ya uchumi shindani, usitarajie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi? Unajenga *VETA* 64 vitahitaji walimu, vitahitaji vifaa unapataje kwa asilimia mbili? Unajenga shule za amali 96 vitahitaji walimu, vitahitaji vifaa

unapataje kwa asilimia mbili. Unajenga *technical secondary schools* 100 kuanzia mwakani unahitaji walimu, utataka vifaa utapataje kwa asilimia mbili. Nataka kuiomba Serikali kwa dhati kabisa umefika wakati kupitia bajeti hii ione umuhimu wa kuongeza fedha kwenye Wizara ya Elimu. Bila kuongeza fedha kwenye Wizara ya Elimu ili eneo ambalo sisi tunataka tupate vijana wenye ujuzi hatutaweza kuwapata vijana hawa matokeo yake tutakuwa tunahangaika kuweza kuwaajiri vijana wote ambao wanajisomea kwenye maeneo mengine wakati ujuzi hawana, kwa sababu huko tunapotaka waende mahudhui ambayo tumeyatengeneza hatuna walimu, hatuna vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuiomba Serikali ione umuhimu kwenye eneo hili ili ifanyie kazi. Mwaka jana tulitenga fedha kwenye Hospitali yangu ya Rufaa ya Singida ya Mkoa zaidi ya shilingi bilioni nne kwa isivyo bahati fedha hiyo haikuweza kufika na mradi wetu ule wa jengo ambalo unaendelea ambao ungeweza kufanya hospitali yetu ifanye kazi yake vizuri; fedha hiyo haikuweza kufika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 2.5 bado ninaona kuna tatizo kubwa sana hapa. Niwaombe wenzetu wa Wizara ya Afya tunalo jukumu kubwa katika Mkoa wa Singida ndiyo hospitali pekee tunaitegemea baada ya kuwa tumejenga vituo vya afya vya kutosha, tuna hospitali ya wilaya na wilaya zingine pia zina hospitali. Tunahitaji Hospitali yetu hii ya Mkoa iweze kupata fedha ili kukamilisha majengo ambayo yanatakiwa yakamilike bila kufanya hivyo watu wote wa Singida watakuwa wanakimbilia Dodoma sasa kama wanakuja Hospitali ya Benjamin Mkapa maana yake mzigo mkubwa utakuwa Hospitali ya Benjamin Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kusaidia eneo hili ni vizuri fedha hizi zikapelekwa kwa wakati ili tuweze kumalizia ujenzi wa Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Singida. Niwakumbushe pia tunayo hospitali ya manispaa ambayo tumepewa na sasa inatakiwa ikarabatiwe tuwe na jengo zuri la *OPD* na lenyewe linataka fedha. Nataka niwaombe Wizara ya Fedha pia niwaombe Wizara ya Afya waweze kuweka umuhimu; Singida ni

mji unaokua, mji ambao sasa hivi unahitaji kila *facility* ambayo tunataka iwasaidie wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza lugha ambayo kesho tukikamilisha miundombinu katika Manispaa yetu ya Singida tunataka kuja kuomba sasa Singida iwe Jiji baada ya Dodoma tuelekee Singida, hauwezi kuwa jiji kama miundombinu yote haijakarabatiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru sana na nikupongeze pia kwa kazi nzuri ambayo unaendelea nayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mayenga, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Protas.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Nianze kwa kuipongeza Wizara ya Fedha kwa bajeti nzuri ambayo wametuletea hapa lakini vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri mwema sana, mpambanaji na mzalendo. Vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Rais wetu ni Mama ambaye kwa kweli kabisa kabisa amekuwa akipambana kwa kiwango cha juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amekuwa akihangaika kuhakikisha kwamba sisi wananchi wake wa Tanzania tunakuwa katika maisha bora, vile vikwazo ambavyo vilikuwa vipo katika sekta mbalimbali amekuwa anapambana sana kuweza kuviweka sawa sawa. Mimi leo mchango wangu nina vitu viwili ambavyo ni vidogo lakini vitachukua muda kidogo. Jambo la kwanza labda nianze na ombi kabla ya kuelekea huko kwingine. Ombi langu nilikuwa naomba Wizara ya Maji itusaidie sana kutuletea maji kwenye Mkoa wetu wa Shinyanga kwenye maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mkoa wetu wa Shinyanga zipo wilaya ambazo zina nafuu kulingana na hali halisi ya hali ya hewa lakini zipo wilaya nyingine ambazo zina hali ngumu sana sana sana kutokana na *nature* yake kwa maana ya chini pia

hakuna maji. Mfano Wilaya kama ya Kishapu hakuna maji chini kwa hiyo hata ukichimba maji siyo rahisi kupata maji katika maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, inauma sana Mradi wa Ziwa Victoria unapita pale lakini baadhi ya maeneo yana maji na baadhi ya maeneo hayana maji. Nilikuwa naomba Wizara ya Maji ambayo najua inaongozwa na Mheshimiwa Waziri wetu mwema kipenzi chetu, mchapakazi Mheshimiwa Mheshimiwa Aweso najua kwamba hili lipo ndani ya uwezo wake. Kata kama za Busangwa, Seke Bugoro, Bubiki, Mondo na Mwasubi wanalalamika sana kwamba Mradi wa Ziwa Victoria unapita lakini sisi hatuna maji. Nilikuwa naomba sana sana sana Serikali iweze kuangalia suala la tatizo la maji kwenye Wilaya yetu ya Kishapu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la pili nizungumzie kuhusu suala zima la biashara ya sukari. Mwaka 2002 kwenda 2003 kuna jambo moja lilitokea hapa Tanzania ilikuwa ni kipindi cha Mheshimiwa Rais Mkapa. Serikali ya Japan iliamua kutoa msaada wa mchele kwa Serikali ya Tanzania lakini ilikuwa kuna *option* kwamba aidha mchukue mchele kama matumizi au mchukue mchele muubadilishe kupata pesa kwa ajili ya kufanya matumizi mengine ya miundombinu ya Serikalini na kadhalika kwa ajili ya wnanachi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais akasema kwamba huu mchele ni bora kulingana na changamoto tulizonazo matatizo mbalimbali madawati, kwenye sekta ya afya, sekta mbalimbali na kadhalika, huu mchele tuuze. Kilichofayika huku Serikalini huku, kilichofanyika ni kwamba wakasema sawa tunatangaza itakuwa ni *tender* huru kwa wananchi wote, wafanyabiashara wote wa nchi nzima. Kila mfanyabiashara mwenye uwezo ajitokeze na aweze kuomba *tender* ya kupata huu mchele kwa ajili ya kuuza sisi tunachohitaji ni pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake kilichotokea ni kampuni moja ambayo inajulikana iliamua kuandika *list* ya majina ya kampuni tano lakini ilikuwa inamaanisha ni mtu mmoja. Nataka kusema nini? Biashara ya *cartel*, *monopolization* ya biashara

katika nchi yetu ni suala ambalo limeanza muda mrefu sana lakini yote haya yanasababishwa na rushwa. Baadhi ya viongozi na baadhi ya watu wanakubali kupewa pesa kutuangamiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema namna hii tumekaa hapa juzi juzi tu kwenye suala zima la sukari, suala hili la sukari ni suala ambalo lilikuwa linahusu wananchi wetu, suala hili linahusu wananchi maskini. Bidhaa ya sukari kiuchumi inaitwa *inelastic* yaani kwamba ni kitu ambacho ni nadra sana kukikosa. Wananchi wetu sasa hivi wamekuwa wakilalamika maisha magumu, licha ya mambo yote haya na maboresho yote ambayo yamekuwa yakifanyika lakini bado kuna watu ambao wanaishi kwenye umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati watu wanakunywa chai, watu wanakunywa uji wanaweka sukari kuna wananchi vijijini kule hata miaka 10, miaka 20 iliyopita walikuwa wanakunywa uji kwa chumvi lakini leo hii mimi nasikitika sana suala hili (suala la matatizo ya sukari na *cartel* kwenye biashara ya sukari) limekuwepo miaka mingi sana kabla hata ya Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hajawepo madarakani. Mama Samia ndiyo Kiongozi pekee aliyesema mimi nataka kupambana na suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaniuma sana kuona kwamba Mheshimiwa Rais ana moyo wa kupambana halafu kuna watu Serikalini wanamshika gauni hatuwezi kukubali. Hatuwezi kukubali kwa sababu kama hivi vipesa vidogo vidogo watu mnapewa, peweni huko chukueni na pokeeni lakini sisi tunasema hatuwezi kukubali. Kwenye hili naomba niseme nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwenye hili amefanya kazi kubwa na ameonesha uzalendo usiokuwa na mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani wafanyabiashara wachache yaani wao ndiyo waishikilie nchi *there is no way in the world* wafanyabiashara waka-*regulate* Serikali, Serikali ndiyo ina-*regulate* wafanyabiashara. Sasa watu wanakuja wanakaa Serikali ni moja. Mimi nimekuwa nikisema mara nyingi kwamba Serikali zungumzeni lugha moja. Nyinyi Waheshimiwa Mawaziri ambao

mmeteuliwa huko zungumzeni lugha moja, Mheshimiwa Rais anapowateua anawaamini zungumzeni lugha moja. Nyinyi msipozungumza lugha moja huku chini, huku nyuma mnatutesa sisi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani suala linakaa linazungumziwa biashara ya sukari, matatizo ya sukari, changamoto ya sukari halafu kuna Mheshimiwa Waziri anakuja kumsikia anataka akunong'oneze kwamba unajua hili suala, unajua limekaa hivi na hivi na hivi. Wewe kama umenunuliwa, tutashughulika na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inauma sana, wananchi wetu hapa kipindi hiki isingekuwa hatua za Serikali, isingekuwa hatua za Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba tunapata *alternative* ya mfanyabiashara mwingine kuingiza sukari hali ingekuwa mbaya sana. Ilifika kipindi, vibali vimetolewa, makusudi kabisa wanaamua kwamba sisi hatuendi kuchukua kibali. Kibali kinatangazwa Novemba, Novemba inafika, Disemba inafika, Januari inafika, yaani mtu anaamua tu kwamba mimi siendi kuchukua. Wakikaa huko wanaji-*organise* mwisho wanasema hebu anza wewe kampuni fulani, hebu nenda wewe. Wanakwenda huko, wakishakwenda huko wanakaa, huyu anachukua, kibali unapewa cha tani 10,000 ambacho thamani yake ni sawasawa na dola bilioni nane. Kiwanda chako au kampuni yako ina uwezo wa kuleta, unaleta tani 2,300 mnatengeneza *scarcity* makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani, hatuwezi kukubali hii nchi iendeshwe na watu wachache kwa sababu ya pesa zao, kwa sababu ya utajiri wao. Roho inauma sana, anayeumia ni mwananchi huku lakini watu Serikalini ukiwauliza, watu Serikalini ukiwahoji, ukiongea na mtu hivi Mheshimiwa Kiongozi, hivi hili suala la sukari limekaaje, unajua hili suala linashughulikiwa, yaani anakupa majibu mepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwenye hili, mimi ninampongeza sana Waziri wetu wa Kilimo kwa sababu asingeingilia suala hili chini ya uongozi wa kipenzi chetu Rais wetu hali ingekuwa mbaya sana. Mimi huwa nasema, napenda sana

*style* ya Rais wetu Mama Samia, haya mambo ya kukaa na wafanyabiashara; kwanza naomba kusema, ziara za viongozi, naongea *with due respect*, ziara za Mheshimiwa Rais siku hizi amekuwa akiwabeba wafanyabiashara kwa mapenzi mema anaposafiri nje anakwenda nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo cha kwanza cha hao wafanyabiashara kwenda huko kiwe ni uzalendo. Haiwezekani ukawa wewe umekaa, kampuni zako huku unafanya biashara ya sukari unatuletea cartel mnaji-*organize* huko na rushwa zenu mnatafuta watu kwa ajili ya kuwahonga, mnawakosa wengine halafu unamaliza pale tunakuona kwenye ziara ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inauma sana yaani umekaa unaangalia *TV* unaona na mfanyabiashara fulani yule halafu huku ndiye yeye ambaye anashughulika kuhakikisha kwamba sukari isipatikane. Kigezo cha kwanza cha wafanyabiashara kwenda kwenye ziara za Mheshimiwa Rais kiwe ni uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na nina uhakika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, Mayenga kengele ya pili.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ujumbe umefika vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, ajiandae Mheshimiwa Protas, ajiandae Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi, lakini naomba nishukuru kwa kupata fursa ya kuchangia Bajeti ya 2024/2025 ndiyo bajeti ambayo Waheshimiwa Wabunge tutaisimamia vizuri, lakini bajeti tukayoipitisha mwakani inawezekana tukaja kuikuta au tusiikute. Nilitaka niwakumbushe kwamba mwakani mkipitisha bajeti kama hii mwaka unaofuata tutakuwa wachache humu wengine

tutaangalia wenzetu kupitia kioo. Kwa hiyo, hii bajeti ni muhimu sana kuisimamia tukatende wema kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu ningepata nafasi ya kusema mafanikio na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa Jimbo la Tarime Vijijini nitachukua muda mwingi. Itoshe kusema namshukuru Mheshimiwa Rais kwa yale ambayo amewatendea watu wa Tarime Vijijini. Ninapozungumza wanafahamu maeneo ambayo amepeleka shule, amepeleka maji, amepeleka barabara, amejenga zahanati na watu wanaendelea kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wako Mawaziri ambao wamefanya kazi nzuri sana kwa miradi yao katika jimbo langu. Siwezi kuwataja wote lakini itoshe kusema wanajijua ambao wameenda jimboni kwangu wametoa mambo mzuri na wananchi wangu wametulia katika eneo lile. Hata leo ninaposema Mkoa wa Mara umetulia, Mkuu wa Mkoa wa Mara Kanali Mtanda anafanya kazi nzuri na *DC* imebaki sehemu moja tu juzi mliona, pale kuna tatizo naomba lifanyiwe kazi. Juzi mliona pale kuna tatizo, narudia tena kule kuna shida kubwa ile ifanyiwe kazi, vinginevyo moto unavuka na kule kwetu utachoma na kwa wa Tarime tunajuana vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Mawaziri wawili, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba wakati mimi nakuwa Rais wa Chuo alikuwa *Campaign Manager* wangu, lakini pia Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ni mwanafunzi wangu kisiasa lakini mimi pia kitaaluma amenifundisha *Adolescence* pale Mlimani. Kwa hiyo, ndio Maprofesa wote na ni wajukuu wangu, lakini naomba wasikilize kuna maeneo yana changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, eneo la TAMISEMI-*TARURA*, mahitaji ya fedha ambayo yalipaswa kwenda kwa dharura wanadaiwa shilingi bilioni 226 mpaka sasa. Kulikuwa na bajeti ya nyongeza shilingi bilioni 350 hazikwenda katika eneo hilo. Tungetamani kuona namna fedha inaenda kwenye maeneo ya dharura kurekebisha miundombinu ya *TARURA*, lakini pia kuongeza bajeti katika miundombinu ambayo Wabunge tuliahidi katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna changamoto kwenye afya na elimu, fedha zimesomeka kwenye mfumo lakini miradi pia haitekelezeki. Kwangu Tarime naona kuna hiyo shida sijui wenzangu hali ikoje katika maeneo yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi ya maji kule Tarime tuna 30% ya vijiji mbalimbali ambavyo havina maji lakini wanadaiwa fedha (madeni). Mkoa wa Mara katika Idara ya Maji, RUWASA zaidi ya shilingi bilioni 5.3, wanadaiwa hiyo hela ipelekwe ili miradi ya maji iweze kukamilika katika maeneo yale. Miradi mingine pia kuna changamoto hiyo. Tuna Mradi wa Ziwa Victoria ambao mimi nautegemea sana katika jimbo langu, fedha ni pungufu katika eneo hilo hazijatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara ya Ujenzi, Barabara ya Zanzate - Nata, wanadaiwa deni la shilingi bilioni 6.049, Mugabiri - Nyamongo wanadaiwa shilingi bilioni 6.865, Uwanja wa Ndege - Musoma wanadaiwa shilingi bilioni 3.471, Barabara ya Tarime – Mugabiri - Nyamongo - Mugumu wanadaiwa shilingi bilioni 7.991. Jumla ya deni katika Wizara ya Ujenzi wanadaiwa shilingi bilioni 24.776, hizi zinatakiwa ili Mkoa wa Mara tupate huduma katika maeneo ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu, Chuo cha *VETA* Nyamongo kimesimama kabisa hakuna ujenzi, maana yake hakuna fedha. Wizara ya Kilimo, ujenzi wa soko la mazao ya kimataifa pale mpakani Sirari eneo la Ng'ereng'ere shilingi bilioni 1.6 hazijaenda na hili soko halijaanza kujengwa, lakini kwenye Madini, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri juzi alikuja kule Nyamongo akatoa taarifa njema kwa vijana kwamba wametoa maeneo kwa wachimbaji wadogo. Vilevile, tumeomba tupewe mtambo wa uchimbaji kwa Tarime tu kwa sababu ukienda Tarime Mjini, Vijijini na maeneo mengine vijana wanachimba ili waweze kupata usaidizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda mawasiliano, ukanda wa kutoka Rorya, nenda Sirari, Mtemurabu kule, Nyasincha mpaka Nyanungu hakuna Redio Tanzania, hakuna minara ya simu. Watu wangu wanapata Mawasiliano ya habari za Kenya kama mnavyoziona kwenye mitandao na ndiyo maana wakati

mwingine siasa yetu pia imefanana fanana kwa sababu watu wetu hawaoni mambo mazuri ya Watanzania hata hotuba za Mheshimiwa Rais mpaka upeleke kwenye *smartphone* na wachache hawana. Hapa fedha inatakiwa ili tupate huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na changamoto ya Mfumo unaitwa *NeST,* huu mfumo ni mpya umetolewa ghafla nchi nzima, watu wanahangaika nao wataalamu hawajafundishwa vya kutosha. Kwa hiyo, kuna changamoto, lakini nilishangaa Katibu Mkuu alitoa mwongozo kwamba angalau kwa ngazi ya chini kwenye halmashauri, kata na vijiji waendelee na utaratibu wa kawaida wakati wanaendelea kuwa *familiar* na mfumo huu. Akaandika barua kwa wakurugenzi akawapa, Mtendaji Mkuu wa *PPRA* naye akaandika barua akafuta barua ya Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashangaa, Katibu Mkuu wa TAMISEMI anaandika barua ya kutoa maagizo ili miradi isikwame kule kwa sababu fedha zipo, Mtendaji Mkuu wa Idara anafuta ile barua. Sasa sielewi, Serikali mtanisaidia sijui labda mambo yamebadilika lakini kwamba inakuwakuaje imeleta mkanganyiko. Vilevile, malipo yamechelewa sana, wazabuni hawalipwi, makandarasi hawalipwi. Mheshimiwa Waziri, hili pia ni jambo la kufanyia kazi. Ukisema fedha ipo, inaonekana kule, watu wafanye kazi watu wetu waweze kupata huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, matumizi mabaya ya Serikali; niseme tu kwamba katika eneo ambalo Serikali inapaswa kujikita; tunaona kwenye mitandao huwa haipendezi, hata haya mabishano ambayo Mheshimiwa Lucy Mayenga amemaliza kuchangia ni maneno ambayo kwa kweli nilitaka niwashauri Waheshimiwa Wabunge. Kama mnaona kuna wizi kwa sababu imeandikwa kwenye mitandao na wananchi nao wanasoma, kwamba wao wanashida ya maendeleo wanachangishwa fedha kwenye miradi ya maendeleo, wanalipa kodi halafu wanaona viongozi ambao wamepewa heshima na imani na Mheshimiwa Rais kwenye nafasi mbalimbali wanaonekana wanafuja mali na hakuna mtu wa kuweza kuwakemea, jambo hili siyo ssawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nataka niwashauri kama Bunge, habari ya sukari mnatuchanganya sana akili, mnapozungumza habari ya rushwa, mimi sijaenda kwenye viwanda vinavyozalisha wala sijaenda nje, jambo hili ni la Watanzania na ni la Wabunge; kama kuna Waziri amekula rushwa au Mbunge amekula rushwa hao watu watajwe hapa washughulikiwe, tusichafuane humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo namwomba Mheshimiwa Rais na wewe Mheshimiwa Spika, mlisimamie tujue ukweli ni upi ili tuweze kuliamua. Mambo ya kuanza kutambiana hapa, mmetunisha misuli, haiwezekani. Hili ni Bunge la Watanzania tena liko *live*, mnataja habari ya rushwa kwamba kuna Waziri ameleta mipango humu ndani kazi yake amepiga *deal.* Kuna Waziri mwenzake ndani ya Serikali anamuhujumu, hawa wanamuhujumu Mheshimiwa Rais, likitokea la kutokea sisi wote humu ndani tutahukumiwa, hatuwezi kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jambo la sukari lifanyiwe kazi. Tuitwe kama ni semina iwe ni *open discussion* tuelezwe faida ya kuleta sukari kutoka nje ni ipi bila chenga chenga na faida ya kuimarisha viwanda vya ndani ni ipi, tuamue kama Watanzania, tusiamuliwe na watu kulishana matango pori hapa, siyo sawasawa. Hili ni Bunge la Watanzania, jambo muhimu sana hili lisifanyiwe kampeni, kama kuna mtu ameenda kwenye *corridor* atajwe na hao hawafai kuendelea kuwa Wabunge wa Bunge hili kwa sababu hawana uzalendo wowote ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa habari hapa ya ushoga, sasa nataka nirudi kwenye hii hoja vizuri. Nataka nioneshe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba tunayo shida na tuna tatizo la kitaifa. Habari ya ushoga, usagaji, ubahasha na ulawiti ni kubwa, jambo hili limeingizwa kwenye *Twitter(X)* kwamba kutakuwa na maudhui ya ushoga na ngono. Nampongeza Mwenyekiti wa Vijana, Kawaida ametoa kauli lakini sijaona kauli ya Serikali. Tunajua kuna vitu vingi kwenye *Twitter* lakini ni vizuri kama Serikali kama Taifa tukubaliane mambo gani tuoneshe na mambo gani tusioneshe. Haya mambo yametolewa na yanaendelea na hakuna tamko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuoneshe, tarehe 31 Mei kuna yule Meneja wa Lamada ambaye alionekana kwamba ameteuliwa kuwa rais wa mashoga hapa Tanzania alifanyiwa sherehe, halafu tunaambiwa kwamba amekimbia. Hivi amepita katika mpaka upi? Hakuwa na *passport*, wakati wanafanya sherehe hakuna viongozi wa Serikali katika eneo hilo? Huu ni usanii. Wizara ya Mambo ya Ndani ilikuwa wapi katika jambo hili? Yaani mtu ameteuliwa kuwa rais wa mashoga, yaani nchi hii tuna Rais wa Nchi halafu tuna rais wa mashoga, *shame on us* haiwezekani. Haya ni mambo ambayo hayafurahishi, lazima yafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwaambie Waheshimiwa Wabunge hiyo haitoshi, yapo mambo ya kihuni mengi, hii Kampuni ya Athumani Kapuya ambayo tarehe 3 Juni ilikamatwa, nimpongeze Mheshimiwa *RC* Paul Chacha, hiyo ndio tabia ya Wakurya bwana kwamba unatakiwa kuwa na msimamo. Ameshughulika na wale watu lakini maswali yafuatayo yajibiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ile Kampuni Makao Makuu ni Dar es Salaam, Dar es Salaam wanasema nini? Kule kwenye eneo lile alikuwa na vitabu zaidi ya elfu nane, vitabu vile vina maudhui ya ngono na ushoga lakini vimeteketezwa. Sasa mpaka leo hivyo vingine Waziri wa Elimu anasema…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, ahsante, kengele ya pili.

*(Hapa Mhe. Mwita M. Waitara aliendelea kuzungumza bila ya kutumia kipaza sauti)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, unachukua nafasi za watu wengine. Unachukua muda wa Wabunge wengine, muda wako umekwisha, unga mkono, mengine andika kwa Waziri.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Protas, jiandae Mheshimiwa Mtaturu, jiandae Mheshimiwa Latifa Juwakali, jiandae Mheshimiwa Dkt. Kabati na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuwa miongoni mwa wachangiaji kwenye Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza nianze kuipongeza Serikali kwa namna tangu 2020, 2021, 2022, 2023 na leo tupo 2024, imekuwa ikileta Bajeti za Serikali zenye mikakati madhubuti kwa nia ya kuwaletea maendelea wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine leo tunapitisha bajeti ambayo itakwenda kutibu wananchi ambao tuliwaahidi kuwaletea maendeleo mbalimbali katika maeneo yetu. Mimi nimwombe Mheshimiwa Waziri katika bajeti hii ninaamini tunakwenda mwishoni mwa miaka mitano ya Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi, kuna mambo ambayo niliyaongelea kwenye Wizara za Kisekta lakini sasa niongelee kwenye suala hili kwenye Wizara ya Fedha ambayo ndiyo yenye jukumu la kuleta fedha ili zikalete maendeleo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo nataka nisisitize, Mheshimiwa Waziri, tuna mradi mkubwa wa *SGR* ambao umepita katika Jimbo langu la Igalula. Mheshimiwa Waziri, kule kuna watu mmeshawawekea X kwenye nyumba zao, mmefukua makaburi yao hasa wa Kata ya Igalula, Goweko na maeneo mengine hamjawalipa fedha zao. Sasa mimi nikuombe tukimaliza bajeti hii kesho, kuanzia tarehe moja anza kuwalipa kwanza watu mliofukua makaburi yao ili sasa ule uchungu mliowarudishia waweze kuona Serikali yao imewajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nina Mradi wa Ziwa Victoria katika maeneo ya Kigwa, Goweko, Igalula na Nsololo, mradi huu una changamoto nyingi lakini changamoto kubwa mojawapo ni upatikanaji wa fedha kwa wakati. Sasa mimi niombe, nimepiga kelele kuanzia 2021/2022 mnaniletea hela kidogo kidogo, peleka fedha ukamalize mradi huu kabla ya 2025 tunapoenda kuwaambia wananchi tumetekeleza lipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni barabara, nadhani kila Mheshimiwa Mbunge anasema eneo lake barabara nyingi zimeharibiika, hasa mimi Barabara ya Ndevelwa - Igalula-Goweko imekufa kabisa wananchi wanapata shida. Mheshimiwa Waziri nikuombe kwenye bajeti hii najua fedha za barabara zipo achana na kwingine kote anzia kwangu peleka fedha ili wananchi wapate barabara waanze kutengeneza uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali, kiongozi mzuri ni yule ambaye linapotokea tatizo anachukua hatua kwa haraka kutatua tatizo. Siyo kiongozi linapotokea tatizo naye anakuwa sehemu ya kulalamika juu ya tatizo hilo. Mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchukua hatua madhubuti ya kutatua changamoto ya upatikanaji wa sukari katika nchi yetu. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri Bashe kwa kuthubutu na kuona umuhimu wa kuwasaidia Watanzania kwenye upatikanaji wa sukari katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la sukari, hapa ndugu zangu Wabunge mimi niombe, sisi Wabunge tumekuwa watetezi wa wananchi, ilikuja hapa hoja ya kupanda kwa bei ya mafuta, Wabunge wote tuliweka mikono chini tukaweka hoja ya dharura tukaanza kuilalamikia Serikali wakati tukijua kabisa nchi yetu hatuna kisima hata kimoja cha kuchimba mafuta. Ila tulilalamika kwamba kwa nini bei ya mafuta imepanda ghafla na wananchi wetu kule gharama zimeongezeka? Lakini Serikali ilichukua hatua ya kuweza kupunguza ukali wa bei ya mafuta, wakaweka ruzuku kwenye mafuta na ukali wa bei ya mafuta ukashuka moja kwa moja kwa wananchi. Hapo hapo Serikali iliona hii ni dharura ikaamua kwenda kule ile fedha ambayo tuliipeleka kule ya ruzuku haikuwemo hata kwenye bajeti, kwa sababu ya udharura wake tuliipeleka kwenye kuokoa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zozote ambazo tunazitengeneza humu Bungeni zinatengenezwa kutokana na mazingira yaliyotokea kwa wakati huo. Kama kuna sheria mbayo

inatengenezwa haina mwelekeo kwa wananchi ni lazima tuivunje.

Mheshimiwa Naibu Spika, turudi kwenye suala la sukari; hili jambo siyo la kubeza, kwenye tasnia ya sukari tumeiachia soko huria. Leo hii Serikali haijui uzalishaji wa sukari kwenye viwanda vyetu na yenyewe Serikali kwanza inabidi tuilaumu kwenye hili. Leo kwenye sekta ya mafuta wanaofanya biashara ya mafuta ambayo inaingiza uchumi mkubwa kwa wananchi wetu, leo Serikali ina mkono wa moja kwa moja licha ya sekta binafsi kufanya biashara ya mafuta. Leo *EWURA* kila mwezi inapanga bei elekezi kwenye sekta ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe Serikali, kwa sheria hii ambayo tunakwenda kuipitisha, kwa sheria hii ambayo Serikali imeileta ya kuipa Serikali *power* ya kujua kinachoendelea kwenye tasnia ya sukari. Waheshimiwa Wabunge, mimi naomba tuunge mkono na mapendekezo yetu yawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu uwezo wa viwanda vyetu uzalishaji wake kwa mwaka ni kiasi gani, sasa kwa nini tuwe tunasubiri mpaka tumefika kwenye *penalty box* ndiyo tunaanza kutoa vibali vya kwenda kuagiza sukari? Kwa nini tunakuwa tunasubiri upungufu wa sukari ndiyo tutoe vibali?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niiombe Serikali, Sheria hii imekuja hapa ikiomba Bunge hili lipitishe ya kwamba *NFRA* wapewe *mandate* ya kuagiza sukari *sugar gap,* ule upungufu tu lakini jukumu bila kuathiri uzalishaji ambao unazalishwa ndani ya viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine leo Bodi ya Sukari inafanya kazi gani? Inasimamia kitu ambacho haikijui. Haijui uzalishaji ni shilingi ngapi, wakulima wanaenda kununuliwa miwa kwa kiasi gani, vilevile wamekaa tu pale hawaelewi kinachoendelea, lakini sheria hii itataka wale wazalishaji wa viwanda kule kwenye sukari, viweze kupeleka gharama halisi ili tuweze kutoa bei elekezi ya sukari iuzweje kwenye Mikoa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwatolee mfano katika jimbo langu la Igalula, sukari ilifika mpaka 11,000. Simu wananchi walikuwa wanalalamika sana, sasa sisi tunakwenda kupunguza bei kule watu wanaanza kutuvuta shati. Mimi nawaomba wananchi watuangalie na sisi tunaokuja humu inaweza kuwa tuna matatizo mengi kushinda hata haya.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana kwenye masuala ambayo tunatakiwa kuisaidia nchi, tuende kwenye kuisaidia nchi. Kwenye masuala ya kisiasa tuende kwenye siasa lakini kwenye masuala ya maslahi ya nchi ni lazima tuelekeze nguvu zaidi ya kuwatetea Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kuna mambo ambayo Serikali inatakiwa iangalie kwa umakini. Kuna mambo ambayo haitakiwi kuachiwa sekta binafsi bila kuingiliwa. Kwa mfano, sekta ya mafuta lazima Serikali iingie, sekta ya nishati ya umeme Serikali lazima iangalie. Tukiruhusu sekta binafsi wakafanya yao kuna siku Taifa hili litaingia kwenye giza, mtamuuliza nani? Vilevile, mitandao ya simu ndiyo maana tukasema Mkongo wa Taifa urudi Serikalini kwa sababu ulikuwa unamilikiwa na sekta binafsi. Ilipozimwa tu *internet* hapa siku mbili watu walianza kupiga kelele *internet* haipatikani hii ni kwa sababu walikuwa wanamiliki makampuni binafsi. Ilivyoingia Serikali iliona namna gani ya kufanya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Mtaturu, jiandae Mheshimiwa Latifa Juakali, Mheshimiwa Kabati na Mheshimiwa Kigwangala, jiandaeni.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja mbili ambazo ziko mbele yetu zilizowasilishwa na Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha Ndugu yangu Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Waziri wa Mipango na Uwekezaji Ndugu yangu Profesa Kitila Mkumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, leo tunajadili Bajeti Kuu ambayo ameipatia baraka na bajeti hii itakapotoka ndiyo itakwenda kuhudumia bajeti za Wizara za Kisekta ambazo tumepitisha katika kipindi kilichopita. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais kwa maono yake ameonesha wazi anataka kuisogeza nchi mbele zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeangalia katika taarifa zilizosomwa na Mawaziri, zimeonesha wazi Taifa limepiga hatua kubwa, kwenye hili tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na sisi Wabunge tumuunge mkono kwa kupitisha bajeti hii ambayo inakwenda kujibu matatizo ya wananchi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, shukrani na pongezi zimetolewa. Nikianza kueleza kwenye eno langu la Jimbo la Singida Mashariki namna ambavyo Serikali imetuletea fedha nyingi tutakesha kwa kusikiliza jambo hilo, itoshe tu kwa kusema tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutuletea miradi mingi ya maendeleo na tunaamini katika bajeti hii tutaletewa fedha nyingine za kuleta maendeleo katika Jimbo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia taarifa ya hali ya uchumi katika mwaka 2023 na mpango wa maendeleo wa mwaka 2024/2025 imeeleza kwamba ukuaji wa uchumi wa Pato la Taifa ni trilioni 148.3 toka trilioni 141 ya mwaka uliopita sawa na ongezeko la asilimia 45.1 kutoka asilimia 4.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini msingi wa maelezo yangu? Ninachotaka kusema ni kwamba jitihada zilizowekwa na Serikali ni kubwa katika sekta ya uzalishaji. Sekta ya uzalishaji ndiyo muhimili wa mapato haya na ndiyo muhimili wa kuuza mazao nje ya nchi, kuweza kufanya biashara za madini na utalii. Kama ambavyo tumeeleza utalii umetoka katika ile hatua ya nyuma zaidi na sasa hivi utalii umeongezeka sana, hii inatokana na jitihada za Mheshimiwa Rais kuweza hata kucheza ile filamu ya *Royal Tour* imeongeza watalii wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Arusha hakuna nafasi hata ya kukanyaga, leo biashara imekua na hata wanaouza

mbogamboga pale Arusha wanapata fedha na hiyo ndiyo namna pekee ambayo Serikali inaweza kusaidia wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka niseme kwamba nitaeleza maeneo manne ambayo nadhani naweza nikachangia mchango wangu ili tuongeze pato hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni sekta ya biashara. Sekta ya biashara imetajwa kwenye Ilani ya Uchaguzi na kwa msisitizo mkubwa sana. Ilani ya Uchaguzi imesema wazi kwamba, sekta ya biashara kwenye ile Ibara ya 49 ukurasa wa 60 imeeleza kwamba: Chama cha Mapinduzi kinatambua kuwa biashara ni chanzo cha mapato na hivyo kitaendelea kuelekeza Serikali kuimarisha biashara ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha miaka mitano Chama kitahakikisha mchango wa sekta ya biashara kwenye Pato la Taifa unaendelea kuimarika".

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kukumbusha kwenye eneo hili kwamba, sekta ya biashara ikisimamiwa vizuri inaweza kuongeza mapato ya nchi. Pia, fedha ambazo leo tuna changamoto kwenye miradi tukiweza kuwekeza vizuri tutaweza kufanya miradi yetu vizuri. Kwa hiyo, leo Wabunge wanaeleza habari ya barabara, maji, shule na vitu kama hivyo, vikiwekezwa vizuri kwenye biashara Taifa litapata maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nieleze leo biashara katika nchi hii kuna urasimu mkubwa, leo mtu akitaka kuwekeza kwenye biashara yoyote ni lazima aache kazi nyingine zote ashughulike na kuanzisha biashara. Kama lengo letu ni kutaka kukuza biashara, tuondoe urasimu katika nchi, sekta kwa maana ya taasisi zetu zinazosimamia utoaji wa vibali vya kuweza kuanzisha biashara zitazamwe upya, ninaamini tukitazama kwenye eno hilo itasaidia uwekezaji na kuvutia.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Rais analeta wawekezaji katika nchi lakini mtu ili aweze kuanzisha kampuni inamchukua mwezi mzima, hivi unategemea utapata wapi kodi wakati mtu hajaanzisha biashara bado? Hili nadhani liangaliwe vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nikupe mfano na nataka niseme kwenye eno hili, leo mtu akitaka kujenga hoteli ya ghorofa hata ikianza ghorofa moja, mbili anaanza kupewa kikwazo kwamba kuna watu wa Zimamoto nao wanataka fedha kwa ajili ya kupitisha hiyo ramani, tunataka kwenda wapi? huyu mtu atakuja kulipa baadaye *service levy*, kodi na *VAT* kwa nini umpe kikwazo leo unamwambia alipe 1,700,000 ili ramani yake ipitishwe, maana yake ni kwamba hii ni changamoto na wengi wao wamejitoa kwenye biashara kwa sababu wameona hatufanyi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sheria nyingi zimeanzishwa unasema hii imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wizara labda ya Viwanda, hii labda ni Wizara ya Mambo ya Ndani, hii ni Wizara nyingine, maana yake nini nataka kusema? Ni kwamba unampa kikwazo mfanyabiashara huyu aingie ofisi hii na hii wakati mwisho wa siku anakwenda kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana tukitaka kwenda vizuri na mpango huu tuliousema hapa, tuweze kuondoa urasimu katika eneo hili la biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni suala la miundombinu. Miundombinu ni uti wa mgongo wa biashara za nchi hii, leo tunaongelea habari ya barabara za usafirishaji, tunaongelea habari ya bandari, ndege zetu na usafirishaji wa bidhaa zetu mbalimbali. Tunapokuwa na usafirishaji wa bei nafuu utasaidia kupunguza ushuru na bidhaa mbalimbali zinazofanywa katika nchi yetu. kwa hiyo, ombi langu ni kwamba mpango wa kujenga barabara zetu uendelee kuongezewa nguvu ili kuhakikisha kwamba nchi inafunguka zaidi na tunakwenda mbele tulipopalenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo ninaipongeza Serikali kwa kuwaruhusu watu wa bandari kuchukua kodi ya *wharfage* ambayo haikuwepo. Nimeona hapa kwenye taarifa kwamba wanakwenda kutoa azimio na watu wa bandari wanakuwa wanapata ile *wharfage* wao wenyewe, hii itasaidia kuondoa urasimu ambao ulikuwepo na kuwafanya wawe na nguvu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilitaka niombe kwenye eneo hili la barabara hatujafanya vizuri kwenye zile barabara za *EPC+F*. Tulisainiwa mkataba toka mwaka jana mpaka tunavyoongea leo mwaka unaisha mwezi wa Sita mwingine barabara hazijaanza. Barabara zenye urefu wa kilometa 2,035 leo barabara za kule kwenye maeneo mbalimbali ya kufungua ikiwemo ile barabara ya kutoka Singida – Kwa Mtoro – Kiberashi Tanga barabara kilometa 460 haijaanza kufanyakazi, wale wananchi tunawambia nini? Wanapokuja hapa ku-*wind up* watuambie wameweza kufanya nini kutatua tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye barabara tunaona kuna fedha zimeongezwa, tuhakikishe tu kwamba barabara zilizofumuliwa na madaraja yajengwe ili kuongeza usafirishaji wa wananchi na bidhaa zao ili kuweza kuongeza biashara katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa ardhi. Ardhi ni msingi katika ujenzi wa Taifa letu. Katika nchi hii kuna migogoro mingi ya ardhi katika maeneo mbalimbali, leo hii watu wakitaka kutumia ardhi unaambiwa hii ardhi ni ya mtu fulani amechukua eka zaidi ya 1,000 au zaidi ya 2,000 mtu mmoja peke yake. Watu wanaotaka kuwekeza katika nchi yetu wanakosa maeneo ya kuwekeza. Hatujapima ardhi yetu, kupima ardhi na kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi ndiyo utaondoa migogoro katika nchi yetu. Kwa hiyo, niombe sana bajeti hii ikajibu changamoto ambazo zipo za wakulima na wafugaji katika maeneo yetu ili kuongeza uwezo wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni Kilimo. Kilimo ndicho kinachoajiri wananchi zaidi ya asilimia 65. Pia, ni uti wa mgongo wa Taifa kama ambavyo unasikia. Ibara ya 35 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 33, inasema kilimo ndicho kitaendelea kuwa ndiyo muhimili wa nchi yetu, ninaomba sana, jitihada zinazofanyika tunaziona, uwekezaji wa mbolea, ruzuku tumeona kwenye mbegu na utaalam mbalimbali, tuendelee kuongeza uwezo wa wale watumishi wa kilimo ambao kwenye maeneo yetu wakiwemo Maafisa Ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni suala la uzalishaji wa sukari. Eneo hili ni tete ni lazima Serikali iingilie ili iweze kusimamia sukari katika nchi yetu. Hatuwezi kuacha soko huria kwa jambo ambalo ni muhimu kwa wananchi. Hiki kilicholetwa hapa tupitishe ili *NFRA* waweze kununua sukari kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Watanzania. Leo hatuwezi kuwa watu wanazunguka wanaitumia sukari kuwa siasa, hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali makini, kiongozi makini anaposikia changamoto atafute njia ya kutatua. Mojawapo ya njia ya kutatua ni hii ambayo tunayo sasa hivi ya kuweza ku-*monopoly* soko la sukari ili kuwafanya Watanzania wawe salama. Sukari leo ndiyo kila kitu, ndiyo Maisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge tupitishe jambo hili…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili hiyo.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kuunga Mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Latifa Juwakali, Mheshimiwa Kabati, Mheshimiwa Kigwangala.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, kwa hakika sisi vijana wa Tanzania anaendelea kututia moyo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tumtie moyo Mheshimiwa Rais na tunamwambia kwamba vijana wa Tanzania hatuko nyuma yake bali tuko bega kwa bega na yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapomshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunampongeza kwa kazi mbalimbali ambazo anaendela kuzifanya ikiwemo ukamilifu wa miradi mikubwa ya kimkakati. Sasa hivi tunavyoongea kumekamilika kwa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Pia, kuna ukamilifu wa treni hii ya *SGR* na juzi tumeanza kuona Loti hii ya kwanza imekwishakamilika na watu wameanza kupanda kuanzia Dar es salaam mpaka Morogoro, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunampongeza kwa ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo shule, miundombinu ya barabara, hospitali za kila Wilaya na tunampongeza kwa miradi mikubwa hii ambayo inaenda kukamilika na kuwaletea tija wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha sote tunajua kwamba sasa hivi dunia yetu iko katika ushindani wa kuleta maendeleo ya kidunia lakini na sisi kama Tanzania tuko kwenye kuhakikisha tunaendana na *millennium goals*. Sote tunafahamu kwamba kwenye *millennium goals* kuna *goals* 17. Mimi leo nitajikita katika *goal* ya kwanza ambayo ni n*o poverty*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *goal* hii ili kuweza kuondoa umasikini kwa wananchi hasa kwa vijana wetu wa Tanzania, nataka niishauri Wizara ya Fedha kupitia Wizara mbalimbali za kisekta kwamba sasa hivi vijana wa Tanzania tuko *above* asilimia 50 na kwenda mbele. Vilevile, kwa mantiki hii haitoshi tu kuona kwamba Serikali inaendelea kutenga asilimia nne kwa vijana wa Tanzania tena kupitia katika Halmashauri. Ni lazima Serikali tuende katika *extra mile* ya kuona kwamba tunawasaidia na kuwaanzishia vija wetu fursa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwemo Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika Wizara hizi za kisekta sasa tunataka kama kwenye sekta ya Kilimo tuone kuna asilimia nne au asilimia tano ya vijana, Wizara hizi nyingine ikiwa Wizara ya Elimu, Wizara ya Miundombinu na Wizara mbalimbali za kisekta ili kuweza kuwakomboa vijana hawa na kuwaondoa katika janga hili la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo sasa ni lazima Wizara kuja na mikakati maalumu sasa ya kuweza kuliokoa kundi hili la vijana ambalo ndilo kundi kubwa katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu sote tunaelewa kwamba Mheshimiwa Rais amezirejesha zile asilimia nne katika Halmashauri zetu. Lakini zile asilimia nne katika Halmashauri zetu bado hazitoshi kuwa ni kielelezo cha kuwasaidia vijana kwa sababu vijana ni wengi na wanahitaji fursa zaidi ili kuweza kujikomboa na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue nafasi hii kumuomba sana Waziri anayehusika na masuala ya vijana, bado zipo fursa mbalimbali zinazojitokeza katika Ofisi ya Waziri Mkuu lakini hii imeendelea kuwa ni changamoto kwa sababu bado vijana hawazielewi hizi fursa ambazo zinatoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema sasa kupitia Wizara hii wakaanzisha mafunzo mbalimbali na kuweza kuwaelewesha vijana fursa mbalimbali ambazo zinajitokeza katika Ofisi hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili utaenda kwenye sekta ya elimu. Nataka nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuamua maksudi sasa kubadilishwa kwa mitaala ya elimu ya Tanzania ili kuweza kukidhi vijana waweze kujiajiri na waweze kuajirika. Vilevile, waweze kuendana na soko la nchi yetu ya Tanzania na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kuna changamoto moja hapa, haiwezekani kwamba tumetumia fedha kubwa kubadilisha mitaala hii lakini wale *implementor* hatujaweza kuwaandalia fedha na kuwaandaa vizuri ili waweze kwenda kuwasaidia vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kwamba tumeandaa mitaala hii lakini mafunzo maalum hayajaandaliwa kwa walimu maalumu wanaokwenda kuwasomesha hawa wanafunzi wetu. Ni vema mafunzo haya yaandaliwe kwa walimu wenyewe na siyo

walimu wa Mikoa, Afisa Elimu Mikoa au Walimu Wakuu. Ni vema wapewe walimu wenyewe ambao wanakwenda kuwafundisha wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nichukue nafasi hii kumshauri Mheshimiwa Waziri wetu wa Elimu tunao hawa wanafunzi wetu ambao wamejifunza au wanaendelea kujifunza katika Vyuo vya *VETA* na hawa naweza kusema wanamnasaba na maboresho yetu haya ya elimu, naomba kitolewe kibali maalum sasa kwa hao wanafunzi ambao wanahitimu katika Vyuo vya *VETA* waende wakapewe elimu maalum na isiwe *refresher course* ikiwezekana hata iwe *intensive course* kwa ajili ya kuwa-*train* masuala ya saikolojia, masuala ya namna ya kufundisha na baadaye tuweze kuwaajiri waweze kuwasidia hawa wanafunzi wetu katika huu mtaala wetu ambao tumeuandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu nataka nizungumzie hili suala la *TRA* pale bandarini. Hii imeendelea kuwa changamoto kubwa kwa wananchi mbalimbali ambao wanatoka Visiwani Zanzibar, wakiwa wanasafiri na baadhi ya mizigo yao, unafika pale bandarini inawezekana ikawa ni haki yao au ni haki yetu wananchi kulipa kodi, lakini bado wananchi wetu hawana elimu ya kutosha kuhusiana na masuala ya kodi pale bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha ikikupendeza tunaomba uendelee kutoa elimu kwa wananchi wajue ni kipi kinastahiki kulipwa na kipi hakistahili kulipwa pale bandarini kwa sababu imekuwa ni kero kubwa sana na sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani unapita pale na sukari yako kilo tano unatakiwa ulipe na hapo ulipoinunua umeilipia na pale unapita unatakiwa nayo ulipie. Mheshimiwa Waziri unapita na mapazia matano unatakiwa uyalipie pale bado hii imeendelea kuwa ni changamoto kubwa mimi siwezi kuita kama ni kero ya Muungano siyo kero ya Muungano bali inawezekana ikawa kuna *shortage* ya elimu na elimu inahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ikikupendeza tunaomba hata wale watu wa *TRA* pale bandarini utuletee sisi Wabunge wa Zanzibar tuongee nao ili tuweze kubadilishana nao Mawazo, watueleweshe na sisi tuwaeleweshe ya kwetu ili tuweze kuona namna gani suala hili linaweza kuisha na kuwa *solved.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nataka nikutolee *scenario* moja, mimi siku moja nilipita pale kuna mama anapita pale ana *Blender* tu yake ya mkono, anafika pale, tena wale watu wa *TRA* pale *chap* tu, unaambiwa lete mama nenda ukalipie hapo, lipia maana yake hii, mama anamwambia nikalipie nini? Akaambiwa unatakiwa ulipie hii kwa sababu umeinunua maana yake unalipia *wharfage,* sijui nini na nini vitu ambavyo havieleweki! Mheshimiwa Waziri yule mama kwa hasira ile blender aliitupa kwa hiyo blender aliitupa na kodi hakulipa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ajiandae Mheshimiwa Ditopile.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Bajeti ya Serikali. Naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake kwa kuwasilisha bajeti nzuri sana hapa Bungeni, vilevile nimpongeze sana Waziri wa Mipango, Profesa Kitila pia nimpongeze Naibu Waziri Mheshimiwa Nyongo ambaye ameteuliwa hapa juzi tuna imani kabisa unakwenda kusaidia mipango ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze pia na Makatibu wote wa Wizara na Watendaji wote wa Wizara. Pia naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu

Hassan Mama yetu ambae kwa kweli amefanya kazi nzuri sana katika nchi na anaendelea kufanya kazi nzuri sana, vilevile kwa kutenga fedha nyingi sana katika miradi na pia katika Mkoa wetu wa Iringa tumepata fedha nyingi sana za miradi, hongera sana Mama yetu na sisi tuko pamoja na wewe wanawake wote tunakukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi kwa kweli zinatengwa, je, zina-*impact* gani? mnaweka *impact* gani? kwa sababu huwa napata shida sana ninapoona *CAG* analeta taarifa hapa Bungeni halafu kuna pesa nyingi sana katika Taasisi katika Idara zetu kunakuwa na upotevu mkubwa. Je, mnaweka mkakati gani kuhakikisha kwamba haya mapato ambayo tunayatenga hapa hayapotei au miradi inakuwa mibovu sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachukua hatua gani kwa sababu hata katika Mwenge unakuta kuna miradi mingine imeharibiwa kwa hizi pesa ambazo tunazitenga ambazo nyingine tumezikopa, deni kubwa sana la Serikali, lakini kama haichukuliwi hatua zozote bado tunakuwa kama tunaweka maji halafu yanachuruzika. Tunaomba hili jambo liangaliwe kwa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, huwa tunapima matokeo ya mipango yetu? Kwa sababu Serikali imekuwa na mipango mizuri sana. Kwa mfano tulikuwa tuna mpango mzuri kila Wizara imeweka pikipiki kilimo, maji na mifugo lakini sasa je, mnapima baada ya kuona tumeshaboresha hayo maeneo, baada ya hayo kuna kuwepo na maboresho yoyote yaani mnaona kuna *impac*t gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ifike sehemu Serikali iangalie changamoto tunazisema mnaboresha je, baada ya maboresho kuna mapato yanaongezeka? Au ndiyo hasara zinazidi kuongezeka? Na ukiangalia hizi pikipiki watu wameshaanza kulalamika kwamba hawana mafuta hazifanyiwi *service*. Sasa je, mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba mnapeleka mapikipiki kunakuwepo na mafuta kunakuwepo na kuzikarabati hizi pikipiki ili ziendeleze kuleta mapato mazuri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee pia kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutenga pesa nyingi sana za kilimo kwa sababu kila mwaka tunaona pesa inaongezeka na sasa hivi zaidi ya trilioni moja katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wetu Bashe ambaye kwa kweli amejitahidi sana kuhakikisha amekuwa na mipango mizuri kutumia hizi pesa za kilimo kwa sababu asilimia zaidi ya 80 ya watanzania ni wakulima na pia hata katika Mkoa wetu wa Iringa zaidi ya silimia 30 ni wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wetu wa Iringa uchumi wetu unategemea barabara zetu unaona barabara nyingi sana za kiuchumi zinakuwa bado hazitengenezwi hazikarabatiwi haziwekewi lami kwa hiyo unapokuja sasa wakati wa msimu wa mazao pamoja na kuwa tumetenga pesa nyingi za kilimo unaona zinapotea porini hazifiki katika masoko. Kwa mfano, pale Kilolo barabara nyingi sana hazipitiki kwa sababu kuna mvua mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa kweli Serikali iwe na mpango mkakati kuhakikisha kwamba barabara za kilimo zinapitika wakati wote ili mazao haya tunayoyalima basi yaweze kufika katika masoko tutakuwa tumejitendea haki na tumetendea haki wananchi na kilimo chetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nipongeze mpango wa *BBT* kwamba, vijana wengi sasa wanavutiwa kwenye kilimo kwa sababu ya mpango mzuri ambao umewekwa kwamba vijana wengi wajiajiri kupitia kilimo. Ninawapongeza sana vijana wetu wa Iringa ambao wameamua kuungana wote na kutengeneza sasa shamba kubwa kwa ajili ya mbegu ya parachichi, kwa hiyo nina imani kabisa linaenda kuzinduliwa na Waziri Mkuu na Mheshimiwa Bashe nafikiri utakuwepo, hili ni jambo zuri ambalo vijana sasa wameamua kulitumikia taifa hili kupitia kilimo. Hongera sana Mheshimiwa Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tunatenga pesa nzuri, kuna changamoto katika mizani yetu naomba iangaliwe. Natoa mfano mmoja tu, tarehe 17 kuna njegere

zilipitishwa pale Wenda, zikapimwa ikaonyesha kwamba zile njegere ziko sawa, lakini zimefika kwenye mzani wa Mikumi ikaonesha kwamba imezidi, wale watu wenye gari Namba T719 BP, hili gari limekaa siku mbili pale Mikumi njegere zimeharibika kuna hasara zaidi ya milioni sita, sasa wakulima wanalima lakini kwa nini hii mizani inapima tofauti? Mimi naomba iangaliwe huwa inapimwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hasara kubwa sana na siyo huyo tu kuna wengi wanalalamika kwamba mzani mmoja unapima vizuri ukienda mwingine mzani unapima tofauti, mimi naomba iangaliwe kwa sababu tunapoteza mapato makubwa ya wakulima na nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilikuwa naomba pia tuangalieni haya mageti ya ushuru kwenye maeneo yetu. Serikali iliruhusu kwamba kuanzia tani moja watu wanajua kwamba hii ni chakula tu cha kutumia wapitie bila kulipia ushuru lakini sasa hivi gunia moja linalipishwa ushuri shilingi 5000, nusu gunia wanatozwa ushuru sasa hii kwa kweli hatuwasaidii wananchi, tuangalieni sana mambo ya mageti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikizungumzia kuhusu kuna mchanganyiko kuhusu mazao ya misitu yetu hii. Pale Kilolo watu wengi sana wanalima misitu ya mbao ili iweze kuwasaidia, lakini inapofika labda ana tatizo ameamua kupanda miti ili baadae aje auze mbao anatakiwa awe na mashine ya *EFD* na yeye siyo mfanyabiashara. Labda Serikali ingeangalia kama kuna uwezekano hii mashine ya *EFD* ikae labda aidha kwa Mtendaji wa Kata au kwa Mtendaji wa Kijiji ili mkulima yeyote anapoamua kwenda kuuza basi akipitisha pale ichukuliwe ndivyo hivyo kuliko ilivyo sasa mwananchi anashindwa kuuza mbao zake ili aweze kusomesha mtoto au aweze kufanya matumizi mengine. Mimi naomba hili pia liangaliwe kwa uzani mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna changamoto nyingine ambayo madeni ya taasisi za Serikali kwenye miradi ya maji. Nimelizungumzia sana hili ni kwa nini haya madeni hayalipwi? tunapitisha hapa bajeti zile *OC* zinakwenda wapi?

Naomba bajeti hii sasa basi yale madeni yalipwe ili miradi ya maji iishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameamua kumtua mwanamke ndoo kichwani na sera yake, lakini kama miradi haiishi bado tutakuwa hatujitendei haki na hatumtendei haki hata Mheshimiwa Rais, ambaye ameamua kwamba hii sera itumike wanawake wote wote sasa ndoo tusiweke kichwani tuweze kupata maji ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna huu Mfuko wa Maji tulitunga sheria hapa Bungeni kwamba zikiwa *ringfencing* asilimia 100 ziende kwenye Mfuko wa Maji lakini mimi naona kama vile zinacheleweshwa kwa sababu miradi mingi inayohudumiwa na Mfuko wa Maji wanakuwa ndiyo wale wakandarasi hawapewi hela kwa wakati, sasa tunafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaombeni hizi pesa kama mmezi-*ringfence* basi ziende moja kwa moja kusiwe na msululu mkubwa kwamba zinatoka *TRA,* tena ziende Hazina basi kwa nini zisitoke tu *TRA* zikaenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa Maji ili ziweze kuwasaidia makandarasi ambao wamekuwa mara nyingi wakifanya hizo kazi walipwe kwa wakati ili ziweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine nilikuwa naomba kuhakikisha kwamba sasa hivi wanawake tuanze kufundishwa kuwa na viwanda vidogovidogo. Viwanda vidogvidogo ndiyo vitasaidia sana wanawake, kwa sababu tumekuwa na hii mikopo ya akina mama, kama hatutawafundisha wanawake kuwa na viwanda vidogvidogo bado itakuwa haisaidii kitu chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa mfano tu kidogo kwamba pale Kilolo wakulima wa nyanya wanapoteza sana malighafi za nyanya, kwa sababu nyanya nyingi wafanyabiashara wakija wanachagua wakishachagua yale masalu yanakuwa hayasaidii kitu chochote, lakini kama tungekuwa na viwanda vidogovidogo hizi nyanya zingeweza kusindikwa na wanawake tungeweza kupata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kigwangalla, ajiandae Mheshimiwa Ditopile.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa fursa ya mimi kusema hapa Bungeni siku ya leo. Awali ya yote nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai lakini kwa kutuwezesha kukutana hapa kwenye kikao chetu siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nimshukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya na tatu niwapongeze Mawaziri wote wawili ndugu yangu Dkt. Mwigulu na Profesa Kitila kwa mpango lakini pia kwa bajeti nzuri inayotoa dira ya maendeleo katika mwaka unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee ninaomba na mimi nitoe mchango wangu kidogo kuhusiana na hii hoja ya sukari ambayo inazungumzwa sana humu ndani na hata huko nje, mchango wangu utajikita kwenye misingi kwamba mimi kabla sijaingia kwenye siasa na kuwa Mbunge nilikuwa nikifanya biashara ya mazao yaani *commodities.* Kwa hiyo ni eneo ambalo ninalielewa siyo kwa nadharia lakini kwa vitendo na katika uelewa huo nakumbuka nilipokuwa Mbunge kipindi cha kwanza niliwasilisha Bungeni hoja ya kuanzishwa kwa mfuko wa kulinda bei *(price stabilization)*. Nilipowasilisha hoja ile japokuwa hatukufanikiwa kuipitisha, mchakato ulienda baadae ilikuja ikaletwa Sheria hapa Bungeni ikapita, lakini lengo hasa la hoja yangu binafsi ya kuwasilisha mapendekezo ya kuundwa kwa *price stabilization fund* yalikuwa ni kujaribu kutengeneza ulinzi wa bei ya mlaji wa bidhaa kule mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba ndani ya Serikali kuwe kuna mfuko ambapo bei zikishuka ule mfuko unatumika kununua baadhi ya bidhaa zinatunzwa kwenye Serikali, bei zikianza kupanda kwenye soko Serikali inazirudisha zile bidhaa ili kuweza ku-*stabilize* bei ya bidhaa kwenye soko lakini vilevile bei ya

mazao. Kwa mfano, kama ni kwenye pamba basi wakati bei zikishuka ule mfuko ungepaswa kutumika kulipa pesa ya ziada kwa wakulima ili wakulima wasiathiriwe na kuanguka kwa bei ya kwenye Soko la Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiona anachojaribu kufanya Mheshimiwa Waziri Bashe kwenye sekta ya kilimo ni kujaribu kuanzisha mfumo wa kununua sukari kuitunza kwenye *Central Government* halafu pale bei zitakapopanda ile sukari inarudishwa kwenye soko na matokeo yake mlaji haathiriwi na bei, ni aina fulani ya *price stabilization* kama ambavyo miaka zaidi ya kumi iliyopita niliwahi kuwasilisha hoja hiyo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huwezi kutarajia wazo wa aina hii liungwe mkono na watu ambao wanafaidika na kukosekana kwa sukari nchini, huwezi kutarajia na pengine mawazo haya kwamba pengine biashara yao itaathirika ndiyo yanayopelekea hii vuguvugu ya changamoto anayopambana nayo Waziri Bashe na Serikali kwa ujumla katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale wazee wenzangu tuliokuwepo hapa Bungeni kwa muda mrefu watakubaliana na mimi kwamba hoja za aina hii huwa ni hoja ambazo huwa zinamsukumo mkubwa sana wa wafanyabiashara wakubwa ambao wanafaidika na mfumo kandamizi kwa walaji wa mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mimi nina viwanda, sasa kama kiwanda chako kinazalisha biashara bidhaa fulani unaingiza kwenye soko huwezi kuwa na mashaka na mfumo wa kutunza tu sukari unaotekelezwa na Serikali wewe inakuhusu nini huu mfumo? Wewe una biashara yako, una mashamba yako, lima miwa yako chakata sukari yako weka sokoni, uza, siku sukari yako ikiisha Serikali itatoa kwenye *stock* yake itaweka sokoni. Sasa kitu kama hicho kinakuathiri nini kama wewe ni mwekezaji kwenye sekta ya viwanda?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo hata wale wenzangu wanaotoa hoja kwamba pengine uwepo wa Mfuko huu utaathiri viwanda vya ndani nadhani hawajafanya tafakuri ya kina kwa

sababu sioni inawaathiri vipi kwa sababu anachojaribu kufanya ndugu Waziri ni kutengeneza mfumo wa kuwalinda walaji na sisi kama wanasiasa tena wana siasa tunaotokana na Chama cha Mapinduzi tunapaswa kwa kweli kumsaidia na kumtetea Waziri kwa wazo hili, kwa sababu anaenda kuwalinda wananchi wa hali ya chini kabisa kiuchumi ambao ndiyo wateja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ukiwa mwanasiasa hauhudumii tu watu wenye uchumi wa juu *the way to do,* Hapana! Unahudumia kwa kiasi kikubwa watu wenye uchumi wa chini ambao kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ni zaidi ya asilimia 61 hii sensa ya mwaka juzi. Sasa huwezi kuwafaidisha watu wachache ukawapuuza watu waliowengi. Kwa hivyo, sisi kama wanasiasa na kama kweli tuliomba nafasi za kisiasa kuja kuwawakilisha wenzetu, ni lazima tuone *merit,* ni lazima tuone faida ya mpango mzuri ambao unapendekezwa na Serikali na ni lazima tuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa nijielekeze kwenye kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa, mchango wangu unaanzia kwenye Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka juzi ambayo inaeleza kwamba zaidi ya asilimia 69.6 ya Watanzania ni wenye umri wa miaka chini ya 29, maana yake ni kwamba idadi hii ya watu Tanzania tuna *the youngest population* katika kipindi chochote kile cha historia ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba katika kipindi kijacho cha miaka takribani 26 ijayo kufikia mwaka 2050, ambapo taarifa ya *Department of Social and Economic Affairs* ya Umoja wa Mataifa kwenye ripoti yao ya World *Population Prospect* ya mwaka 2017 wanatukadiria kwamba tutakuwa katika nchi yetu tumefikia watu milioni 140. Kwa maana hiyo, changamoto kubwa tatu ambazo tunazi-*face* leo kwa kipindi hicho zitakuwa kubwa zaidi. Changamoto zenyewe ni kukosekana kwa ajira, kukosekana kwa uhakika wa chakula na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa naibu Spika, sasa katika muktadha huo ukichanganya na zama tulizopo sasa, ambapo kwa kiasi kikubwa uchumi umefika katika *Forth Industrial Revolution* (Mapinduzi ya

Viwanda ya Awamu ya Nne) ambapo unazungumzia taaluma za *block chain technology, artificial intelligence* pamoja na *internet of things* kuteka uchumi wa Dunia, Tanzania katika mpango huu na katika ile *Vision 2050* inayoandaliwa tumejiandaaje ku-*tap* hiyo fursa ya kutumia *technology* kuweza kufaidika na *demographic dividend* ambayo tunaitarajia kuwepo katika kipindi cha miaka 26 inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo napenda Waziri Prof. Kitila Mkumbo atakapokuja ku-*wind up* hoja yake atuelezee, tunajipangaje kukabiliana na hizi changamoto nne, hususan hii ya ongezeko kubwa la watu, uharibifu wa mazingira na kukosekana kwa uhakika wa chakula ambao utakikumba kizazi chetu miaka 26 tu inayokuja, sisi tumejipangaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, inakadiriwa katika nchi zote duniani Tanzania tutakuwa miongoni mwa nchi tisa ambazo zitakuwa kwa ujumla wake zinachukua zaidi ya nusu ya idadi ya watu watakao kuwepo duniani mwaka 2050 ambayo ni miaka 26 tu ijayo, sasa kwa maana hiyo kwa hapa Afrika ya Mashariki, nchi nyingine ambazo zipo ni pamoja na *Democratic Republic of Congo (DRC)* Ethiopia na Uganda, tuko nchi nne katika hizo nchi tisa. Je, sisi Tanzania tunafanya uchaguzi upi, *what choices are we making* kwa ajili ya kujipanga kwenda huko mbele, ukizingatia idadi kubwa ya watu ambao tutakuwa nayo eneo hili, uharibifu wa mazingira na ufugaji holela, vilevile kilimo holela na mipango ya makazi holela, Tanzania tunajipangaje leo kwa ajili ya kuiokoa nchi ya watoto wetu na wajukuu zetu katika miaka 26 inayokuja, tunajipanga vipi?*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kigwangalla kengele ya pili.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ditopile, jiandae Mheshimiwa Lusinde. Mheshimiwa Ditopile endelea.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema aliyetupa kibali kuwepo hapa leo, lakini naendelea kuungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais na kuwapongeza Mawaziri wetu wawili, Waziri wa Fedha na timu yake na Waziri wetu wa Uwekezaji na timu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita sana kwenye Sekta ya Kilimo. Kwanza, napenda sana nichukue fursa hii kuipongeza sana Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)*. Benki hii tumeona, kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, imefanya mambo makubwa, ilipanga kukusanya shilingi bilioni 45 lakini imekusanya shilingi bilioni 41.56 ambayo ni sawa na asilimia 92.15 ya malengo iliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki hii ilipanga kukuza faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 18.50 imeweza kukusanya shilingi bilioni 18.79 ambayo ni zaidi ya asilimia 107 ya malengo iliyojiwekea. Pia benki hii ilijapanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 120 imeweza kutoa mikopo ya shilingi bilioni 161.6 ambayo ni sawa na asilimia 134.67 ya malengo iliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, benki hii imeweza kukuza thamani ya mali zake na walijipanga kwa shilingi bilioni 600.6 huku walipanga kukuza mali hizo kwa shilingi bilioni 562.7 ambayo ni sawa na asilimia 100.786 ya malengo waliyojiwekea, lakini hii ni benki inayotoa mikopo, walijipanga kurejesha mikopo ya shilingi bilioni 62 lakini wameweza kurejesha mikopo ya shilingi bilioni 92 sawa na asilimia 148.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona ufanisi huu, naiomba Wizara iweze kuendelea kuiamini benki hii na kuweza kuwaongeze mtaji ili sasa kwa sababu imekuwa ni mkombozi kwa wakulima, wafugaji na wavuvi, basi wawaongezee mtaji ili sasa waweze kushuka chini kwenda kuwafuata wakulima na wafugaji kule walipo. Kwa hiyo, naiomba nitoe pongezi binafsi kwa

Mkurugenzi mkuu Ndugu Frank Mgeta, kwa kweli anachapa kazi na ana kila sababu ya kuungwa mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijikite kwenye sakata hili la sukari linaloendelea. Naomba ku-*declare interest,* mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge inayosimamia Viwanda, Biashara, Kilimo pamoja na Mifugo. Bunge hili hili ndiyo lilipitisha sheria kwa nia njema kabisa ya kuwapa vibali wazalishaji wetu wa sukari kwa maana ya viwanda ili wao waweze kuingiza *sugar gap*, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge sheria tunatunga zinaenda kutungiwa kanuni na zinaenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo siyo dhambi kukaa kujitathmini na kujisahihisha. Kama sheria kwenye utendaji kazi imeleta matatizo kwa wananchi, siyo dhambi. Kwa hiyo, mimi kwa unyenyekevu mkubwa sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwenye haya mabadiliko ya sheria ya sukari naomba tuiunge mkono Serikali kwa sababu nia ni ile ile njema ya kwenda kuwagusa na kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yaliyotokea miaka hii ya karibuni 2019 na mwaka huu 2024 tuna kila sababu sasa kuona na kusema sukari ni bidhaa nyeti, tuna kila sababu kuiamini *NFRA* kwa niaba ya Serikali iweze kudhibiti uingizwaji na usambazaji wa bidhaa hii nyeti kwa maslahi mapana ya wananchi wetu. Hili jambo mimi nawaambia ni la kizalendo. Naomba niunge mkono sana mchango aliotoka kutoa Mheshimiwa Kigwangala kwamba, wanaenda kuweka akiba *buffer stock* ili inapotokea dharura tumeishiwa huko kwenye viwanda wao wanaenda kuleta *consensus* ili tusilete taharuki, tumeona jamani. Kule kwetu Kondoa huwa jioni tunapenda kukaa kwenye vijiwe vya kahawa, kule kwenye vijiwe vya kahawa ndiyo tunaongea mambo ya Bunge, mambo ya maendeleo na mambo yanayoendelea kwenye jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, *weekend* hii nilikuwa kule na nikawaambia wazee wangu naenda kuchangia suala hili la sukari. Kwanza, wameniambia nisimamie haki na niseme ukweli. Wakati bei zinapanda tulikuwa tunakaribia Mwezi Mtukufu wa Ramadhan na walikuwa wana wasiwasi sana bei ya sukari

itakuwaje Ramadhan na watakunywaje uji. Kwa hiyo, wanampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pia wanampongeza Waziri Hussein Mohamed Bashe kwa maamuzi ya kizalendo, uthubutu na kiutu ya kulinda maslahi ya Mtanzania mnyonge.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria tunatunga tunampa Waziri mamlaka ya kutunga kanuni za kutekeleza ile sheria. Ametumia kanuni zake kutokana na *emergence* iliyokuwepo ili kutoa taharuki iliyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyetu vinafanya kazi kubwa na naomba Waheshimiwa Wabunge tusipotoshwe na tusitoke kwenye hoja ambayo Serikali inataka kutuelekeza, kwa sababu hawa wanaosema kwamba sisi tunaenda kuua viwanda ni waongo. Hakuna tasnia iliyolindwa na Serikali zote tangu Awamu ya Tatu ambapo ndiyo viwanda hivi vilianzishwa mpaka Awamu hii ya Sita. Wamepewa mashamba bure hawa, hata hayo marekebisho ya sheria tuliyowaruhusu wao kuingiza vibali ilikuwa ni kwa ajili ya kuwalinda. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tumemuona kaingia madarakani alienda Kagera kutembelea kiwanda na hadi msikiti walioujenga wao kaenda kuufungua, leo hii mtasema kweli anataka viwanda vife?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunasimamia hii sekta kwa niaba ya Bunge, yapo malalamiko mengi sana kwa sababu wanasema wao wanauliwa lakini nenda kachunguzeni, wakulima wana matatizo mengi na hivi viwanda lakini sisi tunawaita mezani na tunaweka hali sawa ilimradi wasitoke kwenye sehemu yao ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kuna kiwanda kinanunua miwa shilingi 100,000 kutoka kwa mkulima lakini kuna kiwanda kinanunua shilingi 70,000 na wakulima wanalalamika. Serikali imekuwa katikati ikilinda maslahi ya mkulima na maslahi ya mzalishaji, kwa maana ya mmiliki wa viwanda. Haijawahi kumkandamiza yeyote kati ya hao, kwa hiyo wakati sisi tunawapa hii *mandate* ya wao kuingiza ile *sugar gap* yapo makubaliano na makubaliano makubwa ni kumlinda mlaji, aidha kwa maksudi au kwa bahati mbaya, wameshindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilitakiwa wawe na *buffer stock* ili sukari inaposimamisha uzalishaji waiingize kwenye soko, hawakuwa nayo, baada ya mamlaka ya *TMA* walipewa vibali, na kweli uharibifu wa *El-Nino* umekuwa mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge tulienda kujionea kule Mtibwa na uone sasa kama Serikali inaona tija ya uzalishaji wa sukari hata Serikali yenyewe, Wabunge si hapahapa tulipitisha kwenda kuanzisha kiwanda kile cha Mkulazi. Kwa hiyo, hata Serikali yenyewe inazalisha sukari, utasemaje inaenda kujihujumu yenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilichokuwa nataka kusema ni kwamba viwanda hivi vimebebwa sana na nia ni njema. Hata mtoto akiwa mchanga anabembelezwa na analishwa lakini kadri anavyokua anaenda anakula mwenyewe lakini unafika muda sasa mtoto anaenda kujisimamia mwenyewe, ameshakua mkubwa. Kwa hiyo, kwa ajili ya maslahi mapana ya wananchi walio wengi ambao wanatumia bidhaa hii, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu muda utakapofika wa *Finance Act* tuiunge mkono Serikali kwa nia njema na tuweze kupitisha sheria hii kwa maslahi mapana ya wapiga kura waliotuamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Rais, hatumpangii lakini Mawaziri hawa ambao wanajitoa muhanga katika kulinda hadhi na heshima yake wakati…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam kengele ya pili hiyo.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja tu, wakati sukari imepanda bei matusi yote yalikuwa kwa Rais wetu, ndiyo maana Waziri akajitoa muhanga kwenda kuhakikisha Rais Samia anakuwa shujaa kwenye suala la sukari, lakini wako wengine siwataji majina wanamrudisha nyuma Mheshimiwa Rais, kwa kweli tunaomba utulindie Mheshimiwa Mohamed Bashe na anakusaidia sana katika sekta hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilimtaja Mheshimiwa Lusinde, hayupo, atachangia Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kulihutubia Taifa kutoka Bungeni hapa ili wananchi wa Kinondoni waweze kunisikia Mbunge wao nikichapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Prof. Kitila kwa hotuba nzuri, hotuba ambazo ukizichambua unaweza ukaona ni kwa jinsi gani taswira ya Rais wetu anavyotaka Taifa hili liweze kujipeleka katika masuala mazima ya uchumi, hongera sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikichangia katika Bajeti ya TAMISEMI tarehe 15 Aprili, niliweza kutoa takwimu na maelezo mengi juu ya mikakati ambayo Serikali imetufanyia wananchi wa Kinondoni kutuletea maendeleo na kwa hali hiyo napenda nimpongeze tena Mheshimiwa Rais kwa kazi ambayo ameifanya Kinondoni. Kinondoni sasa inang'ara nampongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie miradi ya *DMDP* tu. Pale Dar es Salaam kuna mradi unaitwa *DMDP Two (A*wamu ya Pili). Sasa hapa ukiangalia Kinondoni kama Wilaya tumetengewa kilomita 48.33. Kinachochukiza Jimbo la Kinondoni tumepewa kilomita mbili tu kati ya kilomita 48, nyingine karibu kilomita 46 zimepelekwa Jimbo la Kawe, hili jambo siyo zuri, halileti uwiano stahiki na linachukiza, si jambo zuri sana.*(Makofi)*

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nataka kumtaarifu pacha wangu, rafiki yangu na ndugu yangu mwema kwamba sababu ya kupelekwa Jimbo la Kawe ni kwa sababu Jimbo la Kawe peke yake lina

*network* ya barabara kilomita 1,300 wakati Jimbo la Kinondoni *network* ya barabara ni kilomita 100 tu, hiyo ndiyo sababu namtaarifu pacha wangu.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba, taarifa.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, *aah*! hii taarifa siipokei, yeye siyo mpangaji, bahati mbaya sana pacha wangu siyo mpangaji na dakika zangu naomba unilindie.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo linachukiza na nitaendelea kulisema na kulilalamikia kwa sababu si jambo zuri kwa mustakabali wa wananchi wa Jimbo la Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuna matatizo pale Dar es Salaam, hasa mashimo na wala tusilalamikie mvua. Mashimo katika barabara yanaleta taswira mbaya sana katika Jiji la Dar es Salaam. Najua utaratibu wa sasa hivi ulivyo mashimo yakitokea wanapewa Makandarasi binafsi kwa minajili ya kuziba mashimo yale, kazi haifanyiki vizuri. Mwaka 2022/2023 Serikali ilitumia shilingi milioni 831, mwaka huu wametumia shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya uzibaji wa mashimo. Rai yangu ni kwamba katika ufanyaji ule wa kazi hatuoni *value for money*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba kwa kuwa Halmashauri zetu zinajiweza turudishe mfumo wa zamani tuwe na karakana zetu, Kinondoni kuwe na karakana, Temeke kuwe na karakana na Ilala kuwe na karakana ama tuwe na karakana moja ambayo kazi yake itakuwa ni kutengeneza mashimo ya barabara za Dar es Salaam ili barabara zetu ziweze kupitika na walipa kodi waweze kuona faida yake katika jambo hili. Naamini kabisa hili linawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa Tanzania unahitaji sana *private sector.* Nilikuwa nikiangalia kuna andiko moja la Tanzania *Private Sector Foundation,* wameliita *Feasibility for the Annual State of the Private Sector Report* ya Mwaka 2023. *Private Sector* inachangia zaidi ya asilimia 80 ya Pato la Taifa. Mzunguko wa fedha katika Taifa hili kwa hali kubwa kabisa unategemea *private sector,* lakini *private sector* hii ukiangalia upande wa

wafanyakazi ambao wako viwandani ajira kubwa inatolewa na *private sector* asilimia 96.5, watu 300,025 wameajiriwa kupitia *private sector.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa *REPOA*, *REPOA* ni ile *Research for Poverty Alleviation* wanasema *Private Sector* inachangia asilimia 80 katika makusanyo ya fedha za Serikali. Sasa kama *private sector* ina nguvu kiasi hiki ni kwa vipi basi haipewi ule uzito unaostahiki? Ukiangalia katika hotuba zetu hizi utaona kwamba *private sector* imetajwa kwa kupita lakini haijapewa nguvu stahiki, kwa hali hiyo ukiwauliza *private sector* katika tafiti zangu wanasema bajeti hii inauma na kupuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini inakuwa hivyo? Inakuwa hivyo kwa sababu nchi inaonekana kana kwamba tunakwenda zaidi katika *trading* badala ya kuvisimamia viwanda vyetu ambavyo ndivyo waajiri wakubwa katika taifa letu hili. Tusipoangalia upelekaji wa msukumo, hasa katika masuala mazima ya kuvilinda viwanda vyetu, wasiwasi wangu ni kwamba biashara nyingi zitakuwa zinafanyika kwa wale ambao wanatuletea vitu. Leo hii ukitembea vitu vya Uturuki vimejaa lakini kuna viwanda hapa, hata soda nyingine zinazozalishwa hapa zina mpinzani wa soda kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia vilevile hata vinywaji vikali vina ushindani wa vinywaji vya nyumbani na vya nje. Nguo hali kadhalika, sasa viwanda vyetu vitafanya kazi gani zaidi ya kufanya *trading*? Na hili ndiyo tatizo tunalopata sasa hivi katika masuala ya sukari, viwanda vipo lakini sukari ya nje vilevile inaletwa. Sasa hilo mimi sitaki kuingia huko kwa sababu mimi siyo mnywaji sana wa sukari, nafuata sana ushauri wa Dkt. Janabi na ningependa Watanzania wafuate sana ushauri wa Profesa Janabi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba tuangalie tatizo la ufanyaji wa biashara katika Taifa letu la Tanzania. *Blueprint* haijatajwa kwa uzito wake katika bajeti hizi zote mbili. Kwa hali hiyo, napata wasiwasi kwamba sioni mkakati wa Serikali kuinua *rank* ya Tanzania katika ufanyaji wa biashara, tumebaki nchi ya 141 katika nchi 190. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashindwa na Rwanda, Rwanda ni nchi ya 38 katika urahisi wa ufanyaji wa biashara. Kenya ni nchi ya 56 na Uganda ni nchi ya 116. Januari mwaka huu Umoja wa Nchi za Ulaya, *European Union*, wametuchangia shilingi bilioni 63. Kwa minajili gani? Kwa minajili ya kuweza kuifanya Serikali itekeleze *blueprint*. Sijui kama Waheshimiwa Wabunge mnafahamu hivi, hela hizo zimetolewa kwa minajili ya kuisaidia Serikali ije na mipango mizuri ya utekelezaji wa *blueprint*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimekuwa nikiteta na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara ni kwa jinsi gani wamejipanga. Nikamuuliza, je kuna hata Kamati zinazokaa kuangalia ni jinsi gani tunaweza kuleta vile vipaumbele vilivyopo katika *blueprint*? Pako kimya. Sasa mimi wasiwasi wangu ni nini? Wasiwasi wangu hata hii kauli ya Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dkt. Tausi Kida, anasema hizi fedha zitakwenda kutusaidia kuhakikisha kwamba *blueprint* inakwenda kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali kwa Mheshimiwa Mwigulu pamoja na Mheshimiwa Dkt. Kitila wakija watuambie Serikali imejipanga vipi kwa mipango thabiti kabisa siyo ya kuchota chota hapa kidogo, pale kidogo, mipango thabiti ya kwenda kutekeleza *blueprint*…*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba kengele ya pili hiyo.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naam.

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi mimi naunga mkono lakini ningependa Serikali iweze kuja na mpango wa kutusaidia kutekeleza *blueprint* ipasavyo. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba unazungumzia *DMDP II* siyo?

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** *DMDP I* ulipata kilometa ngapi?

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kidogo sana.

**NAIBU SPIKA:** Kilomita moja wewe ulikuwa siyo Mbunge? Katika shilingi bilioni 600 za *DMDP I* Kinondoni mmechukua asilimia nyingi za barabara na Jimbo la Ilala lilipata kilomita tatu tu basi.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasemea…

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasemea ndani ya Jimbo, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko hayupo, Mheshimiwa Mohamed Issa, Mheshimiwa Kamguna ajiandae.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya ya kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu hili ili na mimi niweze kuchangia katika hoja ambazo zipo mbele yetu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nianze kwenye jambo ambalo limeleta taharuki wakati huu tulionao, jambo la sukari. Kwa kweli jambo hili kama nisingeweza kulichangia ningeona kwamba sikuwatendea haki Watanzania. Kwa kweli mimi kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, kwa hatua ambazo amezichukua ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanaondokana na kadhia hii ya ukosefu wa bidhaa muhimu ya sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninapata mshangao kabisa kwamba ni kwanini watu hawataki kuwahurumia Watanzania? Tuliona hapa kipindi kifupi kilichopita ilikuwa hadithi ni moja tu,

sukari. Sukari ni bidhaa muhimu ambayo inahitajika kwa kila mwanadamu. Sukari tunaitumia kwenye mambo mengi, tunaitumia katika chai, vinywaji, chakula, inatokea mpaka wakati mwingine unakosa samaki au nyama unatumia sukari ili kuhakikisha kwamba maisha yanakwenda. Bidhaa hii ni muhimu, ni bidhaa ambayo inaweza kulisaidia taifa hili kupakwa matope. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili la upungufu wa sukari lilivyotokea ilionekana kwamba hii kazi yote aliyoifanya Mheshimiwa Rais ya kulijenga taifa hili ya kusema kwamba kazi iendelee, kuichukua miradi mikubwa ambayo iliachwa na mtangulizi wake ambayo tuliona kwamba asingeiweza na ameweza, Daraja la Busisi, reli ya *SGR* na mambo mengine makubwa kama Barabara, sasa jambo hili lingeweza kuja kutia doa kazi yote hii ambayo ameifanya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi chama changu cha ACT-Wazalendo kina kauli mbiu, "Taifa la wote, maslahi kwa wote", haiwezekani taifa hili la watu milioni 60 na kitu kuja kupata maslahi watu saba, hili haliwezekani. Tulinde maslahi ya watu saba, tuue watu milioni 60, hili haliwezekani kabisa. Mimi nakupongeza Mheshimiwa Bashe kwa kuleta *Finance Bill* hii ambayo itakuja kuwa muarobaini. Tuliona hapa sukari ilitoka shilingi 2,600 mpaka shilingi 10,000, wananchi walikuwa wanahangaika, wanalalamika hawajui wafikie wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza kabisa, mimi ni muumini wa viwanda na ninawapongeza wenye viwanda na hatutaki kuua viwanda lakini tunataka kuwalinda wananchi wote. Kwa maana hiyo, ni vizuri sana kuleta sheria hii ili tukiona kwamba hawa ambao tumewapa dhamana ya kuzalisha sukari kwa ajili ya wananchi wetu wamekosea kidogo, Serikali ichukue nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ndiyo ambayo wanaweza kuulizwa, hatutawauliza wenye viwanda kwanini sukari imekuwa chache? Tutamuuliza Mheshimiwa Rais, watu wanamtaja Mheshimiwa Rais. Kuna watendaji wengi, kuna Katibu Mkuu, kuna

Waziri, kuna watendaji wengi sana lakini viwanda hata havikutajwa, imetajwa Wizara, ametajwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwanini Rais akiona anachafuliwa na hali ana uwezo anao na Msaidizi wa Rais ni Waziri. Sasa kama amechukua nafasi hata kwa namna yoyote ile ya kuondosha tatizo hili, mimi naona amefanya vizuri kuwaondoshea wananchi tatizo na mimi naunga mkono, tunasubiri sheria hii ya *Finance Bill* ili *NFRA* waje wawe *solution* kwa nchi hii kutokukosa sukari ambayo ni bidhaa muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikomee hapo niende kwenye suala lingine. Suala la faini kwa wafanyabiashara ambao hawakutoa risiti. Jambo hili litaleta taharuki sana kwa wafanyabiashara. Wafanyabiashara hawa wenzetu nao pia ni wazalendo, tumekuwa tukisema kwamba walipa kodi wakubwa ni hawa watu wa kati, wafanyabiashara wa kati na ndiyo hawa ambao tunakwenda kuwawekea faini hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakumbuka ilipokuja hii sheria ya *VAT* kwamba unalipa faini shilingi milioni nne na mwaka mmoja jela watu wengi walifunga biashara na wakakimbia nchi hii na nchi ilikosa mapato. Sasa leo kwanini tunakuja kuleta tafrani kama hii? Hii itasababisha *negotiation* kwa sababu hii haikuweka kwamba ni shilingi milioni 15, ni mpaka shilingi milioni 15. Yule afisa anaweza kumwambia, wewe ili nisikuwekee faini hii basi fanya hivi. Tunakaribisha rushwa, jambo hili siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni njia ya mapato basi nchi hii juzi tu tumewaleta hawa watu wa DP World na tulisema hapa watachangia asilimia 62 ya mapato yetu, kwani haitoshi kuwa mapato? Pia, sekta ya madini sasa hivi inachangia mpaka asilimia 10 ya uchumi wa nchi yetu, kilimo kimepandisha, sasa tuna hofu ya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninachokisema, Serikali yetu iangalie wafanyabiashara hawa iwalinde, isiongeze tu faini, ikiwezekana kama shida yao ni kodi, na kodi ndiyo inayoendesha nchi mimi nakubaliana na Serikali, sasa wangefanya *calculation* zao, ile *VAT* pale ikapungua na

wakaongeza *import duty* lakini ikawa ime-*balance*. Kwamba, mapato ni yale yale ili huku kwenye kuwachaji wananchi iwe wanaona kwamba wanalipa kidogo lakini tayari fedha imeshalipwa wapi, kule kwenye kuingia, ikiwa ni bandarini au kwenye mipaka yetu. Sasa kwenda kuongeza faini hizi itasababisha *disaster* kubwa kwa wanachi na wananchi hawatafurahia jambo hili na wataiona Serikali yao haiwatendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee na mchango wangu, suala moja hapa la uchumi wa bluu, mimi napongeza Serikali zote mbili kuliona suala la uchumi katika bahari zetu kwa sababu muda mrefu uchumi huu ulikuwa unachukuliwa na wageni. Wageni wanakuja na meli kubwa wanavua lakini mapato hayaingii kwetu yanakwenda nje, lakini kwa kuliona hili napongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu hii ilianza kusema kwamba itanunua meli nne za uvuvi mwaka juzi, mpaka leo hii hatujaona meli hata moja. Mbaya zaidi niliwahi kuuliza nikaambiwa kwamba upande wa Zanzibar hazitatengenezwa tena kwa sababu wenyewe wana muundo tofauti. Sasa jambo hili kwa vile tumeshapitisha hapa lilitakiwa liende vile vile ili wananchi waone kwamba kila mmoja amefaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa jambo hili kule Jimboni kwangu Konde kumetokea kadhia kubwa sana. Wale wananchi wangu asilimia 80 ni wavuvi na wamekuwa wakivua tangu enzi na enzi, ndiyo uchumi wao, sasa leo eti kwa sababu tuna nia ya kukuza uchumi wa bluu wamekuwa wakizuiwa kwenda kuvua kwa kutumia mitumbwi yao pamoja na nyavu sasa wanaambiwa wakavue kule. Ni jambo zuri, tunalipongeza lakini Serikali ingewezesha kama ilivyoahidi, Serikali iliahidi kutoa vyombo vikubwa ambavyo wananchi watapata kuvua pamoja na vitu vingine ikiwemo *fish finder, cool box* pamoja na vitu vingine lakini mpaka sasa hivi hawajatoa, vile walivyotoa havikutosha na havikufaa pia, maana yake vilikuwa na kasoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Serikali haitakiwi kuwakataza wananchi kuvua kule kwa sababu ndiyo uchumi wao. Hawana ajira, hakuna kiwanda, hakuna chochote zaidi ya samaki. Asilimia 20 tu ndiyo wanafanya biashara, kuwakataza wananchi kwenda kuvua kule Jimboni kwangu kwakweli ni kuwasababishia matatizo na njaa wawe ombaomba matokeo yake waichukie Serikali, jambo hili siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, tumeona hapa katika bajeti hii kumewekwa kodi kubwa kwenye vinywaji vikali. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, inatosha.

**NAIBU SPIKA:** Wageni wa Waheshimiwa Wabunge waliopo Bungeni mchana huu ni wageni 29 wa Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *UDSM*, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 19 wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, uongozi pamoja na wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu kutoka Mara, *Victoria Divas*, wanaoshiriki *Taifa Cup*, mashindano yanayoendelea viwanja vya Chinangali, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 44 wa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau ambao ni walimu na wanafunzi kutoka Shule ya Msingi, Laalakir kutoka Kiteto, Mkoa wa Manyara, kaibuni. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Joseph Kakunda, viongozi wa Shirikisho la Walimu Tanzania, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 41 wa Shule ya Msingi Rasaisei ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanachama 80 wa Jukwaa la Wazalendo Huru kutoka Mikoa mbalimbali Tanzania, karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 50 na walimu nane wa Shule ya Msingi Amani kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wanafunzi 41 na walimu saba wa Shule ya Msingi Ushirika kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Vijana 58 wa kanisa la *Baptist Church of Tanzania* kutoka Kigoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, nilishamuita Mheshimiwa Aleksia, wajiandae Mheshimiwa Mtemvu na Mheshimiwa Neema Mwandabila. *(Makofi)*

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupatia uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi zote ambazo anazifanya kwa kutupambania Watanzania, Waheshimiwa Mawaziri wote, ndugu zangu, Mheshimiwa Spika mwenyewe na Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa leo nazungumzia kuhusu mambo ya bima ya majanga. Kwanza, nawaunga mkono na ninawapongeza kwa bajeti ambayo mmeileta, bajeti ambayo inakubalika, bajeti ambayo imepitia viwango vyote, tunawashukuru sana kwa hayo. Hata hivyo, mimi ninajikita upande wa majanga ya bima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kukata bima siyo lazima lakini ni wajibu kwa ajili ya usalama. Ukiangalia katika nchi yetu kwa sasa hivi, unakata bima kwa amani lakini unapopata majanga katika fidia inakuwa ni tatizo kuipata hiyo haki yako ya bima. Kwanini nasema hivyo? Kwa sababu nafikiri tulio wengi hatujui bima ni nini na hata kama tukijua bima ni nini, kwani faida ya bima ni nini? Kama siijui bima ni nini maana yake hata faida yake sitaijua ni nini.

Kwanini nasema hivi? Kwa sababu watu wanakata bima, wakishakata bima kwa makubaliano kabisa lakini ukishakata ile bima, ukipata janga kupata fidia yako ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unajiuliza, nilikata bima kwa mapenzi yote, wanakaa wanakuelewesha lakini ukishapata majanga wanakusumbua. Kwa mfano, mtu anakata bima ya *comprehensive* ambayo ni bima kubwa kabisa. Unakata bima labda ya shilingi milioni 40 halafu ukishapata janga mtu bima ile anakupa thamani ya shilingi milioni 10, ambayo lile janga ni *total loss*. *Total loss* maana yake ni kwamba, kama ni gari, nyumba, tuchukulie gari, kama ni gari *total loss* maana yake wanatakiwa wakulipe kiasi chote, asilimia 100, la sivyo, *total loss* hatuna kiwanda ambacho kinaweza kikatengeneza magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inatakiwa lile gari lipelekwe nje aidha Japan, kama limetengenezwa Ujerumani basi lipelekwe Ujerumani. Sasa tunaposema *total loss* mtu ameweka *comprehensive* halafu unampa *percent* ya ile bima tutengenezee ile gari anafanyaje? Ina maana kwamba lile gari litakaa, kama ni mfanyabiashara, kama ni lori lake litakuwa linakaa ndani au linakaa linasubiri hiyo bima kwa muda wa mwaka mmoja. Je, hiyo Serikali tunazalisha au tunarudi nyuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunarudi nyuma, kwanini watu wa bima wasiwalipe wale wenye bima kwa wakati? Hilo la kwanza. Jambo la pili kama ni *total loss*, mtu amekata *comprehensive*, kwa nini usimpe kiasi chake chote badala yake unasema kama ni shilingi milioni 40 unasema unampa shilingi milioni 10 akatengeneze kwenye gereji za watu binafsi, sasa *total loss* mtu anatengeneza kwenye gereji binafsi, hiyo gereji binafsi ina uwezo wa kutengeneza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake *total loss* ni kwamba gari haliwezi tena kutengenezeka, huwezi kutembea, maana yake ni kwamba linatakiwa lirudishwe kiwandani. Sasa, mimi naiuliza Serikali haioni kwamba katika hali hii mtu amepata *total loss* halafu watu wa bima hawamlipi, wanachukua lile gari wanalipeleka kwenye gereji zetu za Tanzania, hawaoni kwamba

ile kampuni ya bima inachangia kuleta ajali? Maana ukishatoka pale ni lazima utaendesha lile gari na gari kama limeshaharibika asilimia 100 kwa vyovyote vile kwa uwezo tulionao lile gari halitengenezeki linatakiwa kwenda kiwandani. Je, kwa nini hawa watu wasilipwe madai yao yote na fidia zao kama walivyokubaliana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwanini? Hii hali imewafanya Watanzania wengi wamekata tamaa kukata bima. Watu hawakati bima kwa sababu watu wanavunjika moyo na hata kama wakikata bima wanakata wachache, hawaoni faida ya bima. Nakata bima, napeleka hela zangu kwenye bima lakini siku ya kulipwa, kukopa harusi kulipa matanga. Sasa mtu anaona kwa nini? Bora niendeshe hivyo hivyo bila ya bima, lakini wanapoendesha bila bima wanakosesha Serikali mapato. Sasa yale mapato ambayo Serikali wanayakosa kwa sababu pale wangelipwa kodi, unapoenda kukata bima, matokeo yake watu wengi hawaendi kukata bima Serikali inakosa mapato, matokeo yake watu wengi hawaendi kukata bima, Serikali inakosa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiuliza Serikali, kwa nini watu wanakwepa hiyo bima, Serikali inafahamu au haifahamu? Mtu anajiuliza na kama sikati bima, kwani nisipokata bima napata hasara gani, kama hapati hasara kwenye bima, kwa nini nipoteze hela zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu anajikuta anafika mahali, hakati bima. Naiuliza Serikali, hao watu ambao hawawalipi watu bima zao au kuwafidia kufuatana na makubaliano, mpaka sasa hivi wameshachukuliwa hatua gani? Maana Watanzania wengi wana hicho kilio, siyo cha mtu mmoja wala siyo cha watu wawili. Watanzania wanahangaika hawana kwa kusemea, wanatuomba sisi ambao ni wawakilishi wao tuwasemee kwamba hizo kampuni za bima au mawakala wao wanawatesa Watanzania ambao wanawadai bima zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iliangalie hilo, wajue kwamba kweli Watanzania wanahitaji malipo yao ya bima kufuatana na kiwango ambacho mtu amekata ili waweze

kuendelea na maisha yao, badala ya *blah blah*. Wakati mwingine wanakuambia kwamba mimi sikulipi mpaka tuende kwenye usuluhishi. Mimi naiuliza Serikali, kwani wakati wanapokata bima, wale watu wa bima huwa wanawapa elimu ya bima kwamba hapa nisipokulipa unaenda kwenye usuluhishi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huku ni kupoteza muda, badala ya kutumia muda kuzalisha mali, mtu anatumia muda leo nenda bima, kesho rudi, keshokutwa bima, keshokutwa unarudi. Kwa hiyo mimi naomba Serikali ikija, ituambie, kutokana na usumbufu huo kwa nini mtu wa kawaida akate bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulipa fidia ya bima ni hisani au ni wajibu? Mimi naomba Serikali iniambie hilo. Hao ambao hawataki kuwalipa, wanachukuliwa hatua gani mpaka sasa hivi au Serikali ina mkakati gani wa kuwachukulia hatua watu ambao hawawatendei haki hawa Watanzania ambao walio wengi ni wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la pili, nazungumzia kuhusu Kijiji cha Ngombo. Kijiji cha Ngombo ni Kijiji ambacho kilihamishwa kwa ajili ya kupisha Bwawa letu la Mwalimu Nyerere. Maji mengi yaliyoko kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere yanatoka sehemu ya Bonde la Kilombero hususan Kijiji cha Ngombo, lakini mpaka sasa hivi wale wananchi wameambiwa wahame, wamethaminiwa tayari lakini hawajapata haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikifika wakati wa kulima, wanawaambia wale watu wahame lakini inapofika wakati kama huu wanavuna, wamemaliza, Serikali inakaa kimya. Serikali tunaiomba, tunajua Serikali yetu ni sikivu, tunaomba wale watu, nendeni sasa hivi kipindi hiki ambacho watu wamemaliza kulima, mkawape fidia zao wahame wajue wanaelekea wapi, wale watu wanateseka, kwa sababu mtu hawezi kujenga nyumba, mtu hawezi kulima, hajui aelekee wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kuna shule, wale wanafunzi wataelekea wapi, watasoma au hawasomi? kuna hospitali pia. Kwa hiyo, tunaomba Serikali mkae mjipange, mjue mwaka huu angalau tunaelekea wapi watu wa Ngombo kwa sababu Serikali

imesema tuhame, tumekubali kuhama, lile Bwawa la Mwalimu Nyerere limetumia hela nyingi sana na sisi tumekubali lakini sasa na sisi pia mtuangalie katika hali yetu ya maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu nataka kuzungumzia kuhusiana na wanyama hawa tembo. Jamani Mkoa wa Morogoro, ni Mkoa ambao tumepata bahati, tuna hifadhi nyingi, kuna Mikumi, kuna Selous, kule Udzungwa zote hizi zinazunguka Morogoro lakini wakazi wa maeneo haya jamani tunateseka na tembo. Tumeiomba Serikali, mtatumia mkakati gani kwa sababu leo wanasema kwamba watatumia sijui mbinu ya sasa hivi, lakini ukiwapiga sehemu moja, wanakimbilia sehemu nyingine, watu wanaumia, watu wanateseka, watu wanakufa. Serikali je, mmejipangaje kulimaliza hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali mlimalize hili ili wale watu kwa sababu kama Mkoa wa Morogoro mwaka huu ni mwaka ambao una matatizo, utakuwa na njaa sana kwa sababu ya mafuriko.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili hiyo.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yale mafuriko tayari na hapohapo tena na tembo wanakuja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili hiyo, ahsante.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, jiandae Mheshimiwa Matiko.

Mheshimiwa Issa Mtemvu, jamani mko Bungeni mko wapi humu? Ajiandae Mheshimiwa Neema halafu atakuja Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Nami natumia nafasi hii sana kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye nchi yetu ni dhahiri maendeleo tunayaona wazi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuwapongeza sana Mawaziri wangu hawa wawili, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri mwenye dhamana ya Fedha kwenye nchi yetu kwa maana ni mbobezi, Daktari na kama mtaalam wa eneo hili sina mashaka naye kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za ziada ziende kwa pacha wangu Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo na Waheshimiwa Manaibu wao wote. Kwa kweli Profesa unaweza ukamuona ni mtaalam wa masuala ya elimu lakini ameuvaa kama vile ni mchumi mbobezi kwenye eneo hili, kwa hiyo mimi naendelea kumpongeza sana na natambua sasa hivi anaendelea na kuandaa Dira ya Miaka ya 2050 tukiwa tunaendelea kukamilisha lengo la Dira ya 2025, namtakia kila la kheri kwenye jukumu hili alilonalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaendelea kupongeza tu katika maeneo mbalimbali kwenye bajeti hii. Kwanza mpango wenyewe na bajeti yenyewe, kwa kweli vimebeba kila jambo muhimu kwa Watanzania katika maeneo mengi sana, lakini kubwa kwenye hali ya umaskini na maendeleo ya watu ambalo linazungumzwa kwenye mpango. Tunatambua, kufikia lengo la Dira ya Taifa ya Mwaka 2025, Serikali imeendelea na jitihada mbalimbali za kuboresha pato la mtu mmoja mmoja lakini na pato la jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona takwimu zinaonesha, pato limeongezeka kutoka shilingi 2,800 mpaka shilingi 3,050. Hii maana yake nini, maana yake kama nchi imeendelea kuwa katika kundi la nchi zenye kipato cha kati cha chini. Kwa hiyo hii naendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa maana ameendelea kusimamia huu uchumi mpaka unakwenda katika njia ambayo kama Taifa, tunakuwa katika hali nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano, umetoa viashiria vingi vya kuonesha hali ya umaskini na maendeleo ya watu, tuko katika hali nzuri kama Taifa. Unaweza ukaona kwenye kutoa elimu ya msingi na sekondari bila ada. Sasa hivi Serikali inatumia zaidi ya shilingi bilioni 766.1, naendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwenye hili maana yake tunaendelea kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara za kufungua fursa za kiuchumi unaweza ukaona, ndani ya Jimbo langu pale ile barabara ya njia nane ambayo inatokea Kimara – Kibaha. Watu wanaweza wakashangaa, njia nane. Zamani tulikuwa tunakaa barabarani zaidi ya masaa kumi, hufiki Posta, lakini leo tunakwenda vizuri. Nami nampongeza sana Mheshimiwa Rais na naamini barabara hii imeshakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba sana Mheshimiwa Rais, wakati ukifika, aje aifungue barabara hii na wananchi wa Jimbo la Kibamba waweze kumuona na kumsalimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa vituo vya afya, hospitali, na zahanati nyingi na kadhalika, kila sehemu watu tumeona na jimboni kwangu tumefaidika sana kupata hospitali, lakini kupata vituo vya afya lakini na zahanati mbalimbali. Kubwa na ziada nimeona niliseme ni hili la kuongezeka kwa vyuo vya elimu ya juu, vya kati na vya ufundi stadi. Mheshimiwa Rais ana maono makubwa sana ya kuona wananchi wetu wanaondokana na umaskini lakini hali yao ya maendeleo inakua kupitia viashiria hivi vya mpango wetu wa tatu wa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ni hili la kuendelea na kuboresha upatikanaji wa huduma za maji mijini na vijijini. Sasa, kwenye eneo hili la maji, bado tunayo changamoto sana, juzi nilichangia na nikasema Mheshimiwa Rais katusaidia vyanzo vya kuhifadhia maji yaani matanki makubwa na sasa hivi linaendelea kujengwa lile la Bangulo kule Ilala la ujazo wa lita 9,000,000 ambalo litaendelea kutusaidia. Tunatambua chanzo chetu cha maji bado ni Ruvu toka mwaka 1967 tunafanya sensa ya kwanza, hadi leo mwaka 2022 tumefanya ya tano au ya sita, bado tuna hali ngumu ya usambazaji wa maji kwenye Jimbo la Kibamba.

Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, kwenye Wizara ya kisekta nilisema eneo hili, tunahitaji ukweli uwekezaji wa fedha pale Ruvu kwenye pampu lakini tuone vile vifaa vya maji vinapata maji wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nazungumza, zaidi ya miezi mitano wananchi wa Jimbo la Kibamba, kuyaona maji katika viunga vingi, hawana maji kabisa safi na salama, hawana maji. Jana nilichomoka hapa na Mheshimiwa Kundo nikaenda naye Msumi, wananchi wanaambiwa wachimbiwe visima, Dar es Salaam, ndiyo maana mimi huwa nasema Dar es Salaam vijijini hamnielewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameshatujengea Tegeta A lita 6,000,000, Goba ametujengea Mshikamano ujazo wa lita 6,000,000. Kuunganisha hizi, vinataka mabomba, mabomba tu, ni fedha, kwa nini hamzipeleki? Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakuomba sana, sana, msaidie Waziri wa Kisekta Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge, aweze kupata fedha hizi ili wananchi waweze kupata maji. Maji kwa maana ya usambazaji juu ya pampu mbovu, zitengenezwe pampu nyingine kama zipo, lakini vilevile fedha kwa ajili ya miundombinu mipya ikamilike Dar es Salaam Jimbo la Kibamba. Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana Waziri wangu wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ambayo mimi naiona kwenye eneo hili na namwambia Mheshimiwa Aweso, pampu ni moja, umeme kukatika katika kila siku tunaambiwa tu hili jambo, tujitahidi sana Mheshimiwa Waziri anayehusika na Nishati, namuona dada yangu yuko hapo na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pia anaweza akawa analisikia hili. Lakini kuna hujuma, hili naliseme, nimesema vikao vya ndani vinavyonihusu kwenye chama changu lakini na nje. Nataka kuwaambia, Wilaya ya Ubungo ile, hujuma ikiendelea hivi ni hujuma kubwa. Wananchi wasipoendelea kupata maji, tunaelekea kwenye Serikali za Mitaa, tutakutana na shida, nawaomba sana kama Serikali, mtusaidie wananchi wapate maji, hujuma zipo za kusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ruvu imejaa maji lakini wananchi hawana maji, kwa nini? Mheshimiwa Rais katujengea matanki ya kuhifadhia maji matanki yana maji lakini maji hayaendi kwa wananchi, kuna kusudi kubwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimeona sijui kama ni suala la muda, lakini naendelea kupongeza bajeti, katika maeneo mengi sasa hivi bajeti imekuwa ni nzuri, ni nzuri sana. Ziada la maslahi ya watumishi na wastaafu, mmeweka kikokotoo kizuri na malipo ya waliopandishwa vyeo lakini na masuala mengine. Nawashukuru sana, Serikali mmefanya jambo zuri sana katika eneo hili la watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema, jiandae Mheshimiwa Matiko, jiandae Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii ili mimi pia niweze kutoa mchango wangu katika Mpango huu na Bajeti hii ambayo imeweza kuwasilishwa ambayo tunaendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia natumia nafasi hii kuweza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameweza kuyatafakari maumivu ya watumishi wa umma ambao walikuwa wako kwenye kikokotoo cha asilimia 50, wakarudisha kwenye asilimia 33, na sasa amewapa wamekuwa asilimia 40. Hii inaashiria ni kwa namna gani Mheshimiwa Rais Mama yetu ni msikivu na anawapenda watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimwa Mawaziri, Mheshimiwa Waziri Mwigulu pamoja na Mheshimiwa Waziri Kitila Mkumbo na Naibu Mawaziri wao Mheshimiwa Chande pamoja na Mheshimiwa Nyongo. Mimi binafsi nasema, Wizara hizi zina watu ambao kwangu ninawaamini na ninawapenda sana, ninaamini ni watu ambao wamekuwa wakifanya kazi kubwa kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kazi ya kukusanya fedha na kutunza fedha siyo kazi nyepesi lakini wenzetu wamekuwa wakiendelea kupambana kuhakikisha nchi inasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutoa mchango wangu, kuna mambo ambayo natamani kuishauri Serikali yangu na ninajua sisi kama Waheshimiwa Wabunge kazi yetu sana ni kushauri kuliko kuikandamiza Serikali kwa maneno magumu. Ninataka kuongelea na ninarudi kwenye eneo la bidhaa zilizouzwa nje na bidhaa ambazo zimekuwa zinaingizwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatamani kuendelea kusisitiza kwamba, ipo haja ya kuweka mkakati maalum wa kuzuia kuingiza bidhaa nyingi nchini kuliko bidhaa tunazozitoa. Hii tunaweza kuifanya kwa kuipa mikakati Wizara zetu kutengeneza wasajiriamali mbalimbali wakubwa, wadogo ambao wataweza kutusaidia kufanya *export* kwa kuuza bidhaa zao au huduma zao nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ambayo imewasilishwa, tunaona kabisa kwa mwaka 2023 bidhaa zilizouzwa nje zilikuwa ni asilimia 8.8. Lakini kwa mwaka 2022, bidhaa zilizouzwa nje zilikuwa asilimia 9.1 na kwa mwaka 2021, bidhaa zilizokuwa zimeuzwa zilikuwa ni asilimia 9.4. Kwa hiyo kadiri miaka inavyozidi kwenda, tunaona kwamba kuna wastani wa asilimia 0.3 tunaendelea kushuka, sasa badala ya kupanda, sisi tunashuka. Kwa hiyo, eneo hili natamani kulikazia kwa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa ambazo tumekuwa tunanunua kutoka nje, tunaona kwa mwaka 2023, tuliweza kununua bidhaa nje kwa 17.4% ambapo kumekuwa na ongezeko la 3.9% kutoka mwaka 2022, kwa huduma ambazo tumenunua kutoka nje, tunaona kwa 2023 tulikuwa na 20.4% na kuna ongezeko la 4.8%. kitu ambacho tunaona kabisa kiwango chetu cha kununua huduma nje kinaongezeka kwa kasi sana kuliko sisi uuzaji wa huduma nje, kwa hiyo hili natamani Waheshimiwa Mawaziri na timu yao nzima waangalie namna ya ku-*control* eneo hili ili kuweza kulinda fedha za kigeni kwenye nchi yetu, pia

wanaweza wakatengeneza mikakati kupitia na Balozi zetu, wakashirikiana kufanya jambo hilo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itu kingine ambacho natamani kuweza kuongelea, kama Taifa tunahitaji kuona hali ya umaskini inashuka kutoka kwa mtu mmoja mmoja. Tumekuwa na programu ya *TASAF* kwa miaka mingi sasa lakini katika taarifa ya *TASAF*, hatuoneshwi ni watu wangapi ambao wameweza ku-*improve* kutoka hali ya umaskini kuja kwenye angalau kipato cha kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi natamani, kama nchi, kama Serikali yetu itakuwa ina nia ya dhati ya kupunguza umaskini kwa watu, ni lazima iwatambue hawa watu maskini kwa ujumla wao, ukiacha hawa ambao wako kwenye *TASAF* tu na kuwe na mkakati maalum wa kuwajengea uwezo kama maskini. Hizi programu tunazokuja nazo za jumla jumla labda mikopo, sijui nini, kilimo, sijui nini, yaani kama hizo programu sijui za vikundi na nini, tuainishe vikundi vya watu maskini *per se* kwamba hawa tunataka tuwatoe hapa, waende hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani ipo haja kama Serikali kuwatazama hawa watu wanaoitwa maskini kwa jicho la tofauti kwa sababu tunaweza tukawa tunadhani shida yao ni fedha, kumbe wana changamoto zingine ambazo zinawafanya waendelee ku-*stuck* pale walipo siku zote. Mimi binafsi nashauri kwanza hata hiyo programu ya *TASAF* ni kama iondolewe kwa sababu ndiyo inayoendelea kuwalemaza watu, inawafanya wasiwe na fikra pevu za kupambana kutafuta fedha, wanakaa wanasubiria hiyo shilingi 20,000 mwisho wa mwezi lakini kama tukiwatengenezea uwezo ambapo watapewa fedha, wakafundishwa biashara, kama ni kilimo wakafundishwa kilimo kizuri watapata fedha nyingi kuliko hiyo shilingi 20,000 wanayoisubiri kwa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ninachotaka kuongelea, ninataka kuongelea kwenye suala la ukusanyaji wa mapato. Ninafahamu Serikali inatamani iweze kukusanya fedha kwa 100% kama ilivyojipangia kwenye mikakati yake, lakini tunafahamu kuna wakati wanapata changamoto mbalimbali, wanashindwa kufikia malengo yao kama walivyojipangia.

Tunafahamu, kwa upande wa *TRA*, nataka kuongelea kwa upande wa *TRA* au maeneo yote ambayo unakuta kama ni Halmashauri, wamewaweka watu wakusanye mapato, wale watu wakusanya mapato huwa wanakuwa na fedha nyingi, kama nchi mimi sijui kama huwa tuna utaratibu wa kuchukua kuwajua kwamba kabla hajaingia kwenye eneo la ukusanyaji wa mapato, huyu mtu ana uchumi wa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, anapoingia kwenda kukusanya mapato baadaye, je huwa tunawa-*monitor* kwamba wamejiongezea pesa kwa kiwango gani? Kwa sababu tuwe wakweli, ukiajiriwa eneo la ukusanyaji mapato, hiyo ni fursa ambayo mtu anashangilia na wengi wamekuwa ni wezi, wengi wamekuwa ni watu ambao wanatumia mbinu wanavyoweza wenyewe kuweza kupata fedha isivyo halali na zinahalalishwa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo namuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie, watu wake wa *TRA*, watu wake wa Halmashauri wanaohusika na ukusanyaji wa mapato, tunaomba, wale watu watazamwe kwa macho mawili mawili ili waache kuwa na uharibifu wa kuzuia mapato yasiingie kwenye Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mfano tu mzuri wa magari tunayopaki pembeni mwa barabara. Kijana anakuja anakwambia haku-*scan* gari, anakwambia haa niachie hata ya maji. Sasa una-*imagine,* kama yeye anakuja anaomba hela ya maji na ana-*force* na changamoto iliyopo pale ni kwamba mimi nimepaki gari yangu ambayo inatakiwa ikusanywe hiyo hela kwa ajili ya *parking,* nawaza kwamba tu je, hili zoezi la ukusanyaji wa kodi tutafika kweli kwa *style* hiyo? Ndicho kinachotokea kwenye masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tukienda kwenye maduka mtu anakuhoji kabisa je, nikupe risiti au nisikupe risiti kwa bei ambazo yeye amezitofautisha. Kwa hiyo, sasa kama tunaweza kuajiri vijana wakawa wanawakamata watu ambao hawana risiti kwa nini tusitengeneze mfumo wa kila duka, kwa sababu maduka hayo tunayafahamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo *sites* za kibiashara zote tunazifahamu kwa nini tusitengeneze au tusiwe na ubunifu wa kutafuta mfumo ambao utakuwa unawa-*monitor* kila duka, ikiwezekana hata kwa nini tusianzie kuanzia muuza duka anapoingiza *stocks* zake dukani ili tuweze kufutilia hiyo hali.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema, ahsante kengele ya pili hiyo.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ok, kwa kumalizia naomba waitazame Mkoa wa Songwe kimkakati waje waangalie fursa za kiuchumi ambazo ziko pale.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko, jiandae Mheshimiwa Kakoso. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko samahani dakika moja.

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 40 wa Mheshimiwa Luhaga Mpina ambao ni wananchi kutoka Wilaya ya Meatu, Mkoa wa Simiyu, karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Matiko endelea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia fursa nami niweze kuchangia kwenye mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niseme naungana na maoni ya Kamati ya Bajeti ambayo wameyaleta hapa Bungeni na nitaomba Serikali iweze kuyachukua na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaenda kuchangia kwanza kabisa kwa kujielekeza kwenye Ibara ya 148 ambayo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri anaonesha Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta ambapo anaonyesha Sura Na. 220 kwa kuweka tozo ya shilingi 382 kwenye gesi asilia. Dunia kwa sasa wamejielekeza kwenye matumizi ya nishati safi na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa ni kinara wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa maana ya *clean cooking. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivi karibuni tulimuona akiwa Ufaransa – Paris kwa *the same thing.* Sasa, Serikali leo kuja kuweka hii kodi ni kama vile wanaenda kinyume, *you are going against the campaign* ambayo mmekuwa mkiifanya. Sasa hata dunia itatushangaa, kwa sababu kuweka kodi kwenye matumizi ya magari ya gesi asilia ambayo pia yanasaidia kuondoa uchafuzi wa mazingira kwa matumizi ya *diesel* na *petrol* inakuwa inachafua mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mki-*impose* hii kodi ina maana mnaenda kinyume. Rais ana-*advocate* hiki na dunia nzima inafanya hivyo, leo tena mnaleta hii kodi ambayo ita-d*iscourage* hata watu kuweza kutumia, kuweza kubadilisha na kutumia magari na hata wawekezaji kuweza kujenga vituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba wanatarajia kukusanya bilioni 9.5 kitu ambacho hakina uhalisia. Tunavyoongea sasa hivi tuna vituo viwili mama, kwa maana cha Ubungo na kile cha *Airport* ambacho ndiyo kinataka kianze kufanya kazi na kile cha *TAZARA* ambacho ni kidogo. Kituo cha Ubungo kwa tafiti nilizozifanya kwa mwezi wanauza tani 210 ambayo ni kilo laki mbili na kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiweka hata hiyo kodi yenyewe unapata sana milioni 962 kwa mahesabu ambayo

nimeyafanya kwa mwaka. Hatujui kituo cha *Airport* kitakuwa kinauza kiasi gani? Kituo cha *TAZARA* kile ni kidogo, sasa hayana uhalisia, kwa mara ya pili ni kwamba mpaka sasa hivi pamoja na kwamba imechukua miaka kumi na tano tangia tuanze huu mfumo wa matumizi ya gesi kwa Tanzania *it's only* magari 5,000 ambayo yameweza kufanyiwa *conversion* kwenda kwenye mfumo wa gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ambayo yameingizwa hata kumi hayafiki. Ukiangalia magari ambayo yameishaingia Tanzania ni zaidi ya milioni sita kwa maana haya magari ambayo tunayo sasa hivi ambayo yanatumia mfumo wa gesi ni *hardly* 0.083 *percent less than one percent*. Hasa unavyoenda ku-*impose* hii gesi ina maana una-*discourage* hata hao wenye magari waweze kubadilisha kwenye mfumo huu kwenda pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vituo vichache, hao wachache ambao 5,000 wameweka wanapanga foleni Dar es Salaam *over three hours* wanapanga foleni. Hii yenyewe tu *time-consuming* ina m-*discourage* mtu wa *pull out,* ukiweka na kodi ndiyo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kwa sababu tuna nia njema, gesi asili ni ya kwetu sisi *we are not importing it*. Tukiitumia gesi asili inamaana tutapunguza hata matumizi ya kuingiza mafuta na upatikanaji, yaani tutakuza shilingi yetu itakua zaidi kuliko ambavyo tunatumia dola kuweza ku-*import* mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikajaribu kwenda mbali zaidi kufanya ulinganisho basi hata wa kiuchumi maana yake kimazingira tumeona. Tukienda hata kichumi sasa wanakwambia kilo moja ya gesi ni sawa sawa na lita 1.7 ya *petrol* lakini kilo moja ya gesi *as of June* inauzwa shilingi 1,550 wakati *petrol* kulingana na *EWURA* waliotoa tarehe 5, Juni wanauza 3,261 kiuchumi kabisa ukifanya *correspondence analysis* hapo, 1,550 ni sawa sawa na shilingi 5,543 kwa ambao wanatumia *petrol. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona gharama za maisha ni kubwa sana kwa sababu ya kupanda bei za mafuta. Usafirishaji

unakuta vyakula vinakua juu, bidhaa za ujenzi zinakua juu hata raia tu wanatumia bei za gharama, nauli zimekua juu sana. Nikaenda mbali basi, hawa watu wetu wa *Bolt* na *Uber* ambao wana IST wenyewe wakiweka kilo moja ya gesi wana uwezo wa kwenda kilomita 25 mpaka 30. Wakati wakiweka *petrol* wanaenda kilomita 12 mpaka 18 *so economic wise* gesi lazima tui-*advocate* iweze kutumika na ni mali yetu hapa hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima kama nchi badala ya kuweka hizi kodi twende mbali zaidi tuhamasishe ujenzi wa vituo vya gesi. Leo ukiweka kodi mimi kama Mwekezaji nilikuwa nataka kuwekeza kwenye kujenga kituo cha gesi nita-*pull out* sina uhakika na soko la gesi tena kama magari yatakuja yatakuwa mengi. Sasa ili kuhamasisha lazima tuondoe kodi tuweke *public awareness* ili watu wote haya magari milioni sita walau yafike 30 *percent* ambayo yamekuwa *converted* kwenda gesi ili sasa tuweze kupata wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hao wawekezaji napendekeza tuwe walau *after* kilomita 150 kwenye hizi barabara kuu za kwenda Mikoani na Wilayani kuwe na kituo cha gesi ili sasa Wanatanzania wengi waweze kuhamasika, waweze kuwekwa wakijua nikitoka Dar nitafika sehemu fulani nitaweka mpaka nafika Tarime nina uhakika gari yangu nitakuwa naweka mafuta mpaka nafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kuhakikisha sasa hata Serikali kwa mfano pale Dar es salaam ndiyo tuna hivi vituo, kwa tafiti zangu nimeona kuna magari ya taasisi mbalimbali za Serikali takribani 2,000 ni magari ya *petrol*, kwa nini msiweke wawe katika mfumo wa gesi, *you lead by example!* Sasa hivi tunavyoongea ni gari moja tu la Serikali ndiyo ambalo lina mfumo wa gesi. Kwanza ukiweka hivyo utapunguza na matumizi ya Serikali ukitumia mfumo wa gesi kama ambavyo nimeanisha mwanzoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhakikishe kwamba tunabadilisha magari ya *diesel* ambayo mengi ni mabasi na malori kuja kwenye mfumo wa gesi. Imekuwa kuna *bureaucracy*. *DIT* walipata mshirika kutoka Poland Kampuni ya *EPI Gas* ambao walikuwa

wapo tayari kuja Tanzania washirikiane na *DIT* ili kuweza sasa kubadili na magari ya mfumo wa *diesel* kwenda kwenye gesi lakini kukawa na *bureaucracy* nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wamefatilia mambo ya Nje ili waweze kufanya *vetting* kwa maana uhalali wa ile kampuni wakaambiwa wapeleke sijui watumishi kule Poland hawana huo uwezo, lakini hapa Tanzania tuna Ubalozi wa Poland ambao ulifanya *verification* na ukasema ile kampuni ni *reliable* imekuwa kwenye masoko zaidi ya miaka 25 na wana ujuzi wa kutosha na wana *interest* ya kuja kushirikiana na *DIT* ili tuweze ku-*convert* magari ya *diesel* yaweze kwenda kwenye gesi ili sasa tuweze kutumia gesi zetu kwa nini mna *deal dully* au kuna *interest* ya watu ambao wamewekeza kwenye mambo ya mafuta na *diesel* hawataki watanzania waweze kunufaika, kwanza ni *cheap environmentally friendly* na itapunguza sana na italeta ajira nyingi kwa nini tuna- *hesitate* katika hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kupunguza kodi ya vipuli ambavyo vinatumika ku-*convert* kutoka kwenye *petrol* kwenda kwenye gesi na kwa baadaye kama tutaenda kwenye *diesel* kutoka kwenye *diesel* kwenda kwenye gesi. Tukipunguza ile ita-*attract* watu wengi waweze kubadilisha magari yao kuja kwenye mfumo wa gesi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nampongeza mchangiaji kwa mchango wake lakini naomba kumtaarifu kwamba ku-*convert* magari haya kwenda kwenye mfumo wa *gesi* tayari tupo kwenye *process* za kwanza. Kwa sababu hata Dangote ameanza ku-*convert,* kwa hiyo, napenda tu kumpa taarifa tayari tunafanyia kazi. Hata hivyo, tumefanya jitihada sana kubwa kwenye vituo kufikia mwakani tutakuwa tuna jumla ya vituo 30 na *conversion centers* zile ziko

nane na siyo tano. Tunafanya kazi kubwa kuhakikisha tunapiga hatua, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko, taarifa hiyo.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu hata, walikuja wakatupa semina hapa mwaka jana Novemba, kwa hiyo, nimetumia kabrasha lao la semina mwaka jana Novemba, Wizara hii hii ya Nishati ilileta wadau, nikaongeza tafiti zangu kuanzia mwaka jana Novemba mpaka sasa hivi. Sasa mdogo wangu Mheshimiwa Naibu Waziri *just take note* na mhakikishe mna-*implement for the betterment* ya watanzania na Taifa letu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemaliza hapo kwenye mambo ya gesi. Kwenye *Finance Act* Ibara ya 69 (a) na (b) wameleta hii tozo kwa hiyo nitaleta marekebisho ya sheria kuondoa kabisa hii tozo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili hiyo.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo kengele ya kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *no no!* Ulianza 22, tazama saa ile pale. Mheshimiwa Matiko, kengele ya pili kaa chini.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mengine kikokotoo na nini nitaandika kwenye mchango wangu wa maandishi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kunipa nafasi ya kuwa sehemu ya wachangiaji kwenye bajeti kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa kuleta miradi ya maendeleo mingi kwenye Mkoa wa Katavi na Wilaya ya Tanganyika ambako wananchi wamenufaika sana kwa miradi ambayo imeletwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ninawashukuru sana Serikali kupitia Waziri wa Fedha kuondoa sehemu ya miradi ya maendeleo iliyopo kwenye mamlaka ya bandari. Kamati ilishauri sana juu ya *wharfage* mmeisikiliza na mmeona umuhimu sasa wa kuachia bandari iweze kutengeneza mifumo ambayo wataendeleza miradi endelevu, hilo tunaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali kwenye eneo la Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, eneo hili ni muhimu kama walivyoachia *wharfage*, tunawaomba na eneo la viwanja vya ndege kwenye *passenger service charge* wawaachie ili waweze kujiendeleza. Hili mtakuwa mnawaonea kwa sababu Mamlaka ya Anga wanachukua fedha zote *KADCO* wanachukua fedha zote, mliowapa dhamana ya kusimamia viwanja vyote mnawawekea kipingamizi. Niombe sana eneo hili mlifanyie kazi ili kuruhusu Mamlaka iweze kufanya kazi ambayo itawasaidia wananchi na kuweza kuhudumia viwanja vya ndege ambavyo viko chini ya mamlaka husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kodi ambazo zimependekezwa kwenye Wizara ya Kilimo. Mimi sioni sababu ya kugombana na wakulima nchini, tunaenda kutafuta migogoro ambayo kimsingi haitatusaidia sisi, wananchi na Serikali kwa ujumla. Kodi ambayo imependekezwa hasa kwenye *AMCOS* tunaenda kutafuta mgogoro mkubwa sana. Naishauri Serikali yangu eneo hili kwa mapato yanayozidi shilingi milioni 11, hili msilijaribu kulifanya kwenye utekelezaji italeta shida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkumbuke mkulima huyo kwenye *withholding tax* analipa 2%, kwenye *cess* ya Halmashauri analipa tatu, *export levy* analipa 0.25% lakini mnakuja tena na gharama hiyo mnayoipendekeza ya makato ya pato ambalo mkulima akizalisha mapato yakizidi milioni 11 mnamkata kodi. Hili eneo Mheshimiwa Waziri utagombana na wakulima wa pamba,

mnaenda kugombana na wakulima wa korosho , wakulima wa chai, wakulima wa kahawa, nchi nzima itaingia kwenye tafrani kwenye eneo hili na mapato siyo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili uliangalie kwa kina ili tuweze kuwasaidia hawa wakulima, ukumbuke kwenye eneo hili la kilimo mkulima huyo anatoa gharama kubwa kupitia kwenye pembejeo analipa kodi, ambazo ziko kwenye kodi ya pembejeo. Kwa hiyo, mtaangalia maeneo haya myafanyie kazi ili tusije tukawaingiza kwenye tafrani kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri maeneo ambayo mnaweza mkapata fedha za kodi ambayo ipo na mnaweza mkaifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilichangia juu ya uvunaji wa *carbon credit,* nchi yetu ina misitu mingi, tuna misitu zaidi ya hekta milioni 48 ambayo haijafanyiwa kazi vizuri, mkiielekeza kwenye eneo hili mnaweza mkapata mapato makubwa sana. Eneo hili pekee Mheshimiwa Waziri mkifanya utafiti mkashirikisha taasisi ambazo zinasimamia maliasili mnao uwezo wa kupata karibu trilioni tisa mnaweza mkazipata na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba eneo hili Mheshimiwa Waziri mkalifanyie utafiti na muandae wataalam watafute masoko ambayo watatumia kwenye maeneo ya uwekezaji kwenye sekta ya maliasili ikiwemo misitu inayomilikiwa na Serikali na hifadhi ambazo ziko chini ya Taifa letu. Nina ushahidi juzi Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika kwa hekta chache sana ambazo zinavuna hewa ya *carbon* tumekabidhiwa kila kijiji bilioni moja sawa na shilingi bilioni 14 ambazo zinapata kupitia vijiji vinane. Kwa hiyo, naamini kwa nchi nzima ambayo imezungukwa na misitu tukiitumia vizuri tunaweza tukapata fedha ambazo zitaendesha na kusaidia bajeti yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na shida ya kila mwananchi au Mbunge ambaye yuko humu anazungumzia tatizo la barabara. Ili tuweze kupata fedha za kujenga miradi ya Barabara ni lazima tuhakikishe tunawasadia *Road Fund*

wanapata fedha za kutosha. Fedha hizo ndizo zitakazokuja kutengeneza barabara ambazo zimepotea, barabara nyingi zimeharibika kwa sababu zina muda mrefu, naomba Serikali kwa mahitaji ambayo yapo Mfuko wa Barabara unahitaji trilioni mbili ili uweze kusimama na kutengeneza barabara ambazo zimeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo fedha ambazo tumepitisha kwenye bajeti trilioni 1.7 ambazo asilimia kubwa zitaenda kulipa madeni ya wakandarasi, naishauri Serikali na Wabunge wenzangu ili tuweze kuwasaidia wananchi na sisi Wabunge ambao tuna miradi mingi ambayo imesimama ni vyema tukatunisha mfuko wa barabara ili ule mfuko wa barabara uweze kuja kutengeneza barabara zilizoharibika na sehemu ya fedha itakayobaki ianzishe miradi mipya ambayo itafanya kazi ya kujenga barabara hapa nchini. Maeneo haya ni muhimu sana kwa ajili ya kuwasaidia wananchi na miradi ambayo Serikali inaitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe kwenye eneo jingine najua ni kengele ya mwisho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili hiyo…

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, awamu ya mchana imekamilika panapo majaliwa jioni tutaanza na Mheshimiwa Stella Fiyao, Condester Sichalwe, Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mheshimiwa Butondo, Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mheshimiwa Kasaka Njelu, Mheshimiwa Yustina Rahhi na Mheshimiwa Dkt. Chaya.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka Saa Kumi na Moja jioni leo. *(Makofi)*

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**24 JUNI, 2024**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**na**

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano, Tutaanza na Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wametajwa awali, halafu wengine wataendelea kutajwa kadri muda unavyokwenda.

Mheshimiwa Stella Simon Fiyao atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mheshimiwa Leah Komanya ajiandae.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hizi muhimu, Wizara ambazo ni *engine* ya maendeleo ya Taifa letu. Tunatambua umuhimu wa Wizara hizi na tunajua bila Wizara hizi hakuna kitu kitasogea.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na *issue* ya Barabara, natamani kujua mpango wa Serikali ni upi kwenye ujenzi wa barabara. Ninajua kwamba, Serikali ilikuwa na mpango na ilikuwa imefika hatua fulani kwenye barabara ya kutoka Igawa – Tunduma, hasa kwa kujua kwamba, barabara hizi zilikuwa katika

mpango wa *EPC+F* na mitakaba ilikuwa imesainiwa tayari, lakini kutokana na hali tunayoiona ya kukwama kwama kwa miradi ya *EPC+F*, nataka kujua mpango wa Serikali ni upi kuhakikisha barabara hizi zinajengwa kwa wakati, hasa ukizingatia changamoto kubwa ambayo wananchi wa Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Songwe tumekuwa tukikutana nayo, ikiwa ni pamoja na mrundikano wa malori makubwa kutoka Bandari ya Dar es Salaam, pia na ajali nyingi ambazo zimeendelea kujitokeza na kupoteza mamia ya Watanzania katika ile Barabara ya kutoka Igawa – Tunduma?

Mheshimiwa Spika, nataka kujua mkakati wa Serikali ni upi hasa kwa kuwa tunaona *issue* ya *EPC+F* kuna mkwamo mkubwa. Natamani kujua mkakati wa Serikali ni upi ili kuhakikisha barabara hii inajengwa kwa wakati na kukomboa wakati? Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nilikuwa nataka nipate ufafanuzi ni suala la kodi. Sisi sote tunajua ya kwamba, mtu anatakiwa atoe kodi kutokana na faida anayoipata kwenye biashara yake, lakini kumekuwa na changamoto kubwa ambazo wananchi wamekuwa wakikutana nazo. Mwananchi anatakiwa kutoa kodi pale anapofungua biashara yake tu. Sasa unaanza kujiuliza huyu mwananchi anakuwa amezalisha saa ngapi, mpaka wakati wa kufungua biashara anatakiwa kulipa kodi. Jambo hili limekuwa likiwatesa sana wafanyabiashara wengi, limekuwa likiwaumiza sana. Mimi nataka kujua kwa nini kodi idaiwe mapema wakati mfanyabiashara bado hajafanya biashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni muhimu kama mtu anafungua biahsara *either* duka au biashara yoyote, afike mahali auze apate faida halafu Serikali ndiyo iende kudai kodi, lakibni kwa *style* inayoendelea huko mitaani ni rahisi sana wafanyabiashara wetu kufilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa na mimi nataka nipate ufafanuzi, kuna kitu ambacho mimi najiuliza sana. Hivi kweli sisi Tanzania ni maskini? Hili ni jambo ambalo mimi najiuliza sana, nimesoma taarifa ya mpango nimeona, lakini

nabaki kujiuliza hivi kweli Tanzania nchi yetu ni maskini ya kiwango kinachotajwa humu kwenye hii taarifa? Kama kweli ni maskini hizi rasilimali tulizonazo ndani ya nchi yetu zinatusaidiaje kutukomboa kutoka kwenye hiyo hali ya umasikini ambayo inatajwa miaka nenda rudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania imepata uhuru Mwaka 1961. Lengo la kupata uhuru ni kujikomboa kupata uhuru. Lengo lilikuwa ni kujikomboa. Kama lengo lilikuwa ni kujikomboa mimi ninachokiona hapa ni kweli tumeweza kuwaondoa hao watawala waliokuwa wakitutawala kimwili lakini kifikra bado wanatutesa. Haiwezekani leo nchi yetu ambayo inatajwa kuwa na rasilimali mbalimbali inakuwa miongoni mwa nchi maskini Afrika, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wakati ninapata mashaka ni lini tutajikomboa kutoka kwenye hizo fikra za umaskini, ili tujione kwamba nchi yetu ni tajiri kutokana na rasilimali nyingi tulizonazo. Haiwezekani leo Tanzania kutajwa kuwa miongoni mwa nchi maskini wakati tuna madini mbalimbali ambayo yapo ndani ya nchi yetu. Tuna rasilimali za kutosha, wanyama, mbuga za wanyama maeneo mengi mbalimbali za kuvutia ambazo watu wanatoka maeneo mbalimbali kuja kutazama wanyama ndani ya nchi yetu, lakini Tanzania inakuwa miongoni mwa watu maskini. Mimi nakaa mahali najiuliza ni lini tutatoka katika fikra hizo za kutawaliwa ili tufike mahali tujiendeshe wenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo watu wanapiga kelele hapa tunazungumzia masuala ya ushoga na uasagaji, kuna vitu havitaondoka kwenye Taifa kama tutashindwa kubadilisha fikra zetu na kujua ya kwamba, Tanzania tunaweza hata bila kuwezeshwa. Rasilimali tulizonazo zinaweza kutufanya kuwa matajiri kwa sababu tunafika mahali tunaona hata hao watu ambao tunategemea maeneo mengine mikopo na mambo mengine kutoka kwao, utajiri wanaoendeshea nchi zao wanachukua Afrika na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni madini ya Tanzanite. Madini ya Tanzanite ni madini pekee ambayo yanapatikana Tanzania peke yake dunia nzima, lakini turudi kwenye hali halisi,

nchi zipi ambazo zinaongoza kuuza kwa Madini ya Tanzanite, utaona Kenya na maeneo mengine. Kwa nini sisi Tanzania ambao ndio wazalishaji wakubwa wa haya Madini ya Tanzanite hatuoneshi kuwa kipaumbele kwenye suala zima la biashara ya Tanzanite. Kwa nini? Maana yake kuna sehemu tunafeli kifikra, hatujakubali kujikomboa kutoka kwenye wimbi la umaskini na kubadilika kujiona sisi ni matajiri na tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukiangalia Bunge hili toka tumeanza wiki nzima tunazungumzia *issue* ya sukari, lakini ukijiuliza hivi kweli Tanzania hatuna ardhi na mabonde ya kutosha ambayo tunaweza kulima miwa na vitu mbalimbali vikatuzalishia sukari, kweli hatuna? Kama tunavyo ni kitu gani ambacho kimetufikisha hapa leo tunajadili *issue* ya sukari kuagiza kutoka nje na wakati hata Tanzania tunaweza kuzalisha sukari ya kutosha, kutosheleza nchi nzima na tukaitoa nje ya mataifa mengine ni wapi tunakwama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachotukwamisha ni fikra zetu zilizotawaliwa ambazo bado zipo chini ya utumwa. Ni lazima kama Tanzania tukubali kubadilika, utafika wakati wajukuu na vitukuu vyetu watatamani kupiga viboko makaburi yetu. Maana wataona kama tulifeli kwenye eneo fulani. Leo tunajadili sukari wiki nzima, kwa nini tusijadili tunaanzaje ili tuwe na viwanda vya kutosha ndani ya nchi, tuwe na miwa ya kutosha kwenye maeneo mbalimbali ambayo inaweza kuzalisha sukari ya kutosha nchini, hata tukaweza kuuza kwenye mataifa mengine?

Mheshimiwa Spika, leo hii tunatumia fedha nyingi kuagiza vitu nje ya nchi wakati hata Tanzania tunaweza kuzalisha, haiwezekani. Ni lazima tukae chini tutafakari ni wapi tunakwama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye *issue* ya mauzo ya bidhaa za nje utaona namna ambavyo tunafeli. Taarifa inaonesha kwamba, kwenye bidhaa za mauzo toka nje kwa miaka 5 mfululizo sekta imechangia kwa asilimia 17.1 miaka 5 mfululizo, maana yake hatujafika hata kwenye lengo la kuchangia ile asilimia 24. Sasa unaanza kujiuliza hivi hizo sekta hazina wataalam ambao waliona mwaka wa kwanza, mwaka

wa pili, mwaka wa tatu, mwaka wa nne mpaka mwaka wa tano tunafeli wakashindwa kushauri ni wapi tunakwma na tuanzeje ili tusogee mbele. Hii ina maana kuwa hata kwenye hizo sekta tuna watu ambao ni mizigo na wavivu wa kufikiri hawawezi kulishauri Taifa kwamba ni wapi tunakwama tifanye nini na tusogee mbele. Pia, hao ni watu ambao wanalipwa kodi za watanzania na wanashindwa kuishauri Serikali ni kitu gani tufanye ili tutoke kwenye mkwamo wa kukwama kwenye mauzo ya bidhaa nje ya nchi, hii haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwa na watu mizigo kwenye sekta mbalimbali ambao wanashidwa kulisaidia Taifa kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine. Leo hii tunazungumzia mpango, utakuwa mpango hauna maana kama tutajadili hapa mpango ukiletwa kwenye makaratasi, halafu ukashindwa kupelekwa kwenye uhalisia kwa maana ya kufanyiwa kazi, bado hili Taifa tutaendelea kupiga kelele kwamba sisi ni maskini na tutashindwa kutoka hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, kama tuna watu ambao wamewekwa kwa ajili ya kushauri na kulitumikia hili Taifa, basi watimize majukumu yao kuhakikisha tunatoka tulipo na tunaenda maeneo mengine maana hawa watu wanalipwa kodi za watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye *issue* ya vitu au bidhaa ambazo tunanunua kutoja nje kuleta ndani ya nchi, kuna mahali utajiuliza hivi kweli Tanzania ni wapi tunakwama? Ukiangalia kuna baadhi, unakuta hata mafuta ya kupikia tunaagiza kutoka nje kuyaleta ndani. Sasa ukikaa kujiuliza hivi kweli Tanzania hatuna ardhi ya kuzalisha mbegu zinazoweza kutoa mafuta kwa wingi na kuwahudumia wantanzania? Kama tu kwenye *issue* hiyo tunakwama na ukiangalia kwenye mpango wa Wizara ya Kilimo utaona ardhi iliyotumika ni kidogo kuliko iliyopo. Wapi tunakwama? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, kwa nini hizo fedha zinazopeekwa nje kwenda kununua bidhaa na kuletwa ndani zisitumike kuwawezesha watanzania ili bidhaa zizalishwe kwa wingi na mwisho wa siku tuziuze nje kwa mataifa mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii adhimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miradi yote ya maendeleo ambayo tumepata ndani ya Jimbo la Momba pamoja na Mkoa mzima wa Songwe, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye kushauri namna ambavyo sisi kama Taifa tunaweza tukatumia rasilimali ambazo tumepewa na Mwenyezi Mungu, kuongeza vyanzo vya mapato. Rasilimali zile zile ambazo tumepata tunaweza tukatumia kuongeza vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kwenye huo ushauri naomba niongelee eneo dogo. Waziri wa Mipango kwenye hotuba yake alikuwa ameongelea namna ambavyo mipango izungumzie namna ya kuwaendeleza watu ambao wanaishi kijijini. Uendelezaji wa maisha ya watu wa vijijini. Sasa hivi tupo kwenye karne ya 21 lakini mpaka tunavyoongea sasa ni zaidi ya watanzania 80% bado wanalima kwa kutumia jembe la mkono. Kwa kuwa mpango unasema kwa ajili ya kuwawezesha watu wanaotoka vijijini na shughuli yao kubwa ni kilimo na shughuli nyingine kama ufugaji. Tunaomba mikopo kwa wakulima waliopo kule vijijini waweze kuwezeshwa ili waweze kuondokana na kutumia jembe la mkono na hata hayo mafuta ya kupikia

ambayo tunaagiza nje, kama wakulima waliopo vijijini wakawezeshwa mikopo wanaweza wakasaidia kuzalisha mbegu nyingi za alizeti na sisi tukatoa mafuta nje ya nchi badala ya kuagiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa kuongelea uwezo wa watu hawa wa kawaida waliopo vijijini pamoja na mijini. Nimekuja na fomu moja hapa kutoka kwenye shule yako moja pale Mbeya Mjini, Shule ya Kata inaitwa Sinde *Secondary School.* Ndiyo nakusemea kidogo mdogo wako na watu wengine. Sera yetu ya elimu bila malipo naona kama inakinzana na uhalisia uliopo mtaani na kwa wazazi.

Mheshimiwa Spika, ninayo fomu hapa ambayo inasema maelekezo ya kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule za Sekondari Tanzania. Fomu hii ni ya mwanafunzi ambaye ametoka shule ya Kata anakwenda Nsimbo *Secondary School* kule Katavi, nitakupatia fomu hii uweze kuipitia. Nikianza kwenye orodha ya kwanza waliokuwa wameorodhesha vitu mpaka (xxi), mwanafunzi huyu mambo yake binafsi ambayo yanamuhusu inabidi anunuliwe na wazazi, yanazidi zaidi ya shilingi 200,000. Ukienda kwenye kipengele kingine cha pili kwa sababu ya muda nataka kuongea vitu vingi, vitu vilivyoorodheshwa mpaka (xxii) ambapo kwenye hiyo kuna mpaka vitabu vya masomo ya tahasusi husika, mzazi inabidi anunue.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tumesema elimu bila malipo. Basi mimi nilikuwa nafikiri TAMISEMI tuwambie wazazi ukweli kwamba, tunaomba mfanye kazi kwa bidii ili muweze kumudu mahitaji ya watoto wetu, kwa sababu kauli ya Mheshimiwa Rais ambayo alisema amefuta ada kutoka *kindergarten* mpaka *form six* mbona inakinzana na huu uhalisia? Sasa, nguo za mtoto mzazi anunue mpaka vitabu vya kufundishia, haya mambo kwa kweli yanakinzana kabisa na sera yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaondoka kwenye hilo eneo ni mwanafunzi huyo huyo mmoja, mimi nikiwa nasoma kule *o-level* ada ilikuwa shilingi 40,000 baadaye ikashuka ikawa shilingi 20,000. Hapa kuna michango mingine mbalimbali amewekewa mwanafunzi ambaye atakaa bweni. Mchango wa uendeshaji wa

shule shilingi 65,000, tahadhari shilingi 5,000, nembo shilingi 5,000, kitambulisho shilingi 5,000 jumla shilingi 80,000 na amewekewa akaunti ya shule aweze kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ni elimu bila malipo huu tena mchango wa kuendeshea shule unatoka wapi? Sasa hiyo elimu bila malipo ni ipi? Mimi nafikiri hakuna sababu sisi tunaweka sera wenyewe halafu inakinzana na uhalisia. Mimi nafikiri liwe jambo moja, *either* michango yote iondoke mzazi amnunulie mtoto wake mahitaji tu kama *uniform* na vitu vingine, lakini hata *ream paper* mtoto anatakiwa akazikute shuleni kwa sababu ni elimu bila malipo, lakini ikiwa uhalisia ndio huu tuifute hii kauli ya kusema elimu bila malipo kwa sababu inakinzana na uhalisia na hatuna sababu ya kujitekenya halafu tunacheka wenyewe. Naondoka kwenye hili eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ulishasema mambo ya sukari ya yakajadiliwe na Kamati ya Maadili ila kwa sababu watumia sukari ni wanyonge. Unajua kuna watu wapo nchi hii *whether* wawe ni wafanyabiashara au ni watu ambao Mungu amebahatika kuwapa nafasi mbalimbali. Unajua wasiwafanye wenzao ni kama hawajui kabisa wanachokfanya. Kuna watu kwenye hili sakata la sukari wanajijua kabisa wanachokifanya mwanzo mwisho wanajua, lakini hapa tutaenda mpaka watu watagombana. Ma-*deal* yao ambavyo wanavyofanya wanajua wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Condester nasema hivi Mungu wa Isaka na Yakobo tunaomba watu hawa akutane nao kwa sababu siri za moyoni mwao wao wanajua wanachokifanya, mipango na madili yao wanafahamu na mimi nitumie nafasi hii kumuomba Waziri wa Kilimo. Maadam alisema mbele ya Bunge Tukufu hapa kwamba, wale ambao aliwaruhusu waingize sukari hapa nchini, aliwaondolea kodi, tunaomba basi tuone sukari sasa hivi ishuke mtaani, kwa sababu mpaka sasa hivi bado sukari ni bei ghali.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sukari iuzwe kuanzia shilingi 1,500 mpaka 2,000 kwa sababu watu hawakulipa kodi. Sasa kama zile hela ni kweli walipunguziwa kodi na ilidibi tuzipate sukari

ishuke, ili tuone huo uhalisia *otherwise* kwa sababu moyoni mwao wanajua tunaomba tu Mungu anayejua mambo ya sirini akutane nao, maana yake hapa watu watashinda tu kugombana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapotaka kuongelea vyanzo vya mapato, tumwombe kwanza Waziri wa Fedha, kuna kipindi baadhi ya Wizara za Kisekta wakati zinachangia hapa, ziko Wizara ambazo pia Wabunge walikuwa wanashauri kwamba wamewekewa bajeti ndogo, Wizara mojawapo ni pamoja na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, mimi nimepata kuhudumu kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali kule, pamoja na kiwango kidogo ambacho Wizara wanatengewa lakini tumwamini *CAG*, *CAG* ni Mtanzania huyu ambaye ameteuliwa na Mheshimiwa Rais ili afanye kazi ya kukagua hesabu. Pia, *CAG* anapoleta taarifa akienda kwenye taasisi yoyote, ana *entry meeting* na *exit meeting*, kwa hiyo, wakati mwingine tusijifiche sana kwenye kile kichaka ambacho *CAG* anawapa watu Hati Safi. Wanapewa Hati Safi kwa sababu walifuata utaratibu, lakini kuna watu wanajua kuiba kwa kufuata utaratibu, yaani kafuata utaratibu lakini kaiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niombe kwamba, kwanza Mheshimiwa Waziri pamoja na kiwango kidogo hiki ambacho Wizara za Kisekta zinatengewa, wajitahidi kwanza kuziba mianya yote ya upotevu wa pesa ambayo *CAG* anairipoti, ndipo itatusaidia hata hiki kiwango cha pesa ambacho tunakiona ni kidogo, kinaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye vyanzo vya mapato; sisi kama nchi tumebahatika kupakana na nchi nyingi na katika hili nitaendelea kuliongea kila wakati na kulihubiri kila wakati. Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu, tunakushukuru mwaka 2021 uliweza kufanya ziara kwenye Jimbo la Momba na tukaonyesha kukupa sifa kwa nini tunatamani tupate geti la pili kutoka kwenye mpaka wa Tunduma. Nchi ya Tanzania kwa kupakana na Nchi ya Zambia, nyuma yake kuna nchi nyingine zaidi ya nane. Sasa, litakuwa ni jambo la kusikitisha na kushangaza kwamba, pamoja

na nchi nyingi ambazo ziko kule nyuma, tuna geti moja tu, geti moja tu. Kwa hiyo, inawezekana urasimu wote unaofanyika Tunduma, magendo yote ambayo yanapita ni kwa sababu; tungeongeza geti la pili, macho yakaongezeka kuwa mengi ingewezekana kuongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ni ukweli usiofichika, mahali kote ambao kuna biashara za mipakani kumeonekana kuchachua sana uchumi wa maeneo hayo. Benki zimekuwa zikifanya biashara nzuri, hoteli zimejengwa mahali hapo lakini hata wananchi wa kawaida wamekuwa wakijiajiri kwenye sekta zisizo rasmi kupitia hiyo mipaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niendelee kukuomba Mheshimiwa Waziri, kuna haja tena kuona namna ambavyo geti la Tunduma linapaswa kuongezeka kwa kutumia Geti la Momba, kwa sababu hata ule upande ambao tulienda kukuonesha geti, wenzetu wa Zambia kwa sababu barabara ile ndiyo inaenda *DRC* kirahisi, wameweza kuweka *Toll Gate*, kwa hiyo, maana yake ni eneo la kimkakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa; kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. CONDESTER M. SICHWALE:** Mheshimiwa Spika, dakika moja tu namalizia kwenye chanzo cha mapato.

**SPIKA:** Sekundi 30 badala ya moja.

**MHE. CONDESTER M. SICHWALE:** Mheshimiwa Spika, kwenye chanzo kingine cha mapato, ni muhimu nchi ninarudia tena, tujenge barabara kutoka upande wa Tanzania kule Kalema kwenda *DRC*, kwa sababu tunapoteza mapato mengi sana kwa kuiacha nchi ya *DRC* kufanya nao biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *China* wameshafanya, Kenya hatupakani nao kwa pamoja lakini wanafanya biashara kubwa na kujiongezea mapato, sisi kama nchi tunasubiri nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo na Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa maoni yangu katika hoja iliyoko mbele, pia ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili niweze kuchangia. Ninaungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya katika sekta mbalimbali, kazi kubwa imefanyika ikiwemo katika Jimbo la Meatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Afya, yapo mafanikio makubwa ambayo yamefanyika katika Sekta ya Afya ikiwepo kuongezeka kwa vifaatiba vya kisasa vya uchunguzi na ugunduzi wa magonjwa. Kwa mfano, zimenunuliwa *Digital X-Rays* 346, *Ultrasound Machines* 677 lakini pia zimenunuliwa mashine za ku-*scan*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ameboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya na ujenzi wa vituo zaidi ya 1324, ikiwemo Jimbo la Meatu, tulipatiwa kituo kimoja lakini bado hakijakamilika. Ninaamini Serikali itakamilisha ujenzi wa kituo hicho ili wananchi waweze kukitumia, waweze kunufaika kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Rais kupitia Wizara ya Fedha ameipatia Bohari Kuu ya Dawa mtaji wa shilingi bilioni 100. Ninaomba niungane na uchambuzi wa Kamati ya Bajeti kwamba, Bohari ya Dawa iendelee kupewa mtaji ili iweze kumudu majukumu yake. Iweze kununua dawa na kuwepo na *stock* ya dawa, isisubiri dawa zinapohitajika ndiyo iende kutafuta, dawa zinapohitajika ziwe zimeshanunuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iendelee kulipa madeni ya Washitiri, iendelee kulipa madeni ya Bima ya Afya ili Bima ya Afya iendelee kujiendesha vizuri. Serikali iendelee kutoa vibali vya ajira; bado tuna upungufu mkubwa katika maeneo

yetu ya kutolea huduma ya afya katika zahanati, vituo vya afya pamoja na Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, binafsi mimi nilikuwa ninaomba Bima ya Afya ya Watoto iweze kurejeshwa wakati Serikali inafanya mipango mingine. Kwa kuwa tukiangalia watoto hawa ni wadogo sana hawawezi kujitafutia; wanategemea wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia, kama itamlazimu mzazi ajiunge kwenye hivi vifurushi vinavyotolewa na Bima, itabidi mtu mmoja ajiunge na mtoto. Gharama zake ni kubwa; kuanzia shilingi 300,000 hadi shilingi 888,000, kulingana na umri wa mzazi utakavyokuwa. Zipo familia ambazo hazina uwezo kabisa wa kumudu hata ile shilingi laki tatu, wakati tungeweza kumwacha yule mtoto shilingi 50,000 ambayo wazazi wanaimudu, aendelee kupata matibabu ili tuweze kuwaokoa tusipoteze kizazi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi nzuri imefanywa nchini ya usambazaji wa Umeme wa *REA* awamu ya tatu; katika Jimbo la Meatu, vijiji vyote vimesambazwa kwa asilimia 100. Wakati Awamu ya Sita inaingia madarakani ni asilimia 40 tu ilikuwa imesambazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wameweza kununua mashine wamesimika; mindombinu ya kusukuma maji ya *diesel* tumeiyondoa tumeweka ya umeme; wananchi wanajishughulisha na biashara lakini changamoto kubwa iliyopo ni kukatikakatika kwa umeme katika Jimbo la Meatu na Wilaya ya Meatu kwa ujumla kutokana na kwamba iko pembezoni ukilinganisha na wilaya nyingine kwa sababu Mkoa wa Simiyu hatuna Kituo cha Kupozea Umeme. Wilaya nyingine zinapata umeme kutoka Bunda, nyingine zinapata Mabuki, nyingine zinatoka Ibadakuli Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuja na mpango wa kutekeleza mradi wa umeme katika Kijiji cha Imalilo-Bariadi lakini kumekuwa na kusuasua kwa wakandarasi kutekeleza mradi huo. Kwa mfano, mkandarasi anayejenga *Transmission Line* hadi sasa kazi yake ni asilimia 36 lakini anatakiwa akabidhi kazi Septemba 2024, ana

*invoice* saba anazodai Serikalini; anadai jumla ya shilingi bilioni 7.4, tunaomba Serikali iweze kumwezesha. Tuna mkandarasi ambaye anajenga *substation*; yeye kazi yake iko asilimia tano na anatakiwa awe amekamilisha Julai, 2025 lakini ameshindwa kuendelea kwa sababu hajalipwa *advance* ya shilingi bilioni 7.3.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iwawezeshe hawa wakandarasi na sisi Wilaya ya Meatu tuweze kunufaika na Uchumi wa Kati. Mkandarasi huyu wa *transmission* amefanya manunuzi mengi sana ya vifaa lakini ameshindwa kuendelea kwa kukosa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, ninaungana na uchambuzi wa Kamati kulipa Hati za Madai za wakandarasi zilizowasilishwa Wizara ya Fedha, kuwasilisha kiasi chote cha Tozo ya Mafuta kinachokusanywa ili Mfuko uweze kutekeleza miradi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* wawasilishe asilimia tatu ya mauzo ya umeme kwenye Mfuko kama sheria inavyoelekeza. Hii itatusaidia sana kuweza kukabiliana na kusuasua kwa miradi hii mikubwa. Umeme una matumizi mengi, ikiwemo kusukuma maji, leo hii Wilaya ya Meatu tunahangaika na mgao wa maji, siyo kwamba hakuna miradi ya maji iliyotekelezwa. Miradi mingi ya maji imetekelezwa na mifumo tumeibadilisha kwenda ya umeme lakini tunapata changamoto kutokana na kukatikakatika kwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Elimu, kazi kubwa nayo imefanyika, nipongeze imeongezewa bajeti kwa asilimia 17 kutoka shilingi trilioni 1.6 hadi shilingi trilioni 1.9, lakini sasa, hakuna bajeti yoyote iliyotengwa kwa ajili ya kutekeleza mitaala na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 23.

Mheshimiwa Spika, idara hii bado kuna uhaba mkubwa wa walimu; walimu hususan kwenye masomo ya Sayansi na Hisabati. Walimu wa Mafunzo ya Amali, lakini walimu wa Elimu Maalum bado tuna changamoto ya upungufu wa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini bado kuna upungufu wa miundombinu ya kujifunzia kwa mfano, bado kuna msongamano mkubwa wa wanafunzi madarasani hususan katika shule za msingi. Niipongeze Serikali angalau kwa sekondari, kupitia UVIKO tulikabiliana sana na msongamano wa wanafunzi lakini changamoto iko katika shule za msingi kwa sababu maboma yapo yameshindwa kuendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi nilitembelea shule zangu; mfano, Mshikamano na Mshikamano B kuna mlundikano mkubwa wa wanafunzi hadi 120. Shule ya Msingi Mwambiti kuna msongamano mkubwa; Shule ya Msingi Mwabuzo na nyingine zipo zina msongamano mkubwa wa wanafunzi na nyingine zina vyumba vichache ukilinganisha na vile vinavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna matumizi haba ya TEHAMA kutokana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia inayotokea duniani lakini ikiwepo usambazaji wa umeme katika maeneo yetu. Kila shule inatamani kupata vifaa vya TEHAMA, sasa, Serikali iangalie namna gani inaenda kuzisaidia shule zetu ili ziendane na mabadiliko yaliyopo kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi bado ninaendelea kuunga mkono kuwepo kwa chakula shuleni, nimetembelea katika shule zangu za msingi; kwenye muda wa saa tano nimeingia darasa la tatu, la nne, la tano, unakuta Watoto wamechoka wanasinzia, unawauliza kwa nini hivi? Mlitamani Mbunge wenu afanye nini? Aseme nini Serikalini? Majibu yao tupate uji shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali angalau iangalie uwezekano wa uwepo mlo mmoja tu wakati wa mchana shuleni.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana; Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa dhati, nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kuhusu Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali pamoja na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, nimepitia Bajeti ya Serikali, nimepitia Mpango wa Maendeleo lakini katika kupitia Nyaraka zote hizi mbili za Serikali sijaweza kukutana na neno linalosema Ujamaa, nikaone aidha ni kusahau au ni kutokuzingatia. Nilitaka nichukue nafasi hii kwanza nikumbushe; kwenye Mpango wa Maendeleo, nchi yetu na uchumi wetu na Taifa letu, sisi tuko kwa Falsafa ya Ujamaa, falsafa ya Ujamaa na Ujamaa wenyewe upo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ukienda Sura ya Kwanza Kifungu cha 3 ina-*cite* pale na kusema kwamba, "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi ya Kidemokrasia na ya Kijamaa". Ukienda Sehemu ya Pili, Kifungu cha 9 inasema, "Lengo la Katiba hii ni kuwezesha ujenzi wa Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au wa chochote kati ya Vyombo vyake na udugu na amani kutokana na kufuata Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imeenda mbali; katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwenye utangulizi wake inaongea habari ya kwamba, Chama Cha Mapinduzi ni chama cha kijamaa. Lakini mwisho kabisa kwenye Ilani katika Ukurasa wa 297 inaelezea misingi na sura hii katika kutekeleza Siasa yetu ya Ujamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nikimnukuu Shivji katika kitabu chake cha 'Insha na Mapambano ya Wanyonge' anasema kabisa na ninaomba ninukuu kwamba, "Nchi yenye Ujamaa kamili ni nchi ya wafanyakazi, haina Ubepari wala Ukabaila, haina tabaka mbili za watu; Tabaka la Chini la watu wanaoishi kwa kufanya kazi na Tabaka la Juu la watu wanaoishi kwa kufanyiwa kazi. Katika Nchi ya Ujamaa kamili mtu hamnyonyi

mtu, bali kila awezaye kufanya kazi hufanya kazi kwa kila mfanyakazi kupata pato la haki kwa kazi anayoifanya". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona ni-*cite* sana kwenye suala la Ujamaa; inawezekana tunasahau au tunazoea au tunaona kama kawaida. Ukienda Nchi ya China wameendelea sana na wanasema tunajenga uchumi wa China, tunajenga uchumi wetu kwa sifa za Kichina na sisi Watanzania nchi yetu ni ya Kijamaa na hili lazima tukubali sisi ni Wajamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ujamaa hauna neno la Kiingereza; siyo *Socialism*, ujamaa ni Ujamaa, kwa hiyo, Ujamaa ni *brand*. Ninachopata wasiwasi; kama ndani ya Bunge hili neno Ujamaa halitamkwi, je tukienda nje tunajitambulisha kama nani? Nilitaka niliseme hili na ndugu yangu Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, ni *generation* ambayo tumeimba sana habari za Ujamaa, kwa hiyo, niwakumbushe msisahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Ujamaa ni Falsafa, Mwalimu Nyerere alisema, katika Ujamaa tunapigana na maadui watatu; Ujinga, Umaskini na Maradhi. Sasa, katika kutekeleza Sera ya Ujamaa, kwamba tunaangalia katika wengi, kuanzishwa kwa *TARURA* ile ni Sera ya Ujamaa. Kwamba tulete maendeleo vijijini ambapo ndiko kuliko na watu wengi wakulima lakini ndiko kuliko na maskini waweze kupata huduma za kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *REA* ni zao la Ujamaa; kwamba tuweze kusambaza umeme vijijini na ufike mpaka vitongojini kwa watu maskini. Elimu bure na Bodi ya Mikopo, pale tunataka tuondoe unyonge katika elimu naku-*empower* familia zetu ili kwamba tuwe na *learned society* na hii ni *inclusive* kwamba tuwe na jamii ambayo imeelimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika misingi ya mwisho kabisa niweze kuisema kwenye Ujamaa, Mwalimu Nyerere anasema, "Binadamu anapokosa haki yake ya utu kupitia ujinga atanyayasika, kupitia umaskini atadhalilika lakini vilevile katika kupitia maradhi atadhalilika". Kwa hiyo, nilitaka niseme kwamba na tuendelee

kuamini katika hili, nchi yetu ya Kijamaa na Falsafa ya Ujamaa ndiyo uwe msingi wa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisema kwamba bajeti hii inatokana na *vision* katika kuunda 2020 – 2050, dira ile, bila Falsafa ya Ujamaa ni meli ambayo inasafiri haina mwelekeo na haijui inakoelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika suala zima la utekelezaji wa Bajeti ya Serikali; tuna siasa ambayo inaitwa Siasa ya Mfumo wa Malipo ya Serikali unakuwa umejifunga kuanzia mwezi wa saba, wa nane, wa tisa na wakati mwingine inasogea mwezi wa 10. Jambo hili ni lazima tulikemee, inavyofika mwezi wa saba, wa nane, wa tisa, Serikali inakuwa haifanyi kazi kwa kisingizio kwamba mifumo imefungwa, na hata tunavyoingia mwezi wa saba utekelezaji wa bajeti imekuwa ni kisingizio kikubwa. Kwa hiyo mimi ninachoiomba Serikali walau mfumo kufungwa iwe ni mwezi mmoja lakini kwenda miezi mitatu ni *sabotage* ya uchumi wetu lakini vile vile na ni kichaka cha watu wengine kutokutimiza wajibu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nije katika Jimbo langu la Bahi, miradi ya maendeleo katika suala zima la maji, Wizara ya Maji haijapata fedha na miradi mingi bado haijatekelezwa. Naiomba sana Serikali iweze kuangalia namna ya kutekeleza miradi ambayo mingi imeshafanyika wakandarasi wanasubiri kulipwa.

Mheshimiwa Spika, lakini katika suala zima la umeme, vitongoji vingi bado havina umeme na umeme sasa siyo anasa ni jambo la lazima, mtaa ule kuna umeme huku kwingine kuna giza, inaleta madaraja na *disturbance* ambayo wananchi wengine wanajiona kama ni wanyonge. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kufanya hima jambo hili kwamba suala la umeme liweze kusambaa katika vitongoji vyote.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TAMISEMI ilitoa mwongozo kwamba zipo halmashauri ambazo zitakuwa na mgao wa asilimia 20 kwa 80, kwa maana kwamba zikikusanya zitumie asilimia 80, asilimia 20 ndiyo iende kwenye maendeleo. Jambo hili kwa halmashauri ambazo hazina kipato kama Wilaya ya Bahi inaathiri

sana utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ukikusanya shilingi bilioni moja, shilingi milioni 200 tu ndiyo inaenda kwenye maendeleo, ukikusanya shilingi bilioni mbili milioni 400 tu ndiyo inaenda kwenye maendeleo, jambo hili inaifanya halmashauri isiweze kutekeleza kazi zake na kuwaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi naishauri sana Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI waangalie ikiwezekana tuje na ule mtindo wa asilimia 60 kwa 40 lakini ukiweka kwa 80 kwa 20 hakuna kinachotekelezeka, hamuwezi mkajenga madarasa, hamuwezi mkaweka madawati, hamuwezi hata kukarabati *floor*, maana yake fedha yake inakuwa ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ipo siasa ambayo imeingia ya mfumo unaitwa *NEST*, ile nayo ni aina ya siasa, siyo chama cha siasa ila ni aina ya siasa, nayo imeletwa na Serikali. Tulikuwa na utaratibu wa *force account* na jambo hili tumelifanya vizuri lakini kupitia *NEST*, kununua spanaa lazima mtu atoke Mtwara aje anunue spanaa Bahi, kununua taili lazima mtu atoke Tarime awe mnunuzi pale Bahi, jambo hili linatuchukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, mimi katika jimbo langu wakati naingia vijiji 19 havikuwa na zahanati, tumejitahidi kupitia *force account*, tumejenga zahanati 14 ambazo tumepauwa na kuweka marumaru na tunasubilia umaliziaji kidogo. Kutokana na *NEST*, zipo fedha ambazo zilitengwa kutoka mfuko wa jimbo mpaka sasa hazijaweza kufanya kazi kwa sababu tunasubiri foleni ya manunuzi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, kupitia mfumo huu wa *NEST*, ni mfumo ambao ni mzuri lakini unatufunga pingu hatuwezi kutembea. Miradi yetu ambavyo tulikuwa tunajenga kwa kasi haiwezi kufanyika, kwa hiyo jambo hilo nilikuwa naliomba kwenye suala zima la *NEST* muweze kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa niseme kama nilivyouelezea ujamaa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka ajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hii Bajeti Kuu. Kwanza ninaomba niwapongeze sana mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Naibu Waziri wake. Lakini nichukue fursa hii kumpongeza Profesa Kitila Mkumbo pamoja na Naibu wake ndugu yangu Nyongo na wakati huo nikupongeze sana kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kupewa imani kubwa ya kumsaidia Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo katika wizara hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwa kweli kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kuiongoza nchi hii kwa mafanikio makubwa sana. Sote tumeendelea kushuhudia miradi mingi ya kimaendeleo ikipigwa katika nchi yetu, kuanzia miradi ile ya kimkakati imekuwa ikienda kwa kasi kubwa lakini miradi mingine katika majimbo yetu, wilaya zetu na maeneo tunapowakilisha inakwenda vizuri sana kwa sababu tumekuwa tukipokea fedha nyingi kuliko kipindi chochote ambacho kwa kweli tumeshuhudia nchi yetu ikipiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu na tunamtakia afya njema, aendelee kuchapa kazi na sisi tupo nyuma yake tunapambana kuhakikisha kwamba maendeleo kwa Watanzania yanaendelea kuwepo zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nianzie katika eneo la miundombinu na hasa Barabara, tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita, kwa namna ambavyo imekuwa ikileta mtiririko

mzuri wa fedha na hasa baada ya kuongeza kipengele cha mfuko wa jimbo, ambazo tumekuwa tukipata karibu shilingi milioni 500 katika kila jimbo, lakini tumekuwa tukipata fedha ya tozo shilingi bilioni moja na milioni zaidi ya 890 ambazo tumekuwa tukizipata kupitia *road fund*, ni fedha ambazo kwa kweli zimekuwa zikiharakisha maendeleo, na hasa barabara zetu kuimarishwa. Lakini hivi juzi tumepata changamoto kubwa na hasa baada ya mvua nyingi zilizonyesha barabara ambazo zilijengwa kwa kweli zimekwenda na maji sana na hapa nazungumzia upande wa *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli tumeomba fedha ilimradi tuweze kurudishia miundombinu hii, na mimi katika wilaya yangu nimeomba zaidi ya shilingi bilioni 3.7 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunarudishia miundombinu iliyoharibika na hii ni baadhi ya maeneo tu niyataje machache ambayo hayapitiki na hapa ni karibu kilometa 500 sasa hazipitiki kati ya kilometa 1024.6 tulizo nazo katika wilaya nzima, kilometa 500 zipo katika hali mbaya hazipitiki, hii ni baada ya madaraja kuvunjika na baadhi ya barabara kabisa kuchotwa na maji, na kwa hali hiyo kwa kweli naomba sana wenzetu wa *TARURA* hasa Meneja Seifu kwa sababu ni mwenyeji wa maeneo haya wahakikishe urejeshaji ama kuleta fedha ambazo tumeomba kama *special request* ilimradi maeneo haya yaweze kurudishiwa na wananchi wakulima na wananchi kwa ujumla kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kimaendeleo waendelee kufanya kazi sawa sawa. Hii itasaidia sana kwa kweli kuharakisha maendeleo katika jimbo langu la Kishapu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine ambalo ningependa kushauri sana na hasa kwa sababu tunao wenzetu wa Wizara ya Mipango na Uwekezaji na hasa katika eneo zima la ugawaji wa fedha hizi, hii shilingi bilioni moja kwa ajili ya tozo, shilingi milioni 500 kwa ajili ya mfuko wa jimbo lakini na hii 880 ya *road fund* katika mgawanyo kwenye majimbo suala hili mimi naliona halipo sawa.

Mheshimiwa Spika, nataka niishauri Serikali na hasa wenzetu hawa wa Mipango na Uwekezaji, washauri mipango mizuri ya namna ya kugawanya hizi fedha ilimradi fedha hizi ziwe zinagawiwa kulingana na ule ukubwa wa *network* ya barabara

katika kila wilaya. Tukiwa tunagawa tu katika fomula ya usawa hatupo sawasawa kwa sababu jimbo moja unakuta lina kata 29, nimezitaja hapa kilometa 1026.4 za wilaya nzima ya Kishapu lakini wilaya zingine unakuta zina mtandao wa barabara kilometa 500 lakini zinapewa katika kugawiwa sawa, siyo sawasawa. Hili ni lazima litizamwe upya, ukubwa wa eneo lakini mtandao wa barabara ndiyo uwe una-*determine* kupelekewa fedha kwa ajili ya kukarabati barabara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo la kupeleka katika usawa siyo kweli kabisa, hatutendi haki…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Butondo, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge, kwa mfano Jimbo la Sengerema tu lina kilometa 1,770 lakini linapata mgao wa shilingi milioni 710, hii siyo sawa, endelea mchangiaji. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Butondo, endelea na mchango wako.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Tabasam.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni upande wa ahadi za viongozi wetu wakuu, zimekuwa zikitolewa ahadi nyingi sana, ahadi hizi Serikali yetu isipokuwa makini hii haitujengi haituletei afya. Ni lazima uratibu katika eneo hili, na amini Mheshimiwa Jenista Mhagama, ndiye anayeshughulika na eneo hili, ni lazima uratibu wa hizi ahadi ufuatiliwe kwa karibu na usimamizi kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi hizi uwe unatekelezwa. Kilometa nne ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kilometa tano, ni kilometa moja tu imetekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na ahadi pia ya ukamilishaji wa ujenzi wa barabara, Kolandoto kuja Kishapu kwenda Mwangongo kilometa 63, mpaka leo. Kwa hiyo, ahadi zote nchini ziratibiwe lakini tujipange kama Serikali tuweze kuzitimiza, hazituletei afya hata kidogo. Kwa hiyo, hili nilikuwa nataka niombe sana na lenyewe kwa sababu halitujengi kiafya linatuharibu tuweze kulikamilisha kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie upande wa *RUWASA*, unapokuwa unaomba lazima uanze kwa kushukuru, sisi watu wa Kishapu tunaanza kwa kushukuru. Katika kipindi cha kutoka mwaka 2020/2021 mpaka sasa tumepokea zaidi ya shilingi bilioni 16.5 kwa ajili ya maji, ni hatua ambayo haijawahi kutokea miaka yote na haya siyo maji ya kawaida, maji ya Ziwa Victoria tumesambaza katika kata 10, kabla ya hapo tulikuwa na kata mbili zilizokuwa na maji ya Ziwa Victoria, hii ni hatua kubwa sana ya Serikali ya Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan, sisi wana-Kishapu tunarudisha shukurani kabisa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo mipango mikubwa ambayo hata sasa hivi tunaendelea nayo, ipo miradi ambayo tumesaini mikataba ambayo inathamani ya zaidi ya shilingi bilioni nne. Kwa hiyo, tunakwenda kwenye shilingi bilioni zaidi ya 20 katika kipindi kifupi cha miaka mitatu, hatua tunakwenda nayo vizuri na tumejipanga kuhakikisha tarafa zote ikiwemo Mondo, Tarafa ya Negezi, Tarafa ya Kishapu kusambaza maji ya kutosha, tunaomba tupewe nafasi kwa sababu kwa kipindi kifupi kama tumeweza kusambaza katika kata 10 na sasa tunakwenda kusambaza katika kata sita, hakuna jambo linaloshindikana maadamu tupo kazini na Chama Cha Mapinduzi kinaendelea kutafuta fedha chini ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan, haya yote yanawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilikuwa naomba nizungumzie upande wa miradi viporo, ipo miradi 35 upande wa afya, 25 miradi mingine lakini upande wa elimu sekondari na msingi 85, Serikali ni lazima ijipange ilimradi ikamilishe miradi hii iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi, tutakwenda kuwakatisha wananchi tamaa kama hatutaweza kuitekeleza miradi hii.

Ninaomba sana jambo hili kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Mwingulu, mjipange vizuri muweze kuweka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la sukari, sukari ni la muhimu, ni bidhaa muhimu kwa sababu kila siku tunahitaji sisi watu wa kilimo tunaolima tunahitaji Sukari kwa wingi lakini wananchi kama kawaida wanahitaji sukari hata katika maeneo mengine, sukari ilipanda mpaka shilingi 12,000 kwa kilo lakini Serikali ya CCM chini ya Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan, jitihada zikafanyika haraka za kuhakikisha sukari inaagizwa kuja kuziba *gap*. Sasa leo wapo watu wanabeza kwamba Serikali imetumia utaratibu gani, ni sheria ipi ambayo Serikali imekosea? Tutambue kwamba suala la *food security* ni suala ambalo ni la kisera, ni lazima Serikali isimame imara katika maeneo muhimu kuhakikisha kwamba pale panapokuwepo na changamoto ya chakula haraka ichukue hatua na kuagiza sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halipo eneo ambalo Mheshimiwa Waziri alikosea na jambo hili limekuwa likifanyika katika awamu mbalimbali, mwaka 2018/2019 tulikuwa na tatizo kubwa la watu wa Korosho, Serikali iliingilia kati Korosho zikanunuliwa. Mwaka huo huo watu wa pamba tulipata mgogoro mkubwa Serikali iliingia kati na Serikali ikanunua Pamba, haya ndiyo majukumu ya Serikali ya kisera ambayo ni lazima ihakikishe inaingilia inafanya kazi pia… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Butondo, kengele ya pili imegonga.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii jioni hii ya leo, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya tele,

amani na baraka zake katika Taifa letu kwa kuwa sisi ni moja ya Taifa ambalo duniani linajifunza na mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, nichukue pia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa iliyofanyika katika Jimbo langu la Mbulu Mjini. Kwa kweli kazi kubwa imefanyika na hatujatarajia, mimi ni mwaka wa nane nipo Bungeni lakini kila tulipoenda kuahidi kwenye uchaguzi hatukuwa na matamanio ya kufikiri kwa mambo haya yangeweza kutekelezeka na hata alipokuja kuniombea kura mwaka 2020 aliniambia niahidi, sikuwa nafikiri kama utekelezaji wa zile ahadi yanatekelezwa, na yametekelezwa kwa sehemu kubwa sana. Kwa hiyo, kwetu sisi Mbulu Mjini tunamshukuru Mheshimiwa Rais, tunamtakia kila lililojema na afya tele. Lakini pia tunasubiri tumpe maua yake wakati wa uchaguzi kwa sababu mambo yale yaliyofanyika yalikuwa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, ninazungumza haya kwa sababu kuna miradi ambayo ilikuwa imechukua miaka 40 haikutekelezwa, haikuwezekana kwa ajili ya ukosefu wa fedha lakini pia kwa ajili ya uwezo wa Serikali na sasa imetekelezwa chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunamtakia kila lililojema, tunamshukuru kwa utekelezaji wa ilani lakini kwa miradi mingi sana iliyotekelezwa katika jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi yakujifunza katika Taifa letu, mimi nizungumzie jambo hili kwa msingi wa kwamba katika kupitisha mipango ya maendeleo na kutekeleza miradi ya maendeleo kuna mambo makuu mawili, kwanza uibuaji wa ile miradi lakini baadaye kwenda kwenye sura ya utekelezaji kwa ajili ya miaka ile mitano na kwenda kwenye mwaka mmoja mmoja wa utekelezaji wa miradi au utekelezaji wa mipango ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mipango hii inaanzishwa kwa *D by D* kutoka ngazi za wananchi kule chini na sasa utekelezaji wake unakuja katika sura ile ya mwaka mmoja mmoja, kuna mambo mengi yanafanikiwa na mengine yanakwama, nini ushauri wangu kwa Serikali? Niiombe Serikali yetu irudi upya itazame miradi hii ambayo pengine imeanzishwa na wananchi lakini nyingine pia Serikali Kuu kupitia mipango yake ya

maendeleo kwa ajili ya vipaumbele vya wananchi. Kwa nini jambo hili linakuwa gumu? Ni kutokana na ule upatikanaji wa fedha. Kwa hivyo ushauri wangu kwenye eneo hili ni kwamba miradi ipi iliyoanzishwa, imekaa muda gani na fedha sasa zitapatikanaje ili utekelezaji wake ufanikiwe.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii ni muhimu kwa sababu tulipokuwa tunaanzisha ile miradi ilikuwa ni uwekezaji wa muda mrefu kupitia michango ya wananchi lakini na fedha za Serikali na kwa kuwa miradi inakaa muda mrefu, kwa mfano tunaviporo vya majengo ya wananchi kwenye Sekta ya Afya, Elimu pamoja na maeneo ya utawala kwenye vijiji na kata zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mpango huu ambapo unahitaji kutekelezwa tusiporudi nyuma inapofika mwezi Juni, miradi ile ambayo imekosa fedha mwaka wa Serikali unakuta hazijawekwa kwenye mpango wa mwaka unaokuja. Kwa hivyo sababu ya kurudi nyuma ni kutazama upya namna gani ile miradi ambayo imerukwa na haikupata fedha inaingia katika mwaka ule unaokuja kwa ajili ya tathimini ya kujua idadi ya miradi na namna ya kufanikisha. Kwa eneo hili tuna miradi hiyo ambayo michango ya wananchi ilipochangwa ilikuwa ni vipaumbele kwao, wao sasa wanasubiri Serikali ije iwashike mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni miradi mikubwa ya Serikali tunayotekeleza, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu, nimekuja kwako mara nyingi nimekuomba kuhusu masuala ya barabara ya Karatu, Mbulu, Hydom na ile barabara ya Mbulu Garibabi na barabara zingine za *EPC+Finance* hizi barabara zinasubiriwa sana na wananchi. Mimi niombe sana Serikali yetu namna ambayo barabara hizi zitapata fedha ili utekelezaji wake uanze tusije tukapata mgogoro na wananchi pamoja na Serikali kwa kupitia imani yao waliyojenga kwa miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza ilipoibua na sasa tunapoenda kwenye utekelezaji na namna hii ni namna nzuri ya kuona miradi ile iliyoanzishwa inapata kutoa huduma kwa wananchi lakini pia miradi ya barabara ni miradi muhimu katika uchumi wa Taifa letu na kuongeza mapato. Sisi Wilaya ya Mbulu, tupo juu ya bonde la ufa, mzunguko wa bonde la ufa unatufanya

mlango wetu wa kutoka uwe ni Karatu kuja Mbulu kwa ajili ya Arusha, Karatu, Mbulu na Mbulu kwenda Hydom kuelekea maeneo ya Tabora, Singida na huko Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, sasa tusipofungua hiyo barabara ya Karatu, Mbulu, Hydom bado tumejifunga kwenye mzigo ambao mwisho wa siku Mbulu inazidi kurudi nyuma, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, umeniahidi mara nyingi, niombe Serikali ijitahidi kutafuta fedha na mkandarasi wa Garibabi arudi na ile barabara ya *EPC+Finance* na barabara zingine nchini zipate kufunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine, kwa kuwa tupo hapa kuwawakilisha wananchi, kupitia Bunge hili na Bunge lipo *live*, wanatusubiri! Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri wa Utumishi ulituahidi ajira ya vijana 46,000 au ajira mpya 46,000, tunaomba Serikali ije ione namna yakutoa zile nafasi za ajira ili vijana wapate ajira nchini na walau kiu yao kwa ile sehemu ambayo tayari Waziri ameahidi kama Serikali utekelezaji wake uwepo kwenye huu Mpango kwa ajili ya Julai, kwa sababu mwaka umeshaisha. Kesho kutwa ni Juni, 28 tunahitimisha Bunge hili na tarehe 1, Julai ni mwaka mpya wa Serikali ili ajira hii iweze kuwa chachu kwa vijana wetu ambao wanaisubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kwa sababu ya muda ni eneo la Uwanja wa Ndege Manyara; Uwanja wa Ndege Manyara, umekuwepo kwenye vitabu vya bajeti kwa takribani miaka kumi sasa tukililia huku Bungeni. Tunaomba huu Uwanja wa Ndege Manyara uweze kuanza utekelezaji wake kama ilivyo Mikoa mingine nchini ili walau Mkoa wetu usiachwe nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia Mradi Mkubwa wa Maji kule Mbulu Mjini wa Tarafa ya Nambis, naishukuru Serikali imeweka kwenye Mpango, basi fedha zile bilioni 52 hata kama hazitapatikana kwa mara moja ziwekwe kwenye mipango ya awamu ili mradi huu utekelezwe kwa sababu Tarafa hii ilikuwa haijapata maji muda mrefu na kwa sasa wananchi wanasubiri kwa hamu kubwa sana ili tuweze kufanikiwa na tuangalie utaratibu huu unakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni hatua ya upatikanaji wa sukari, lakini pia kufungua mazingira ya sukari kutokuwa na urasimu na mazingira ambayo ni kinzani kwa wananchi wetu, tunaishukuru Serikali kwa mpango wake wa kutazama jambo hili.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mfanyabiashara mdogo, lakini sukari kwa mfumo tunavyokwenda ni nafuu tukubaliane na Serikali kwa wazo liloleta kwa sababu upande ule wa kwanza ulishashindikana ili tuweze kuona huu upande wa pili. Kitendo cha sukari kuadimika na kuwa na gharama kubwa sana kwa wananchi kwa kweli wananchi wetu wametulilia sana jambo hili muda mrefu, na sasa kwa sababu tayari Serikali imekuja na utaratibu huu mpya tunaishukuru sana Serikali na sisi Wabunge tukubaliane wote kukubali kwa mawazo ya Serikali na mapendekezo ya Serikali ili sukari walau mfumo huu wa sasa tuutazame utatufikisha wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni maombi kwa fedha za Chuo cha Tango; naishukuru Serikali inakuja na Mpango wa kujenga Shule ya Amali katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu, kwa maana ya Mbulu Mjini hatutapewa *VETA* tutapewa shule hiyo ya ufundi kwa ajili ya eneo hili la kuwajengea vijana wetu uwezo wa kitaaluma lakini pia uwezo wa ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Tango, tulianza kujenga majengo ya Chuo cha Tango, yaliyojengwa na wakoloni toka mwaka 2015. Ninaishukuru Serikali kwa kujenga nusu ya majengo yale kwa upya, kwa hiyo, yale majengo yaliyobaki nusu tunaomba pia mwaka huu wa fedha tupate fedha ya kumalizia yale majengo yote ambayo ni magofu hayatumiki kwa sasa ili Chuo hicho kiweze kutoa huduma bora kwa wananchi wa Mbulu, lakini Pia nawananchi wa maeneo mengine ambayo wanatarajia kupata taaluma hiyo na pia vijana wanapata ujuzi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni Sheria za Kodi, niiombe Serikali mapendekezo ya faini milioni 15 yanayotarajiwa kuletwa huku Bungeni kwa kweli hayatafanana na uhalisia wa biashara nchini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga, Mheshimiwa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu faini hiyo ni kubwa sana na tunapoteza mapato makubwa kwa ajili ya faini hizi za vitisho.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nikuombe, naunga mkono hoja nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshishimiwa Masache Njelu Kasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Dkt. Chaya, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, nami kupata nafasi niweze kuchangia kwenye Bajeti Kuu ya Serikali. Nitoe mchango wangu ili tuweze kuboresha bajeti hii ili iweze kwenda kufanya kazi vizuri sana kwa Watanzania na hasa hasa namna ambavyo miradi inatekelezeka, na sisi Watu wa Chunya na Watanzania kwa ujumla tumeona miradi mingi inatekelezeka chini ya Serikali ya Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, niwapongeze Mheshimiwa Waziri Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na Waziri wa Mipango kwa kweli mmeonesha weledi mkubwa sana kwenye hoja hii ya bajeti ambayo ipo mbele yetu na sasa tunaijadili. Tunaomba haya, ambayo yapo kwenye Mipango yaweze kwenda kwenye utekelezaji na wananchi wetu wengi waweze kuona matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wetu wengi huko na Wananchi wetu wa Chunya na baadhi ya maeneo mengineyo huko wanataka kuona vitu vinatekelezeka, wanataka kuona miradi inatekelezeka na miradi inapotaka kutekelezeka hii tayari wameshaona kwenye mwaka huu ambao unakwenda kumalizia na hii miaka mitatu ya Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, namna ambavyo miradi kwenye Majimbo yetu lakini miradi mikubwa ya kimkakati imeweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuona haya yanatekelezeka vizuri zaidi; lazima Watanzania wajue kwamba hizi fedha zinatokana na kodi zetu. Sisi kama Watanzania jambo la kwanza lazima tuweke msisitizo kwenye kulipa kodi na tunapoenda kuweka msisitizo kwenye kulipa kodi Serikali kazi yake kubwa ni kwenda kukusanya hii kodi. Hivyo basi, kwa mujibu wa takwimu sisi takribani Watanzania zaidi ya milioni 60 walilipa kodi ni takribani milioni tano tu, ambao ni kiasi kidogo mno na katika hawa takribani watu 600,000 ndio ambao huwa wanafunga hesabu zao kwa mwaka kwa hiari, hivyo, watu hawa ni wachache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukitaka tuweze kukusanya kodi nyingi na kubwa zaidi lazima tuongeze wigo wa walipa kodi. Nimepitia kwenye Mpango wa Serikali 2025/2050 lakini na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, sijaona namna ambavyo mmeelekeza Mipango ya Serikali kuongeza wigo wa walipa kodi. Bila kuongeza wigo wa walipa kodi tutakuwa tunaendelea kwenda kuwadai na kwenda kukusanya kodi kwa wafanyabiashara wale wale, tutakuwa kila siku tunabadilisha majina ya kodi, leo tunakwenda mtindo huu, kesho tunaenda mtindo mwingine lakini walipa kodi ni wale wale. Sasa tukienda kwa mtindo huu kwa walipa kodi wale wale matokeo yake ndio haya ambayo leo tunaweza kuyaona migomo ya wafanyabiashara wetum, kwa sababu wafanyabiashara ni wale wale na sisi tunahitaji kodi zaidi ili tuweze kupata fedha kutekeleza hii miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe Mheshimiwa Waziri na nishauri mnapokuja kwenye kuhitimisha hoja hii, mtueleze Mipango ya Serikali ni nini kuhakikisha kwamba wigo wa walipa kodi unazidi kuongezeka? Tukusanye fedha nyingi zaidi ili miradi yetu hii iweze kutekelezeka vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Miji yetu inakuwa na biashara zinakuwa na biashara kila siku zinaanzishwa biashara mpya. Wigo wa Maafisa wa *TRA* ni mdogo sana kwenda kuwafikia walipa kodi wa nchi hii. Leo biashara zipo ndani ya majumba yetu, ukitoka tu nje ya nyumba yako unakuta kuna fremu, kuna biashara ipo. Je,

hawa walipa kodi tumewafikia? Je hawa wapo kwenye *data base* yetu yote ya kuweza kulipa kodi?

Mheshimiwa Spika, tuone namna iliyokuwa nzuri na bora zaidi tuweze kwenda kuwafikia hawa na ikiwezekana ile hali ya watu Maafisa wa *TRA* kwenda kukusanya kodi kwa *block farming* sasa tutoke pale, tuajiri Maafisa Kodi kwenye ngazi ya Kata, kwenye ngazi ya Mitaa na ngazi hata ya Kijiji ikiwezekana, kwa sababu kama tumeweza kuajiri Maafisa Elimu Kata kwenye Kata zetu, Maafisa Maendeleo ya Jamii kwenye Kata zetu, Maafisa Elimu na wengineyo kwenye Kata zetu, kwa nini tushindwe kuajiri Maafisa Kodi kwenye Kata zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kuwa na fedha za kutosha, bila kukusanya fedha na kodi ya kutosha kila siku tutakuwa tunapiga *mark time* hapa hapa. Tunaweza tukaanza kwa *pilot area* kwa baadhi ya Miji mikubwa tukaanza Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Mbeya twende tukaanze kabla haijaenea kwenye nchi nzima ili tuweze kwenda kuwafikia walipa kodi wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili nchi yetu iweze kukuwa zaidi kiuchumi, lazima pia tuweze kuendelea kuwekeza kwenye viwanda. Bila ya kwenda kuwekeza kwenye viwanda sisi Watanzania tutabakia kuwa wachuuzi kwenye nchi yetu. Kazi yetu itakuwa kuagiza mizigo na huku pia tunaenda kuiuza, hivyo, uchumi wetu utakuwa unaenda unakuwa kidogo kidogo ambapo sisi Watanzania na ukuwaji wa Taifa letu hili tutakuwa bado hatujafikia malengo yetu, na kwa nini, tunasema haya? Kwa sababu, tukiwezesha viwanda vyetu hapa vya kutosha, kwanza tutakuwa na uhakika wa kodi ya kwetu, lakini la pili tunaanzisha ajira nyingi za kutosha ambazo Watanzania wengi hasa vijana hawa ambao ndio wengi sana kwenye takwimu wataweza kupata ajira za kutosha na wao wataweza kulipa kodi vizuri zaidi, tukipata fedha miradi mingi itaweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunasifu miradi mikubwa ya kimkakati Bwawa la Mwalimu Nyerere, limekamilika sasa hivi linazalisha. Ule umeme mwingi tunaozalisha tuna upeleleka wapi? Kama hatuna viwanda vya kutosha ambavyo vitaenda kulisha kule. Kwa hiyo,

umeme tunaouzalisha wa kutosha tuweze kwenda kwenye viwanda ili upelekwe kule ili uzalishaji uweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunafurahi kwamba Reli yetu ya *SGR* imeweza kukamilika, leo tumeanza *lot* ya kwanza kusafirisha kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro na baadaye itafuata kuja mpaka Dodoma, lakini kama hatuwezi kusafirisha mizigo, kama hatuwezi tukazalisha tukasafirisha sisi wenyewe hii itakuwa ni hasara kwenye nchi yetu, kusafirisha abiria pekee yake ni hasara. Naomba tuwekeze huku kwenye viwanda, tuwekeze mashambani kule, ili hizi reli zetu hizi ziweze kufanya kazi vizuri zaidi, ndio tutaweza kupata mapato mengi ya kutosha na wananchi wetu wataweza kunufaika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Wilaya ya Chunya shughuli zetu kubwa zaidi za kiuchumi ni kubwa mbili; Moja ni uchimbaji wa madini ya dhahabu lakini la pili ni kilimo hasa kilimo cha tumbaku. Kwenye upande wa uchimbaji wa madini ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo sisi Watu wa Chunya ndio wazalishaji wa pili kwa sasa hivi kwa Tanzania kwa kuzalisha takribani kilo 300 kwa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi kilo 300 kwa mwezi ambazo tunazalisha sisi Watu wa Chunya tunalipa kodi ya moja kwa moja ambayo tunasema Murabaha asilimia sita na *inspection fee* asilimia moja takribani bilioni tatu kwa mwezi tunailipa kutoka Chunya. Lakini je, sisi tunachangia kwenye pato hili la Taifa kwa mwezi zaidi ya bilioni tatu sisi huku tunapata nini?

Mheshimiwa Spika, leo ukiangalia miundombinu yetu hasa ya barabara ya kuelekea kule tunakokwenda kuzalisha ni mibovu. Barabara ya kutoka Matundasi kwenda Itumbi ambako uzalishaji ni mkubwa mbovu, barabara ya kutoka Njiapanda kwenda Sangambi kwenda Ifumbo kwenda Mawelu na kwingineko, hizi zote barabara ni mbovu. Niiombe Serikali kule ambako tunapata mapato ya kutosha ndio tupeleke pesa miundombinu ikae vizuri ili tuweze kupata pesa nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tuiwezeshe pia *TARURA,* sisi watu wa Wilaya ya Chunya kijiografia kwa Mkoa wa Mbeya tuna

takribani asilimia 39.5 ya Mkoa nzima. Lakini bajeti ambayo tunaipata ya fedha inalingana na Wilaya nyingine ambayo hii kwa maana kwamba tukipiga kimahesabu sisi pia tunapunjika. Niiombe Serikali inapogawa hizi isigawe kwa usawa tu iangalie na ukubwa wa maeneo yetu, ukubwa wa kilomita za kimraba, ukubwa wa barabara zetu na fedha ndio tupeleke huku ili wananchi wetu waweze kunufaika na barabara hizi kwa namna moja au nyingine ziweze kukamilika. *(Makofi)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache, kuna taarifa kutoka kwa nani?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, nipo hapa.

**SPIKA:** Aah, Mheshimiwa Kunambi.

**TAARIFA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nampa taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza kwamba anachokisema ni sahihi kabisa na anajenga hoja ya msingi. Taarifa yangu ni kwamba kuna halmashauri nchini ambazo kimsingi zina uwezo wa kifedha kupitia mapato ya ndani zingeweza kupunguza mzigo kwa Serikali Kuu kwa kutenga bajeti ya mapato ya ndani kwenda *TARURA* na fedha hizi nyingine vijana wa halmasahuri ambazo ni changa. Kwa mfano, Halmashauri ya Kinondoni wao wameweka 10% kwenye barabara Majiji mengine wangefanya hivyo na Manispaa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hii kwa mikono miwili, kwa sababu hata sisi Wananchi wa Chunya kwenye halmshauri yetu kwenye bajeti hii ambayo tunaendelea nayo makusanyo yetu tulikadiria bilioni tano lakini tuliweza kukusanya bilioni nane mpaka sasa hivi. Tuna wastani wa zaidi ya asilimia 142 ya makusanyo tunayoendelea nayo, hivyo

naipokea kwa mikono miwili, kwa sababu na sisi tumeweza kupata fedha hizi hapa na barabara hizi zingeweza kutengenezwa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara yetu inayotuunganisha kuanzia Mkoa wa Mbeya na Tabora Mheshimiwa Rais alivyokuwa Singida kule aliitolea maelezo kwamba fedha zitoke ili barabara iweze kutengenezwa lakini mpaka leo fedha hazijatoka. Sijajua Waziri wa Fedha, tunakwama wapi? Kuhakikisha kwamba hii barabara yenyewe inakwenda kutengenezwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili tayari, Mheshimiwa.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nimeongea na wewe mara kadhaa, nimeongea na Waziri wa barabara hapa kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa, lakini mpaka leo barabara haijaweza kutengenezwa na kwenye Mpango haipo. Niombe sana tuweze kupeleka fedha hapa ili barabara iweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, afuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia hoja hii ya bajeti yetu ya Mwaka 2024/2025. Lakini kwa nafasi ya pekee nawapongeza Mawaziri wote kwa sababu bajeti hii ya Taifa ni *consolidated budget* ambayo imetoka kwenye Wizara zote.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa nafasi ya pekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumeona *progressively* bajeti yetu tuliyomalizia kutekeleza ikiwa ya trilioni 44.3 lakini sasa tumeenda mpaka kwenye trilioni 49. Nampongeza sana kwa hatua hii na ukizingatia kwamba bajeti yetu ni *cash budget*

tunachokikusanya ndiyo ambacho kinaenda kwenye maendeleo, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchangua, nimepitia bajeti ya Wizara hii kwenye hotuba yake sura ya 9 amejaribu kuonesha vipaumbele, na lazima tuende na vipaumbele kwa sababu *resource* ni *scarce*. Kwenye vipaumbele hivi Mheshimiwa Waziri amejaribu kueleza dhima ya mpango wetu ni kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa ajili ya maendeleo ya watu lakini kupitia kuchochea uchumi shindani na shirikishi na kujenga uwezo wa viwanda vya ndani ili viweze kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, roho ya uchumi wetu ni viwanda, tusipoweza kuwajengea uwezo viwanda vyetu vya ndani na tusipovilinda hatuwezi kwenda mbali katika uchumi. Tumeona mifano mingi ya nchi ambazo duniani zimefanya vizuri sana kiuchumi, kwa mfano Nchi ya China na wengine kwenye miaka 60 ndiyo tulikuwa tupo pamoja sasa hivi huwezi kulinganisha na sisi kwa sababu wali-*opt* kwenda kuboresha viwanda vyao na viwanda vya ndani na walikuwa wanavilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sisi Tanzania kwa kweli vigezo vya kuona ni kiasi gani kweli tumemaanisha kulinda viwanda vya ndani ni kuangalia vigezo vya bei ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi yetu na zinazotoka nje. Ukiona kwamba bidhaa zinazotoka nje siku zote bei yake ipo chini kuliko tunazozalisha ndani basi ujue kwamba tunazalisha kwa gharama kubwa lakini hapo hapo kuna utitiri mkubwa sana wa kodi ambazo zipo ndani ya viwanda vyetu kwa hiyo hapo hatuwezi kwenda kwenye ushindani hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nchi yetu sasa iangalie ni namna gani ya wawekezaji tunaowataka katika nchi yetu ili kupunguza ushindani wa viwanda vyetu na viwanda vya nje. Kwa mfano kama tunataka wawekezaji waje wafanye ushindani kwenye viwanda vyetu pengine vya kusindika au hata viwanda vya sementi tunavyotengeneza wenyewe humu ndani halafu tunaweka yale mazingira tunayosema mazingira rafiki kwa wawekezaji. Kwa mfano tukasema tunawapa *grace period* wasilipe kodi kwa muda fulani, tumeona mara nyingi *is like a*

*cheating,* tunawapa *a grace period* wanafanya kazi ikifika mahali wanasema hawajapata faida wana-*phase out* halafu kiwanda hicho hicho anachukuwa mtu mwingine kinachofanyika pengine hiyo *firm* ni kubadilisha tu jina na nchi inaendelea kukosa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natamani tuone ni maeneo gani kweli tunahitaji wawekezaji na ambao wanastahili kweli kupata huo unafuu ambao sisi tunafikiri ndiyo mazingira mazuri ambayo tunawawekea wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwanda vingine ni muhimu sana katika kuchochea uchumi wetu, kwa mfano, viwanda vya maziwa; tuna viwanda 152 vya maziwa Tanzania lakini tuna viwanda sita vikubwa vinavyosindika maziwa mojawapo ikiwepo cha Asas. Tumeona kazi nzuri ambayo Asas wanafanya, mara nyingi wamekuwa kwenye viwanja vya Bunge hasa kipindi cha Bajeti ya Wizara ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mambo mengi sana ya kuiga kutoka Asas, Asas wanafuga ufugaji wa kisasa, ni rahisi watu kwenda kujifunza pale kuona wanafuga kwa kiasi gani. Lakini hawa wanasindika maziwa, wameajiri Watanzania zaidi ya 400, wananunua maziwa kutoka kwa wenyeji *(out growers)* pia wanagawa mitamba kwa wafugaji wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Asas kwa sababu wamekuwa peke yao sasa wanaoenda kutekeleza *master plan* ya Wizara ya Mifugo ya kwenda kuzalisha maziwa ya unga. Pia, utaona kwamba kama kweli nia yetu ni kujengea uwezo viwanda vya ndani na kuvisaidia, kiwanda hiki sasa kinakusanya maziwa kwa watu, inasindika na sasa imeenda ku-*park* maziwa ya unga lakini ndiyo ina *withholding tax* kubwa, ina *income tax,* ina *VAT tax* kiasi kwamba tutaona nchini kwetu maziwa yote yanayotoka nje kwa asilimia 100 ni maziwa ya nje. Sasa haya ya ndani tukiweka kodi nyingi nyingi hivyo haviwezi ku-*compete* na maziwa yanayotoka nje, na sisi Tanzania tumeweka *duty reserve exemption* kwa maziwa yanayotoka nje na tunapoteza dola za kimarekani takribani milioni 8.1 kwa kila mwaka kwa kuingiza maziwa ya nje nchini mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hebu jaribu kuiona Mheshimiwa Waziri kama kweli tunamaanisha kuvilinda viwanda vyetu vya ndani basi hizi *withholding tax* ambazo zipo kwenye *products* hizi ambazo zinanunuliwa kwa wafugaji wetu tuone namna gani tunafanya. Pia tunahitaji ku-*prolong availability* ya bidhaa kama maziwa ukizingatia *per capital consumption* ya maziwa kwa Watanzania ipo chini. Watanzania wanakunywa maziwa labda kwa lita 47 mpaka 50 kwa mwaka ambapo *recommended* ingetakiwa kila Mtanzania awe anakunywa maziwa lita 200 kwa mwaka; na ndiyo maana asilimia 30 ya watoto wetu wana udumavu ambacho ni kitu kibaya sana. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri kama tunamaanisha kulinda viwanda vyetu vya ndani hicho nacho utakiangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine ni wa *TRA*, nawapongeza sana *TRA* wameweza kutusaidia kukusanya mapato tena kwa asilimia 79 *almost* asilimia 30. Wanafanya kazi nzuri nawapongeza na pengine wanatekeleza sheria ambazo wenyewe tumezipitisha.

Mheshimiwa Spika, *TRA,* wadau wao wakubwa ni wafanyabiashara, ni muda sahihi kabisa kwamba hao, wajisogeze zaidi kwa wafanyabiashara na wafanye wadau wao wa muhimu na kufanya nao urafiki. Kipindi hiki ambacho ndiyo kipindi cha kukadiria kodi za wafanyabiashara hao ni kipindi ambacho *TRA* wanapaswa kuwa karibu na hao wateja wao. Kuna wanaofanya *self-assessment* wanapeleka mahesabu wanakadiriwa kodi lakini bado *TRA* wana *room* ya kukaa nao na kukubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hao ambao wao unawakadiria mapato, *TRA* wana nafasi ya kwenda kukubaliana nao mapato na pia wana nafasi ya kwenda ku-*review* mapato ya wateja wao nusu mwaka. Sasa hii habari ya kwenda kuangalia mahesabu ya nyuma ya miaka miwili, mitatu halafu unaenda kuwapiga faini wafanyabiashara asilimia 10 ya *gross* (mapato) waliyopata katika miaka miwili iliyopita ni kuwa-*embarrass* wafanyabiashara, ni kuwavunja moyo lakini ni jambo ambalo linajenga mazingira ya rushwa, hili kwa kweli mliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hili la faini ya *EFD Machine receipt,* sijui kama hii kweli ni *realistic*. Tulikuwa tunapiga faini kwa risiti ambayo haikutolewa hata moja kwa shilingi milioni 4.5 lakini sasa naona tumeenda mpaka kwenye milioni 15, hivi kweli hii ni *realistic?* Ni kwa kiasi gani? Kama ni mtu ameuziwa labda kitu cha shilingi elfu tano, elfu kumi, laki moja kwa bahati mbaya hakutoa risiti unaenda kumpiga faini ya milioni 15 kweli hii ni *realistic?* Nilikuwa nafikiria vitu hivi tuviangalie vipo kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili la *VAT 18%,* sijajua tumekokotoa kwa kiasi gani hadi tumekuja na *VAT* ya asilimia 18, najua hii ni kodi inayokusanywa kutoka kwa walaji, badala ya ile *development levy* ya kulipa kodi ya kichwa tunaona tu kwamba tutachukuwa kodi kwa wananchi wetu kwa kupitia *VAT*. Lakini tuangalie kwa nini watu wanakwepa kwepa hii *VAT*? Ni kweli tumekaa *round table* tukaona kwamba *a good figure is 18%* ya kwenda kui-*tax* hii *VAT*? Ndiyo maana unaona kwamba wafanyabiashara kwanza hii *VAT* inakwenda kwa watu wenye sifa ya kukusanya. Kuna wafanyabiashara wengine hawana *VAT, automatically* bidhaa ambayo unanunua ui-*sort VAT* bei yake itakuwa chini na ile ambayo utanunua na *VAT* bei yake itakuwa juu. Sasa ona ni nani anaweza kwenda kufanya biashara kule ambako kuna *VAT*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana ukienda dukani, mfanyabiashara anakwambia kabisa kama unataka risiti *VAT included* utalipa, kama hutaki risiti anakupa. Sasa haya mazingira ya kukwepa kwepa pengine tungeangalia kwamba *is this 18%* ni *reasonable,* tuna-*tax* wakandarasi, tuna-*tax* hata wakati mwingine hata watalii wanaoingia nchini mpaka na wao kila kichwa inatakiwa ilipe *VAT 50%* ndiyo maana utakuta *sometimes* wanalala nje ya nchi lakini wanakuja kufanya ziara nchini mwetu. Kwa hiyo, hii ni vizuri kuiangalia, ni vizuri basi kama itakuwa hivyo ikawekwa *reasonable amount* lakini wafanyabiashara wote pengine wakalipa hii *VAT* ili kusiwe kuna kukwepa kwepa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu kuwajengea uwezo wajasiriamali, kuna kikundi kikubwa sana cha Watanzania ikiwepo vijana wanaomaliza chuo kwa kweli ajira ni

changamoto na tunawajengea mazingira kwamba wapate mkopo ya kutoka halmashauri *(own source)* na kwa vyovyote vile nampongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan kuweza kutenga bilioni 18.5 ambayo ameweza kuipitisha kwenye benki zetu, nilikuwa naomba ziungane hizo kufanya menejiment nzuri ni *SIDO*. Ingeweza kupitia *SIDO* wakatoa mafunzo, wakatoa teknolojia pamoja na mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru sana wewe kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara ya Fedha, lakini vilevile kuhusu Wizara ya Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwanza kwa kazi kubwa ambazo anazifanya katika Taifa letu la Tanzania. Lakini sisi kule Manyoni Mashariki kwa kweli Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa sana, nikisema niyataje hapa leo inawezekana yakajaa hili jumba lako. Kwa hiyo, mimi nichukue nafasi hii kwa niaba ya Wananchi wa Manyoni nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa miaka hii mitatu ameweka rekodi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina maeneo manne ningependa kuyachangia leo na eneo la mwisho litakuwa ombi. Eneo la kwanza nitachangia kuhusu mfumo wa uagizaji wa sukari ile *sugar gap* lakini eneo la pili nitachangia kuhusu kikokotoo na eneo la tatu nitachangia kuhusu utafiti kwenye masuala ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sukari, Wabunge wengi wamechangia humu, nikiri kusema kwamba huko zamani wale ambao tulisoma *micro, macro-economics* tulikuwa tunasoma *luxurious good, public goods,* sijui *basic good, normal goods,* tulikuwa tunaona kipindi kile sukari ni kama *luxurious goods* yaani ni huduma ya watu fulani wenye vipato. Lakini sasa hivi sukari ni bidhaa ambayo inatafutwa zaidi na watu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hilo? Inawezekana humu wengi tumesomeshwa na mama zetu wakipika pombe za kienyeji, ili uweze kupika pombe ya kienyeji unahitaji sukari. Lakini tumesomeshwa na mama zetu wengi humu walikuwa wanapika vitumbua, ili uweze kupika vitumbua lazima uwe na sukari. Maana yangu ni nini? Sukari ni mojawapo ya bidhaa ambayo ni ya muhimu sana kwa watu wanyonge na kwa watu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimesikiliza hoja za Wabunge wenzangu wakilalamika kuna kipindi kwamba bei ya sukari ilipanda sana, wote ni mashahidi kuna kipindi ilifika 4000 – 5000 - 7000 na kadhalika lakini kukawa na hoja kwamba inapotokea upungufu wa sukari, tunatumia mfumo gani kwenye kuagiza? Kwamba kuna wafanyabiashara na viwanda tumevipa jukumu la kuagiza.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ipo hapo, hoja yangu ni kwamba nadhani sisi kama nchi lazima tuje na mfumo mzuri wa kuhakikisha kwamba sasa tutakuwa na taasisi ya Kiserikali tunayoiamini kwamba ikitokea kuna *sugar gap,* hizo riziki inachukuliwa na Serikali. Sukari ni vita na ushauri wangu ni nini? Namshukuru Mheshimiwa Bashe kwa kuja na wazo kwamba na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, sasa tunaenda kuipa *NFRA* jukumu la kuagiza sukari *in case* ikitokea kuna upungufu wa sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili linakwenda kupunguza malalamiko ya wananchi lakini linakwenda kupunguza malalamiko yale tunasema kuna watu wanahujumu hii nchi, *NFRA* haitaweza kihujumu hii nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sanjari na hilo kwenye suala la sukari sisi kama nchi lazima tuwekeze ndani hususani kwa wakulima wa sukari. Kule Morogoro tuna wakulima wengi sana wadogo wadogo wa miwa, ni muda muafaka sasa Waziri wa Fedha na Waziri wa Kilimo hebu angalieni sekta ya kilimo tuwekeze kwenye wakulima wa miwa ili tuweze kuhakikisha kwamba tuna miwa ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia upungufu mkubwa wa sukari kwa sisi ambao tupo Kamati ya Uwekezaji tulitembelea yale mashamba, uzalishaji umekuwa wa chini, viwanda vimekosa *raw material.* Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo Mheshimiwa Waziri wa Fedha nikuombe ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nakuamini sana Daktari wa uchumi, hebu toa fedha saidia kwenye upande wa kilimo wananchi walime miwa ya kutosha, tuwekeze kwenye viwanda ili tuzalishe sukari ndani, hili ni eneo ambalo mimi nilishauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine kama kuna watu wanahujumu sekta ya sukari, ni muda muafaka Serikali ikawachukulia hatua kali sana. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Bashe wekeni sheria kali, ikitokea kuna upungufu wa sukari, kuna mtu anaficha sukari, wekeni sheria kali, aidha, mmfungie mfanyabishara na vitu vingine, haya ndiyo maeneo ambayo mimi ningependa kushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kikokotoo, nikiri kabisa Mheshimiwa Rais amefanya maamuzi ya tija kabisa ya kuongeza kikokotoo...

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Condester Sichalwe.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nataka tu kumuongezea taarifa Mheshimiwa Dkt. Chaya kwamba ambaye anabidi alete sheria kali sio Mheshimiwa Dkt. Mwigulu wala Waziri Bashe ni sisi Bunge ndiyo inabidi tutunge hiyo sheria. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Chaya unaipokea taarifa hiyo? *(Kicheko)*

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa taarifa ya Mheshimiwa wangu dada yangu nakubaliana na yeye. Tunahitaji kuleta sheria kali na Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa

Dkt. Mwingulu naomba msimamie hiyo sheria ije ili tuhakikishe kwamba wale ambao wanaihujumu Serikali tuweze kuwabana.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu kikokotoo, mimi nilichangia hapa Bungeni, kilio cha Watumishi wa Umma walikuwa wanapata asilimia 33 lakini Mheshimiwa Rais ameongeza saba sasa hivi wanaenda kupata asilimia 44, hayo ni mafanikio makubwa. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nikushukuru nikushukuru na umekiri uchumi utakapoimarika…

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Katani.

**TAARIFA**

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa Dkt. Pale ni asilimia 40 sio 44, ili ikae sawa hiyo asilimia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya unapokea taarifa hiyo?

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, mimi nilisema asilimia 40 sio 44. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, ameongeza asilimia saba kutoka 33 hadi 40, hili ni ongezeko kubwa sana kwa sisi ambao tulisoma arithmetic's tunajua. Lakini Mheshimiwa Dkt. Mwigulu umeahidi kwamba uchumi utakapotengamaa hebu sogeza sogeza ifike 50 lakini asilimia 40 mimi nina uhakika Mheshimiwa Rais anaenda kufanya. Lakini nina uhakika uchumi ukitengamaa na mapato yakitengamaa ile 50 ataifikia. Mheshimiwa Rais amefanya mambo makubwa sana sidhani kama atashindwa kufika asilimia 50 kama tumeweza kufanya mambo makubwa kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la utafiti kwenye kodi, wewe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni mtafiti wa uchumi *you are an academician.* Sidhani kama tunafanya tafiti za kutosha kwenye

masuala ya kodi, hili ni eneo tunahitaji kuliangalia na tafiti zetu tunazozifanya ni za aina gani? Tuna tafiti za aina nyingi, tunataka tafiti ambazo matokeo ya tafiti yataenda moja kwa moja kusema je, hii aina ya kodi ina tija? Je, ni kodi gani zina kelele? Je, tuongeze aina gani ya kodi? Mheshimiwa Dkt. Mwigulu naomba ushirikiane na Vyuo Vikuu, wanafanya tafiti nyingi lakini ukiangalia zile tafiti nyingi hazina tija.

Mheshimiwa Spika, Kuna tafiti moja inaitwa *action-oriented research, action-oriented research* ni *research* ambayo inaenda kufanya tafiti moja kwa moja yale matokeo yanaingizwa kwenye utekelezaji. Tafiti zetu nyingi Mheshimiwa Dkt. Mwigulu zinafanywa za kodi zinaingia kwenye *shelf*. Tunahitaji kuboresha sekta ya kodi, ili uweze kuboresha sekta ya kodi Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nilitegemea *TRA* wenyewe wafanye *operational research* wenyewe, wasitegemee watu wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, wanapofanya wenyewe tayari wanajua maeneo gani ya kodi ambayo hayafanyi vizuri *then* zile feedback za kutoka kwenye zile *research* wataziingiza moja kwa moja kwenye utekelezaji. Hili ni eneo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nikushauri ndugu yangu na kaka yangu hebu wekeza kwa *TRA*, fanyeni tafiti za mara kwa mara ili tuweze kuboresha suala la kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi, Mheshimiwa Dkt. Mwingulu wewe unatoka Singida na ni shahidi na huwa unapita wakati fulani ile barabara yangu ya daraja la Sanza. Lile daraja lipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kulingana na taarifa niliyopewa na Waziri wa Ujenzi kwamba mkandarasi alitakiwa kusaini mkataba kabla ya huu mwezi haujaisha, tuna kama siku 10 hivi mwezi uishe. Nikuombe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Rais alipokuja mwaka jana Manyoni aliwaahidi wananchi daraja linaenda kujengwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu una mradi wako pale Manyoni wa ukaguzi wa magari wa pamoja ule wa Mhalala. Ule mradi ulisimama mwaka 2016 umeshatumia zaidi ya bilioni 6, limeshakuwa pori Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, nikuombe Mheshimiwa Waziri, ule mradi wako kaufufue, tayari

umeshaanza kuleta kelele, najua nia ni njema na nina uhakika kabisa Mheshimiwa Rais atakwenda kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nina Mradi wa Kintinku Silile, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Aweso, mpaka sasa hivi ule mradi upo takribani asilimia 90 ya utekelezaji lakini mkandarasi kuna vihela hela vidogo vimebaki. Ningemuomba Waziri wa Fedha, basi mkamilishie yule mkandarasi vile vihela kwa sababu watu tayari wameshakunywa maji lakini mkandarasi yeye hajanywa hela, sasa asije akatufungia yale mabomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni tuliowapata katika kipindi chetu hiki kwa hiyo niwatangaze kwenu kabla hatujaaendelea na ratiba.

Wapo wageni 15 wa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina ambao ni Umoja wa Mapikipiki Jimbo la Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 37 wa Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, ambao ni Wanafunzi Kutoka Chuo Cha Ustawi wa Jamii Kampasi ya Kijitonyama Dar es Salaam wakiongozwa na Mbunge wa Bunge la Wanafunzi wa Chuo hicho. Sasa sijui na yeye anaitwa Mheshimiwa lakini hapa imeandikwa Ndugu Ngerekae Mshamu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 24 wa Mheshimiwa Joseph Anania Thadayo, ambao ni Jukwaa la Walimu Wazalendo kutoka Mwanga Mkoa wa Kilimanjaro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 61 wa Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, ambao ni Wanakwaya wa Kanisa la *PEFA* kutoka Kigoma Mjini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, ambaye ni mpigakura wake kutoka Korogwe Vijijini Mkoa wa Tanga. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu:-

(a) Maoni ya Kamati juu ya Ushahidi wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge, kuthibitisha Tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo kusema uongo na kulipotosha Bunge; na

(b) Uchunguzi wa Kamati juu ya Tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge, kudharau Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Maoni ya Kamati juu ya ushahidi wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge, kuthibitisha Tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo kusema uongo Bungeni na kulipotosha Bunge na Uchunguzi wa Kamati juu ya Tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge, kudharau Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Haki Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Ally Juma Makoa, aje awasilishe Maoni ya Kamati.

**MHE. ALLY J. MAKOA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kutokana na muda naomba Taarifa yote ya Kamati iingie kwenye kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu: - Maoni ya Kamati kuhusu ushahidi wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge, kuthibitisha tuhuma dhidi ya Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mbunge, kusema uongo Bungeni na kulipotosha Bunge; na Tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, kudharau Mamlaka ya Spika, Bunge na Mwenendo wa Shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utangulizi; kwa mujibu wa Fasili ya 4(2) na (3) ya Nyongeza ya 8 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati kuhusu: -

(a) Maoni ya Kamati kuhusu ushahidi wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kuthibitisha Tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe kusema uongo Bungeni na kulipotosha Bunge; na

(b) Uchunguzi wa Kamati kuhusu tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kudharau Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru wewe binafsi kwa weledi, busara na hekima unazozitumia katika kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Bunge letu kwa Miongozo na maelekezo wanayoipa Kamati yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 18 Juni, 2024 kwa mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 na Fasili ya 4(1)(a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ulielekeza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kutoa maoni na kutoa ushauri kuhusu masuala yaliyotajwa hapo juu. Hadidu za rejea zilielekeza: -

(a) Kutafakari jambo lililofanywa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na kutoa maoni na mapendekezo ya nini kifanywe na Bunge;

(b) Kufanyia kazi ushahidi uliowasilishwa kwa Mheshimiwa Spika na kutoa maoni iwapo ushahidi huo unathibitisha tuhuma kwamba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amesema uongo Bungeni na nini kifanywe na Bunge;

(c) Kuwasilisha Taarifa kwa Spika Jumatatu tarehe 24 Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chimbuko la shauri, tarehe 4 Juni, 2024 katika Kikao cha 40 cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge wakati wa mjadala wa Hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mbunge, pamoja na mambo mengine, alichangia kuhusu upungufu wa

sukari nchini *(gap sugar)* kwamba, kampuni na viwanda vya sukari nchini, vilivyopewa dhamana na Serikali ya kuhakikisha kunakuwa na sukari ya kutosha nchini, vimeshindwa kutekeleza wajibu huo kwa kushindwa kuagiza na kusambaza sukari kutoka nje ya nchi kama ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe alieleza kuwa, hali hiyo imesababisha kuendelea kuwepo kwa tatizo la uhaba wa sukari nchini. Aidha, Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe alieleza kuwa jambo hilo lilichangia bei ya sukari nchini kupanda hadi kufikia shilingi 10,000 kwa kilo moja.

Mheshimiwa Spika, miezi michache iliyopita Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe alieleza kuwa kutokana na hali hiyo Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha sukari ya kutosha inakuwepo nchini. Miongoni mwa hatua hizo ni kuipa idhini Wakala wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* kuingiza sukari nchini, kutoa vibali kwa makampuni ili kuagiza sukari na kusamehe kodi na ushuru kwa sukari itakayoingizwa kutoka nje ya nchi na makampuni na viwanda vya sukari. Maelezo hayo yapo kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge za tarehe 04 Juni, 2024 zinazomnukuu Mheshimiwa Hussein Bashe akisema ifuatavyo: -

> *"Mheshimiwa Spika, naomba nitoe elimu ndogo, gap sugar huwa tunaitoa kwa ajili ya window ya mwezi Machi, Aprili na Mei, miezi mitatu. Kutokana na mvua za El-Nino, baada ya TMA kutoa utabiri wa hali ya hewa, tuliyapatia makampuni na viwanda walete tani 50,000, mpaka mwezi Februari walikuwa hawajaleta hata kilo moja ya sukari na walipoingiza walifungia kwenye ma-godown yao...mwaka jana tulivyowapa vibali vya kuingiza na mpango mkakati ukiongozwa na TSPA, Tanzania Sugar Association ambaye Mwenyekiti wa Taasisi hii ni owner wa Mtibwa na Kagera Sugar…tumekaa Disemba, hakuna kilo moja iliyoingia, Januari, hakuna kilo moja iliyoingia.*

*Mwishoni mwa Januari wameingiza tani 250 wakati wakifahamu sugar na buffer stock ya mwaka wa nyuma wa uzalishaji hawakuingiza hata kilo moja, kwa hiyo Taifa lilikuwa halina sukari…tumewapa bei elekezi … shilingi 2,300 na 2,500. Waliwauzia distributors kwa shilingi 2,800 na 3000 na sukari waliyoingiza bandarini tuliyowapa VAT exemption, hata wao tumewapa VAT exemption. Wameingiza bandarini wanaenda kuiuza mfuko wa kilo 50, Dar es Salaam shilingi 150,000 mpaka 160,000 mlaji wa Nzega ale kwa shilingi ngapi?"*

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe akizungumza, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge, alipata nafasi ya kutoa Taarifa kuhusu mchango huo. Taarifa ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ilieleza kuwa, Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe alikuwa analidanganya na kulipotosha Bunge kwa sababu, maelezo hayo hayana ukweli wowote na alikiuka Sheria katika zoezi la kutoa vibali vya kuagiza sukari na kwa kusamehe kodi ya Serikali. Kwa mujibu wa Kumbukumbu Rasmi za Bunge za tarehe 4 Juni, 2024 Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mbunge, alinukuliwa akisema ifuatavyo: -

*"Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zipo taarifa za wazi kwamba Waziri hata hao waliosema kwamba aliwapa kibali cha kuingiza sukari, hakutangaza tender yoyote na haijulikani aliwapataje, lakini nyaraka zote zipo, na kuwa kuagiza sukari zaidi ya gap sugar ni makosa kisheria. Na kwa kuwa pia kuwaruhusu watu ambao hawaruhusiwi kwa mujibu wa Sheria tuliyonayo sasa ya sukari ni makosa kisheria...Uagizaji wa gap sugar huwa unakuwa established na ile Timu ya Bodi ya Sukari ambayo inafanya na inawajulisha na wadau.*

*Sasa Waziri anasema kwamba ametoa Kibali cha tani 410,000 kama gap sugar…mpaka sasa hivi taarifa zilizopo katika hiyo tani 410,000 zimeshaingia tani 220,000…huu ni mwezi wa sita…gap sugar ambayo imekuwa established na hiyo Timu ya ushauri ya Bodi ya Sukari ni tani 120,000 siyo tani 410,000 na nchi yetu*

*haijawahi kuwa na importation ya namna hiyo hata kama uzalishaji huo anaousema yeye.*"

Mheshimiwa Spika, baada ya Taarifa hiyo ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge, ulitoa ufafanuzi kuhusu masharti ya Kanuni ya 70(1)(2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Inayosimamia suala la Mbunge kutosema uongo Bungeni. Kanuni inamtaka Mbunge yeyote anayetoa tuhuma kwamba Mbunge mwingine anasema uongo Bungeni, hutakiwa kuwasilisha ushahidi ili kuthibitisha uongo huo. Hivyo, kwa kutumia Kanuni hiyo, ulielekeza Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina awasilishe ushahidi kuthibitisha tuhuma kwamba Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe amelidanganya Bunge tarehe 14 Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 14 Juni, 2024 Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina aliwasilisha Ofisi ya Bunge barua yenye nyaraka za ushahidi kama ulivyoelekeza. Hata hivyo, kabla Bunge halijachukua hatua yoyote ya kujiridhisha kuhusu ushahidi huo, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina aliitisha Mkutano wa Waandishi wa Habari ambao aliutumia kueleza na kufafanua maudhui ya ushahidi aliouwasilisha kwa Spika.

Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni ya 4 ya Nyongeza ya 8 na Kanuni ya 84 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ulielekeza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itoe maoni kuhusu ushahidi uliowasilishwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na kufanya uchunguzi wa kitendo cha Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kuitisha Mkutano wa vyombo vya habari na kuzungumzia ushahidi aliouwasilisha kwa Spika. Aidha, ulielekeza Kamati kutoa mapendekezo kwa Bunge kuhusu hatua za kuchukua. Kamati ilielekezwa kukamilisha Taarifa ya Kamati ifikapo Jumatatu tarehe 24 Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchunguzi wa Kamati, Maoni ya Kamati kuhusu ushahidi wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kuthibitisha tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe kusema uongo Bungeni na kulipotosha Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika uchunguzi wa suala hili Kamati iliwaita mashahidi ambao ni Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe. Mashahidi hao waliitwa kwa *summons* zilizowataka kufika kwenye Kamati kutoa ushahidi na kuwasilisha nyaraka. Mashahidi walitii Wito wa Kamati na walitoa ushirikiano kwa kutoa ushahidi ulioisaidia Kamati kupata maoni kuhusu uchunguzi uliokuwa umefanywa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchunguzi wake kuhusu Taarifa iliyotolewa Bungeni kumlalamikia Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe kwamba alisema uongo Bungeni. Kamati imezingatia maelezo yaliyotolewa na Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na yaliyotolewa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina pamoja na vielelezo vyote walivyoviwasilisha mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa Kamati ulijikita katika Taarifa kuhusu uongo uliosemwa Bungeni tarehe 14 Juni, 2024 iliyotolewa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kuhusu maelezo yaliyotolewa na Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe kwa kufanya rejea ya *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa hoja zote zilizowasilishwa na pande zote mbili uchambuzi na maoni ya Kamati ni kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alisema kuwa waziri alilidanganya Bunge kwa kusema mwaka jana nchi hii ilikuwa na *gap* ya tani 60,000; tulimpa Kagera *Sugar*, Mtibwa, Bagamoyo, *TPC*, lakini hakuna aliyeingiza hata kilo moja, alidai kuwa Viwanda viliingiza sukari kwa mwaka huo. Mheshimiwa Waziri aliieleza Kamati kuwa ni kweli Viwanda alivyovitaja havikuingiza hata kilo moja. Alifafanua kuwa walioingiza sukari ni Kiwanda cha Kilombero na Kampuni nyingine ambayo si mzalishaji. Hivyo, maelezo ya Mheshimiwa Waziri yalikuwa ya ukweli kama ambavyo alivyoeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye jambo hili ni kwamba, ukichukua *Hansard* halafu ukasoma yale maneno ya Mheshimiwa Bashe, utagundua alitaja viwanda *specific* ambavyo ndivyo vilikuwa havijaingiza sukari. Kwa maana hiyo, ieleweke kwamba viwanda ambavyo havikuingiza sukari ni vile viwanda alivyovitaja kwenye *Hansard*. *(Makofi)*

Aidha, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alieleza kuwa Waziri alidanganya kwa kusema *sugar gap* kwa mwaka 2022/2023 ilikuwa tani 60,000. Alitoa ushahidi kuwa Bodi ya sukari ilieleza kuwa *sugar gap* ni tani 30,000. Waziri katika utetezi wake alileta ushahidi wa Muhtasari wa Kikao cha Waziri na Wadau wa Sukari cha tarehe 13 Februari, 2023 ambacho kiliidhinisha *gap sugar* ya tani 30,000 na *buffer stock* ya tani 30,000 hivyo kufanya jumla ya upungufu wa tani 60,000 za sukari. Kamati baada ya kupitia maelezo hayo imejiridhisha kuwa, maelezo na vielelezo vya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina yalikuwa sahihi kwa upande wa *sugar gap* na maelezo ya Mheshimiwa Waziri hayakulipotosha Bunge kwakuwa aliongelea *gap sugar* pamoja na *buffer stock*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alimtuhumu Mheshimiwa Waziri kuwa amelidanganya Bunge kwa kusema wamebadili kanuni za *National Food Reserve Agency* kuruhusu *NFRA* kuwa na *mandate* ya kuingiza sukari wakati hakuna Tangazo la Serikali *(GN)* iliyotangazwa kuipa *NFRA mandate* ya kuingiza sukari.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliieleza Kamati kuwa walitumia Sheria ya Usalama wa Chakula Sura ya 249 kukabiliana na uhaba wakati wa dharura kupitia *NFRA*. Alisema kuwa wameanza mchakato wa kubadilisha Sheria ili *NFRA* waruhusiwe kuagiza, kuhifadhi na kusambaza sukari hata kwa kipindi kisicho cha dharura na mchakato huo ulianza kwa kutoa Tangazo la Serikali Na. 225B la tarehe 01 Aprili, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tasnia ya Sukari kuhusu wanaoruhusiwa kuingiza sukari na kupitia Kifungu cha 15 cha Sheria ya Usalama wa Chakula, 1991 na kubaini kuwa kwa wakati wa dharura kama iliyojitokeza Sheria

ya Usalama wa Chakula inakuwa na nguvu zaidi kuliko Sheria ya Tasnia ya Sukari. Kamati ilipata nafasi ya kujiridhisha kuhusu uwepo wa *GN* Na. 225B ya tarehe 1 Aprili, 2024 na kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha iliona mapendekezo ya marekebisho yaliyoelezwa na Waziri. Kupitia *Hansard* na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, Kamati ilikuwa na maoni kuwa hakuna uongo uliozungumzwa na kwamba hakuna ukiukwaji wa Sheria uliofanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alimtuhumu Mheshimiwa Waziri kwa kutoa vibali vya tani 410,000 kinyume na *sugar gap* iliyoidhinishwa ya tani 100,000. Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa Kamati ya Ufundi ya Bodi ya Sukari ilibaini upungufu ni tani 220,000 hadi Aprili, 2024. Hata hivyo, kutokana na tathmini iliyofanywa na Wizara ilibainika kuwa uzalishaji uliathirika kutokana na *El-Nino* na kutokana na uhaba uliokithiri kwa miezi ya Januari na Februari, 2024 nchi ilihitaji kuwa na uhakika wa sukari kwa ziada "*buffer stock*" hivyo kuidhinisha makisio ya *gap sugar* ya tani 410,000.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliileza Kamati yetu kuwa vibali vilitolewa kwa tani 220,000 pekee na kwamba mpaka sasa zimeingia tani 180,000. Tani zilizosalia bado hazijatolewa vibali na kwamba wataendelea kufuatilia mwenendo wa uzalishaji na upatikanaji wa sukari nchini kabla ya kuamua kutoa vibali vingine au kusitisha kabisa uagizaji kwa mwaka 2023/2024 kama hali ya viwanda itaendelea kuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika kuwa Kiwango cha tani 100,000 alichokisema Mheshimiwa Luhaga Mpina ni maksio yaliyofanyika mwezi Disemba, mwaka 2023. Kiwango hicho kilifanyiwa marekebisho mwezi Aprili, 2024 ambapo Kamati ilioneshwa Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Ufundi kilichobainisha ongezeko la *sugar gap* kutoka tani 155,000 hadi tani 220,000. Kiwango cha tani 410,000 alizozisema Mheshimiwa Waziri zilijumuisha mahitaji yaliyokadiriwa mwezi Aprili, na tathmini iliyofanyika baadaye iliyobaini kuwa hadi Mei, 2024 viwanda havikuwa vimeanza uzalishaji hivyo mahitaji pamoja na *buffer stock* kufikia Disemba, 2024 ni tani 410,000 hivyo kutoa idhini ya tani hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ifahamike hapa kilichotoka kwa Serikali ni idhini siyo vibali, idhini ya tani 410000 lakini vibali vilivyotoka mpaka sasa ni 220000 peke yake na sukari iliyoingia ni hiyo tani 180000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alimtuhumu Mheshimiwa Waziri kuwa hakuwaita wenye viwanda kukaa nao kuhusu suala la sukari. Mheshimiwa Waziri amesema kuwa hakukataa kukutana na wazalishaji isipokuwa aliwapa masharti ya kutangaza mawakala kwa kila mkoa na kufungua maghala kila mkoa kabla ya kukutana nao. Baada ya Kamati kusikiliza ushahidi iliridhia kuwa Mheshimiwa Waziri hakukutana nao kwakuwa hawakuwa wametekeleza masharti aliyokuwa amewapa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina anamtuhumu Waziri wa Kilimo kwa kukiuka Sheria wakati wa kutoa vibali kwa makampuni ambayo si wazalishaji wa sukari bila kutangaza zabuni. Mheshimiwa Waziri alieleza Kamati kwamba vibali vilitolewa wakati wa dharura baada ya kufanya utafiti na kujiridhisha kuhusu uwezo wa kampuni hizo. Aidha, alieleza kuwa katika mazingira ya dharura na kwa kuzingatia kuwa fedha zinazotumika sio za umma, hakukuwa na ulazima wa kutumia Sheria ya Ununuzi. Vilevile Mheshimiwa Waziri aliwasilisha ushahidi wa leseni za biashara na nyaraka za usajili wa kampuni hizo zinazowaruhusu kufanya biashara ya sukari. Kamati ilijiridhisha kwamba utaratibu uliotumika ulikuwa ni wa hali ya dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa Kamati kuhusu tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kudharau Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge. Baada ya kamati kupokea Hadidu za Rejea kuhusu kufanya uchunguzi wa tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, tarehe 18 Juni, 2024 ilikutana kujadili na hatimaye ikaamua Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina apewe Wito wa kufika mbele ya Kamati ili aweze kujibu tuhuma zinazomkabili.

Mheshimiwa Spika, wito huo ulimtaka Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina atoe maelezo ya kwanini asichukuliwe hatua kwa

kukiuka Kifungu cha 26(d)(e) na 34(1)(g) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi za Bunge Sura ya 296 pamoja Kanuni ya 84(1)(j) na (k) ambazo zinakataza kudharau Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa shughuli za Bunge. Tarehe 19 Juni, 2024 Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alikabidhiwa Hati ya wito huo na kufika mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Katika kushughulikia suala hili, ili Kamati iweze kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma hizo, ilijielekeza kwenye hoja za uchunguzi *(issues)* zifuatazo:

(a) Je, ni kweli kwamba Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) aliitisha Mkutano na vyombo vya habari na kuzungumza kuhusu maudhui ya ushahidi aliouwasilisha Bungeni kabla Bunge halijaufanyia kazi na kukamilisha uchunguzi wake?

(b) Endapo hoja (a) itathibitika, Je, kitendo cha Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kuzungumza na Waandishi wa Habari kuhusu ushahidi alioupeleka kwa Spika ni kudharau mamlaka ya Spika na mwenendo wa Shughuli za Bunge?

(c) Endapo hoja (a) na (b) ni kweli, Je, ni hatua gani za Kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake?

Mheshimiwa Spika, Katika uchunguzi wake, Kamati ilirejea Sheria, Kanuni za Kudumu za Bunge, Taarifa Rasmi za Bunge na ushahidi wa picha za *video* za Mkutano wa Waandishi wa Habari na Mheshimiwa Luhaga Mpina. Rejea hizo ilikuwa ni:

(a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

(b) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023;

(c) Kumbukumbu Rasmi za Bunge za tarehe 4 Juni, 2024, tarehe 18 Juni, 2024;

(d) Ushahidi uliowasilishwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kwa Spika;

(e) Mahojiano na nyaraka za ushahidi zilizowasilishwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alipokuwa mbele ya Kamati;

(f) *Video* ya tarehe 4 Juni, 2024 iliyoonesha majadiliano ya Bunge kuhusu mchango wa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussen Mohamed Bashe; na

(g) *Video* inayomuonesha Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina akiongea na Mkutano wa Waandishi wa Habari aliouitisha.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu hoja ya kwamba je, ni kweli kwamba Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) aliitisha Mkutano na vyombo vya habari na kuzungumza kuhusu maudhui ya ushahidi aliouwasilisha Bungeni kabla Bunge halijaufanyia kazi na kukamilisha uchunguzi wake? Kamati ilianza kuchunguza Shauri hili kwa kuangalia picha za *video* za Mkutano wa Waandishi wa Habari ulioitishwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina (Mb) tarehe 14 Juni, 2024. Sehemu ya maelezo ambayo Kamati iliyaona na kuyasikia kutoka kwenye *video* hiyo yalieleza kuwa:-

Mheshimiwa Spika, "kufuatia maagizo ya kiti nalazimika kuandaa maelezo na kuwasilisha kwa Mheshimiwa Spika leo tarehe 14 Juni,2024 nikiwasilisha ushahidi wa vielelezo vya kuthibitisha uongo wa Waziri Bashe aliousema bungeni tarehe 4 Juni, 2024. *Gap sugar* iliyoidhinishwa kwa msimu wa mwaka 2022/2023 ni tani 30,000 sio 60,000 kama alivyosema Waziri wa Kilimo. Rejea barua ya Bodi ya Sukari Tanzania yenye Kum. *Ref.No.SBT/DGO/26-38* ya tarehe 29 Machi, 2023 iliyoandikwa na Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari, Profesa Bengesi kwenda kwa Katibu Mtendaji wa *TCS SAD*"

Mheshimiwa Spika, Baada ya kuangalia *video* na kuchambua nyaraka zilizowasilishwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kwa Spika, Kamati ilimuita Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ili aweze kutoa utetezi wake.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kufika mbele ya Kamati alitoa maelezo kuwa Kamati haina mamlaka ya kusikiliza shauri kwa kuwa vifungu vilivyotajwa katika Hati ya Wito ambavyo ni 26(d)(e) na 34(1)(g) pamoja na Kanuni ya 84(1)(j) na (k) vinatofautiana na kifungu kilichotajwa katika Taarifa ya Spika ya tarehe 18 Juni, 2024 ambacho ni kifungu cha 29(d) na (e). Kwa maoni yake, Mheshimiwa Mbunge alieleza kuwa kifungu hicho ndicho Mheshimiwa Spika alikusudia kukitumia kumshitaki.

Mheshimiwa Spika, katika kupata jibu la hoja hii, Kamati ilirejea Sheria, *Hansard* na nakala halisi ya Taarifa ya Spika na kujiridhisha kuwa vifungu vilivyotumika katika Hati ya Wito aliyopewa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ni sahihi na ndivyo vinavyoipa Mamlaka Kamati kufanya uchunguzi wake. Vifungu vilivyotajwa katika Hati ya Wito ni Kifungu cha 26(d)(e) na 34(1)(g) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge pamoja na Kanuni ya 84(1)(j) na (k) ambavyo ni vifungu vinavyoeleza makosa anayotuhumiwa kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 26 kinaeleza; "26. *Any person who shows disrespect in speech or manner towards the Speaker; or does any other act of intentional disrespect to or with reference to the proceedings of the Assembly or of a Committee of the Assembly or to any person presiding at such proceedings, commits an offence.*" Maneno ya Kisheria hayo mimi siyo mwanasheria. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 34 kinaeleza: "*34*(1) *Any person who publishes, save by the general or special leave of the Assembly, any paper, report or other document prepared expressly for submission to the Assembly before the same has been laid on the table of the Assembly; commits an offence and on conviction is liable to a fine not exceeding five hundred thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding three years or to both.*"

Mheshimiwa Spika, Vifungu tajwa vinazuia vitendo vya dharau kwa Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge. Baada ya kuchambua vifungu hivyo Kamati iliona kuwa hoja ya kwamba

Kamati haina mamlaka ya kusikiliza shauri dhidi yake ni hoja isiyo na nguvu Kisheria. Kwa hali hiyo, Kamati ilifikia uamuzi kuwa inayo mamlaka ya kufanya uchunguzi wa shauri linalomkabili Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujiridhisha kuhusu mamlaka ya Kamati, Kamati ilimtaka Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kutoa maelezo kuhusu tuhuma zinazomkabili. Katika maelezo yake Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alikiri kuwa aliitisha Mkutano wa Waandishi wa Habari kueleza umma kwamba ametekeleza maelezo ya Mheshimiwa Spika kwa kupeleka ushahidi kwa Mheshimiwa Spika ili kuthibitisha tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe kusema uongo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipohoji ni kwa nini alivieleza vyombo vya habari ushahidi aliouwasilisha kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina aliieleza Kamati kuwa alichokiwasilisha kwa vyombo vya habari ni maelezo yake binafsi na siyo vielelezo vya ushahidi alivyopeleka kwa Mheshimiwa Spika ambavyo kwa maoni yake, ndiyo ushahidi. Katika kufafanua jambo hilo, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alieleza kwamba anayo haki kama Mbunge kuwafahamisha wananchi kuhusu namna alivyotekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Spika hivyo hakufanya kosa lolote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina aliendelea kueleza kwamba, Kanuni ya 70 kuhusu kuthibitisha tuhuma za uongo bungeni haina masharti yanayomzuia Mbunge anayethibitisha tuhuma kuzungumza na vyombo vya habari. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alitoa mfano wa Wabunge wengine wanaothibitisha tuhuma za uongo ndani ya Bunge ambao katika kufanya hivyo wanaoneshwa na vyombo vya habari ha hakuna Kanuni inayovunjwa.

Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi kuwa maelezo ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina mbele ya vyombo vya habari ndiyo ushahidi aliouwasilisha kwa Spika. Utetezi wake kwamba, maelezo yake hayakuwa/siyo ushahidi bali vielelezo alivyoambatisha kwenye maelezo yake hauna msingi kwa kuwa,

maelezo na viambatisho vyake vyote ni ushahidi ambao unatakiwa kufanyiwa kazi na Spika kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kuitisha Mkutano wa Waandishi wa Habari muda mfupi baada ya kuwasilisha Taarifa ya Spika Bungeni, Kamati imeona kuwa, hakikuwa na nia njema na hakioneshi heshima kwa Mamlaka ya Spika. Aidha, utetezi kwamba, Kifungu cha 70 hakizuii Mbunge anayetuhumu kuzungumza na vyombo vya habari haukubaliki. Vilevile kitendo alichokifanya ni tofauti na Wabunge wanaokuwa Bungeni na kupigwa picha wakichangia, hii ni kwa sababu upo utofauti wa kimazingira.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 70(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inaweka masharti yanayomtaka Mbunge aliyetoa tuhuma kwamba, Mbunge mwingine amesema uongo kuthibitisha tuhuma hizo. Maelezo ya Shahidi kwamba, ushahidi ni vielelezo hayana uzito kwa sababu, nyaraka zinazopelekwa kwa Spika ikiwemo maudhui ya nyaraka alizowasilisha ndiyo ushahidi wenyewe na haukupaswa kuzungumzwa popote baada ya kufikishwa kwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barua ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina iliyowasilishwa kwa Spika yenye Kumb. Na. MB/KSS/2024/55 ya Tarehe 14 Juni, 2024 iliambatishwa na maelezo na vielelezo (viambatisho) mbalimbali. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina aliziita nyaraka hizo kuwa, ni ushahidi kama inavyoonekana katika kichwa cha habari cha barua yake ambacho kinasomeka, "Yah: Kuwasilisha Ushahidi Kuhusu Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe (Mb) Kusema Uongo Bungeni". Kwa hali hiyo, maelezo na viambatisho ni kitu kimoja, kama barua yake inavyoonesha na huo ndiyo ushahidi aliouwasilisha kwa Spika. Katika hatua hiyo, kwa kuwa, ushahidi huo ulikuwa mikononi mwa Spika, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, hakuruhusiwa kuuzungumzia.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo kamati imejiridhisha kuwa, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina alizungumza na vyombo vya habari kuhusu ushahidi aliouwasilisha kwa

Mheshimiwa Spika kabla ushahidi huo haujafanyiwa kazi na Spika au Bunge, kama inavyoelekezwa na Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, shahidi aliendelea kujitetea kuwa, Kifungu cha 26(d) na (e) na 34(1)(g) pamoja na Kanuni ya 84(1)(j) na (k) ya Kanuni za Kudumu havihusiani na maelezo aliyoyatoa kwenye Mkutano wa vyombo vya habari kwa kuwa, vifungu hivi havina mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Mbunge na Spika. Shahidi aliendelea kufafanua kuwa, maelezo yake kwa wanahabari yalilenga kuwapa taarifa wananchi kuhusu kazi anazozifanya na kuwafahamisha kuwa, ametekeleza maelekezo ya Spika ya kuwasilisha ushahidi.

Mheshimiwa Spika, kamati inaona kuwa, maelezo hayo ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina hayana uzito wowote bali ni uthibitisho kuwa aliongea na vyombo vya habari kuhusu ushahidi aliouleta kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mbunge au mtu mwingine yeyote anao wajibu wa kuheshimu mamlaka, hadhi na heshima ya Spika na mwenendo wa Shughuli za Bunge. Mbunge, kama sehemu ya Bunge na kiongozi wa umma, analo jukumu kubwa zaidi la kuhakikisha kuwa, kila afanyalo na kila analolisema linaakisi heshima na hadhi ambayo Bunge linastahili. Kwa hali hiyo, Mbunge kwa nafasi yake kama kiongozi wa umma, hatakiwi kuzungumza na vyombo vya habari kuhusu jambo lililowasilishwa kwa Spika ambalo linasubiri kufanyiwa kazi na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuthibitisha hoja (a) Kamati ilijielekeza katika hoja, Je, kitendo cha Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kuzungumza na Waandishi wa Habari kuhusu ushahidi alioupeleka kwa Spika ni kudharau mamlaka ya Spika na mwenendo wa shughuli za Bunge?

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 26 (d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura 296 *(The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP 296)* kinakataza vitendo vya kumkosea heshima Spika kwa maneno au vitendo. Halikadhalika, Kifungu cha 26 (e) cha Sheria hiyo kinazuia vitendo vya dharau kwa Mwenendo wa Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kwenda kuzungumza kwenye vyombo vya habari kuhusu maudhui ya ushahidi wa nyaraka alizoziwasilisha kwa Spika muda mfupi baada ya kufikisha ushahidi huo Bungeni ni kitendo cha ukosefu wa nidhamu kwa kutoheshimu Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge. Hivyo, haikubaliki Mbunge kuzungumza na vyombo vya habari kuhusu jambo alilopeleka kwa Spika, ili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kitendo hicho cha Mbunge ni dharau kwa Mamlaka ya Spika na kuingilia Mwenendo wa Bunge. Kwa kufanya hivyo, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ameshashusha hadhi na heshima ya Bunge na kulidhalilisha mbele ya jamii hivyo, kukiuka Masharti ya Kifungu cha 26(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura 296. Vilevile, kitendo hicho ni utovu mkubwa wa nidhamu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) (j) na (k) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Kifungu cha 34(1)(g) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura 296 kinazuia kuchapisha kwa umma taarifa zilizoandaliwa mahususi, kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni na kabla taarifa hizo kuwekwa Mezani. Kitendo cha Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kuitisha Mkutano wa Waandishi wa Habari na kutoa ufafanuzi wa ushahidi alioupeleka kwa Spika ni kukiuka Kifungu cha 34(1)(g) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura 296 kinachokataza kusambaza kwa umma, taarifa zinazofanyiwa kazi na Bunge pasipo kupata kibali cha Bunge.

Mheshimiwa Spika, ushahidi uliopo, kitendo kilichofanywa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, masharti ya Sheria na Kanuni za Bunge, kamati imemkuta na hatia Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) kwa kosa la kudharau Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge. Kitendo hicho kinakatazwa na ni kinyume na Kifungu cha 26(d) na (e) na 34(1)(g) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura 296. Aidha, kitendo hicho ni utovu mkubwa wa nidhamu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1)(j) na (k) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujibu hoja hizo mbili za maswali, kamati ilijielekeza kwenye Hoja ya mwisho. Kwamba, je, ni hatua gani za Kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake, Mheshimiwa Mpina?

Mheshimiwa Spika, katika kujibu hoja hii, kamati ilizingatia Sheria na Kanuni pamoja na kutafakari kwa kina ushahidi uliotolewa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) kuhusu suala hili. Aidha, kamati ilizingatia maelezo yake kwamba, yeye ni Mbunge wa muda mrefu chini ya viongozi wengi wa Bunge, kutowahi kufikishwa mbele ya Kamati ya Maadili na kuwa, yeye ni mtiifu kwa viongozi na shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufikia uamuzi, kamati ilitafakari utetezi wake na ilizingatia aina ya kosa lililofanyika, namna kosa hilo lilivyofanyika na pia, athari ya kitendo hicho kuhusu heshima na hadhi ya Bunge na uongozi wa Bunge. Vilevile kamati ilitilia maanani sifa na uzoefu anaopaswa kuwanao Mbunge katika kupima matendo yake na athari zinazoweza kujitokeza kupitia kauli na vitendo vyake, pamoja na wajibu wake katika kuheshimu Sheria na Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa soika, katika hili Kamati iliona kuwa, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina akiwa ni Mbunge wa kipindi kirefu anapaswa kuonesha taswira njema ya uzingatiaji wa Maadili, Sheria na Kanuni za Bunge, ili awe mfano bora kwa Wabunge wengine. Hivyo, kitendo cha kutoheshimu Mamlaka ya Spika ni jambo linaloshusha heshima ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 33 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura ya 296, kinatoa mamlaka kwa Bunge kupitia Azimio kutoa adhabu kwa mtu ambaye amekiuka masharti ya Kifungu cha 26 au Sheria yoyote kuhusu kudharau mamlaka ya Bunge. Adhabu iliyotamkwa na Sheria ni ya kumsimamisha Mbunge kuhudhuria Vikao vya Bunge kwa namna itakavyoamuliwa kwa mujibu wa Sheria. Kifungu hicho kinaeleza, na mimi nanukuu:-

*"33–(1) Where any Member commits any contempt of the Assembly whether specified in Section 26 or otherwise, the*

*Assembly may, by resolution, either direct the Speaker to reprimand such Member or suspend him from the service of the Assembly for such period as it may determine. Provided that, such period shall not extend beyond the last day of the session next following that which the resolution was passed or of the session in which the resolution is passed as the Assembly may so determine".*

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za kudumu za Bunge zinaweka adhabu kwa vitendo vilivyovifanywa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, kama ifuatavyo:-

(a) Ikiwa kosa ni la kwanza, Mbunge kutohudhuria Vikao vya Bunge visivyopungua kumi na visivyozidi vitano, na visivyozidi kumi na tano, *I am sorry*, narudia. Ikiwa kosa ni la kwanza, Mbunge kutohudhuria Vikao vya Bunge visivyopungua kumi na visivyozidi kumi na tano;

(b) Ikiwa ni kosa lake la pili au zaidi Mbunge kutohudhuria vikao vya Bunge visivyopungua kumi na tano au visivyozidi ishirini; na

(c) Kanuni ya 84(4) inaweka masharti kwa Bunge kuzingatia ushauri mwingine wowote utakaotolewa na kamati kuhusu adhabu anayostahili kupewa Mbunge aliyekiuka masharti ya kanuni hii.

Mheshimiwa Spika, huo ndio ulikuwa uchunguzi wa kamati kuhusu Shauri la Kuwasilisha Nyaraka za Ushahidi kwa Spika na wakati huohuo kwenda kuzungumza kwenye vyombo vya habari kuhusu maudhui ya ushahidi huo kabla haujafanyiwa kazi na Spika na Bunge kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Spika, kamati imejiridhisha kuwa, kitendo alichofanya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ni utovu mkubwa wa nidhamu kwa Bunge kwa sababu ya kudharau Mamlaka ya Spika, kuingilia Mwenendo wa Shughuli za Bunge na vilevile ni kitendo kinachofedhehesha, kushusha hadhi na heshima ya Bunge. Hivyo, Kamati inaliomba Bunge litafakari shauri hili linalomhusu Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb), ushahidi

uliopo, Sheria na Kanuni na kuuzingatia wakati wa kupitisha Azimio la kutoa adhabu anayostahili kwa kosa alilotenda.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Napenda kutumia fursa hii kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali, ili kuhakikisha kuwa, ustawi wa wananchi ndio kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa shauri la utovu wa nidhamu kwa Bunge na Spika, kudharau Mamlaka ya Spika, kuingilia Mwenendo wa Bunge na kushusha hadhi na heshima ya Bunge. Wajumbe hawa waliofanya kazi hii walizingatia misingi ya haki, bila kumwonea au kumpendelea mtu yeyote. Kwa heshima naomba, kutokana na muda, majina yao yaingie kwenye *Hansard* za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa dhati sana Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *NDC,* kwa kuisaidia kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee nawashukuru Ndugu Pius T. Mboya, Mkurugenzi Idara ya Huduma za Sheria, Ndugu Agnes Ivor Ndumbati, *NDC,* Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Huduma za Sheria, Ndugu Maria Mdulugu, Katibu wa Kamati, Ndugu Ludovick Ringia, Ndugu Thuwaiba Jumbe, Sekretarieti na Ndugu Mainda Shaban kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa, Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupokea maoni na mapendekezo ya kamati, ili baada ya mjadala liazimie kuchukua hatua stahiki kwa kadiri litakavyoona inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasoma na Azimio?

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**24 JUNI, 2024**

**TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE KUHUSU:-**

**1. MAONI YA KAMATI KUHUSU USHAHIDI WA MHE. LUHAGA JOELSON MPINA (MB) KUTHIBITISHA TUHUMA DHIDI YA WAZIRI WA KILIMO, MHE. HUSSEIN MOHAMED BASHE (MB) KUSEMA UONGO BUNGENI NA KULIPOTOSHA BUNGE**

**NA**

**2. TUHUMA DHIDI YA MHE. LUHAGA JOELSON MPINA KUDHARAU MAMLAKA YA SPIKA, BUNGE NA MWENENDO WA SHUGHULI ZA BUNGE – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 **UTANGULIZI**

1.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Fasili ya 4(2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati kuhusu:

a) Maoni ya Kamati kuhusu ushahidi wa Mhe. Luhaga Joelson Mpina kuthibitisha Tuhuma dhidi ya Mhe. Hussein Mohamed Bashe kusema uongo Bungeni na kulipotosha Bunge.

b) Uchunguzi wa Kamati kuhusu tuhuma dhidi ya Mhe. Luhaga Joelson Mpina kudharau Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge.

1.2 **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kukushukuru wewe binafsi kwa weledi, busara na hekima unazozitumia katika kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Bunge letu kwa Miongozo na maelekezo wanayoipa Kamati yangu katika kutekeleza majukumu yake.

1.3 **Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 18 Juni, 2024 kwa mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni

za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 na Fasili ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ulielekeza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kutoa maoni na kutoa ushauri kuhusu masuala yaliyotajwa hapo juu. Hadidu za rejea zilieleza:-

a) Kutafakari jambo lililofanywa na Mhe. Luhaga Joelson Mpina na kutoa maoni na mapendekezo ya nini kifanywe na Bunge;

b) Kufanyia kazi ushahidi uliowasilishwa (kwa Mhe. Spika) na kutoa maoni iwapo ushahidi huo unathibitisha tuhuma kwamba Waziri wa Kilimo amesema uongo Bungeni na nini kifanywe na Bunge; na

c) Kuwasilisha Taarifa kwa Spika Jumatatu tarehe 24 Juni, 2024.

2.0 **CHIMBUKO LA SHAURI**

2.1 **Mheshimiwa Spika,** tarehe 4 Juni, 2024 katika Kikao cha 40 cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge wakati wa mjadala wa Hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Mohamed Bashe, (Mb) pamoja na mambo mengine, alichangia kuhusu upungufu wa sukari nchini *(gap sugar)* kwamba, kampuni na viwanda vya sukari nchini, vilivyopewa dhamana na Serikali ya kuhakikisha kunakuwa na sukari ya kutosha nchini, vimeshindwa kutekeleza wajibu huo kwa kushindwa kuagiza na kusambaza sukari kutoka nje ya nchi kama ilivyotakiwa.

2.2 **Mheshimiwa Spika,** Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe alieleza kuwa, hali hiyo imesababisha kuendelea kuwepo kwa tatizo la uhaba wa sukari nchini. Aidha, Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe alieleza kuwa jambo hilo lilichangia bei ya sukari nchini kupanda hadi kufikia shilingi 10,000/= kwa kilo

moja. Miezi michache iliyopita Mhe. Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe alieleza kuwa kutokana na hali hiyo Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha sukari ya kutosha inakuwepo nchini. Miongoni mwa hatua hizo ni kuipa idhini Wakala wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) kuingiza sukari nchini, kutoa vibali kwa makampuni ili kuagiza sukari na kusamehe kodi na ushuru kwa sukari itakayoagizwa nje ya nchi na makampuni na viwanda vya sukari. Maelezo hayo yapo kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge za tarehe 04 Juni, 2024 zinazomnukuu Mhe. Hussein Bashe (Mb) akisema ifuatavyo:-

> *"**Mheshimiwa Spika, mwezi Januari na Februari nchi hii sukari ilifika shilingi 10,000, makampuni na viwanda hivi tunavyoviita tuvilinde vilipewa vibali vya kuingiza sukari, havikuingiza sukari….mwaka jana nchi hii ilikuwa ina gap sugar ya tani 60,000 tulimpa Kagera Sugar, tulimpa Mtibwa, tulimpa Bagamoyo, tulimpa TPC, hakuna aliyeingiza hata kilo moja, mlitaka nikae naangalia? Tulitumia nini? Tumeenda kubadili Kanuni za National Food Reserve Agency kuruhusu NFRA kuwa na mandate ya kuingiza sukari (makofi). Mimi niingie on record na nitatoa takwimu kwa nini tumetoa vibali kupitia NFRA vya tani 400,000, numbers don't lie….***
>
> ***Mheshimiwa Spika, naomba nitoe elimu ndogo, gap sugar huwa tunaitoa kwa ajili ya window ya mwezi Machi, Aprili na Mei, miezi mitatu. Kutokana na mvua za El-Nino, baada ya TMA kutoa utabiri wa hali ya hewa, tuliyapatia makampuni na viwanda walete tani 50,000, mpaka mwezi Februari walikuwa hawajaleta hata kilo moja ya sukari na walipoingiza walifungia kwenye ma-godown yao……mwaka jana tulivyowapa vibali vya kuingiza na mpango mkakati ukiongozwa na TSPA, Tanzania Sugar Association ambaye Mwenyekiti wa Taasisi hii ni***

***owner wa Mtibwa na Kagera Sugar…tumekaa Disemba, hakuna kilo moja iliyoingia, Januari, hakuna kilo moja iliyoingia.***

***Mwishoni mwa Januari wameingiza tani 250 wakati wakifahamu sugar na buffer stock ya mwaka wa nyuma wa uzalishaji hawakuingiza hata kilo moja, kwa hiyo taifa lilikuwa halina sukari…tumewapa bei elekezi … shilingi 2300 na 2500. Waliwauzia distributors kwa shilingi 2800 na 3000 na sukari waliyoingiza bandarini tuliyowapa VAT exemption, hata wao tumewapa VAT exemption. Wameingiza bandarini wanaenda kuiuza mfuko wa kilo 50 x- Dar es Salaam shilingi 150,000 mpaka 160,000 mlaji wa Nzega ale kwa shilingi ngapi?"***

2.3 **Mheshimiwa Spika**, wakati Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe akizungumza, Mhe. Luhaga Joelson Mpina, (Mb) alipata nafasi ya kutoa Taarifa kuhusu mchango huo. Taarifa ya Mhe. Luhaga Joelson Mpina ilieleza kuwa, Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe alikuwa analidanganya na kulipotosha Bunge kwa sababu, maelezo hayo hayana ukweli wowote na alikiuka Sheria katika zoezi la kutoa vibali vya kuagiza sukari na kwa kusamehe kodi ya Serikali. Kwa mujibu wa Kumbukumbu Rasmi za Bunge za tarehe 4 Juni, 2024 Mhe. Luhaga Mpina (Mb) alinukuliwa akisema ifuatavyo:-

"***Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zipo taarifa za wazi kwamba Waziri hata hao waliosema kwamba aliwapa kibali cha kuagiza sukari, hakutangaza tender yoyote na haijulikani aliwapataje, lakini nyaraka zote zipo, na kuwa kuagiza sukari zaidi ya gap sugar ni makosa kisheria. Na kwa kuwa pia kuwaruhusu watu ambao hawaruhusiwi kwa mujibu wa Sheria tuliyonayo sasa hivi ya sukari ni makosa kisheria….Uagizaji wa gap sugar huwa unakuwa***

***established na ile Timu ya Bodi ya Sukari ambayo inafanya na inawajulisha na wadau.***

***Sasa Waziri anasema kwamba ametoa Kibali cha tani 410,000 kama gap sugar…mpaka sasa hivi taarifa zilizopo katika hiyo tani 410,000 zimeshaingia tani 220,000…huu ni mwezi wa sita…gap sugar ambayo imekuwa established na hiyo Timu ya ushauri ya Bodi ya Sukari ni tani 120,000 siyo tani 410,000 na nchi yetu haijawahi kuwa na importation ya namna hiyo hata kama uzalishaji huo anaousema yeye.”***

2.4 **Mheshimiwa Spika,** baada ya Taarifa hiyo ya Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb) ulitoa ufafanuzi kuhusu masharti ya Kanuni ya 70 (1) (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Inayosimamia suala la Mbunge ‘Kutosema Uongo Bungeni’. Kanuni inamtaka Mbunge yeyote anayetoa tuhuma kwamba Mbunge mwingine anasema uongo Bungeni, hutakiwa kuwasilisha ushahidi ili kuthibitisha uongo huo. Hivyo, kwa kutumia Kanuni hiyo, ulielekeza Mhe. Luhaga Joelson Mpina awasilishe ushahidi kuthibitisha tuhuma kwamba Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe amelidanganya Bunge tarehe 14 Juni, 2024.

2.5 **Mheshimiwa Spika**, Tarehe 14 Juni, 2024 Mhe. Luhaga Joelson Mpina aliwasilisha Ofisi ya Bunge barua yenye nyaraka za ushahidi kama ulivyoelekeza. Hata hivyo, kabla Bunge halijachukua hatua yeyote ya kujiridhisha kuhusu ushahidi huo, Mhe. Luhaga Joelson Mpina aliitisha Mkutano wa Waandishi wa Habari ambao aliutumia kueleza na kufafanua maudhui ya ushahidi aliouwasilisha kwa Spika.

2.6 **Mheshimiwa Spika,** Kwa mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni ya 4 ya Nyongeza ya Nane na Kanuni ya 84 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ulielekeza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itoe maoni kuhusu

ushahidi uliowasilishwa na Mhe. Luhaga Joelson Mpina na kufanya uchunguzi wa kitendo cha Mhe. Luhaga Joelson Mpina kuitisha Mkutano wa vyombo vya habari na kuzungumzia ushahidi aliouwasilisha kwa Spika. Aidha, ulielekeza Kamati kutoa mapendekezo kwa Bunge kuhusu hatua za kuchukua. Kamati ilielekezwa kukamilisha Taarifa ya Kamati ifikapo Jumatatu tarehe 24 Juni, 2024

3.0 **UCHUNGUZI WA KAMATI**

**MAONI YA KAMATI KUHUSU USHAHIDI WA MHE. LUHAGA JOELSON MPINA KUTHIBITISHA TUHUMA DHIDI YA MHE. HUSSEIN MOHAMED BASHE KUSEMA UONGO BUNGENI NA KULIPOTOSHA BUNGE**

3.1 **Mheshimiwa Spika,** katika uchunguzi wa suala hili Kamati iliwaita mashahidi ambao ni Mhe. Luhaga Joelson Mpina na Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe. Mashahidi hao waliitwa kwa *summons* zilizowataka kufika kwenye Kamati kutoa Ushahidi na kuwasilisha nyaraka. Mashahidi walitii Wito wa Kamati na walitoa ushirikiano kwa kutoa ushahidi ulioisaidia Kamati kupata maoni kuhusu uchunguzi uliokuwa umefanywa na Kamati.

3.2 **Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchunguzi wake kuhusu Taarifa iliyotolewa Bungeni kumlalamikia Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Mohamed Bashe kwamba alisema uongo Bungeni. Kamati imezingatia maelezo yaliyotolewa na Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Mohamed Bashe na yaliyotolewa na Mhe. Luhaga Joelson Mpina pamoja na vielelezo vyote walivyoviwasilisha mbele ya Kamati.

3.3 **Mheshimiwa Spika,** uchunguzi wa Kamati ulijikita katika Taarifa kuhusu uongo uliosemwa Bungeni tarehe 14 Juni, 2024 iliyotolewa na Mhe. Luhaga Joelson Mpina kuhusu maelezo yaliyotolewa na Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe kwa kufanya rejea ya *Hansard.*

3.4 **Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa hoja zote zilizowasilishwa na pande zote mbili uchambuzi na maoni ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Luhaga Joelson Mpina alisema kuwa waziri alilidanganya Bunge kwa kusema mwaka jana nchi hii ilikuwa na *gap* ya tani 60,000 tulimpa Kagera *Sugar*, tulimpa Mtibwa, tulimpa Bagamoyo, tulimpa *TPC*, hakuna aliyeingiza hata kilo moja. Alidai kuwa Viwanda viliingiza sukari kwa mwaka huo. Waziri aliieleza Kamati kuwa ni kweli Viwanda alivyovitaja havikuingiza hata kilo moja. Alifafanua kuwa walioingiza sukari ni kiwanda cha Kilombero na Kampuni nyingine ambayo si mzalishaji. Hivyo maelezo ya Waziri yalikuwa ya ukweli kama ambavyo alivyoeleza.

Aidha, Mhe. Luhaga Joelson Mpina alieleza kuwa Waziri alidanganya kwa kusema sugar gap kwa mwaka 2022/2023 ilikuwa tani 60,000. Alitoa ushahidi kuwa Bodi ya sukari ilieleza kuwa sugar gap ni tani 30,000. Waziri katika utetezi wake alileta ushahidi wa Muhtasari wa Kikao cha Waziri na Wadau wa Sukari cha tarehe 13 Februari, 2023 ambacho kiliidhinisha gap sugar ya tani 30,000 na buffer stock ya tani 30,000 hivyo kufanya jumla ya upungufu wa tani 60,000 za sukari. Kamati baada ya kupitia vielelezo hivyo imejiridhisha kuwa maelezo na vielelezo vya Mhe. Luhaga Joelson Mpina yalikuwa sahihi kwa upande wa sugar gap na maelezo ya Waziri hayakulipotosha Bunge kwakuwa aliongelea gap sugar pamoja na buffer stock.

b) **Mheshimiwa Spika,** Mhe. Luhaga Joelson Mpina alimtuhumu Mhe. Waziri kuwa amelidanganya Bunge kwa kusema wamebadili kanuni za *National Food Reserve Agency* kuruhusu *NFRA* kuwa na *mandate* ya kuingiza sukari wakati hakuna Tangazo la Serikali *(GN)* iliyotangazwa kuipa NFRA

mandate ya kuingiza sukari. Waziri aliieleza Kamati kuwa walitumia Sheria ya Usalama wa Chakula Sura ya 249 kukabiliana na uhaba wakati wa dharura kupitia *NFRA*. Alisema kuwa wameanza mchakato wa kubadilisha Sheria ili *NFRA* waruhusiwe kuagiza, kuhifadhi na kusambaza sukari hata kwa kipindi kisicho cha dharura na mchakato huo ulianza kwa kutoa Tangazo la Serikali Na. 225B la tarehe 01 Aprili, 2024.

c) **Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia kifungu cha 14 cha Sheria ya Tasnia ya Sukari kuhusu wanaoruhusiwa kuagiza sukari na kupitia kifungu cha 15 cha Sheria ya Usalama wa Chakula, 1991 na kubaini kuwa kwa wakati wa dharura kama iliyojitokeza Sheria ya Usalama wa Chakula inakuwa na nguvu zaidi kuliko Sheria ya Tasnia ya Sukari.

Kamati ilipata nafasi ya kujiridhisha kuhusu uwepo wa GN Na. 225B ya tarehe 1 Aprili, 2024 na kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha iliona mapendekezo ya marekebisho yaliyoelezwa na Waziri. Kupitia Hansard na maelezo ya Waziri Kamati ilikuwa na maoni kuwa hakuna uongo uliozungumzwa na kwamba hakuna ukiukwaji wa Sheria.

d) **Mheshimiwa Spika,** Mhe. Luhaga Joelson Mpina alimtuhumu Waziri kwa kutoa vibali vya tani 410,000 kinyume na sugar gap iliyoidhinishwa ya tani 100,000. Waziri alieleza kuwa Kamati ya Ufundi ya Bodi ya Sukari ilibaini upungufu ni tani 220,000 hadi Aprili, 2024. Hata hivyo, kutokana na tathmini iliyofanywa na Wizara ilibainika kuwa uzalishaji uliathirika kutokana na elnino na kutokana na uhaba uliokithiri kwa miezi ya Januari na Februari, 2024 nchi ilihitaji kuwa na uhakika wa sukari kwa ziada "*buffer stock*" hivyo kuidhinisha makisio ya gap sugar ya tani 410,000.

Waziri aliileza Kamati yetu kuwa vibali vilitolewa kwa tani 220,000 pekee na kwamba mpaka sasa zimeingia tani 180,000. Tani zilizosalia bado hazijatolewa vibali na kwamba wataendelea kufuatilia mwenendo wa uzalishaji na upatikanaji wa sukari nchini kabla ya kuamua kutoa vibali vingine au kusitisha kabisa uagizaji kwa mwaka 2023/2024.

e) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhika kuwa Kiwango cha tani 100,000 alichokisema Mhe. Luhaga Mpina ni makisio yaliyofanyika mwezi Disemba mwaka 2023. Kiwango hicho kilifanyiwa marejeo (review) mwezi Aprili, 2024 ambapo Kamati ilioneshwa Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Ufundi kilichobainisha ongezeko la sugar gap kutoka tani 155,000 hadi tani 220,000. Kiwango cha tani 410,000 alizozisema Waziri zilijumuisha mahitaji yaliyokadiriwa mwezi Aprili na tathmini iliyofanyika baadaye iliyobaini kuwa hadi Mei, 2024 viwanda havikuwa vimeanza uzalishaji hivyo mahitaji pamoja na buffer stock kufikia Disemba, 2024 ni tani 410,000 hivyo kutoa Idhini ya tani hizo.

f) **Mheshimiwa Spika,** Mhe. Luhaga Joelson Mpina alimtuhumu Waziri alidanganya aliposema Makampuni na viwanda vilivyopatiwa vibali vya kuingiza sukari tani 50,000 hayakuwa yameingiza sukari hata kilo moja Februari na walipoingiza walifungia kwenye magodown yao. Mhe waziri mbele ya kamati alieleza kuwa makampuni yote aliyoyataja yalikuwa hayajaingiza sukari isipokuwa Kilombero sugar ambayo iliingia tarehe 29 Januari, 2024 na kwenda sokoni tarehe 5 Februari, 2024. Kamati imepitia vibali vilivyotolewa kwa makampuni na viwanda na kubaini kuwa Idhini ilitolewa kuanzia 29 Disemba, 2023 vibali vimetolewa tarehe 4 Januari, 2024. Kwa mazingira haya, isingewezekana kuingiza sukari mwezi kwa Disemba. Katika Hansard Mhe. Waziri ameleza wazi

kuwa mwishoni mwa Januari, Kilombero sugar iliingiza tani 250.

g) **Mheshimiwa Spika,** Mhe. Luhaga Joelson Mpina alimtuhumu Waziri kuwa hakuwaita wenye viwanda kukaa nao kuhusu suala la sukari. Waziri amesema kuwa hakutakataa kukutana na wazalishaji isipokuwa aliwapa masharti ya kutangaza mawakala kwa kila mkoa na kufungua maghala kila mkoa kabla ya kukutana. Baada ya Kamati kusikiliza ushahidi iliridhika kuwa Waziri hakukutana nao kwakuwa hawakuwa wametekeleza masharti aliyokuwa amewapa.

h) **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina anamtuhumu Waziri wa Kilimo kwa kukiuka Sheria wakati wa kutoa vibali kwa makampuni ambayo si wazalishaji wa sukari bila kutangaza zabuni. Waziri alieleza kwamba vibali vilitolewa wakati wa dharura baada ya kufanya utafiti na kujiridhisha kuhusu uwezo wa kampuni hizo. Aidha, alieleza kuwa katika mazingira ya dharura na kwa kuzingatia kuwa fedha zinazotumika sio za umma, hakukuwa na ulazima wa kutumia Sheria ya Ununuzi. Vilevile, Waziri aliwasilisha ushahidi wa leseni za biashara na nyaraka za usajili wa Kampuni hizo zinazowaruhusu kufanya biashara ya sukari. Kamati imejiridhisha kwamba utaratibu uliotumika ulitokana na hali ya dharura.

**UCHUNGUZI WA KAMATI KUHUSU TUHUMA DHIDI YA MHE. LUHAGA JOELSON MPINA KUDHARAU MAMLAKA YA SPIKA NA MWENENDO WA SHUGHULI ZA BUNGE.**

3.5 **Mheshimiwa Spika,** baada ya kamati kupokea Hadidu za Rejea kuhusu kufanya uchunguzi wa tuhuma dhidi ya Mhe. Luhaga Joelson Mpina, tarehe 18 Juni, 2024 ilikutana kujadili na hatimaye ikaamua Mhe. Luhaga Joelson Mpina apewe Wito wa kufika mbele ya Kamati ili aweze kujibu tuhuma zinazomkabili.

3.6 **Mheshimiwa Spika,** Wito huo ulimtaka Mhe. Luhaga Joelson Mpina atoe maelezo ya kwanini asichukuliwe hatua kwa kukiuka Kifungu cha 26(d) (e) na 34(1)(g) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi za Bunge Sura ya 296 pamoja Kanuni ya 84(1) (j) na (k) ambazo zinakataza kudharau Mamlaka ya Spika na mwenendo wa shughuli za Bunge. Tarehe 19 Juni, 2024 Mhe. Luhaga Joelson Mpina alikabidhiwa Hati ya wito huo na kufika mbele ya Kamati.

3.7 **Mheshimiwa Spika**, Katika kushughulikia suala hili, ili Kamati iweze kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma hizo, ilijielekeza kwenye hoja za uchunguzi (*issues*) zifuatazo:

(a) Je, ni kweli kwamba Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb) aliitisha Mkutano na vyombo vya habari na kuzungumza kuhusu maudhui ya ushahidi aliouwasilisha bungeni kabla Bunge halijaufanyia kazi na kukamilisha uchunguzi wake?

(b) Endapo hoja (a) itathibitika, Je, kitendo cha Mhe. Luhaga Joelson Mpina kuzungumza na Waandishi wa Habari kuhusu ushahidi alioupeleka kwa Spika ni kudharau mamlaka ya Spika na mwenendo wa shughuli za Bunge?

(c) Endapo hoja (a) na (b) ni kweli, Je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake?

3.8 **Mheshimiwa Spika**, Katika uchunguzi wake, Kamati ilirejea Sheria, Kanuni za Kudumu za Bunge, Taarifa Rasmi za Bunge na ushahidi wa picha za *video* za Mkutano wa Waandishi wa Habari na Mhe. Luhaga Mpina. Rejea hizo ni:

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

(ii) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023

(iii) Kumbukumbu Rasmi za Bunge za Tarehe 4 Juni, 2024, tarehe 18 Juni, 2024;

(iv) Ushahidi uliowasilishwa na Mhe. Luhaga Joelson Mpina kwa Spika;

(v) Mahojiano na nyaraka za ushahidi zilizowasilishwa na Mhe. Luhaga Joelson Mpina alipokuwa mbele ya Kamati;

(vi) Video ya tarehe 4 Juni, 2024 iliyoonesha majadiliano ya Bunge kuhusu mchango wa Waziri wa Kilimo Mhe. Hussen Mohamed Bashe; na

(vii) Video inayomuonesha Mhe. Luhaga Joelson Mpina akiongea na Mkutano wa Waandishi wa Habari aliouitisha.

3.9 **Mheshimiwa Spika,** katika kujibu hoja ya kwamba Je, ni kweli kwamba Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb) aliitisha Mkutano na vyombo vya habari na kuzungumza kuhusu maudhui ya ushahidi aliouwasilisha Bungeni kabla Bunge halijaufanyia kazi na kukamilisha uchunguzi wake? Kamati ilianza kuchunguza Shauri hili kwa kuangalia picha za video za Mkutano wa Waandishi wa Habari ulioitishwa na Mhe. Luhaga Mpina (Mb) tarehe 14 Juni, 2024. Sehemu ya maelezo ambayo Kamati iliyaona na kuyasikia kutoka kwenye video hiyo yalieleza kuwa:

> ***"…kufuatia maagizo ya kiti nalazimika kuandaa maelezo na kuwasilisha kwa mheshimiwa Spika leo tarehe 14 Juni,2024 nikiwasilisha ushahidi wa vielelezo vya kuthibitisha uongo wa Waziri Bashe aliousema bungeni tarehe 4 Juni, 2024….Gap sugar iliyoidhinishwa kwa msimu wa mwaka 2022/2023 ni tani 30,000 sio 60,000 kama alivyosema Waziri wa Kilimo. Rejea barua ya Bodi ya Sukari Tanzania yenye Kum. Ref.No.SBT/DGO/26-38 ya tarehe 29 Machi, 2023 iliyoandikwa na Mkurugenzi wa Bodi ya***

***Sukari, Prof. Bengesi kwenda kwa Katibu Mtendaji wa TCS SADC…***
***Maelezo ya Waziri kwamba, uzalishaji ukashindikana katika nchi yetu kuanzia Oktoba, Novemba, Disemba, Januari, Februari na Machi…maelezo hayo ni uongo…taarifa ya TSPA inaonyesha uzalishaji wa Sukari mwaka 2023/2024 ambapo uzalishaji ulifikia tani 394,829 (Kiambatishwa No.6)….***

***Waziri hakusema ukweli, kwani hajawaita wazalishaji wa sukari ili akae nao kujadili changamoto zinazowakabili badala yake ni wazalishaji wa sukari waliomba kuonana na Waziri kupitia barua yenye Kumb. Na. TSPA/SI-Gen/27/01/2024 ya tarehe 14 Februari, 2024 iliyoandikwa na Katibu Mtendaji wa TSPA, Deo Lyato kwenda kwa Waziri wa Kilimo (Kiambatisho Na.9) …..waziri wa kilimo aliwajibu wazalishaji wa sukari nchini kwamba atakutana nao pale tu wazalishaji sukari watakapokuwa wamekamilisha kutekeleza masharti waliyopewa ya kujenga maghala kila mkoa……rejea barua yenye Kumb. Na. SBT/DGO/01/33-33 ya tarehe 20 Machi, 2024***

3.10 **Mheshimiwa Spika**, Baada ya kuangalia video na kuchambua nyaraka zilizowasilishwa na Mhe. Luhaga Joelson Mpina kwa Spika, Kamati ilimuita Mhe. Luhaga Joelson Mpina ili aweze kutoa utetezi wake.

3.11 **Mheshimiwa Spika,** Mara baada ya Mhe. Luhaga Joelson Mpina kufika mbele ya Kamati alitoa maelezo kuwa Kamati haina mamlaka ya kusikiliza shauri kwa kuwa vifungu vilivyotajwa katika Hati ya Wito ambavyo ni 26(d)(e) na 34(1)(g) pamoja na Kanuni ya 84(1)(j) na (k) vinatofautiana na kifungu kilichotajwa katika Taarifa ya Spika ya tarehe 18 Juni, 2024 ambacho ni kifungu cha 29(d) na (e). Kwa maoni yake, Mhe. Mbunge alieleza kuwa kifungu hicho ndicho Spika alikusudia kitumike kumshitaki.

3.12 **Mheshimiwa Spika,** Katika kupata jibu la hoja hii, Kamati ilirejea Sheria, *Hansard* na nakala halisi ya Taarifa ya Spika na kujiridhisha kuwa vifungu vilivyotumika katika Hati ya Wito aliyopewa Mhe. Luhaga Joelson Mpina ni sahihi na ndivyo vinavyoipa Mamlaka Kamati kufanya uchunguzi wake. Vifungu vilivyotajwa katika Hati ya Wito ni Kifungu cha 26(d)(e) na 34(1)(g) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge pamoja na Kanuni ya 84(1)(j) na (k) ambavyo ni vifungu vinavyoeleza makosa anayotuhumiwa kuyafanya. Kifungu cha 26 kinaeleza:-

***"26. any person who-***

**(d)** ***shows disrespect in speech or manner towards the Speaker; or***

**(e)** ***does any other act of intentional disrespect to or with reference to the proceedings of the Assembly or of a Committee of the Assembly or to any person presiding at such proceedings, commits an offence."***

Kifungu cha 34 kinaeleza: -

***"34.-(1) Any person who-***

**(g)** ***publishes, save by the general or special leave of the Assembly, any paper, report or other document prepared expressly for submission to the Assembly before the same has been laid on the table of the Assembly;***

***Commits an offence and on conviction is liable to a fine not exceeding five hundred thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding three years or to both."***

Vifungu tajwa vinazuia vitendo vya dharau kwa Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge. Baada ya kuchambua vifungu hivyo Kamati iliona kuwa hoja ya kwamba Kamati haina mamlaka ya kusikiliza shauri dhidi yake ni hoja isiyo na nguvu kisheria. Kwa hali hiyo, Kamati ilifikia uamuzi kuwa inayo mamlaka ya kufanya

uchunguzi wa shauri linalomkabili Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

3.14 **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kujiridhisha kuhusu mamlaka ya Kamati, Kamati ilimtaka Mhe. Luhaga Joelson Mpina kutoa maelezo kuhusu tuhuma zinazomkabili. Katika maelezo yake, Mhe. Luhaga Joelson Mpina alikiri kuwa aliitisha Mkutano wa Waandishi wa Habari kueleza umma kwamba ametekeleza maelezo ya Spika kwa kupeleka ushahidi kwa Spika ili kuthibitisha tuhuma dhidi ya Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe kusema uongo Bungeni.

3.15 **Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipomuhoji ni kwanini alivieleza vyombo vya habari ushahidi aliouwasilisha kwa Spika, Mhe. Luhaga Joelson Mpina aliieleza Kamati kuwa alichokiwasilisha kwa vyombo vya habari ni maelezo yake binafsi na siyo vielelezo vya ushahidi alivyopeleka kwa Spika ambavyo, kwa maoni yake, ndiyo ushahidi. Katika kufafanua jambo hilo, Mhe. Luhaga Joelson Mpina alieleza kwamba anayo haki kama Mbunge kuwafahamisha wananchi kuhusu namna alivyotekeleza maelekezo ya Spika hivyo hakufanya kosa lolote.

Mhe. Luhaga Joelson Mpina aliendelea kueleza kwamba, Kanuni ya 70 kuhusu kuthibitisha tuhuma za uongo Bungeni haina masharti yanayomzuia Mbunge anayethibitisha tuhuma kuzungumza na vyombo vya habari. Mhe. Luhaga Joelson Mpina alitoa mfano wa Wabunge wengine wanaothibitisha tuhuma za uongo ndani ya Bunge ambao katika kufanya hivyo wanaoneshwa na vyombo vya habari ha hakuna Kanuni inayovunjwa.

3.16 **Mheshimiwa Spika,** hakuna ubishi kuwa maelezo ya Mhe. Luhaga Joelson Mpina mbele ya vyombo vya habari ndiyo ushahidi aliouwasilisha kwa Spika. Utetezi wake kwamba maelezo yake, hayakuwa siyo ushahidi

bali vielelezo alivyoambatisha kwenye maelezo yake hauna msingi kwa kuwa maelezo na viambatisho vyake vyote ni ushahidi ambao unatakiwa kufanyia kazi na Spika kwa mujibu wa Kanuni. Kitendo cha kuitisha Mkutano wa Waandishi wa Habari muda mfupi baada ya kuwasilisha Taarifa ya Spika Bungeni Kamati iliona kuwa hakikuwa na nia njema na hakioneshi heshima kwa mamlaka ya Spika. Aidha, utetezi kwamba Kifungu cha 70 hakizuii Mbunge anayetuhumu kuzungumza na vyombo vya habari haukubaliki, Vilevile, kitendo alichokifanya ni tofauti na Wabunge wanaokuwa Bungeni na kupigwa picha wakichangia, hii ni kwa sababu upo utofauti wa kimazingira.

3.17 **Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 70(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inaweka masharti yanayomtaka Mbunge aliyetoa tuhuma kwamba Mbunge mwingine amesema uongo kuthibitisha tuhuma hizo. Maelezo ya Shahidi kwamba ushahidi ni vielelezo hayana uzito kwa sababu nyaraka zinazopelekwa kwa Spika, ikiwemo maudhui ya nyaraka alizowasilisha ndiyo ushahidi wenyewe na haukupaswa kuzungumzwa popote baada ya kufikishwa kwa Spika.

3.18 **Mheshimiwa Spika,** barua ya Mhe. Luhaga Joelson Mpina iliyowasilishwa kwa Spika yenye Kumb. Na. MB/KSS/2024/55 ya tarehe 14 Juni, 2024 iliambatishwa maelezo na vielelezo (viambatisho) mbalimbali. Mhe. Luhaga Joelson Mpina aliziita nyaraka hizo kuwa ni ushahidi kama inavyoonekana katika kichwa cha habari cha barua yake ambacho kinasomeka:

> ***"Yah: Kuwasilisha Ushahidi kuhusu Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe (Mb) kusema uongo Bungeni".***

Kwa hali hiyo, maelezo na viambatisho ni kitu kimoja kama barua yake inavyoonesha na huo ndiyo ushahidi aliouwasilisha kwa Spika. Katika hatua hiyo, kwa kuwa

ushahidi huo ulikuwa mikononi mwa Spika, Mhe. Luhaga Joelson Mpina hakuruhusiwa kuuzungumzia.

3.19 **Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo Kamati imejiridhisha kuwa Mhe. Luhaga Joelson Mpina alizungumza na vyombo vya habari kuhusu ushahidi aliouwasilisha kwa Mhe. Spika kabla ushahidi huo haujafanyiwa kazi na Spika au Bunge kama inavyoelekezwa na Kanuni za Bunge.

3.20 **Mheshimiwa Spika**, shahidi aliendelea kujitetea kuwa Kifungu cha 26(d)(e) na 34(1)(g) pamoja na Kanuni ya 84(1)(j) na (k) ya Kanuni za Kudumu havihusiani na maelezo aliyoyatoa kwenye Mkutano na vyombo vya habari kwa kuwa vifungu hivyi havina mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Mbunge na Spika. Shahidi aliendelea kufafanua kuwa, maelezo yake kwa wanahabari yalilenga kuwapa taarifa wananchi kuhusu kazi anazozifanya na kuwafahamisha kuwa ametekeleza maelekezo ya Spika ya kuwasilisha ushahidi.

3.21 **Mheshimiwa Spika**. Kamati inaona kuwa, maelezo hayo ya Mhe. Luhaga Joelson Mpina hayana uzito wowote bali ni uthibitisho kuwa aliongea na vyombo vya habari kuhusu ushahidi alioupeleka kwa Spika.

3.22 **Mheshimiwa Spika**, Mbunge au mtu mwingine yeyote anao wajibu wa kuheshimu mamlaka, hadhi na heshima ya Spika, na mwenendo wa Shughuli za Bunge. Mbunge kama sehemu ya Bunge na kiongozi wa umma analo jukumu kubwa zaidi la kuhakikisha kuwa, kila afanyalo na kila analolisema linaakisi heshima na hadhi ambayo Bunge linastahili. Kwa hali hiyo, Mbunge kwa nafasi yake kama kiongozi wa umma, hatakiwi kuzungumza na vyombo vya habari kuhusu jambo lililowasilishwa kwa Spika ambalo linasubiri kufanyiwa kazi na Bunge.

4.0 **MAONI YA KAMATI**

4.1 **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kujibu hoja (a) Kamati ilijielekeza katika hoja, Je, kitendo cha Mhe. Luhaga Joelson Mpina kuzungumza na Waandishi wa Habari kuhusu ushahidi alioupeleka kwa Spika ni kudharau mamlaka ya Spika na mwenendo wa shughuli za Bunge?

4.2 **Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 26 (d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura 296 *(The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP 296)* kinakataza vitendo vya kumkosea heshima Spika kwa maneno au vitendo. Halikadhalika, Kifungu cha 26 (e) cha Sheria hiyo kinazuia vitendo vya dharau kwa mwenendo wa shughuli za Bunge.

4.3 **Mheshimiwa Spika,** Kitendo cha Mhe. Luhaga Joelson Mpina kwenda kuzungumza kwenye vyombo vya habari kuhusu maudhui ya ushahidi wa nyaraka alizowasilisha kwa Spika muda mfupi baada ya kufikisha ushahidi huo Bungeni ni kitendo cha ukosefu wa nidhamu kwa kutoheshimu mamlaka ya Spika na mwenendo wa shughuli za Bunge. Hivyo, haikubaliki Mbunge kuzungumza na vyombo vya habari kuhusu jambo alilopeleka kwa Spika ili lifanyiwe kazi.

Kitendo hicho cha Mbunge ni dharau kwa mamlaka ya Spika, na kuingilia mwenendo wa Bunge. Kwa kufanya hivyo, Mhe. Luhaga Joelson Mpina ameshusha hadhi na heshima ya Bunge na kulidharaulisha mbele ya jamii hivyo kukiuka masharti ya kifungu cha 26(d) na (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura 296 *(The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP 296)*. Vilevile, kitendo hicho ni Utovu mkubwa wa nidhamu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1)(j) na (k) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

4.4 **Mheshimiwa Spika**, vilevile kifungu cha 34 (1) (g) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura

296 *(The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP 296)* kinazuia, kuchapisha kwa Umma taarifa zilizoandaliwa mahususi kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni, na kabla taarifa hizo kuwekwa Mezani. Kitendo cha Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kuitisha Mkutano wa Waandishi wa Habari na kutoa ufafanuzi wa ushahidi alioupeleka kwa Spika ni kukiuka Kifungu cha 34 (1) (g) vya Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura 296 kinachokataza kusambaza kwa umma, Taarifa zinazofanyiwa kazi na Bunge pasipo kupata kibali cha Bunge.

4.5 **Mheshimiwa Spika,** Ushahidi uliopo wa kitendo kilichofanywa na Mhe. Luhaga Joelson Mpina, masharti ya Sheria na Kanuni za Bunge, Kamati imemkuta na hatia Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb) kwa kosa la kudharau Mamlaka ya Spika na mwenendo wa shughuli za Bunge. Kitendo hicho kinakatazwa na ni kinyume na Kifungu cha 26(d) na (e) na 34 (1) (g) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura 296 *(The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP 296)*. Aidha, kitendo hicho ni Utovu wa nidhamu / Utovu Mkubwa wa Nidhamu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) (j) na (k) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

4.6 **Mheshimiwa Spika,** baada ya kujibu hoja hizo mbili za awali, Kamati ilijielekeza kwenye Hoja ya mwisho kwamba, Je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake?

4.7 **Mheshimiwa Spika**, Katika kujibu hoja hii, Kamati ilizingatia Sheria na Kanuni pamoja na, kutafakari kwa kina kuhusu ushahidi uliotolewa na Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb) kuhusu suala hili. Aidha, Kamati ilizingatia maelezo yake kwamba yeye ni Mbunge wa muda mrefu chini ya viongozi wengi wa Bunge, kutowahii kufikishwa mbele ya Kamati ya Maadili na kuwa yeye ni mtiifu kwa viongozi na shughuli za Bunge.

4.8 **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kufikia uamuzi, Kamati ilitafakari utetezi wake na ilizingatia aina ya kosa lililofanyika, namna kosa hilo lilivyofanyika lakini pia athari ya kitendo hicho kuhusu heshima na hadhi ya Bunge na uongozi wa Bunge. Vilevile Kamati ilitilia maanani sifa na uzoefu anaopaswa kuwa nao Mbunge katika kupima matendo yake na athari zinazoweza kujitokeza kupitia kauli na vitendo vyake pamoja na wajibu wake katika kuheshimu Sheria na Kanuni za Bunge. Katika hili, Kamati iliona kuwa, Mhe. Luhaga Joelson Mpina akiwa Mbunge wa kipindi kirefu anapaswa kuonesha taswira njema ya uzingatiaji wa Maadili, Sheria na Kanuni za Bunge ili awe mfano bora kwa Wabunge wengine. Hivyo, kitendo cha kutoheshimu Mamlaka ya Spika ni jambo linaloshusha heshima ya Bunge.

4.9 **Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 33 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura ya 296 kinatoa mamlaka kwa Bunge kupitia Azimio kutoa adhabu kwa mtu ambaye amekiuka masharti ya kifungu cha 26 au Sheria yoyote kuhusu kudharau mamlaka ya Bunge. Adhabu iliyotamkwa na Sheria ni ya kumsimamisha Mbunge kuhudhuria Vikao vya Bunge kwa namna itakavyoamuliwa kwa mujibu wa Sheria. Kifungu hicho kinaeleza, nanukuu:-

> "***33-(1) Where any Member commits any contempt of the Assembly whether specified in section 26 or otherwise, the Assembly may, by resolution, either direct the Speaker to reprimand such Member or suspend him from the service of the Assembly for such period as it may determine.***
>
> ***Provided that, such period shall not extend beyond the last day of the the session next following that which the resolution was passed or of the session in which the resolution is passed as the Assembly may so determine".***

4.10 **Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za kudumu za Bunge zinaweka adhabu kwa vitendo alivyovifanya Mhe. Luhaga Joelson Mpina kama ifuatavyo:-**

a) **Ikiwa kosa ni la kwanza, Mbunge kutohudhuria Vikao vya Bunge visivyopungua kumi na visivyozidi kumi na tano;**

b) **Ikiwa ni kosa lake la pili au zaidi Mbunge kutohudhuria vikao vya Bunge visivyopungua kumi na tano au visivyozidi ishirini; na**

c) **Kanuni ya 84(4) inaweka masharti kwa Bunge kuzingatia ushauri mwingine wowote utakaotolewa na Kamati kuhusu adhabu anayostahili kupewa Mbunge aliyekiuka masharti ya Kanuni hii.**

4.11 **Mheshimiwa Spika,** huo ndio ulikuwa uchunguzi wa Kamati kuhusu Shauri la kuwasilisha nyaraka za ushahidi kwa Spika na wakati huo huo kwenda kuzungumza kwenye vyombo vya habari kuhusu maudhui ya ushahidi huo kabla haujafanyiwa kazi na Spika na Bunge kwa mujibu wa Kanuni.

4.12 **Mheshimiwa Spika,** Kamati imejiridhisha kuwa, kitendo alichofanya Mhe. Luhaga Joelson Mpina ni utovu mkubwa wa nidhamu kwa Bunge kwa sababu ya kudharau Mamlaka ya Spika, kuingilia mwenendo wa shughuli za Bunge na vilevile ni kitendo kinachofedhehesha, kushusha hadhi na heshima ya Bunge.

Hivyo, Kamati inaliomba Bunge litafakari shauri hili linalomhusu Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb), ushahidi uliopo, Sheria na Kanuni na kuuzingatia wakati wa kupitisha Azimio la kutoa adhabu anayostahili kwa kosa alilotenda.

## 5.0 HITIMISHO

5.1 **Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge na napenda nitumie nafasi hii kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi ndio kipaumbele cha kwanza.

5.2 **Mheshimiwa Spika**, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa shauri la utovu wa nidhamu kwa Bunge na Spika, kudharau Mamlaka ya Spika, kuingilia mwenendo wa Bunge na kushusha hadhi na heshima ya Bunge. Wajumbe hawa walifanya kazi hii na walizingatia misingi ya haki, bila kumwonea au kumpendelea mtu yeyote. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Thea Medard Ntara (Mb) – Makamu Mwenyekiti
2. Mhe. Aloyce John Kamamba (Mb)
3. Mhe. Amour Khamis Mbarouk (Mb)
4. Mhe. Cecilia Daniel Paresso (Mb)
5. Mhe. Christopher Olonyokie Ole Sendeka (Mb)
6. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika (Mb)
7. Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwelwe (Mb)
8. Mhe. Flatei Gregory Massay (Mb)
9. Mhe. Francis Kumba Ndulane (Mb)
10. Mhe. Khadija Shaaban Taya (Mb)
11. Mhe. Haji Amour Haji (Mb)
12. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga (Mb)
13. Mhe. Janejelly James Ntate (Mb)
14. Mhe. Joseph Michael Mkundi (Mb)
15. Mhe. Khalifa Mohamed Issa (Mb)
16. Mhe. Maimuna Salum Mtanda (Mb)
17. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis (Mb)
18. Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi (Mb)

5.3 **Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuisaidia

Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndugu Pius T. Mboya, Mkurugenzi Idara ya Huduma za Sheria, Ndugu Agnes Ivor Ndumbati *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Huduma za Sheria, Ndugu Maria Mdulugu (Katibu wa Kamati), Ndugu Ludovick Ringia, Ndugu Thuwaiba Jumbe Sekretarieti na Ndugu Mainda Shaban kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

5.4 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kujadili na kupokea maoni na mapendekezo ya Kamati ili baada ya mjadala liazimie kuchukua hatua stahiki kwa kadiri litakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE.ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa ananiuliza kama anasoma na Azimio?

Ndio, linasomwa kwa sababu, Waheshimiwa Wabunge wanapokuwa wanachangia, kwa mujibu wa kanuni zetu, wanaweza kuwa na mapendekezo ya mabadiliko ya hili Azimio. Kwa hiyo, na lenyewe unalisoma halafu Waheshimiwa Wabunge wanachangia sehemu zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio.

**MHE. ALLY J. MAKOA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Azimio la Bunge Kuhusu Adhabu kwa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) kwa Kudharau Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge kwa Kuwasilisha Ushahidi kwa Spika na Vyombo vya Habari Kabla Bunge Halijaufanyia Kazi.

Mheshimiwa Spika,

Kwa kuwa, Bunge letu linaongozwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo tulizitunga sisi wenyewe, kwa ajili ya kutuongoza katika kutekeleza shughuli za Bunge.

Na Kwa kuwa, Sheria na Kanuni hizo zimewekewa masharti kuhusu utaratibu wa kufuatwa katika kushughulikia masuala ya Kibunge na kwamba, Wabunge wanapaswa kuheshimu na kutii Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge.

Na Kwa kuwa, Tarehe 04 Juni, 2024 Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) alimtuhumu Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe (Mb) kwa kusema uongo na amelipotosha Bunge kuhusu suala la upungufu wa sukari *(gap sugar)* na uagizaji wa sukari hiyo kutoka nje ya nchi, hivyo Mheshimiwa Spika alimueleza Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina (Mb) kuwasilisha Ushahidi, ili kuthibitisha tuhuma dhidi ya Waziri wa Kilimo kwamba, amesema uongo na amelipotosha Bunge ifikapo Tarehe 14 Juni, 2024.

Na Kwa kuwa, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, (Mbunge), aliwasilisha ushahidi huo Bungeni Tarehe 14 Juni, 2024 na kisha kuitisha mkutano wa waandishi wa habari na kufafanua ushahidi aliouwasilisha Bungeni kabla ya Spika na Bunge halijaufanyia kazi.

Na Kwa kuwa, Tarehe 18 Juni, 2024 kwa mamlaka uliyonayo chini ya Kifungu cha 84 (2) na cha (4) Kifungu kidogo cha Kwanza (A) na (B) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 uliagiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kushughulikia suala la vitendo vya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, kutoa ushahidi aliouwasilisha kwa Siku ya tarehe 14 Juni, 2024.

Na Kwa kuwa, kamati ilichunguza na kumtia hatiani kwa kukiuka masharti ya Kifungu cha 26 (D) na (E) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Hadhi ya Bunge, Sura ya 296 pamoja na Kanuni ya 84, Kifungu Kidogo cha (1)(k) na (j) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kwa kuwasilisha katika vyombo vya habari nyaraka alizowasilisha kwa Spika, kitendo ambacho ni utovu mkubwa wa nidhamu kwa Bunge na Spika, kudharau

Mamlaka ya Spika, kuingilia Mwenendo wa Shughuli za Bunge na kushusha hadhi na Heshima ya Bunge.

Na Kwa kuwa, vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge vinaathiri na kuvunja heshima ya Bunge mbele ya umma na Watanzania, jambo ambalo ni kinyume na Kanuni na Sheria za Bunge.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, apewe adhabu kwa mujibu wa Kifungu cha 84 (3)(a) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ya kumtaka Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, (Mbunge), kutohudhuria Vikao vya Bunge 10 mfululizo kuanzia leo, Tarehe 24 Juni, 2024.

Na Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, linakubaliana kupitisha mapendekezo ya adhabu kwa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, (Mbunge), kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliishaungwa mkono. Kwa hivyo, hili azimio ni sehemu ya hoja yako. Ahsante sana.

**MHE. ALLY J. MAKOA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Taarifa imesomwa na Mwenyekiti, lakini pia, amesoma azimio ambalo limependekezwa kwa Bunge na Kamati. Kama nilivyosema awali Kanuni zetu zinaruhusu Bunge kuweza kujadili hoja hii pamoja na hili azimio na maana niliona kama kuna minong'ono hivi kwa hiyo, tuzipitie Kanuni zetu zinaruhusu kutoa ushauri mwingine kwa Bunge. Kwa sababu, utakachokuwa unasema utakuwa unalishauri Bunge kuhusu adhabu kama iwepo, isiwepo, iongezeke au ipungue, yote hayo yanakuwa yanaelezwa kwa sura ambayo ni mabadiliko kwenye azimio.

Ninayo majina hapa ya Wabunge walioomba kuchangia. Nautazama muda wetu pale umekwenda, lakini kwa ajili ya kutenda haki, Wabunge waliioomba kuchangia hapa watapewa kwa sababu, azimio hili linamhusu Mbunge, kwa ajili ya kupata adhabu. Kwa hiyo, huenda kuna Mbunge ambaye angesema huenda mimi ningechangia, pengine ningechangia tofauti, halafu mambo yangekuwa tofauti kwa hiyo, nitatoa haki kwa Wabunge walioomba hapa mbele kuchangia.

Pamoja na hayo, Waheshimiwa Wabunge tukubaliane, kila Mbunge atakayesimama kuchangia atachangia kwa dakika tano na kengele itagongwa mara moja. Kwa hiyo, muda wako ukiisha ukishaniona tu nimewasha, wewe acha tu kuzungumza kwa sababu, la sivyo muda wa mwenzako utakuwa umekwishautumia.

Tutaanza na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Msukuma. Mheshimiwa Tauhida Gallos Cassian, ajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kuwepo ndani ya Bunge lako Tukufu, lakini pili, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi sana mtoto mchanga akilia mama humbembeleza. Pia, wakati mwingine mama humbebeleza huyu mtoto mpaka kiasi cha mama mwenyewe kulia. Vilevile mtoto huyohuyo aliyebembelezwa na mama akifika darasa la saba akaanza kudeka kama mwanzo, mama yuleyule humchapa. Humchapa kwa nia ya kumrekebisha kwa hiyo, aliyembembeleza mtoto ni mama na anayemchapa ni mama. Mara nyingi huwa hakuna mjadala kwenye jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge Mpina ni hiki ni kipindi chake cha nne kwa hiyo, ni Mbunge mkomavu. Ameshiriki vikao vingi vya kuadhibu Wabunge wenzake na wakati mwingi anazijua Taratibu, Kanuni na Sheria za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuna wengine watajiuliza, ni kweli kwenye mchezo wa mpira wa miguu kuna adhabu zake. Kuna

kadi nyekundu ya moja kwa moja, kuna kadi ya njano, halafu inafuata nyekundu. Pia, ukienda kwenye jeshi kuna *MP* wa Jeshi na ukija kwenye Bunge Kamati ya Maadili ndiyo Polisi wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri leo Polisi ya Wabunge ameletwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Mpina, ambaye amekiuka Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Hii imesababisha hata baadhi ya watu tumemuona Mwanasheria mmoja wa pale Mbeya akitumia nafasi hiyohiyo ya Mheshimiwa Mpina na kuanza kumrushia maneno ya kejeli Spika wetu. Vilevile eti anaomba radhi kwamba, anatoka Mbeya. Hatukumchagua Mheshimiwa Dkt. Tulia kwa sababu anatoka Mbeya, tulimchagua Mheshimiwa Dkt. Tulia kwa sababu ya uwezo alionao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kitendo alichokifanya Mheshimiwa Mbunge kimesababisha baadhi ya watu kuanza kuingiza maneno ya kulidharau Bunge na kumtukana Mheshimiwa Spika. Hili halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri. Kwa kitendo hiki alichokifanya Mbunge mwenzetu tena wa muda mrefu Bungeni, tuchukue hatua kali za kumaliza ile adhabu, tusipunguze. Tuweke ileile 15 ambayo imetamkwa na tuachane na hii 10. Tukiweka 15 Wabunge wengine hawawezi kurudia kufanya makosa ya wazi kama haya aliyoyafanya Mheshimiwa Mpina.

Mheshimiwa Spika, pia, mimi ni Mjumbe wa *NEC,* nikitoka hapa nitakwenda kumshitaki kwenye *NEC*. Ahsante sana, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Gallos Cassian. Mheshimiwa Mohammed Said Issa, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyoletwa mbele yetu. Mimi ni Mbunge wa Awamu ya Pili, lakini Mheshimiwa ambaye tunamjadili hapa ni Mbunge mzoefu. Sisi tumemuangalia wakati hatujaingia humu ndani.

Mheshimiwa Spika, wale Wabunge ambao hawakuwemo Bunge la 11, Mheshimiwa Mpina alifanya kitendo kama hikihiki cha kudharau Bunge. Tumemsema Bungeni, baada ya kutoka hapa akaenda kutushikisha adabu kule *canteen*. Tukaingia humu ikatajwa apelekwe maadili, lakini Mheshimiwa Ndugai akaomba radhi kwenye Bunge tukamsamehe. Sasa hii imekuwa ni tabia.

Mheshimiwa Spika, wetu wewe hapa ni Mbunge, Spika unayeongoza Mabunge ya Dunia. Wale wazungu kukuchagua waliku- *vet* vitu vingi ikiwemo *standard* yako ya kutuongoza humu Bungeni. Sasa kwa sisi ambao tuna wivu na hicho cheo chako cha Kimataifa na tunakuona unafanya kazi vizuri, mimi binafsi napendekeza twende kwenye 15, lakini ni kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaomba vyombo vyetu vya Serikali vitusaidie; wako walioshiriki naye, wamekaa Esperanza pale. Esperanza ina *CCTV* waende wakachukue *data* pale na wengine bado wapo humu ndani. Wamekaa pale na *CCTV* zipo, zinaweza kutusaidia. Vyombo vinaweza kwenda kuchukua ile taarifa ikaja ikatusaidia na wengine tukashughulikanao hata kwenye kesi za uhujumu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, naungana na kamati kwa kitendo walichokionesha, ni cha kiungwana sana. Mawaziri kama Mheshimiwa Bashe tuseme ukweli, kwa haki ya Mungu, ni watu ambao tunatakiwa kuwalinda kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, wakati hali ya sukari ikiwa ni shilingi 10,000 kwa sisi tunaotoka vijijini, kelele ilikuwa ni kubwa sana. Mheshimiwa Bashe umetimiza wajibu wako na Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, Kanuni zetu zinaelekeza wazi na sisi humu tumekaa kiungwana kwa kipindi cha miaka minne, sisi ni ndugu. Unajua unaweza ukakaa na mtu humu ndani kumbe ana msongo wa mawazo.

Mheshimiwa Spika, mimi nakuomba, pamoja na adhabu tutakayoitoa, lakini huyu ni Mbunge mwenzetu. Vyombo vyetu vinavyotuangalia sisi Wabunge wamchunguze afya ya akili, mimi

sina hakika kama bado yuko sawa. Nasema hivyo kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, nilizungumza hapa siku ambayo Mheshimiwa Mpina anakwenda kupima samaki kwa rula. Matendo aliyoyafanya kwenye uwaziri wake wa samaki, Haki ya Mungu, yanamfuata mpaka leo, kabisa. Watu walikufa na mimi mwenyewe nina ushahidi na yeye anafahamu. Umemchomea mtu mitego…

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Achana na Taarifa, wewe ni mtuhumiwa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Achana na Taarifa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu, ni uchangiaji na Bunge bado halijaazimia adhabu kwa Mheshimiwa Mpina. Mheshimiwa Mpina, Taarifa kwa Mheshimiwa Musukuma.

**TAARIFA**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ananisimanga au anachangia? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Musukuma, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, siipokei na bahati nzuri wewe ni Mwanasheria. Wazee wa Mahakama wanavyojigeuza kumshauri hakimu, mtuhumiwa hawezi kuingilia mjadala wangu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninakuomba sana na hili ninamuomba ndugu yetu Mheshimiwa Mpina, pengine sisi

tunaweza kuwa msaada kwako. Tunaweza tukawa tumekaa hapa na mtu ana msongo wa mawazo, hajitambui. Mheshimiwa Mpina anafanya vitu, wewe unajua kabisa kwamba, ume-*submit document* kwa Spika, siku hiyohiyo umekwenda kusoma. Yaani mimi kwa akili yangu ya darasa la saba najiuliza ulifanya makusudi kwa kumuona Spika wetu ni mwanamke au ni nini? Kwa sababu, mimi naamini kabisa ulifanya kitu unachokifahamu na *confidence* ya hatari. Hata pamoja na kwamba, ulikuwa kwenye Kamati, lakini kwenye vijiwe *confidence* yako ilikuwa kama kwamba, wewe uko *above the law*. Hii haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba twende na adhabu ya 15, ili iwe fundisho. Kuna Wabunge wengine wanajifunza humu, sasa ma-*senior* mkifanya hivi kwa kweli, tunalidhalilisha Bunge letu. Pia, mimi ni *M-NEC* kesi ni ile ile, nikitoka hapa, 30 tunae tena.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tauhida Gallos Cassian, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Said Issa. Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, ajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa naanza kwa kuipongeza Kamati yako ya Maadili ya Bunge kwa kuja na ufafanuzi wa kina ikiwa Watanzania wote wanasikiliza. Wakati Kamati inasoma nafikiri kila Mtanzania na wale wanaoandika kwenye mitandao wamefahamu hasa nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu atusaidie Bunge tutende haki kwa Watanzania. Napata shida, kitendo cha kudharau, Mheshimiwa Mbunge mwenzetu hajakudharau wewe, amelidharau Bunge na amewadharau Wabunge.

Mheshimiwa Spika, adhabu hii ya 10 ni ndogo iende kwenye 15 kwa Bunge, isipungue vipindi 15. Hii iwe fundisho kwa yeye aliyeko humu ndani na kwa wanaotaka kujichomoza.

Mheshimiwa Spika, kama Mbunge yuko hapa zaidi ya vipindi vinne haiingii akilini namna anavyotaka kutupeleka au kulipeleka Bunge hili. Haiingii akilini kwamba, sisi Wabunge tumekaa hapa halafu Mbunge mmoja akawa analisanifu Bunge. Kitendo

alichokifanya cha kuonesha dharau ndani ya Bunge kwa kuweza kuwasilisha na bado akatoka kwenye vyombo vya habari, hiki kitendo hakiwezi kuvumilika.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wako hatuwezi kukaa kimya tukaona unadharauliwa. Kitendo cha kudharauliwa wewe pia, tumedharauliwa sisi Wabunge wa CCM tuliokupa kura zote za ndio za kutosha.

Mheshimiwa Spika, nasimama hapa nikiwa pia, ni Mjumbe wa *NEC* niliyepata kura kutoka ndani ya Bunge. Ndani ya chama chetu kuna maadili ambayo Wabunge wa CCM huwa wanafundishwa. Jambo la kwanza ni kuwa na nidhamu kwa kiongozi wako. Wewe ni kiongozi wetu, Mbunge huwezi kuwa unakuwa na jeuri iliyopitiliza ya kumdharau Spika halafu ukasema hakuna kanuni, hakuna Katiba; tutakwenda kwa utaratibu, nchi hii ina utaratibu.

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kufumbia macho vitendo hivi Wabunge wengine wataendelea kututomasatomasa. Ninaomba Mheshimiwa Spika adhabu yako iongezwe na iwe kama inavyosema kwenye Kanuni.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwenye sehemu hii ndogo. Leo Mheshimiwa Waziri anasulubika na anasulubiwa kwa sababu ya kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniweka kwenye Kamati ya Kilimo. Sikuwahi kutafakari kwenda kwenye Kamati ya Kilimo, lakini sasa nazijua shida za Watanzania. Leo Mheshimiwa Waziri anasema tuwasaidie Watanzania, kuna watu wanamsulubu.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kutupa Waziri mzuri ambaye anasimamia haki na anatenda haki. Tunajua mengi, mengine siyo ya kusema hapa kwa sababu, kaka yangu Mheshimiwa Lusinde kasema ataenda kusema *NEC*. Tutaenda kuomba tupewe fursa ya kusema, uvumilivu umetushinda.

Mheshimiwa Spika, haiingii akilini, kisa tu Waziri anawasaidia Watanzania kuona tufanye namna gani. Pia, kamati yako ilitoka Kwenda kuhakiki miwa iliyolala Morogoro kwa kupigwa na mvua na viwanda kushindwa kuzalisha sukari, leo anaenda kusema tuisaidie nchi, tuwasaidie Watanzania. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, yeye anaona ana uwezo wa kununua sukari kwa bei yoyote anayoitaka, lakini kuna wanyonge. Kaka yetu Mheshimiwa Bashe tunakushukuru, tunakwambia ahsante sana na unatutendea haki. Endelea kutenda haki.

Mheshimiwa Spika, kiongozi mnafiki huwa ni muoga, usiwe muoga, kanuni ya unafiki ni kuwa muoga, usiwe muoga. Mnafiki yoyote anakuwa muoga.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, umetupa dakina tano, basi naseme kwa hayo yanatosha na adhabu iongezwe isiwe kama hivyo kamati walivyoileta kamati. Ahsante, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa kwa sababu, wapo Wabunge walioanza kuchangia, lazima tuwe sawa, ili tutakapofika mwisho sote tuwe na uelewa unaofanana.

Mheshimiwa Tauhida Kanuni ya 84 ndiyo ambayo Kamati yetu wameitumia na wao wamependekeza itumike Kanuni ya 84, Fasili ya 3(a) inasema, "Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge visivyopungua 10 au visivyozidi 15", hiyo ni A. Wawili waliofuata, Mheshimiwa Musukuma na Mheshimiwa Lusinde, wamesema 15. B inasema, ikiwa ni kosa lake la pili au zaidi Mbunge huyu asihudhurie vikao vya Bunge visivyopungua 15 au vizivyozidi 20.

Sasa lazima tuwe na uhakika, ili badae saa ya kuhoji niwe najua michango yenu Wabunge. Mheshimiwa Tauhida kati ya hizi, wewe unataja ipi?

**MHE. TAUHIDA CASIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba adhabu yake isipungue vikao 15.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Said Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Emanuel Kingu. Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi, ili nichangie hoja iliyowekwa Mezani na Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge leo hii. Nataka kidogo nitoe kibwagizo kimoja, wakati wa vita vyetu ya Tanzania na Uganda; vita ile ilikuwa ni vita ambayo tulihitaji ushindi. Sasa kuna waliopigana wakiwa ni askari *special,* lakini walichukuliwa mpaka wazee wetu na kufundishwa kwa wiki mbili, hoja ya dharura, ili kutatua tatizo tushinde vita ile.

Mheshimiwa Spika, jambo alilolifanya Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ni jambo la kizalendo na ni jambo la kuungwa mkono na hili ndiyo jambo ambalo lilitakiwa kufanywa na mtu yeyote mwenye mamlaka. Maana ya mamlaka ni kuwa na uamuzi na kujiamini na kutekeleza siyo mamlaka ya kusikiliza hoja ambazo zitakusababishia mamlaka yako kuonekana siyo mamlaka, jambo hili siyo sahihi kwa hiyo, mimi nampongeza sana Mheshimiwa Mohamed Bashe. Nimesikiliza vizuri ripoti hii ambayo imewasilishwa leo na nimeona kwamba, mchakato mzima wa ripoti hii, Mheshimiwa Bashe alikuwa yuko sahihi.

Mheshimiwa Spika, sasa tujiulize, nani mwenye mamlaka unapotokea ukosefu wa sukari nchini, kuhakikisha sukari ya kutosha inapatikana, ni nani? Ni viwanda au ni Serikali ambayo inawakilishwa na Mheshimiwa Mohamed Bashe? Kwa hiyo, mimi naamini Serikali ilifanya kazi yake vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili. Tuangalie kwamba, kwa nini hawa walipewa vibali, lakini hawakuingiza sukari? Na ile ambayo waliingiza, lakini waliificha, sasa tuwaulize wangevaa viatu ya Mheshimiwa Hussein Bashe, je, wao wangechukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, maana kama ni jambo la ukweli, jambo hili alitakiwa Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiuzulu sasa hivi. Je, wao wako tayari kuhakikisha kwamba, ile *mandate* waliyopewa ya kuhakikisha sukari inapatikana nchi nzima kwa

wakati na wananchi wanaipata kwa bei nafuu, wako tayari kuiondosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi jambo hili, naunga mkono hatua zilizochukuliwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe za kuhakikisha Watanzania wanapata sukari kwa wakati na kwa bei nzuri, lakini mpaka sasahivi bei ambayo wanapewa wananchi ni kubwa sana kutokana na ma-*agent* kuwa wachache. Watu wa Kilombero pale, sukari mpaka iende Dar es salaam, irudi Kilombero ndio wauziwe wao. *Cost* hizi za *logistic* ni kwa nini wanatwishwa watu hawa na wanafaida, pale wametoa mashamba yao na kila kitu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naipongeza Serikali kwa kuchukua hatua. Lile suala la kusema kwamba, *Finance Bill* ije hapa tutaiunga mkono, ili tuhakikishe Serikali inakuwa na uhakika wa sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye suala hili la adhabu ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. Huyu ni Mbunge mwenzetu, amefanya kosa kwa kweli, hata mimi naona kwamba, jambo alilolifanya si sahihi. Kwa nini, ameelekezwa na kiongozi wetu ambaye sisi sote tunamheshimu, analiongoza vizuri Bunge, ameambiwa lete ushahidi wako au hakumuamini?

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kwamba, Spika ungetenda haki na angefanya ambayo yanahitajika kwenye suala lake, lakini sasa sijui ni nini. Naamini kuna watu labda wako nyuma yake ambao walim-*push* kufanya mambo hayo, haiwezekani kabisa kwamba hakuna watu ambao walim-*push* mambo haya.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri kwa vile ni Mbunge mwenzetu, basi adhabu ichukuliwe ambayo ni ya kawaida, lakini asirudie tena kufanya kosa kama hili. Mimi naunga mkono adhabu yoyote itakayokubalika kati ya siku kumi ama siku 15.

**SPIKA:** Ahsante sana. Elibariki Immanuel Kingu, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri. Mheshimiwa Augustine Holle Vuma, ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuwa mmoja wa wachangiaji katika Ripoti hii ya Kamati ya Maadili, lakini mimi nasema neno moja, jambo la kujaribu ku-*discredit potential* ya viongozi wa nchi yetu siyo jambo jema sana. Tunaweza tukafikiri kwamba, ni jambo la kuoneana haya kwa sababu, tunakutana hapa Bungeni tunakuwa kwenye kantini tunakunywa chai pamoja, linaweza likajenga utamaduni mbaya sana, hasa sisi viongozi ambao tumeshakomaa tunapaswa kuwa mfano na wengine watuige. Hilo jambo ni la hatari sana.

Mheshimiwa Spika, naweza kusema kwamba, *discreditation* ninayoiongelea hapa, wewe uliona vita tuliyokumbana nayo tulipokuwa kweye kutafuta nafasi yako ya Kiti cha Rais wa Bunge la Dunia. Walewale ambao walitushambulia sana wakati ule wakikufanya uonekane kwamba, haufai katika macho ya Dunia, haohao baada ya tukio la juzi kutokea tumewaona baadhi ndio wamekuwa wa kwanza kuanza ajenda za kuanza kukupa ushauri nini cha kufanya. Kwa hiyo, sisi siyo wajinga Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumemuona Mheshimiwa Tundu Lissu katika Mkutano wake pale Itigi, maneno aliyokuwa akiyazungumza juu ya kutoa maelekezo kwako. Jambo moja ninalotaka kusema kwa faida ya Taifa langu ni, Mwaka 2023 kampuni zinazozalisha sukari kwenye Taifa letu zinafanya kazi kubwa ya kizalendo, tunayashukuru sana, wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2023 palipotokea *sugar gap* kwenye Taifa letu, kampuni hizi zilipewa kazi na Wizara ya Kilimo ziagize sukari. Nataka niliambie Bunge lako Tukufu, hakuna tani hata moja iliingizwa mwaka 2023, sababu ilikuwa ni nini? *To create artificial scarcity,* lakini Waziri huyu, Mheshimiwa Bashe, kwa uzalendo wake na mapenzi yake kwa nchi yake, ilipotokea *sugar gap* mwaka 2024 Kanuni zilikuwa zinamruhusu. Kwa madudu waliyoyafanya mwaka wa nyuma Kanuni zilikuwa zinampa kibali kutokurudia kosa la kuwapa tena vibali vya sukari, lakini Mheshimiwa Waziri Bashe alishuka *to the ground* akatoa vibali kwa kampuni hizi ambazo hazikuweza kuleta sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimejiuliza jambo moja. Nitakuletea ushahidi *from the bottom of my heart,* nimejiuliza, hivi Ripoti ya Mheshimiwa Mbunge, alipata wapi pesa za kwenda kwenye *media house* kuanza kuzishawishi *media house* milioni kumi kila moja ili habari yake ichapishwe? Hela zilitoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisema hapa juzi na ninarudia. Kwa kifupi sana Mheshimiwa Bashe alifanya *intervention* na Serikali kwa lengo la kuwaokoa Watanzania walipakodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Bashe leo asingefanya juhudi za kuhakikisha Taifa linapata sukari, leo tulikuwa tunazungumza bei ya sukari kwenye nchi ilikuwa ifike mpaka shilingi 12,000. Nini lengo lake, kama haikuwa mipango ya kutaka kuiangusha Serikali yetu? Ni nini lengo lake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kauli hizo ninashawishika kabisa ndani ya Bunge hili, kwa dhati ya moyo wangu mimi, Mheshimiwa Mpina ninamheshimu, hata *inbox* nilimfuata kwa *message* nikamwambia. Kaka yangu akaniambia, sikiliza *point,* nilimsikiliza mpaka mwisho.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kingu kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mpina.

**TAARIFA**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, amesema hapa kwamba, Mheshimiwa Mpina alienda kuvishawishi vyombo vya habari kwa milioni kumi-kumi. Najua maamuzi haya ya kuondoshwa Bungeni. Je, atalithibitishia hili Bunge hata mimi nikiwa sipo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina kwanza umesimama kwa Kanuni inayohusu kumpa Taarifa. Kwa hivyo, ukimpa Taarifa wewe unajua maana yake nini? Mimi ninamuuliza yeye anaipokea Taarifa yako au hapana?

Pungufu ya hapo, kama unakusudia na wewe kutumia Kanuni nyingine tumia hizo. Unayo hiyo haki kwa sababu, mpaka sasa hivi bado hujaazimiwa kwa hiyo, soma hapo Kanuni, tafuta Kanuni inayohusika, halafu useme hilo unalotaka kulisema.

Mheshimiwa Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, siipokei hiyo Taarifa yake. Kwanza kitendo peke yake cha kusema anajua maamuzi ya Bunge kumuondoa Bungeni ametoa wapi? *Where did he get these facts*?

Mheshimiwa Spika, tuwe *serious* kwenye mambo *serious* kwa faida ya nchi yetu. Mheshimiwa Mpina amelidhalilisha Bunge siyo wewe, lengo lake pia, ni kujenga taharuki kwamba, Wabunge tulioko humu hatunazo tunapelekwapelekwa, hatujui tunachokizungumza, lakini sisi ni Wabunge makini, siyo watu wa kupelekwapelekwa.

Mheshimiwa Spika, nilisema juzi haipo Serikali duniani itakayoona *abuse* ya *market* inafanyika iache kufanya *intervention* kwa maslahi ya watu wake. Tunaipongeza Serikali kwa *intervention* walizozifanya na kubwa, tunaomba adhabu hii iweze kuwa funzo kwangu na kwa jirani yangu. Akifanya, kesho tandika siku 15 zilizosemwa kwenda mbele, ili kusudi iwe fundisho. Tuheshimiane humu ndani na kuheshimu Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustine Holle Vuma. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, ajiandae

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kipenzi chetu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. Kwanza natanguliza kuipongeza sana kamati yetu chini ya Mwenyekiti, kaka yangu, Mheshimiwa Ally Juma Makoa. Kwa kweli, wamejiongeza na kwa kweli, mmesimamia haki na mmetutendea vyema sisi

Waheshimiwa Wabunge. Ingekuwa tofauti pangechimbika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitangulia kusema siku hizi kule kwetu Kondoa huwa nakaa sana na wazee kwenye vijiwe vya kahawa na nilikaa nao sana *weekend* hii kuongelea hili Sakata. Kwa kweli, nimechota busara na wakaniambia, kama nitapata fursa ya kuchangia niangalie vitu viwili.

Mheshimiwa Spika, Vitabu vya Mwenyezi Mungu vinatuambia alama za mnafiki ni tatu, anapoongea huongea uongo, anapoahidi hatimizi ahadi na anapoaminiwa hufanya hiana, lakini wakaniambia pia, niangalie zile Ahadi za Mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi, zinasema, "nitasema ukweli daima fitina kwangu mwiko". Sasa wanasikitika sana huyu mtovu wa nidhamu, kwa maneno yao wazee wangu kwa sababu, wao wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais na wanamshukuru sana Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe kwa maamuzi magumu aliyoyachukua dhidi ya hili sakata la sukari. Wakasema walimfuatilia sana na huko mbele, Mheshimiwa Mpina, na mimi nitakuja kutoa mapendekezo yangu, kuna vitu tutaomba vyombo vitusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, tunakulinda kwa wivu mkubwa sana, tulikuamini hapa, Dunia ikakuamini. Kitendo hiki cha yeye kukudharau kimetuumiza sana, lakini ndio haya mambo ya mtu mnafiki na anayependa fitina. Amekuja hapa katoa tuhuma zake, hujataka kupendelea upande wowote, umesema lete Ushahidi, lakini hapo ametoka tena anaenda kwenye vyombo, hafuati utaratibu kwa sababu anajua nini kiko nyuma.

Mheshimiwa Spika, huyu jamaa wakati akiwa Waziri wa Uvuvi ameumiza sana Watanzania na ile *operation,* alianza vizuri, lakini kuna harufu ya virushwa-rushwa ndio maana akatoka nje ya dhumuni la ile *operation*. Nina kila sababu ya kusema na kuviomba vyombo visiishie hapa, hebu vichunguze, ni kweli alikuwa na nia ya kusema ukweli kuhusu sakata na maamuzi ya Mheshimiwa Waziri au kuna vitu vimepenyezwa, ili atake kupotosha Bunge na umma wa Watanzania?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninaunga mkono wenzangu waliotangulia kusema kwamba, kwa kweli, ikiwezekana kwa sababu, kule alishatudharau Bunge akapima samaki na *ruler,* sijui, lakini kwa vile ni Bunge lililopita inawezekana kama ni kosa la pili. Kwa vile ni mtu yuleyule mimi ningependa iwe huko 20, lakini kama Kanuni inatubana basi hii 15 siyo mbaya, najua atateleza tena tu na atarudi kwenye 18.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuona Mheshimiwa Bashe atatuvusha wakulima kwa kweli, lakini nikuambie Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, wewe una utu na una utulivu. Ulibezwa sana, lakini ukatulia kijana wa watu umeenda mbele ya kamati, leo ukweli umejulikana. Usife moyo baba, chapa kazi, tupo nyuma yako na tutakuunga mkono na ile dhima yako ya 10/30 itakamilika. Tunamuomba Mheshimiwa Rais, yeye alishasema kuwa, ni chura ambaye hasikii kelele kwa hiyo, hata kwenye nafasi yako ya Uwaziri wa Kilimo awe chura asisikilize kelele utimize malengo yako. Kama anafikiria, basi hiyo nafasi iwe juu zaidi ya hapo isiwe tena sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Augustine Holle Vuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, ajiandae.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia kwenye hoja zilizoko mbele yetu. Kwanza naomba nilishawishi Bunge lako liungane na mimi tukubaliane kwamba, wajibu namba moja wa Mbunge humu ndani na nje ni kulinda Madaraka ya Bunge kwa wivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni sehemu ya wajibu wetu. Bunge letu likidharaulika, likitomaswatomaswa, likakosewa nidhamu, basi maamuzi yetu ambayo tunayafanya yanakuwa hayana maana na vikao vyetu ambavyo tunakaa vinakuwa havina maana. Kwa hiyo, ni lazima tulinde Madaraka ya Bunge, Mhimili wetu, kwa wivu mkubwa sana na hatuishii hapo kwa sababu, Spika ni nembo

yetu, Spika ni alama yetu ya Bunge, Spika ni utambulisho wetu, ukimgusa Spika maana yake ni umegusa sura ya Bunge, hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo alichokifanya Mheshimiwa Mpina cha kukudharau sisi tunaamini kwamba, ametuchokoza na ndio maana tunaamua kunyanyuka kusema, lakini ukiacha hilo imekuwa ni mwendelezo sasa wa utovu wa nidhamu uliopitiliza kwenye mambo mbalimbali na tumelealea vitu hivi. Alianza kutukana Mawaziri, kutukana kila mtu, ame-*advance* sasa amemgusa mpaka Spika, *this is not acceptable,* hatuwezi kukubali hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza vizuri sana Ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati kuanzia hii ya *friction* yake na Bashe, ambayo ukiangalia suala la sukari na mimi nilijua tu litajiibua kwa sababu, sukari ni dude kubwa ambalo Waziri ukijaribu kuligusa, lazima mapapa yajitokeze au wasemaji wao au vibaraka wao wajitokeze. Sasa kibaraka wa kwanza tumemshuhudia, tumemuona huyu hapa, kamati imetuonesha.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kila mtu anamfahamu Mheshimiwa Bashe hapa. Mheshimiwa Bashe ni mtu mtulivu, Mheshimiwa Bashe ni mtu mbunifu, Mheshimiwa Bashe ni mtu muadilifu, Mheshimiwa Bashe ni mtu mchapa kazi na ni mtu anayeweza kufanya maamuzi ndio maana ametutoa sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwenye sekta ya kilimo. Kwa kweli, Wizara ilikuwa ina changamoto nyingi, ni Wizara ambayo watu walikuwa wamekata tamaa, lakini baada ya Mheshimiwa Bashe kufika pale amefanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Bashe hongera mno, sasa haya mengine haya yanayojitokeza ni kawaida, yasikurudishe nyuma, wewe chapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niseme pamoja na kwamba, kabla ya kupendekeza adhabu, kama mchangiaji, kwanza naomba niwashawishi Wabunge tuendelee kumuombea Mheshimiwa Mpina kila mtu kwa imani yake, lakini tatu tumshawishi ajiuzulu Ubunge. Nakwambia tumshawishi ajiuzulu Ubunge kwa sababu, anawezaje kuendelea kuwa Mbunge kwenye Bunge ambalo amelidharau? Anaendeleaje kuwa

Mbunge kwenye Bunge ambalo kiongozi wake wa mhimili amemdharau? Mimi nadhani ni bora ajiuzulu Ubunge aende huko nje apate muda mzuri wa kuongea na vyombo vya habari na kuitukana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naungana na wenzangu angalau vikao 15, maana tungekuwa tunaruhusiwa na Kanuni tungepiga *the maximum.* Sasa hiyo ndio *the maximum* kwa mujibu wa Kanuni, basi *fifteen days*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu na niseme mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Naanza kwa utangulizi ambao naamini wote tutakubaliana kwamba, sukari ni bidhaa muhimu sana na ni hitaji la kila siku la wananchi, lakini sukari ni chakula muhimu kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, tukisema usalama wa nchi watu wanafikiria ni mabomu, risasi au kitu kingine, lakini hata bidhaa kama sukari ni muhimu kwa usalama wa nchi kwa sababu, tumeshuhudia katika baadhi ya nchi huko kwingineko Serikali inaweza ikaondoka madarakani au ikaangushwa kwa jambo dogo sana. Mfano, miaka ya nyuma huko tuliona Ujerumani wananchi wakiandamana, kwa ajili ya mkate tu. Sasa fikiria kuhusu suala la sukari kwa hiyo, ni bidhaa muhimu sana kwa usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale inapotokea mfumo wa kawaida wa soko umefeli, bidhaa zimepanda au hazipatikani au kuna namna yoyote ya bidhaa kutokumfikia mlaji, ambaye ni mwananchi tunategemea hatua ya kwanza ichukuliwe na Serikali kwa maana ya kuwa mdau wa kwanza kufanya *intervention,* ili mlaji asiumie,

ni nani? Ni Serikali. Tunampongeza Mheshimiwa Bashe kwa kufanya *intervention* ya haraka wakati ule wa dharura, wakati ule wa ukosefu wa sukari, wakati ule ambapo sukari ilifika mpaka shilingi 10,000 kwa kilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mjumbe wa Kamati, tumejiridhisha pasipo shaka kwamba, Waziri hajadanganya Bunge, hajavunja Sheria katika suala la sukari na amefuata utaratibu. Mheshimiwa Waziri ametuambia na mimi nataka nikiri kwamba, alichotuambia ni sahihi, alisema hivi tunapotaka kushughulikia mambo magumu, kama Mawaziri, ni lazima mtashambuliwa na kukutana na mambo magumu. Ndio maana baadhi ya Mawaziri wanashindwa kufanya maamuzi magumu kwa sababu, ukijaribu kufanya maamuzi magumu mishale unayoipata inakufanya urudi nyuma na ushindwe kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jukumu la kwanza la Serikali ni kumlinda mlaji, ambaye ni mwananchi. Hatua iliyochukuliwa tunaipongeza na kumpongeza Mheshimiwa Bashe kwa jambo hili, lakini kama haitoshi, kama pia, msingechukua hatua ni sisi-sisi Wabunge tungekuja hapa kusema kwa nini hamkuchukua hatua na kwa nini wananchi hawakupata sukari?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya yaliyofanyika na mambo yote tuliyoyachambua kwenye kamati, masuala ya *gape sugar* na masuala ya *buffer stock,* yote yalizingatiwa na yalifuata utaratibu unaotakiwa. Nakushukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Bashe kwa jambo hili. Ameli-*handle* kwa ustadi mkubwa bila kuvunja utaratibu wowote. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu. Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, lakini najisikia kama nina hasira. Namuomba Mwenyezi Mungu anisimamie kwenye mchango

wangu kwa sababu, naona kabisa moyo wangu unatetemeka. Nakupongeza kwa hatua uliyochukua nami niwe miongoni mwa wakutoa mchango wangu kwa Taarifa ya Kamati ya Maadili, Haki na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naungana na Wajumbe wenzangu, Waheshimiwa Wabunge, ambao wameshachangia. Naunga mkono adhabu ya vikao 15. Mheshimiwa Mpina kwa kweli, ametukosea sana, amekukosea sana wewe na sisi, kama wanawake wenzako. Kwa kweli, ndiyo maana nimesema namuomba Mungu anisaidie nisiwe na hasira kali. Ametudhalilisha sana kama Wabunge, lakini siyo tu Bunge, hata Mhimili kwa maana ya Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mpina amezoea sana, leo hii amebananishwa kwenye 18 kwenye suala la sukari, lakini kabla ya hapo amekuwa akifanya hivyo vitu mara nyingi. Wengine wametoa mfano wa suala la samaki kupimwa na rula, lakini naweza nikasema alisumbua pia, kwenye suala la mbolea hapa ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa nashindwa kuelewa kwamba, shida yake ni Mheshimiwa Bashe? Au shida yake ni uongozi ambao Mheshimiwa Bashe anao? Au shida yake ni kutetea maslahi ya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, nikijaribu kuangalia hapa naona kama mwenzetu amejiegesha kwenye kutetea maslahi ya ma-*tycoon,* jambo ambalo nashangaa sana. Katika maisha yetu haya na tunavyoishi yupo mnyama mmoja ambaye ana tabia tofauti kabisa na wanyama wengine. Huyu mnyama, natoa mfano tu, kama kuna mtu ataunganisha maneno sasa ni yeye. Wanyama wote wana tabia ambazo ziko sawasawa, wanalinda familia zao na nini, lakini kuna mnyama anaitwa nguruwe; huyu mnyama akizaa mtoto wa kwanza lazima ageuke amtafune, ndiyo tabia yake. Awe wa kufugwa au awe ngurue wa pori, hii tabia anaifanya huyo mnyama.

Mheshimiwa Spika, sasa sitaki niende mbali zaidi. Nataka niseme Mheshimiwa Waziri Bashe amefanya jambo kubwa na zuri

sana la kuhakikisha kwamba, anasimama kwenye nafasi yake kutokana na upungufu wa sukari uliokuwa umejitokeza na tafrani iliyojitokeza nchi nzima, kupanda kwa bei kwa kasi. Aliamua kuchukua mamlaka yake aliyopewa Kisheria na kuhakikisha kwamba, sukari inakuja, ili Watanzania walio wengi, Watanzania milioni 60, waweze kunufaika na bei ndogo na waweze kunufaika na punguzo la tozo ambalo linafanyika baada ya Sheria hii ya kuingiza sukari. Kwamba, sukari inaingizwa haitozwi chochote kwa hiyo, Mtanzania apate sukari kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa anajitokeza mtu mwingine ambaye ana nia ovu hataki Wananchi wa Tanzania wapate sukari kwa bei ndogo, badala yake anasimama kama dalali kwa ma-*tycoon* wenye pesa ambao wanafanya biashara kwa maslahi yao, sasa sisi tunashindwa kumuelewa. Naomba niseme kwamba, Mheshimiwa Bashe amefanya kazi nzuri sana katika nchi hii. Tumeona katika utekelezaji wa majukumu yake. Mbolea ilikuwa bei juu na sasa inauzwa kwa bei ndogo.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ooh *my Jesus.*

**SPIKA:** Mheshimiwa muda umekwisha, ahsante sana. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam. Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ambayo imewasilishwa hapa na Kamati ya Haki na Madaraka ya Bunge, ambayo inamhusu Mbunge mwenzetu. Naanza kwa kusema tu kwamba, haki na uhuru wa kujieleza ni haki ambayo ni ya asili kwa binadamu, lakini kwa taratibu za kawaida lazima kuwe na maadili, lakini kuwe na mipaka na unapokuwa una haki, haki yako inapoishia inaanza haki ya mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, lakini Kanuni za Bunge zilizowekwa zinatusaidia sisi kuenenda vizuri katika chombo hiki cha wananchi. Nataka niseme tu kwamba, baada ya kuwa umempa fursa

Mbunge mwenzetu na kumueleza kwamba, akuletee ushahidi tulitegemea akuletee na asubiri maelekezo yako. Kwa hiyo, maadam kwa maelezo ambayo tumeyapata kutoka kwenye Kamati yetu, Serikali ni kama mzazi kwamba, mtoto anapolia basi mzazi ana wajibu wa kumsikia kilio chake. Kilichotokea kwa Waziri, kwa maana ya Wizara ya Kilimo, kupitia Waziri wetu Mohamed Hussein Bashe ilikuwa ni kuchukua hatua za kuokoa tatizo ambalo lilikuwa linai-*face* nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wote wamesema vizuri hapa, bidhaa zote, kila bidhaa ina umuhimu wake, lakini bidhaa kama sukari ina mambo mengi, inahitajika katika nchi yetu, mifano imetolewa. Kama ambavyo umesema wazalishaji au wasambazaji wa sukari wafanyabiashara walitufikisha katika mahali pabaya na baada ya kuwa wamepewa vibali vya kuagiza sukari hawakuleta hata mfuko mmoja. Maana yake ni walitaka wafikishe bei ambayo itaenda kuwaumiza wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini lengo lao halikuwa kuwaumiza wananchi, ilikuwa ni kuiangusha Serikali kwa sababu, panapokosekana huduma kwa wananchi Serikali ndiyo inasemwa na Mheshimiwa Rais ndiye anayesemwa. Kwa hiyo, kilichotokea kwa mwenzetu, Mheshimiwa Mpina, kwa hakika amekukosea na amelikosea Bunge kwa sababu, yeye ni kiongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu kama ambavyo imeelezwa hata alivyoitwa kwenye kamati kwa hakika aliendelea kuona yuko sahihi hajaonesha kwamba, amekiri makosa yake. Hili tu linatosha kuonesha kwamba, hakutii wewe wala halitii Bunge. Kwa hiyo, katika maelezo ambayo nimeyatoa hapa tulikuwa na mifano midogo hata kwenye mafuta. Serikali iliamua kuingiza fedha, Mheshimiwa Rais akaamua kuingiza fedha kuondoa tatizo la bei ya mafuta nchini. Kwenye hili la Serikali kuleta mpango huu maana yake ni kuokoa tatizo lililopo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, leo kila mwananchi anahitaji sukari. Kwa hiyo, kama ambavyo tuliambiwa vikao vilikaliwa, inawezekana kuna msukumo na kuna aina mbalimbali za fujo ambazo ziliendelea. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa

Waziri kwa hatua kubwa aliyochukua ya ku-*rescue* suala la sukari katika nchi. Bei ime-*stabilise* mambo yanaenda vizuri na wakati mwingine Serikali tukiwa na uwezo wa kuagiza sukari itasaidia bei isiendelee kupanda na itaokoa matatizo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya ambayo yamejitokeza naendelea kuunga mkono hoja iliyotolewa na Kamati kwamba, mwenzetu apewe adhabu, ili imsaidie kujirekebisha wakati mwingine. Hivi vikao 10 itakuwa ni sehemu ya funzo kubwa kwake kwa sababu, kwanza atakuwa hapati ile nafasi ambayo alikuwa anaipata humu ndani ambayo kimsingi ndiyo haki ya sisi Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja, lakini naomba nirudie tena kuwaomba Wabunge wenzangu tuendelee kufuata Kanuni na Taratibu, lakini zaidi tuendelee kumheshimu kiongozi wetu ambaye anaongoza Bunge hili na wewe unafanya kazi nzuri ndiyo maana umeweza kuwa Rais wa Mabunge ya Dunia. Maana yake ni hili unalosimamia ni miongoni mwa majukumu yako, iwe ni funzo kwa Mabunge mengine Duniani kwamba, Mbunge akienda tofauti ni lazima achukuliwe hatua, ili kusaidia watu wengine kujirekebisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa adhabu ambayo imetolewa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamis Mwagao Tabasam, atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika. Mheshimiwa Haji Amour Haji ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja iliyo mbele yetu kuhusiana na kadhia hii iliyotokea kwa ndugu yetu Mheshimiwa Luhaga Mpina. Sisi kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kwamba, tunazo Kanuni zinazotupasa kuzichunga. Pamoja na kupaswa kuzichunga sisi Wabunge wageni ndani ya Bunge hili hatuwezi kujua hizi Kanuni zote, lakini kuna Wabunge wazoefu humu ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa nikiangalia makosa haya yaliyotokea na kilichonipa hofu ni nilivyosikia vikao 15 nikajua ni vikao ambavyo Bunge hili linakaa, yaani tunahesabu vikao hivi vinne vya Mwaka vya Kisheria na vikao vingine. Nikajua kapigwa kadi nyekundu mpaka na vikao vingine akija Bunge la 2026 kumbe ni siku 15, hizi ni siku chache tu. Nafikiri siku 15 ndugu yetu akikaa pembeni halafu akajitafakari akaona amekosea wapi basi atarudi tutakuwa nae, lakini hofu yangu kubwa tu ilikuwa ni vikao 15, yaani mpaka Bunge la 2026, ndiyo nilipata hofu. Siku 15 ni chache, hizi atavumilia tu kwa muda mfupi halafu atarudi.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuzungumza ni kwamba, ukishajinasibisha kwamba, ni mtetezi wa wanyonge halafu ghafla ukabadilika ukawa kubwa la maadui la kuwakandamiza wanyonge, nimesumbuka sana kwenye kichwa changu. Kilichonisumbua ni kwamba, kumbe humu ndani ya Bunge wazalendo tuko wachache sana kwa sababu, niliyekuwa namwamini kwamba, ni mtetezi wa wanyonge ghafla kageuka kuwa kubwa la maadui la wanyonge, yaani kutetea *group* la wafanyabiashara saba. Sasa hivi kwa sababu, nchi yetu siyo ya kijamaa hawa wafanyabiashara saba hawa, wenye viwanda hivi kinachoniumiza tu ni kwamba, tumewapa… *(Kicheko)*

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Inatokea wapi?

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, hapa kwa Mheshimiwa Dkt. Bashiru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kakurwa.

**TAARIFA**

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, sina shida na mchango wake, ni maoni yake, lakini nchi hii ni ya kijamaa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naipokea Taarifa, ni nchi ya kijamaa na mimi ndiyo nasema kwenye nchi ya kijamaa kama hii na sisi watetezi wa wanyonge tunaojulikana humu ndani, akiwemo ndugu yangu Mheshimiwa Mpina kageuka kuwa kubwa la maadui la wanyonge, sasa naona hii adhabu inamstahiki. Ninachotaka kuzungumza tu katika *group* la hawa wafanyabiashara ambao sisi tulikuwa tumewapa dhamana ya kumiliki hivi viwanda vya sukari, vingine vilikuwa vya Serikali, leo vinageuka tena kuanza kuwatesa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumetukanwa sana juu ya sukari. Kilichokuwa kinaniumiza ni kwamba, ukijua tu bei ya sukari ya nchi nyingine, kwa mfano Brazil, sukari haizidi senti 60 kwa kilo, hata ukiisafirisha ukaileta hapa. Mimi nimefanya biashara ya sukari na Kampuni inaitwa *Tradeco,* nimefanyanao biashara ya sukari kwa muda mrefu mpaka kampuni ile ikaja ikaondoka, lakini nimefanya biashara ya kuuza sukari rejareja naagiza Malawi, Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, ukichukua gharama hizo za sukari tunapigwa sana kwenye sukari. Maamuzi yaliyochukuliwa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, ni maamuzi ya kishujaa. Kwanza alikuwa anatakiwa Nzega, angechongewa hata sanamu kuonesha kwamba, ni mashujaa wachache wenye kuchukua maamuzi makubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono sana hoja hii, lakini Serikali ichukue nafasi yake na wewe kutukanwa nimeumia sana kwa sababu, umedharauliwa vya kutosha. Adhabu iliyotoka inastahiki kwa ndugu yangu, basi baadae ataomba radhi, atakuja tutaungana nae. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji. Mheshimiwa Janejelly James Ntate ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuongelea

hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote naunga mkono hoja ya Kamati yangu. Suala la sukari ni suala ambalo ni *sensitive* sana. Siku ambapo Mheshimiwa Mpina alisimama na kusema Mheshimiwa Waziri Bashe amesema uongo na amevunja Sheria, sikujua kama nitakuwa mmoja wa watu ambao watakwenda kushughulika na suala hilo na kwa kweli, nataka niongelee kwa kifupi sana.

**SPIKA:** Sasa ngoja Mheshimiwa Deo Mwanyika. Nimejaribu kutafakari hapa kwa sababu, hawa watu pamoja na mambo mengine, lakini walishaomba kuja hapa Bungeni kuonana na kamati, sasa watakapokuja watakutana na kamati ambayo wewe ni Mwenyekiti. Nafikiri wewe usichangie, ili uweze kuwa na nafasi ya kuwasikiliza hao wadau watakapokuja mbele ya kamati yako. Nadhani pengine mchango unaweza ukaja ukaleta changamoto baadae halafu tukapata mushkeli wa kufanya maamuzi. *(Makofi)*

**MHE. DEOGRATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa busara zako.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nadhani Waheshimiwa Wabunge mmenielewa?

Mheshimiwa Haji Amour Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Janejelly James Ntate. Mheshimiwa Prof. Patrick Alois Ndakidemi ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami niseme tu kwamba, ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Maadili iliyoshughulika na shughuli hii iliyopo mbele yako. Kwa kweli, tulikuwa na kazi kubwa, lakini ndiyo wajibu wetu tuliotakiwa tufanye. Kwa kweli, nasema wazi tumepima sana zile hoja ambazo zimekuja mbele yetu. Hoja ya kwanza ni hoja ya utovu wa nidhamu au kusema uongo ambayo ndiyo hasa ilikuwa ni hoja kubwa na hoja ya pili ni kuhusuana na yale yaliyozungumzwa, ya kusema uongo.

Mheshimiwa Spika, nije katika hili suala la hoja halisi ambayo inazungumza suala la sukari. Sukari ni vita na ukweli hakuna mtu

ambaye naweza kumpa pongezi kubwa sana kwa namna ambavyo alikuwa na uthubutu na vilevile kwa namna ambavyo alijieza katika kamati, kama Mheshimiwa Waziri Bashe. Mheshimiwa Bashe ni Waziri ambaye ana uthubutu mkubwa sana na kwa kweli, kaifanyia haki kamati yetu kwa namna alivyoweza kujieleza.

Mheshimiwa Spika, hali hii iliyojitokeza katika Bunge letu hili siyo jambo ambalo ni la kawaida. Hali inayosemwa ya kusema uongo, lakini bahati nzuri sisi Wanakamati tukajaribu kupima maana ya kazungumza uongo sehemu gani?

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri tumejaribu kuchambua sehemu na *element* zote zile ambazo zimeelezwa na shahidi aliyeleta ule ushahidi wa kusema kwamba, Mheshimiwa kasema uongo, lakini ukweli tukaja tukakuta kwamba, Mheshimiwa hakusema uongo.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo lilikuwepo ambalo nalizungumza kwamba, haki na wajibu ni vitu pacha. Kwa kweli, usipoweza kutenda haki maana yake hutoweza kufanya wajibu. Inaonekana dhahiri kwamba, wakati mwingine hapa kuna watu wanasahau wajibu wao. Kama Mheshimiwa Mpina maana yake alijisahau kufanya wajibu. Katenda haki ya kuleta *document* ambazo aliambiwa, lakini wajibu wake wa kusubiri maamuzi ya Bunge, pale kidogo hakufanya wajibu aliotakiwa aufanye.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwa vile nilikuwa Mwanakamati, kwanza naunga mkono hoja zote mbili ambazo tumeziwasilisha katika Bunge letu hili Tukufu na namna ambavyo hukumu ile imetolewa. Sina haja tena kuirudia kwa sababu na mimi ni mmoja wa wanakamati. Kitu cha msingi ni kupima ni hoja zipi zenye nguvu katika hoja ambazo zimeletwa hapa katika ile hukumu ambayo imetolewa na Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi bado nitaendelea kusimama na Kifungu kile kilicholeta hukumu kwa mujibu wa Vifungu vitatu. Hukumu ya mwanzo ni mtu, ambaye atafanya utovu mkubwa sana wa adabu na kumkosea Spika au kulikosea Bunge, maana yake ni kukosa vikao 10 au visivyozidi 10, ya pili ni vikao 15 au

visivyozidi 20 na ya tatu ni maamuzi ya Bunge. Sasa maamuzi ya Bunge nadhani ni kwamba, hata Wabunge wanayo haki ya kusema tunataka aende vipindi 30, hiyo ni haki ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janejelly James Ntate, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi. Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Mimi la kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Bashe. Nampongeza kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu una kijana ambaye amesaidia nafasi yako kwa sababu, mimi nilijiuliza tulikuwa na *crisis* ya sukari na ikaja sehemu mbaya, Wakristo tuko kwenye Kwaresma, Waislamu wako kwenye Ramadhani, ambapo sukari ilikuwa inaliliwa na kila mmoja. Kama Mheshimiwa Bashe asingechukua hayo majukumu sidhani kama Baraza la Mawaziri mngekuwa salama. Wabunge hawahawa ndiyo tungewashughulikia na Mheshimiwa Mpina huyuhuyu ndiyo angewashughulikia ndani ya Bunge hili kwa hii sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nikajiuliza tayari mlishatangaza dharura na Naibu Waziri Mkuu wewe ndiyo ulifungua ile dharura, kutangaza hali ya hatari wakati wa *El-Nino,* na mkaitaka kila Wizara kwenda kujipanga jinsi tunavyotoka kwenye dharura hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bashe akajipanga kwenye sukari na alichofanya ni cha ujasiri. Hongera sana, usibabaike, wewe endelea kusonga mbele na kulitetea Taifa, bila hivyo tungekuwa sehemu ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala la Mheshimiwa Mpina. Mheshimiwa Mpina kulidharau Bunge na kukudharau wewe alifanya makusudi kabisa. Wakati anajieleza mimi nilitoa hata machozi, huwezi kuja unasema kwa nini Mheshimiwa Spika ananileta mimi? Mbona Mheshimiwa Mwigulu alisema tukafanye uganga wa kienyeji hakuletwa? Mbona Waziri Januari alisema

mnaonitaka mnifuate tukamalizane huko nje, hakuletwa? Ina maana alifanya makusudi anakuchokoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu amekuchokoza ni lazima umuoneshe kwamba, wewe ni nani, muoneshe rangi yako. Nitasikitika sana kama utakuja na huruma ya umama kumsamehe. Kwenye hili kusiwe na msamaha kwa sababu, amelidhalilisha Bunge, ametufanya sisi kamati tumekesha usiku kucha, lakini yote ushahidi alioleta haukuthibitisha kama Mheshimiwa Bashe alisema uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaangalia huyu anamtafuta Mheshimiwa Bashe? Anatafuta nini au ni nini kilicho nyuma yake?

Mheshimiwa Spika, unashindwa kuelewa kabisa na ndiyo maana tulikuja na haki. Pale ambapo alisema ukweli, tumesema kasema ukweli, lakini uongo mara 18 haukuwepo. Tulitafuta hata uongo mara mbili hatukuuona, lakini yeye alikuja na ushahidi wa uongo mara 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *NFRA* aliyokuwa anasema imenunua sukari siyo Sheria. Ukienda kwenye Sheria ya *NFRA* kwenye dharura tunatakiwa tuitumie inunue kwa dharura, kama walivyofanya, lakini akasema walikuwa hawana *GN*. *GN* isingeweza kupatikana kwa sababu, sasa hivi ndiyo wameleta kwenye Sheria ya Fedha, ili tuweze kupata *GN* hiyo ya kuifanya *NFRA* iwe inanunua sukari kwa kipindi cha kawaida na cha dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu, inabidi tuwe tunaonyana, inabidi tuwe tunafundishana. Mimi nilimuuliza Mheshimiwa Mpina, mbona mimi nakuamini ni Mbunge wa siku nyingi, una vipindi vingapi? Akasema, mwaka wa 19 huu. Mwaka wa 19 unaweza ukafanya kosa la aina hii? Akasema, siyo kosa.

Mheshimiwa Spika, sasa kama mtu anasema siyo kosa na kafanya kosa na anasema mbona kosa langu linafanana na la mtu fulani, lakini yeye hakuletwa kwenye Kamati hii? Ina maana alikuwa amedhamiria.

Mheshimiwa Spika, nimepata ugumu sana leo wakati tunaangalia adhabu za kuleta. Walikuwa wananitania wenzangu, wewe si ndiyo Mbunge wa Wafanyakazi?

Mheshimiwa Spika, nikasema, ukitaka kumuua nyani usimuangalie usoni. Kwenye hili inabidi tuchukue majukumu magumu na mimi naungana na wenzangu wote, adhabu itoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Bashe, asinyong'onyee. Mheshimiwa Bashe siku aliyokuja kujieleza alikuwa amenyong'onyea sana, yaani anaona anakatishwa tamaa. Unafanya kitu cha kusaidia Taifa, lakini unaonekana hujafanya kitu chochote. Baraza la Mawaziri mimi nawaambia endeleeni kuchapa kazi, msaidieni mama, kazi yenu tunaiona. Msijali hayo mabomu mnayopigwa, kupigwa mawe kupo na miti yenye matunda ndiyo inapigwa mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, atafuatiwa na Askofu Josephat Gwajima. Mheshimiwa Godwin Kunambi ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, na mimi naanza kwa kukushukuru wewe kwanza kwa kuniteua na kunipeleka kwenye hii Kamati ambayo inashughulikia Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Ni Kamati ngumu kweli kweli na hiki kilikuwa ni kikao chetu cha kwanza, tumekaa na baada ya wanakamati wote kulielewa hili suala, tangu nizaliwe sijawahi kuona uzalendo wa namna hii. Watu walikubali hoja, tumezitetea na tukaja na hii ripoti ambayo leo imekuja mbele yako. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitachangia maeneo mawili, eneo la kwanza ni hili ambalo Kiti kimedharauliwa. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika ni Nembo yetu ya Taifa, ni Spika msomi, ni Spika ambaye watoto wetu wa kike na wakiume ambao wanakua wangependa wawe kama yeye. Kwa hiyo, ni mtu ambaye tukubaliane, wote tunatakiwa tumlinde kwa namna

yoyote ile, tumuoneshe heshima zote kwa sababu, ameshaliheshimisha Taifa. Ni nembo yetu na tusikubali kwamba, nabii hakubaliki nyumbani, hiyo tusikubali kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hicho kitu kisije hapa Bungeni. Nabii aanze kukubalika nyumbani, ili huko mbele ya safari tunamuombea vitu vingine vikubwa zaidi kwa hiyo, nakupa pole kwa yaliyotokea. Basi wewe kama mama kuna kusamehe, lakini yale mambo mengine yaendelee.

*(Hapa, baadhi ya Wabunge Walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, siyo kumsamehe mia kwa mia, sijasema hivyo. Kama mama tu wewe nenda, lakini tusikilize Waheshimiwa Wabunge tunakuambia nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ndugu yangu Mheshimiwa Bashe, Waziri wetu, Mheshimiwa Mpina angeleta hii taarifa kwako halafu ukaipangia kamati kwenda kuangalia ni nini kipo pale, lazima ingeonekana kuna mtu aliyesema uongo kwa ngazi yako hiyo na ambaye hakusema uongo. Vile ambavyo Mheshimiwa Bashe hajafanya, ambavyo sasa hivi imedhihirika kwamba, hajakosea tayari imeshakwenda kule na hawezi kurudi tena kule kwenda kujitetea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni funzo kwetu sisi Waheshimiwa Wabunge kwamba, tusiwe tunakurupuka kwa sababu, ukikurupuka unaumiza sehemu nyingi sana. Sasa hivi Mheshimiwa Bashe ameumia na sijui tutamsafishaje kwamba, baada ya kamati kupitia hivi vitu kuna ambavyo hajakosea, tayari vimeshakwenda kule. Niseme tu, Mheshimiwa Mpina, amemuumiza sana Mheshimiwa Bashe na sisi tu…

*(Hapa, kipaza sauti cha Mzungumzaji kilizimika)*

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nani kazima?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, zote zimezima.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, aa, kumbe zote zilizimika. Tumuombe Mheshimiwa Bashe asikate tamaa, aendelee na ujasiri. Aliliingilia hili suala tukiwa na *crisis* kubwa sana ya sukari na mambo mengi aliyofanya kusema ukweli, ni funzo kwa Wabunge kwamba, tafuta kitu ambacho ni halisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mheshimiwa Mpina angefanya *consultation,* angemuona Mheshimiwa Bashe, angempa *data* za upande wake yeye kama Serikali na angelinganisha na zile alizokuwanazo angejua kwamba, Mheshimiwa Bashe hajasema uongo. Kwa kuwa, hakufanya hivyo kwa sababu ambazo hatujui, basi ndiyo yale yaliyotokea yametokea na imemuumiza sana Mheshimiwa Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuliipitia hii ripoti vizuri. Nampongeza sana Mwenyekiti wetu, jana tulitoka pale Saa 7 usiku, tunapambana na hii kazi. Leo mpaka dakika chache kabla ya kuja hapa, tulikuwa tunaifanya Kwa hiyo, tumeifanya kwa uadilifu wa hali ya juu na hatujamuonea mtu. Hivyo nawahakikishia hatujamuonea mtu, ni huyu amefanya hili, huyu amefanya hili, tukaja na msimamo ambao tumeutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Kamati. Nakushukuru sana na mimi naunga mkono hoja ya kamati yangu ya ile adhabu ya vikao 10 ambayo tumeitoa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi. Mheshimiwa Katani Katani ajiandae.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa maneno machache tu, nataka niseme moja kwa moja mdogo wangu, Mheshimiwa Mpina, umekosea. Mdogo wangu umekosea na ni lazima ukubali kwamba, umekosea. Kwenye Biblia Takatifu, Kitabu cha Kumbukumbu la

Torati, Sura ya 27:24, imeandikwa, "amelaaniwa mtu ampigaye ndugu yake kwa siri". Na watu wote waseme amen. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Amen.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, kwenye Bunge hili kuna desturi ya kupiga watu kwa siri kwa makusudi ya kisiasa. Kuna wakati mtu una shida na yeye, mtafute kule nje, usitumie hoja za Kibunge kuangamiza maisha ya mtu. Mheshimiwa Bashe ana mke, ana watoto, ana familia, ana ndugu, ana jimbo, ana shangazi, ana mjomba, kutamka mtu amesema uongo ni kufedhehesha familia yake na watoto wake na ndugu zake. Kwa hiyo, unapofika kutamka hoja kama hizo ni vizuri sana uwe umejizatiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikao hiki kilikaa kunisimamisha mimi vikao kadha wa kadha kwa sababu, nilikuwa nimepinga Chanjo ya *Covid 19*. Hii ni kuthibitisha je, leo umevaa *mask* hapo? Hamna *mask*. Pamoja na kwamba, mimi nilisimamishwa, lakini hakuna mtu mwenye *mask*. Je, *Corona* ipo? Haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niliyasimamia niliyoyaamini ni kweli, lakini Mheshimiwa Mpina umeyasimamia mambo ambayo baadaye yamethibitishwa siyo kweli, umekosea. Kwa namna hiyo, nataka niseme jambo moja kwako Mheshimiwa Mpina, ni vizuri kuomba msamaha. Uombe msamaha wazi kwa Mheshimiwa Bashe, kwa ajili ya kumlindia heshima yake na kuliomba msamaha Bunge pamoja na Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, duniani kuna nguvu nne. Nguvu ya kwanza ni nguvu ya Mungu, nguvu ya pili ni nguvu ya elimu, nguvu ya tatu ni nguvu ya fedha na nguvu inayofuata ni nguvu ya umaarufu. Hizi nguvu zote zinaweza ku-*influence* nchi kuelekea mahali. Ni muhimu sana kuzitumia hizi nguvu ku-*influence* Watanzania kuelekea mahali sahihi. Ukimtaja Mheshimiwa Mbunge mwenzako hadharani kwamba, ni muongo, ume-*damage* maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama wewe busara zisingekuongoza kuiomba Kamati ya Maadili na Kinga za Bunge ichunguze hili, lisemwe, tungekuwa tume-*damage* maisha ya Mheshimiwa Bashe. Mimi nataka kusema, amelaaniwa mtu ampigaye ndugu yake kwa siri, na watu waseme amen. Kwa sababu hiyo iwe ni fundisho kwetu sisi Wabunge wengine, unapokuwa na hoja yako usiijenge kwenye kutafuta ku-*damage* maisha ya mtu. Jenga hoja ya Kibunge, isaidie nchi, wasaidie wananchi na isaidie maisha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho. Mawaziri msiogope kuchukua maamuzi magumu wakati wa dharura. Jambo la dharura linafanyiwa maamuzi ya kidharura na kuna baadhi ya vitu ambavyo unaweza kuvi-*bypass* ukiangalia lengo unalotaka kutimiza. tukikubali jambo hili, basi tutawafunga mikono Mawaziri na linapotokea jambo la dharura watashindwa kutimiza kwa kutumia mamlaka waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. La mwisho, nakuomba pamoja na makosa ya ndugu yetu Mheshimiwa Mpina, Kiti chako kina hekima na kina busara. Mungu akubariki sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Katani. Mwenyekiti wa Kamati ajiandae, mwenye hoja.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. mimi naanza kwanza kwa kukushukuru wewe. Kimsingi *you are an impartial Speaker and thank you for your impartiality*. Kwa nini nimesema maneno haya kama utangulizi?

Mheshimiwa Spika, mimi niliwahi kuwa na hoja hapa inayonihusu dhidi ya Waziri wa Ardhi ulisimama imara na ulikuwa *impartial* kwenye *decision making*. Ahsante sana, hatuna mashaka na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye hoja iliyo mezani. Kabla sijachangia hapa, wakati natafakari nilikuwa nimejiuliza maswali kadhaa. Swali la kwanza nilijiuliza, je, ni kweli sukari ni bidhaa muhimu kwa maisha ya binadamu? Jibu nikapata ni kweli,

hakuna ubishi kwamba, sukari ni bidhaa muhimu kwa maisha ya binadamu kama chakula. Swali la pili nilijiuliza, je, ni kweli kulikuwa na uhaba wa sukari nchini? Jibu likaja ndiyo, hakuna ubishi kwamba, uhaba wa sukari ulikuwepo nchini. Nikajiuliza swali la tatu, je, bei ya sukari ilikuwa juu? Jibu likawa ndiyo, ilitoka shilingi 5,000, shilingi 7,000 hadi shilingi 11,000 katika baadhi ya maeneo. Swali la mwisho nikajiuliza, je, jukumu la Waziri kuagiza sukari nje ya nchi lilisaidia kupungua kwa bei ya sukari? Jibu likawa ndiyo. Sasa sukari inauzwa shilingi 2,300 mpaka shilingi 2,500 katika baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maamuzi ya Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Bashe, unavyozungumzia chakula ni haki ya msingi na hii ni kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 14, inayozungumza kwa habari ya haki ya kuishi. Pia, Ibara ya 25 ya *Universal Declaration of Human Rights* ya Mwaka 1948, Ibara ya 25. Yote haya yanazungumzia habari ya umuhimu wa chakula kwa uhai wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili mtu yeyote mwenye akili timamu inapotokea bidhaa ya muhimu kwa Taifa letu hasa sukari, ambayo watoto wetu wanakunywa uji na sukari, wagonjwa walio hospitali chakula chao ni sukari, hata sisi wenyewe chakula chetu ni sukari. Pia sukari inatumika kama bidhaa kwenye viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nampongeza kwa maamuzi magumu aliyoyafanya kama Waziri. Nilisema hapa, mimi nikipongeza huwa sipongezi hovyo hovyo. Nikipongeza jambo ni kwelikweli, *brother* umefanya jambo la msingi na Mungu akubariki sana kwa maslahi ya Taifa letu. Niseme tu kwa dhati, hapa umeonesha uzalendo, ukiona nimesimama, nasema umeonesha uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nitoe rai yangu kwake. Hii ni *wake up call*, kama Taifa tusiingie tena kwenye mtego wa kupata uhaba wa sukari. Fanya uwezavyo ama kwa wawekezaji ndani ya nchi na tuondoe *monopoly*. Hivi kwanini tunakuwa na viwanda vichache? Kwanini isiwe kila wawekezaji wawekeze kwenye sekta hiyo, ili tuondoe kiburi cha viwanda vichache? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee maneno kwenye Kitabu Kitakatifu cha Biblia. Ayubu anasema, "kutii ni matendo ya imani," "*obedience is ana act of faith.*" Sasa imewekwa hapa hoja Mezani na kaka yangu wa karibu sana. Mimi niseme tu katika jambo hili nikuombe wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mpina ni Mbunge mwenzetu, kama binadamu tumeona makosa aliyoyafanya, lakini ameshauri msemaji mmoja hapa uungwana ni kukiri. Kama atapata fursa, ningekuwa mimi, ya kusema hapa Bungeni angetumia *platform* hiyo kuomba radhi kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi niseme tu kwamba, Mungu akubariki sana. Endelea kuwa hivyohivyo, tuna imani na wewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Katani Katani, Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, ukisoma Quran, Sura ya 94, Aya ya Tano, nilimwambia ndugu yangu Mheshimiwa Hussein Bashe, baada ya kadhia hii ya rafiki yangu Mheshimiwa Mpina, nikamkumbusha maneno ya Mwenyezi Mungu anayosema, *"Fainna Ma'alng'usri Yusra."* Wakati namuambia haya nilikuwa nataka kwamba, awe mvumilivu, hakuna gumu lenye haki linalochelewa. Nilijua wakati wa haki utafika na bahati njema Bunge hili halijakosea, limekupa mamlaka Mheshimiwa Spika ambaye unatenda haki. Ndiyo maana ukalipeleka Kamati ya Maadili jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Bunge na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa mliyoifanya. Mmefanya kazi kubwa ya Bunge na mmemrahisishia sana Mheshimiwa Spika tunapokuja leo. Nitapata shida sana kwa sababu, kamati ile inakaa kwa niaba yetu sote na tayari imeshakuja na mapendekezo. Ukiniuliza mimi, mapendekezo yale aliyozungumza Mheshimiwa Musukuma, mjomba wangu, nayapitisha kabisa 15 na kuendelea, nayapitisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajua ni vitu vya ajabu sana, juzi wakati nachangia hukuwepo hapa, mtu mmoja anajaribu kupoteza *image* ya Taifa hili. Yaani unaamua kupotosha wananchi kwa jambo lililofanywa na Mheshimiwa Waziri, lenye dhamira njema ya kuwasaidia Watanzania wanyonge wa kijijini. Kwa tabia hii ya Mheshimiwa Mpina, kama hakuchukuliwa adhabu nzito, si ajabu siku moja akauliza Mheshimiwa Spika kipindi cha Manyara kile cha mafuriko, akasema na kwenyewe kulikuwa na ajenda.

Mheshimiwa Spika, alivyokwenda Mheshimiwa Bashungwa kwenye kutengeneza barabara Mtwara barabara zimezibwa, watu hawapiti, akaenda akasema lazima barabara ndani ya siku tatu zipitike, huyu bwana mkubwa tukikaa naye humu, anaweza akaleta kizaazaa kikubwa. Haiwezekani Serikali inaona watu wake wanaumia, yenyewe ikae kimya, Serikali ya nchi gani hiyo?

Mheshiiwa Spika, suala la sukari mtu anaweza akadhani ni dogo, lakini linaweza likaleta maandamano ya Taifa hili kwa hiyo, Mheshimiwa Bashe jambo ulilofanya ni la kizalendo. Mimi nashangaa, Mheshimiwa Mpina nilikuwa naye Jeshini, sasa uzalendo uliokuwa unajifunza ulikuwa uzalendo gani? Yaani unataka Watanzania wasipate sukari kwa shilingi 2,800?

Mheshimiwa Spika, kuna mwenzetu amechangia vizuri hapa, hata ingewezekana kushuka bei, ili mama zangu mimi wa Tandahimba kule wapate sukari kwa bei ndogo, ndiyo Mheshimiwa Waziri alichofanya. Kwa hiyo, mimi naungana na mapendekezo yale ya Mheshimiwa Musukuma, tuanze na ile Kanuni ile ya 84 sijui, Kifungu Kidogo cha (3)(b) ya 15 kuendelea mbele, ili wakati mwingine tukija ndani humu, basi tusiwe na mambo ya masihara masihara, lakini kwenye Kanuni zako, ili kulinda heshima ya Kiti chako akitokea mtu akapuuza maamuzi ya Mheshimiwa Spika, sisi vijana wako tupo, weka kipengele kidogo tumalizane nje ya ukumbi pale, itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa anakuja Mtoa Hoja. Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki,

Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Ally Juma Makoa, kuja kuhitimisha hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALLY J. MAKOA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuhitimisha hoja yangu. Ninakushukuru wewe na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wameweza kupata nafasi ya kuchangia hoja yetu hii tuliyoweka mezani.

Mheshimiwa Spika, hoja hii wamechangia Wabunge wanaofika 17 na nimewasikiliza vizuri. Wabunge wote wameonesha ni namna gani walivyokerwa na kitendo cha Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina kukudharau wewe na kulidharau Bunge, lakini ninawashukuru Wajumbe, wengi wamechangia hotuba yetu vizuri. Wabunge wengi wametamani adhabu iliyopendekezwa na Kamati iongezwe kutokana na namna walivyoiona hali hii ya dharau kwa Mheshimiwa Spika na Bunge.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusikiliza hoja za Wajumbe, naomba Bunge lako sasa lihojiwe juu ya adhabu. Walio wengi wamesema vikao 15 na zaidi, wako waliosema vikao 20, lakini kamati ilileta mapendekezo ya vikao 10. Kwa hiyo, ninaomba Bunge lako lihojiwe juu ya adhabu hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nakushukuru na ninatoa hoja.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu wa kawaida nilipaswa hapa kuwahoji. Sasa kabla sijawahoji, adhabu iliyokuwa imependekezwa hapa na kamati ni vikao 10, lakini Wabunge wengi katika uchangiaji wamependekeza vikao 15 na wachache,

nadhani Mheshimiwa Mwenyekiti amesema wachache, ndiyo wamesema vikao 20, siyo? Haya, kwa ile Kanuni ya 84 niliyokuwa nimewasomea hapo inasema nini?

Kwa hiyo, kabla sijawahoji inabidi kwanza niwahoji kwenye ngazi hii ya mwanzo halafu mtakapohojiwa, mtakuwa mnahojiwa sasa hoja nzima, nadhani mmenielewa. Ndiyo utaratibu unavyotakiwa, ili msije mkahojiwa kwenye maamuzi ambayo siyo. Kwa hiyo, wote tuwe tumeelewana kwa sababu, waliopata nafasi ya kuchangia ni wachache kuliko tuliopo hapa Bungeni. Nitaanza na Wabunge wanaoafiki adhabu ya Vikao kumi, halafu Vikao 15 na baadae Vikao 20.

*(Azimio la Bunge la Kumsimamisha Mhe. Luhaga Joelson Mpina kuhudhuria Vikao 15 vya Bunge Lilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu Azimio lilishasomwa hapa Bungeni na sasa nataka kuwahoji kwa Hoja ya Kamati, lakini pia pamoja na Azimio. Sasa pale ilipokuwa inasomeka Kanuni ya 84(3)(a) sasa itasomeka Kanuni ya 84(3), bado ni ya (3)(a), isipokuwa itakuwa inazungumzia visivyozidi 15. Kwa hiyo, hapa kwenye Vikao 10 itakuwa vikao 15 na itakuwa visivyozidi Vikao 15.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nawahoji:-

Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu uchunguzi kwa sababu, ile sehemu ya kwanza lazima tukumbuke haikuwa na maazimio kwa sababu, ilikuwa ni hoja ambayo inatoka kwenye Kanuni inayohusu kusema kama ni ukweli ama si kweli kwa hiyo, ile ilikuwa haina maazimio, lakini ninapowahoji, ninawahoji zote mbili, ili Taarifa yetu ya Kamati iwe imekamilika.

Haya, Wabunge nawahoji sasa; hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Kuhusu Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Kuhusu Maoni ya Kamati Juu ya Ushahidi wa Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina Kuthibitisha Tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe – Waziri wa Kilimo, Kusema Uwongo

Bungeni na Kulipotosha Bunge na Uchunguzi wa Kamati Juu ya Tuhuma Dhidi ya Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina Kudharau Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio Kuhusu Ushahidi wa Mhe. Luhaga Joelson Mpina Kuthibitisha Tuhuma Dhidi ya Mhe. Hussein Mohamed Bashe – Waziri wa Kilimo Kusema Uwongo Bungeni na Kulipotosha Bunge na Uchunguzi wa Kamati Juu ya Tuhuma Dhidi ya Mhe. Luhaga Joelson Mpina Kudharau Mamlaka ya Spika na Mwenendo wa Shughuli za Bunge Lilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Sasa kwa utaratibu wetu, baada ya kuwahoji Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mpina anapaswa abebe vitu vyake, ili aende kutumikia hiyo adhabu ambayo amepewa na Bunge. Kwa hiyo, wakati anajitayarisha kubeba vitu vyake na mimi nitakuwa nasimama kueleza mengine. Mheshimiwa Mpina tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa adhabu hiyo ambayo imetolewa na Bunge leo inamaanisha kwamba, Mkutano huu ambao utakwisha Ijumaa, vikao ambavyo Mheshimiwa Mpina atakuwa hajahudhuria vinaanza kesho, lakini kwa sababu, kwa utaratibu wetu Kikanuni, Bunge linapoazimia, maana yake bado tuko hapa kwenye Kikao. Unapomwambia Mheshimiwa Mbunge atoke, maana yake ni adhabu inaanza kuhesabiwa leo kwa sababu, akitoka maana yake hawezi kurejea kuanzia sasa. *(Makofi)*

Sasa, kwa ufafanuzi ni kwamba, Vikao Vitano vinahesabika kuanzia leo mpaka Ijumaa, halafu Bunge linalofuata lina Vikao Tisa kwa hiyo, nikijumlisha na hivi vitano vinakuwa 14. Kwa hiyo, Kikao kimoja cha Bunge la Mwezi Novemba hatahudhuria, atahudhuria Kikao cha Pili cha Mwezi Novemba. Kwa hiyo, hicho ndicho kipindi ambacho atakuwa nje ya hili eneo la Bunge. Na kama ilivyo ada hataruhusiwa kuja kwenye maeneo ya Bunge na hataruhusiwa kufanya kazi zinazohusu Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, natumia fursa hii kuishukuru sana Kamati yetu ya Bunge kwa kazi ambayo wameifanya katika kipindi hiki kifupi ambacho walikuwa wamepewa kazi hii. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa kufanya kazi hii kwa niaba ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kamati yetu kuwa imekamilisha hii kazi ni muhimu pia, kutoa maelezo kidogo, ili wote tuwe sawa maana wako watu ambao kazi yao ni moja tu, kwa ajili ya upotoshaji. Kwanza, Waheshimiwa Wabunge wote walioomba, kwa ajili ya kuchangia hoja hii wamechangia, hakuna Mheshimiwa Mbunge hata mmoja ambaye hajapewa nafasi.

Sasa, yalikuwepo mapendekezo kadhaa ambayo Waheshimiwa Wabunge hapa mmeyatoa na mmeshahojiwa kwa hiyo, Bunge limefanya maamuzi. Kwa hiyo, isije ikaonekana sijui ni kamati, sijui nani kafanyaje; kamati imeleta hapa na Bunge limefanya maamuzi. Sasa hoja wakati inaendelea hapa wakati mnachangia mlikuwa mnazungumza kuhusu Hoja ya Kudharau Mamlaka ya Spika, lakini wakati huohuo kudharau Bunge.

Sasa, kuna wataalamu huku nje wanaweza wakajitokeza na kusahau kwamba, hata Mheshimiwa Spika ni Mwanasheria. Wanaweza kusema sasa kwa nini alikaa yeye pale mbele wakati na yeye Hoja ilikuwa inamhusu?

Hainihusu Hoja hii mimi binafsi, inahusu Mamlaka ya Kiti. Kwa hiyo, yeyote anayekuja kukaa hapa, maana yake na yeye amedharauliwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, siyo Hoja ya Mheshimiwa Tulia, tutofautishe hapo, ni Hoja ya Mamlaka kwa hiyo, yeyote anayekuja kukaa hapa kwa sababu anakaa kwa niaba yangu na sisi ndiyo tuliopewa kazi ya kusimamia utaratibu hapa Bungeni. Kwa hivyo kukaa kwa Mheshimiwa Spika, watu wasije wakasema Hoja ilikuwa inamuhusu yeye, Hapana. Hii haikuwa Hoja binafsi ya Mheshimiwa Tulia, ilikuwa ni Hoja ya Mheshimiwa Spika na yeyote anayekaa hapa mbele anafanya kazi kwa niaba ya Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo, hilo ni muhimu nilifafanue kwa sura hiyo, lakini pia,

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa uvumilivu wenu. *(Makofi)*

La mwisho kabisa. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali yote, kwa sababu mko hapa, hili suala la sukari ama uhaba wa sukari linapojitokeza kila mwaka, halipendezi. Halipendezi kwa sababu, kama nchi ni lazima kuwa na maandalizi ambayo inajulikana kabisa kwamba, kipindi fulani huwa kunakuwa na changamoto hii. *(Makofi)*

Hivyo basi, kwa hili jambo namna lilivyohitimishwa leo, Serikali ipate picha kwamba, kwa kweli, Bunge halifurahii nchi hii kila wakati kuwa kwenye Hoja hii ya sukari. Kwa hiyo, kwa sababu, viwanda vipo na sasa tumeshapewa picha ya utaratibu huu ambao unataka kuwekwa tunaamini kwamba, jambo hili litakuwa mwisho Mwaka 2024. *(Makofi)*

Huko mbele yanapokuja maana yake Serikali itakuwa imejipanga tayari kuhakikisha hakuna sehemu wananchi wanajikuta kila saa sasa wanasubiria Hoja ya sukari kila inapokuja Ramadhani, Hoja ya sukari kila inapofika mwezi fulani, sasa lifike mwisho. Tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 3.08 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 25 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*